# IERATIKON

**MA IBADA YA LITURGIA YA MT. YOANE KRISOSTOME**

**MT. BAZILI MUKUBWA**

**WENYI KUTAKASWA (PROIGIASMENI)**

**NA MA IBADA NYINGINE NA MA SALA**

**CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE**
**KOLWEZI KONGO**
**2000**

# IBADA YA MANGARIBI (ESPERINOS)

*Elezo: Kama alikuja askofu mu parokie ya padri moja na ilikuja wakati ya Ibada ya Esperinos, askofu atasimama mbele ya Kanisa. Padri mkubwa ao padri mwigine atamupatia kuvaa askofu Mandia kubwa yake na kisha atampatia bakora. Askofu ataingia ndani ya Kanisa, atasimama kati yake na waimbaji wataimba: «***Ee Rabi miaka mengi».** *Askofu anabariki pa fasi ku mbele, kuhume, kushoto na mkongo na atapanda kusimama pa kiti yake, ile ni kati ya Kanisa. Ma Padri wote wataenda kwake, watabusu mukono yake kuomba baraka na wataingia ndani ya Altari Takatifu. Pa njia yao watasema kwa siri: «***Lakini mimi, kwa wingi wa wema wako nitaingia nyumbani mwako; katika kuogopa wewe nitaabudu kwa upande wa hekalu lako takatifu»** *(Zab. 5, 7). Padri atabusu Evangelion Takatifu na Meza Takatifu na Shemasi atabusu mpaka Meza Takatifu. Kisha padri atakamata epitrakilio, ataibariki kusema hivi: «***Tumwombe Bwana. Mhimidiwe Mungu aliyemimina neema yake juu ya mapadri, kama mafuta kichwani, iteremukayo ndevuni, ndevu ya Aaroni na ishukayo mpaka upindo wa mavazi yake».** *Kama ataivaa atasema:* **«Mwimidiwa Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele».**

*Askofu atasema:* **Amina. Njooni tumwinamie**. . . . *(mara tatu) amasoma Zaburi 103 (104). Kama ni Siku Kuu Ukubwa askofu atasimama pa mustari:* **«Kitu unachowapa wanakiokokota**». *Kisha Waimbaji watanza kuimba Aniksantaria ku mustari:* **«Unafunguwa mukono yako. . . . »**

*Kama hakuna Askofu, Msomaji atasoma Saa ya Tisa pa fasi yake. Kisha kuaga yake padri na shemasi watafanya metania mbele ya Kiti ya Askofu kuomba baraka ya Bwana Yesu Kristu. Kisha watafanya metania tatu mbele ya Ikonostasi, watapindula kuomba hurumia ya waaminifu na wataingia mu Altari Takatifu. Shemasi atachukua Stikario na Orarion yake, atasimama mbele ya padri na atamwambia:* **«Ee Rabi bariki Stikarion na Orarion».** *Padri ataibariki kusema:* **«Mwimidiwe Mungu wetu daima, sasa. . . ».** *Padri anabariki epitrakilion yake, anafungua pazia ya mulango kubwa na anasema:* **«Mwimidiwe Mungu wetu daima, sasa. . . ».** *Msomaji moja anasoma Zaburi 103 (194), lakini padri anasimama mbele ya Altari Takatifu na anasoma kwa siri ma Sala hii:*

SALA I

Ee Bwana mwenyi huruma, aendaye polepole kwa hasira na mwenye tele na huruma, usikie ombi letu, sikiliza sauti ya maombi yetu. Utufanyizie kuwa alama ya wema; utuongoze katika njia zako, ili tutembee katika wema wako; Furahisha moyo wetu katika woga wa jina lako takatifu, kwani u Mkuu na unafanya maajabu; u Mungu wa pekee, hakuna afananaye nawe miongoni mwa wakuwako kimungu. Ee Bwana, mwenyezi katika rehema na mwema katika uwezo kwa kusaidia kufariji na kuokoa wao ambao wanatumainia katika jina lako takatifu. Kwa kuwa kwako tunautoa utukufu wote, heshima na uabudu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA II

Ee Bwana, usituajibu katika hasira yako nyingi, usitutwalii tena katika ukali wako; lakini ututendee kadiri ya wema wako, ewe mganga na mponya wa roho zetu; utuongoze bandarini ya mapenzi yako, angaza macho ya moyo wetu ili tupate kujua ukweli wako; utupe kuisha masalio ya siku hii na ya uzima wetu, katika amani na bila zambi; kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi Mungu, na ya watakatifu wote. Kwani kwako tunakutoa nguvu, utawala, uwezo, na utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA III

Ee Bwana Mungu wetu, utukumbuke sisi watumishi wako, watenda zambi na batilifu; tukipokumbuka jina lako takatifu, usituchanganya katika ungojezi wetu wa rehema yako; lakini

utupatie, ee Bwana, wema wote tunaokuomba kwa ajili ya wokovu wetu; uturudishe kuwa wastahilivu wa kukupenda na roho yetu yote, wa kukuogopa na wa kutenda katika vyo vyote mapenzi yako. Kwani u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na tunakutukuza. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA IV

Ee Wewe unaye tukuziwa kwa nyimbo bila kuachilia na nyimbo ya utukuzo wa mfululizo, ya uwezo takatifu, ikipojazwa kinywa chetu na sifa zako, ili tuweze kutukuza jina lako takatifu, utupe sisi fungu na uriti pamoja na wao wote wanaokuogopa katika ukweli, a wanaochunga amri zako; kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi-Mungu, na ya watakatifu wote. Kwani kwako tunautoa utukufu wote, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA V

Ee Bwana, unayeshika ulimwengu mikononi mwako bila doa; u mvumilivu kwetu, na unajitesa kwa vitendo vyetu vibaya; ukumbuke huruma yako na rehema, utuangalie katika wema wako; utupe, kwa neema yako, kwa kukimbia pia, kwa wakati wa masalio ya siku hii, kwa fitina mbalimbali ya mwovu; zuia uzima wetu ku makimbilio ya mitego yoyote kwa neema ya roho yako mtakatifu unapobarikiwa naye, kama vile roho yako mtakatifu kamili. Kwa rehema na upendo kwa ajili ya wanadamu wa mwana wako wa pekee, unapobarikiwa naye, kama vile roho yako mtakatifu kamili, mwema na muletauhai, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA VI

Ee Mungu, mkuu na mwenye maajabu, unatawala na unaongoza ulimwengu na wema usiyoweza kusema na tuzo kubwa; umetupa mali ya ulimwengu huu, na ulipotuongoza kwa mali uliyotupa, unatupa rahani ya ufalme uliyotuhaidia majira ya siku hii mkosama uliyotupa, umetuepusha ubaya wo wote; utupe sisi kwa kuishi bila magombezi, katika ukuwapo wa utukufu wako takatifu, na kwa kukuimba, ewe Mungu wa pekee, mwema kamili na mpenda wanadamu. Kwani u Mungu wetu na tunakutukuza Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA VII

Ee Mungu mkuu na uliye juu, u peke uliye umilele, a unayekaa nuru kutokaribika; na hekima ukafanya kiumbe cho chote, ukatenganisha nuru na giza ukiweka jua kutawala mchana, mwezi na nyota kutawala usiku, isipokuwa zambi zetu, ukatuhukumu wastahilivu, na kusimama, wakati huu, mbele ya uso wako, wa kutangaza jina lako na kukutolea sifa ya mangaribi; ee Bwana rafiki wa watu, peleka wewe mwenyewe sala yetu kama uvumba mbele yako, na uyapokee sawa sawa manukato ya arufu nzuri. Utupe mangaribi na usiku tulivu, utuvike silaha za mwangaza; utuokoe kwa woga kubwa wa usiku na kwa werevu wo wote unaotupeleka gizani; utupe usingizi ambao ulitupatia kama pumziko kwa uregevu wetu, ukipofukuza mbali nao sura yo yote ya kishetani. Ndiyo, ee Rabi, mgawanyi wa wema yo yote, fanya, ili katika usiku huu, ukipenywa na juto la zambi kitandani mwetu, tukumbuke jina lako takatifu na tukiangaziwa kwa usimamizi wa amri zako, tukisimama, roho ikipojazwa tele na furaha, kwa kutukuza wema wako, na kutolea ku huruma yako maombi na sala zetu kwa ajili ya zambi zetu na kwa ajili ya yale ya watu wako; katika rehema yako, utulinde kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi-Mungu, Kwani u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Elezo: Wakati Padri anaposoma Sala saba. Msomaji yeye anasoma zaburi ya mwanzo (IO4) nguvu na kwa sauti tamu.*

*Kama ni Shemasi, atasimama mbele ya Ikonostasi na atasema Irinika. Kana hakuna Shemasi, padri mbele ya Meza takatifu atasema hii Irinika:*

*Msomaji atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

**PADRI***:* Kwa amani, tumuombe, Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya amani kutoka juu, na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya amani ya dunia yote, ya kusimama kuzuri kwa Eklezia Takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya waKristu watawa wa Orthodoksi wote, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya Arkiepiskopu wetu. . *(jina lake)*, ya upresbyteri uheshimiwa, ushemasi katika Kristu, ya wateule wote na ya watu wote, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya mji hii na inchi hii, kila mji na inchi, na ya waaminifu ya wanaoishimo, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya kutupewa na hewa tamu, na manenevuya arzi, na nyakati za amani, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya wasafiri hewani, baharini na nchini, ya wagonjwa, ya wateswa, ya mateka, na kwa ajili ya wokovu wao, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya kutuokolewa na kila sikitiko, gazabu, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.

**PADRI***:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtukufu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmojamwenye we, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.

**MSOMAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI** *na sauti nguvu:*

Kwa kuwa utukufu wote ni wako, heshima na uabudu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

Kama ni Siku Kuu ukubwa, Msomaji atasoma Kipande wa kwanza ya Zaburi wa Kwanza*:* Heri mutu yule asiyekwenda katika shauri la waovu. . . ». Kama hakuna Siku Kuu ukubwa, Zaburi hatusome.

Kisha somo ya Zaburi wa kwanza, Shemasi atasimama mbele ya Ikonostasi na atasema Sinapti Kidogo*:*

**SHEMASI** AO **PADRI***:* Tena na tena kwa amani, tumwombe Bwana.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**PADRI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI** AO **PADRI***:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtakatifu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili nasi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.

**MSOMAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa kwako ni nguvu, utawala, uwezo na utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MSOMAJI***:* Amina.

*Elezo: Kama hakuna Zaburi ya kusoma, kisha Irinika Waimbaji wataimba:* **Bwana nimekuita. . . »** *Wakati Waimbaji wakipofika pa:* **"Sala yangu mbele yako**" *ya Zaburi I4I. Padri anabariki uvumba akisema:*

**PADRI***:*

Tunakutolea uvumba huu, ee Kristu Mungu wetu, kama manukato ya kiroho; ukiyapokea mezani yako mbinguni, ututumie, kwa marudio, neema ya Roho yako Mtakatifu kamili. Anafukiza Meza Takatifu na Nafasi Matakatifu, kiisha Kanisa yote kama kwa zoezo.

*Shemasi atafukiza na chetezo pembeni ya Meza takatifu na kisha inje pembeni ndani ya kanisa. Ya kutoka inje paka ku mulango wa kusini. Hii saa padri, ao Askofu anasema kwa siri Sala ya Kuingia. Ni hii:*

**PADRI***:* Mangaribi, asubui na azuhuri tunakusifu, tunakubariki, tunakushukuru na tunakukililia, ee Rabi wa ulimwengu. Bwana mpenda wanadamu. Pokea sala yetu kama uvumba mbele yako, usiinamishe roho yetu kwa sauti ao kwa mawazo mabaya lakini utuokoe kwa wale wanasakaroho yetu. Kwako, ee Bwana, kunanyanyuka macho yetu; katika wewe tunatumaini, ee Mungu wetu, fanya kusudi tusichanganywi. Kwa kuwa kwako tunautoa utukufu wote, heshima na kuabudu. Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Wakati waimbaji wanaimba Wimbo ya Mtakatifu, ni kusema: Doksastikon:* **Utukufu kwa Baba. . . . »,** *Shemasi anakamata chetezo atakachopeleka mbele ya Padri na atasema:*

**SHEMASI***:* Bariki, ee Rabi, ubani.

**PADRI***:* Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Kisha kwa Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatafu wote wawili wikipofika mbele ya Meza Takatifu, wanainama kwa ajili ya Sala ya kwingia wanayosema kwa sauti ya chini:*

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Bariki, ee Rabi, kuingia huku takatifu.

**PADRI***:* Kubarikiwe kuingia kwa watakatifu wako, wakati wowote, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kama ni Askofu yeye atasema hii sala.*

*Shemasi anafukiza na kusema kwa kupaza sauti:*

**SHEMASI***:* Hekima. Tusimameni.

Mwandamano wa kwingia.

*Shemasi, wakati waimbaji wanaimba Mwangaza Upole (Ilaron), ku mwisho yake anafukiza ma Ikone ya Ikonostasi na anaingia ndani ya Altari Takatifu. Ya kuingia yeye ndani, anamufukiza na chetezo. Padri anainamisha kichwa yake kidogo mbele ya Askofu ao mbele ya Ikone ya Kiti yake na ataingia ndani.*

*Kama ni ma padri mengi na wanataka kufanya Kuingia wote pamoja, mbele watabusu mukono ya Askofu ao watafanya metania kidogo mbele ya Kiti yake na wataingia ndani ya Altare Takatifu. Watabusu Evangelion na Meza Takatifu. Kisha watavaa Felonion na Epitrakilion na watatoka inje katika mustari ya hile tarehe ya Upandirisho wao. Shemasi atasema:* **Hekima. Simameni***. Atafukiza na chetazo Askofu na ma Ikone ya Ikonostasi, wakati mapadri watafika ya kuimba Wimbo:* **Mwangaza upole. . . » pa fasi***:* **Kuangalia mwangaza wa mangaribi».** *Ma Padri kisha watainamisha ma kichwa yao mbele ya Askofu ao Kiti yake na wataingia ndani kuendelea kuimba hii Wimbo:* **Mwangaza. . . »**

**SHEMASI***:* Esperas (Mangaribi) Prokimenon.

*Kama walifanya Kuingia Takatifu ma Padri mengi, hawa wataimba ya kwanza Prokimenon na kisha ma kundi ya waimbaji moja-moja.*

## PROKIMENON YA JUMA MZIMA

Mu Posho*:*

Bwana anatawala, amevikwa utukufu *(mara tatu).*

Siku ya Mungu*:*

Tazama ninyi munaobariki Bwana, ninyi watumishi wote wa Bwana *(mara tatu).*

Mukazi moya*:*

Bwana atasikia wakati ninapomuita *(mara tatu).*

Mukazi mbili*:*
Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu *(mara tatu).*
Mukazi Tatu*:*
Uniokoe, ee Mungu, kwa jina lako na unihukumu kwa uwezo wako *(mara tatu).*
Mukazi ine*:*
Kusaidiwa kwangu kunatoka kwa Bwana aliyefanya mbingu na dunia *(mara tatu).*
Mukazi tano*:*
Mungu ni ngoma yangu wa rehema yangu atanitangulia *(mara tatu).*
*Kama kuna somo la Manabii. Padri atasema:* Tusikilize. Hekima. Tusikilize.
*Elezo: Siku za Siku Kuu, kunafuata usomi tatu wa Biblia. Ambamo Shemasi anasema:*

**SHEMASI***:* Hekima. Simameni.
*Kwa Barua za Mitume anasema:* Tusikilize. Hekima.
*Kisha usomi Shemasi ao Padri anasimama mbele ya Milango Takatifu na sauti kubwa anasema maombi yafwatayo: Msomaji atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
Bwana mwenyezi. Mungu wa mababu, tunakuomba, utusikie na ukatuhurumie.
Utuhurumie, ee Mungu, katika huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.
Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu waorthodoksi wote.
Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu. . . *(jina lake)*
Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristu.
Tena tunakuomba kwa ajili ya kupata rehema, uzima, amani, afya, wokovu, ulinzi, usamehe na maondoleo ya zambi za watumishi wa Mungu, wadini wote na wakristu waorthodoksi ambao wanakaamo na wanakutana katika muji huu *(ao nyumba wa watawa)*, wa parokia, na walakini na wapotani wa hekalu hii takatifu.
Tena tunakuomba kwa ajili ya watulivu na wenye heri, wajengaji wa hekalu hii takatifu, kwa ajili ya Baba na ndugu zetu wanaofariki ambao wanaolala kwa madini na kwa ajili ya waorthodoksi wanaolala hapa na popote.
Tena tunakuomba kwa ajili ya wafazili wa hekalu hii takatifu na heshima kwa ajili ya wapaji, kwa ajili ya wote wanaotumikamo na wanaoimbamo na kwa ajili ya watu wote walipo hapa ambao wanakujongea kwa rehema kubwa na nyingi.
**PADRI***:* Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mpenda wanadamu na tunakutukuza. Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
**WAIMBAJI***:* Amina.

**ASKOFU, PADRI MKUBWA AO MSOMAJI*:***
Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi, umehimidiwa u, ee Mwana na Mungu wa Baba zetu, jina lako limehimidiwa na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi tunavyokutumaini wewe, Ee Bwana umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa u, uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana, huruma yako ni ya milele usitutoangalie sisi, viumbe vya mikono yako. Sifa zakulaiki kukuimbia ni kwako, utukuufu ni wako, wa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha mara moja Shemasi ataendelea kuomba hivi:*
Tuumalize ombi wetu wa mangaribi kwa Bwana.
**WAIMBAJI***:* Bwana, hurumia.
Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.
**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Mangaribi hii kamili iwe timilifu, takatifu, tulivu, yasio zambi, tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji wataimba kisha kila ombi:* Utupe, ee Bwana.

Malaika wa amani, mlinzi wa roho na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe kwa Bwana.

Vilivyovyema na vifaavyo kwa roho zetu, tena kuwe amani katika dunia, tuombe kwa Bwana.

Kuyamaliza maisha yetu inabaki, katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Tuombe ili mwisho wa maisha yetu uwe kiKristu, kwa amani, bila aibu, tena tuone mufano mzuri mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda Malkia wetu mtukufu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**ASKOFU AO PADRI***:* Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Sala ya kuinamisha nayo kichwa kwa sauti ya chini:*

**ASKOFU AO PADRI***:* Ee Bwana Mungu wetu uliyeinamisha mbingu na ukashuka kwa ajili ya wokovu wa binadamu, uwatazamie watumishi wako na uriti wako kwa sababu wewe u Kuhani Mshindaji na rafiki wa watu. Usiyeongoja masaidio ya watu, kwa kuwa wao wamewazia huruma yako na kutumaini ukombozi wako, uwachunge mangaribi na usiku huu hata na wakati wowote kwa maadui, na kwa vitendo vidogo vya Shetani asiye na mafaa ya akili na mwenye mawazo mabaya.

*Padri anapaza sauti.*

**PADRI***:* Kwa kuwa uwezo wa ufalme wako uhimidiwe na utukuzwe Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kama Siku Kuu ni Mkubwa sasa inafuata Ibada ya Artoklasia (Kubariki mikate tano). Ni hii:*

## IBADA YA KUBARIKI MIKATE (ARTOKLASIA)

*Ku Esperinos, kama kwiko baraka ya mkate, kisha sala juu ya waaminifu na kisha kupaza sauti, kwa maandamano tutaenda kwa ukumbi wa Kanisa, mapadri na shemasi watatangulia mbele, padri na mishumaa mikononi atafukiza uvumba. Waimbaji wataimba wimbo ya Mtakatifu wa siku, shemasi atasoma sala na Litania yafwatayo, waimbaji watajibu: « Bwana hurumia» (mara tatu).*

SHEMASI*:* Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na utuhurumie.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wa Kristu wenyi Ibada na wa Orthodoksi wote.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Muarkiaskofu wetu (jina lake), ya wa padri waheshimiwa, ya Washemasi katika Kristu, ya wateule wote na ya watu wote, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya taifa letu na ya wale wanaoitawala tumwombe Bwana.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Watumishi wa Mungu, Wakristu wote wenyi Ibada na wa Ortodoksi, wanaokaa katika mji huu na ya jamii ya parokia, ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, msaada, usamehe na maondoleo ya zambi.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wenyi heri wajengaji wa hekalu hili takatifu.

Tena tunakuomba kwa ajili ya kulinda hii Hekalu Takatifu hii mji, kila mji na kila inchi, na ya wanaoishiimo toka hasira, huzuni, njaa, mtetemeko wa inchi, garika, moto, upanga, mashambulio ya adui, vita kati ya raia, na lufu kwa rafla, ili Mungu wetu mwema kamili na mpenda-wanadamu atufazilie na kuturehemu, aondoe mbali hasira yote na magonjwa yenye kuelekeza kwa sisi, atuopoe toka makamio na atuhurumie.

Tena tunaomba ili Bwana asikilize maombi ya sisi wakosefu na atuhurumie.

**PADRI***:* Utusikilize, ee Mungu Mwokozi wetu, matumaini ya wale wenye kukaa ku mwisho ya dunia na ya wale walio mbali baharini, ee Bwana hurumia zambi zetu na uturehemu. Kwa sababu wewe ni Mungu wa huruma na mpenda-wanadamu, na tunakutolea utukufu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, daima sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina
**PADRI***:* Amani kwa wote.
**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.
**SHEMASI***:* Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.
**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Ee Rabi mwenyi kujaa na rehema, Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, kwa maombezi ya Malkia wetu Mtakatifu kamili Maria Mzazi-Mungu na Bikira daima, kwa uwezo wa Msalaba uheshimiwa na mhuishaji, kwa matunzo ya Majeshi maheshimiwa ya mbinguni yasiyo na mwili, kwa maombezi ya Yoane Nabii Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, watukufu, Wasifiwa kamili, ya wa padri wetu wa Askofu na waalimu wakubwa Basile mkubwa, Grigori Mtheologo na Yoane Krisostomo, ya wa Padri wetu Watakatifu Athanasi na Kirili, ma Patriacche ya Aleksandria, Nikola wa miujiza, arkiaskofu wa Mire katika Likia, ya Mashahidi Watakatifu, watukufu washindaji wazuri, ya wa padri wetu wabebaji-Mungu, ya Mtakatifu. . mlinzi wa hii Hekalu, ya Yoakimu na Anna, wa babu-Mungu, ya (anataja jina la Mtakatifu wa siku ile ile) makumbusho yake leo, hata ya Watakatifu wote,

Pokea maombi yetu,
Ondoa mbali nasi adui wowote.
Leta amani kwa uzima wetu.
Ee Bwana, utuhurumie sisi na dunia iliyo yako,
Okoa roho zetu, Wewe uliye mwema na mpenda-wanadamu.
**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri wa kwanza atafukiza meza ya mikate ao shemasi na anaimba hii wimbo: «Salamu Bikira, ee Mzazi-Mungu Maria, umejaa neema, Bwana ni nawe. Umebariki wewe katika wanawake wote na Mtoto yako amebariki kwa sababu umemzaa Mwokozi wa roho zetu».*

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**PADRI***:* Ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, Wewe uliyebariki mikate mitano jangwani na kulisha watu elfu tano, wewe mwenyewe bariki hii mikate, hii ngano, hii vinyo na hii mafuta, uizidishe katika hii Eklezia Takatifu, katika hii mji *(ao hii kijiji ao Monasteri)* na katika dunia yote, na takasa Waaminifu wote wataipokea.

Kwani unabariki na kutakasa vitu vyote, ee Kristu Mungu wetu, na tunakutolea utukufu, pamoja na Baba yako wa milele, na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji-uzima, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Wote watarudi katika Altari Takatifu, wakiimba hii wimbo (mara moja), lakini waimbaji wataijibu mara mbili:*

«Watajiri wamekuwa maskini na waliona njaa, lakini wenye kumufuata Bwana hawakose kitu».

*Kisha wimbo wa Apostikha, wimbo wa Simeoni, Trisagion na sala ya Bwana, padri atapaza sauti kusema hivi:*

Kwa kuwa utawala, uwezo na utukufu ni Kwako Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Ku Mwisho Padri atasema:*

Baraka ya Bwana itushukie, kwa wema wake kimungu na mapendo yake kwa wanadamu daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha hii Ibada, Shemasi anatosha ma nguo yake takatifu ndani ya Altari Takatifu. Waimbaji wataimba Apostika. Askofu ao Padri atasema ku mwisho:*

Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

**MSOMAJI***:* Amina. Trisagion*:* Mungu Mtakatifu. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa ufalme na uwezo, na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Apolitikion ya ule Mutakatifu Kanisa yetu anashangilia ile siku.*

Utukufu. . Sasa. . . Theotokion ya ile sauti ya hii juma na siku fulani.

**PADRI***:* Hekima.

**WAIMBAJI***:* Himidi.

**PADRI***:* Aliye ahimidiwe, Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MSOMAJI***:* Amina. Bwana Mungu aimarishe imani takatifu, isiyo na lawama ya waKristu Watawa waorthodoksi katika mji na inchi hii milele na milele. Amina.

**PADRI***:* Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

**MSOMAJI***:* Uliye wa thamani kuwashinda wakheruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli, tunakutukuza we.

**PADRI***:* Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

**MSOMAJI***:* Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Bwana hurumia*(mara tatu).* Ee Rabi Mtakatifu bariki.

**PADRI***:* Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wake asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuitaji, kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili, kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtakatifu, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume Watakatifu, watukufu, wasifiwe kamili. . *(kutaja jina la Mtakatifu, wa Kanisa ile),* ya wapateri Watakatifu wetu na Waekumeniki Wakubwa, walimu na Waierarka, ya Washahidi. Watakatifu, Watukufu, Washindaji Wazuri, ya Wapateri Wabebaji-Mungu, ya Mpateri Mtakatifu wetu Yoanno Krisostomo, Mwarkiepiskopo wa Konstantinopoli, ya Yoakim na Anna, Mababu Mungu Watakatifu na wenye haki *(Mtakatifu wa ile siku),* makumbusho yake leo, hata ya Watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe, yu Mungu mwema, Mrahimu na Mpenda wanadamu.

*Elezo: Kama ni Askofu ndani ya Kanisa pa Kiti yake, Waimbaji, mbele ya mwisho ya hii sala ya yulu anayeisema Padri, watapaza sauti kuimba nguvu miaka mengi kwa Askofu hivi:*

«Ee Bwana, umulinde Rabi na Askofu wetu, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi ee Rabi».

*Shemasi atamupatia kwa Askofu Msalaba na yeye atabariki taifa na mara ingine Shemasi atabusu mukono ya Askofu, atabeba Msalaba na ataiacha pa Meza takatifu.*

**PADRI***:* Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

**MSOMAJI***:* Amina.

*Wakati ya Paska Padri anasema ivi:*

Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti; kwa wale walikuwa ndani ya kaburi aliwapatia uzima.

WAIMBAJI*:* Kweli alifufuka Bwana.

## IBADA YA KATI YA USIKU (MESONIKTIKON) SIKU YA MUNGU

**PADRI***:* Abarikiwe. . Mfalme wa mbinguni. . Trisagion. . Utatu Mutakatifu Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku. Baba yetu. . Kwa kuwa. . Bwana *hurumia (kumi na mbili*) Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . Njooni tumwinamie. . Tunasoma Zaburi 50(51).

*Na kisha tunaimba hii wimbo:*

Sauti ya mbili.

Inastahili kweli kukuimbia Utatu kamili kimungu uliye bila mwanzo; Baba Muumba wa vyote. Mwana wasipo mwanzo aliyezaliwa bila Baba, toka kwa Baba mbele ya milele, na Roho Mutakatifu aliyetoka kwa Baba mbele ya wakati.

Inastahili kweli kukutukuza, ee Mungu-Neno mwenye kuogopesha na kutetemesha Wakeruvi na kutuzwa na Majeshi ya mbinguni, uliye fufuka kaburini siku ya tatu, Kristu Mletaji-uzima, tunakutukuza na woga.

Sisi wote tunamuimbia kama inavyofaa wimbo takatifu*:* Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, utawala wa nyuso tatu, ufalme mmoja na uwezo.

Wakati, ee Bikira bila doa, ulipomuona Mwana wako akifufuka kama inavyofaa katika wafu dunia ilijaa na furaha bila kusema na inamutukuza na kumuheshimu.

Uliye wa thamani kuwashinda Wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.

Trisagion*:* Mungu Mutakatifu. . Utatu Mutakatifu. . Baba yetu. . Kwa kuwa. .

*Kisha tunasoma Ipakoi ya sauti ya hii siku* (*angalia Kitabu ya Paraklitiki). Kama ni wakati ya Siku Kuu mkubwa ya Bwana Yesu Kristu ao Mzazi-Mungu tunaimba Apolitikion yake ao Apolitikion ya Mtakatifu mukubwa ya ile siku Kuu.*

*Kisha* Bwana hurumia (*makumi ine).* Utukufu. . Sasa. . . Uliye wa thamani. . Kwa jina la Bwana, bariki, ee Rabi.

**PADRI***:* Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Musomaji*:* Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . Bwana hurumia *(mara tatu).* Rabi Mtakatifu barikia*:*

Aliyefufuka katika wafu Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombezi ya Mama wake Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili; ya Mitume Watakatifu watukufu, wasifiwa kamili na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani ni Mwema na mupenda-wanadamu.

Tuombe kwa ajili ya amani ya dunia, *(Musomaji anasema:* Bwana hurumia*).*

Kwa ajili ya wa Kristiani wa orthodoksi wote.

Kwa ajili ya wakubwa wetu na wale wenye kutuongoza.

Kwa ajili ya Askofu wetu *(jina lake)* na undungu wetu katika Kristu.

Kwa ajili ya wa padri na ndugu hawapo.

Kwa ajili ya wenye kutusaidia na walitusaidia.

Kwa ajili ya wenye kutuchukia wenye kutupenda.

Kwea ajili ya wale walituomba juu ya kuwaombea, japo uovu wetu.

Kwa ajili ya ukombozi ya wafungwa.

Kwa ajili ya wale weko juu ya bahari.

Kwa ajili ya wagonjwa.

Tuombe tena kwa ajili ya ujazi wa matunda hapa duniani.

Kwa ajili ya wapadri wetu na ndugu wenye kawaida ya dini waliyo kufa mbele yetu; wanaopumzika hapa na dunia nzima.

Kwa ajili ya sisi wenyewe tuseme*:* Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Kwa maombezi ya Wapadri Watakatifu wetu, ee Bwana Yesu kristu. Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

# IBADA YA ASUBUI (ORTHROS)

## SIKU YA MUNGU (MU JUMA)

*Kisha mwisho ya Mesoniktikon, Padri anaingia ndani ya Altari Takatifu, anabusu Meza Takatifu na anaweka epitrakilion anasema:* **«Ahimidiwe Mungu wetu daima. . . ».**

**MSOMAJI***:* Amina. Mungu Mutakatifu. . Utukufu kwa Baba. . . Utatu Mutakatifu. . . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Baba yetu. .

**PADRI***:* Kwa kuwa. .

**MSOMAJI***:* Ee Bwana, okoa, taifa lako. . . Utukufu kwa Baba. . . Ewe Kristu Mungu uliyenuliwa kusudi. . . Sasa na siku zote. . . Ewe Mzazi-Mungu, Msifiwa pia. . .

**PADRI***:* Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tuakuomba, utusikilize na utuhurumie.

**MSOMAJI***:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu watawa waorthodoksi wote.

**MSOMAJI***:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya Arkiepiskopo wetu. *(jina yake)* na kwa ajili ya undugu wetu wote.

**MSOMAJI***:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Kwa kuwa u Mungu mwenye huruma, tena Mpenda-wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MSOMAJI***:* Amina. Kwa jina la Bwana himidi, ee Padri,

**PADRI***: (Anapaza sauti):*

Kwa Utatu Mtakatifu, Wenye asili moja, Muumba wa uhai, usiotengeka, utukufu uwe daima. Sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Wakati Msomaji anaposoma Zaburi sita (ao Eksapsalmos), padri anasoma Sala ya Kumi na pili zifwatazo hapa chini kwa siri mbele ya Meza Takatifu bila kofia. Kisha kwa Sala ya Tatu katika pahali Patakatifu, atatokea ku Mlango wa kaskazini sawa tulivyoandika mbele na vivi hivi.*

SALA 1

Tunakushukuru, Bwana Mungu wetu ulipotuamusha toka kitandani chetu na ulipotuuweka juu ya midomo yetu neno moja la sifa kwa kuliabudu na kuita jina lako takatifu. Tunakuomba kwa huruma ambayo umetupa daima uzima wetu, sasa tena, tuma msaada kwa wale wanaosimama mbele ya utukufu wako takatifu na ambao wakiongojea wingi wa rehema yako. Uwape kwa kusifu kwa wema wako usiyokaridika, wakipokutumikia wakati wowote katika woga wa mapendo. Kwani kwako kunatoka utukufu, heshima na ibada, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 2

Usiku, roho yetu inakesha mbele yako, ee Mungu wetu, kwani amri zako ni mwangaza wa dunia. Utufundishe kutimiza haki na utakatifu katika woga wa jina lako, kwani tunakusifu, wewe Mungu wetu. Tega siki lako, utusikilize, na ukumbuke, kwa majina yao, Bwana, wao wanao hapa na wanaoomba pamoja nasi; uwaokoe kwa nguvu yako, Bariki watu wako na takasa urizi wako, ukiwapa mataifa amani yako, kwa makanisa yako, kwa wapadri wako, kwa wenye kutuongoza na kwa watu wote; kwani jina lako kuu na zuri linabarikiwa na kusifiwa, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 3

Usiku, roho yetu inakesha mbele yako, ee Mungu wetu, kwani amri zako ni mwangaza. Utufundishe, ee Mungu, haki yako, amri zako na hukumu yako; angazia macho yetu na usikilizi wetu, kusudi tusipolala katika zambi zinazotupeleka kifoni. Fukuza giza yoyote rohoni mwetu, utupe jua ya haki na chunga uzima wetu bila magombezi chini ya chapa cha Roho yako Mtakatifu. Ongoza hatua yetu katika njia ya amani. Utupatie kuona, katika furaha, alfajiri na muchana, ili tupate kupandlisha kwako maombi yetu ya asubui. Kwa kuwa Kwako nguvu, ufalme, uwezo na utukufu ni wako Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 4

Ee Rabi, Mungu Mtakatifu hawezaye kushikwa hata na mutu moja, umesema kwa nuru kuangazia gizani, unatupumuzisha katika usingizi wa usiku na unatuamusha kwa kusifu na kurongaronga wema wako; achia kwa rehema yako, utupokee, sasa hapa, tunaposujudu mbele yako, na tunakushukuru, kadiri ya uwezo wetu. Utupatie cho chote tunapokuomba kwa ajili ya wokovu wetu; utufanye kuwa watoto wa nuru na wa muchana, warizi wa mali zako za milele. Utajirini ya huruma yako, ukumbuke, ee Bwana, watu wako wote, wenye kuwa hapa wakipoomba pamoja nasi, na wandungu wetu wote, chini na baharini ambao po pote panapotandaza ufalme wako, wasihi mapendo yako kwa ajili ya wanadamu. Gawanya kwa wote huruma yako kubwa, ili tukipookolewa, roho na mwili, tuweze sawa milele na kusifu na uhuru wote, jina lako zuri na barikiwa, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 5

Hazina ya chemchem ya uzuri wote isiokauka Baba Mtakatifu, mtenda majabu, Mwenyezi, Rabi wa ulimwengu, wote tunakuabudu na tunakusihi, tukiita rehema na huruma yako kwa kutusaidia na kutukinga ku uzaifu wetu; utukumbuke, ee Bwana, tunakuomba pokea maimbi yetu ya asubui kama uvumba mbele yako, ili hata mmoja kati yetu asikataliwe, lakini utuchunge sisi wote katika huruma yako. Kumbuka, ee Bwana, wale wanaokesha na kuimba sifa yako, na kwa sifa ya Mwana wako wa pekee. Mungu wetu na kwa Roho yako Mtakatifu. Uwe kwao, msaada na mulinzi; upokee malalamiko yao juu ya altare yako ya kimbingu na ya kiroho. Kwani uko Mungu wetu, na tunakutukuza Bwba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

SALA 6

Tunakushukuru, ee Bwana, Mungu wa wokovu wetu, kwa mema yote unatujalia, ambako unajaza uzima wetu bila ukoma, tunangalia kwako. Mwokozi na Mtenda mema wa mioyo zetu. Ulitupumuzisha kipande ya usiku, na ulituamusha toka kitandani chetu, ukitusimamisha mbele yako kwa kuabudu jina lako tukufu. Tena, tunakuomba, ee Bwana, utupe neema nanguvu, kusudi tuwe wastahilivu wa kukuimba pamoja na kieleo, na bila kuregea pamoja na woga na mtetemeko, tukitikiza huvyo wokovu wetu wa pekee kwa ulinzi wa Kristu wako. Kumbuka, ee Bwana,

wanaokulilia katika wasiyoonekana na akupingana. Kwani wewe ndiwe mfalme wa amani na Mwokozi wa nioyo zetu na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 7

Ee Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristu, umetulamusha kitandani chetu na umetukusanyisha ku saa ya maombi: kubali kufunikiza midomo yetu, pokea shukrani yetu na utufundishe mapenzi yako; kwa sababu hatujuwi ginsi ya kukuomba, isipokuwa kama wewe mwenyewe. Bwana, hautuongozi kwa Roho yako Mtakatifu. Tena, tunakuomba hata na saa hii, hatukutenda zambi, kwa neno, kwa vitendo ao kwa mawazo kwa kusudi ao kwasiyo kusudi, ondoa, rejeza na samehe. Kwani kama unahukumu makosa. Bwana, nani basi ataishi? Lakini karibu nawe kuna wokovu, Wewe peke ndiwe Mtakatifu, wewe msaada wa nguvu na mlinzi wa mioyo zetu, kwako, ee Bwana, kwainuka wimbo wetu wakati wowote ili uwezo wa utawala wako ubarikiwe na utukuzwe Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 8

Ee Bwana Mungu wetu, umefukuza mbali nasi msongonyifu wa usingizi, na ulitualika kwa mwito takatifu ili tuinue mikono wakati wa usiku na kukushukuru kwa uhaki wa hukumu; pokea maombi yetu na haja zetu, nyimbo zetu za utukufu na kazi yetu ya usiku. Utupatie, ee Mungu, ini letu la kitumaini, tumaini sabiti, mapendelezo ya kweli, bariki kuingia na kutoka kwetu, mambo yetu, vitendo vyetu, maneno yetu, tamaa zetu, utupatie kuweza kufika ku mwanzo wa siku hii, kwa kutukuza, kuimba na kwa kubariki wingi wa uzuri wako usiyonewa. Kwani jina lako takatifu kabisa libarikiwe, na utawala wako tukufu utukuzwe, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 9

Ee Rabi, Rafiki wa wanadamu, angazia mioyoni mwetu nuru safi ya ufahamu wa Mungu na fungua macho ya usikilizi wetu ku kieleo ya risala yako ya injili. Weka ndani zetu woga wa amri zako ya haeri, ili zizuwia tamaa yoyote ya uzini, tupate kuendelea katika njia ya kiroho na kuwaza na kutenda vitu vyote, kadiri ya anasa yako mwema. Kwani wewe ndiwe unayetutakasa na kutangaza, na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 1O

Ee Bwana Mungu wetu, uwepatia wanadamu usamehe wa zambi zao kwa toba na umetuonyesha sawasawa mfano wa maarifa na wa ungamo wa zambi kwa ajili ya usamehe, toba ya nabii Daudi, ee Rabi, zambi zetu ni kubwa na nyingi sana ambamo tumeanguka, utuhurumie katika rehema yako kubwa, na katika huruma yako nyingi futa uzalimu wetu kwa sababu tumefanya zambi kwako. Bwana, unajua mafumbo na siri ya Roho za watu, na paka peke yako, una uwezo wa kusamehe zambi, unaumba ndani yetu roho safi, unatusabitisha na roho ya ezi, na unatujalisha furaha ya wokovu wako, usitufukuze mbali ya uso wako, lakini katika fazili yako, rafiki wa wanadamu, utupatie ya kukutolea sadaka ya uhaki hata siku yetu ya lufu, na kuleta zabihu zetu juu ya altare yako takatifu, kwa usamaha, huruma na mapendo kwa watu ya Mwana Wako wa pekee ambaye unabarikiwa naye, kama vile Roho yako Mtakatifu, mwema na mleta uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 11

Ee Bwana Mungu wetu, wewe unayetiisha ku mapenzi yako uwezo wa kieleo na wa roho, tunakuomba na tunakusihi, pokea utukufu wa sifa tunaokutolea, na viumbe vyote kadiri ya uwezo wetu, na utupatie kwa marudio, ipaji vingi vya wema wako kwani kila goti lipigwe mbele yako, la vitu vya mbinguni, na vya duniani na chini ya dunia; na chochote kinachovuta pumzi, kiumbe chochote, kiumbe sifa yako na kukiri ya kuwa Yesu Kristu ni Bwana kweli na mtajiri katika rehema. Kwani uwezo wote wa mbinguni unakutukuza, na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 12

Tunakukuza, tunakuimba, tunakubariki, tunakushukuru, ee Mungu wa mababu zetu kwani umetenga mivuli ya usiku na umetuonyesha tena mwangaza wa muchana; lakini tunasihi wema wako, utupe usamehe wa zambi, na katika huruma yako kubwa, upokee maombi yetu; kwani tunajua kweli ya yhaki wako; angazia usikilizi wetu na ulinde tamaa zetu za mwili; ili tupate

kutembea wastahilivu kwa kufurahi katika nuru tupate halafu kufika ku uzima wa milele, kwa sababu karibu nawe kuna chemchem ya uzima. Kwani, wewe ndiwe Mungu wetu, na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha kuzimaliza Zaburi hizi sita ao Eksapsalmos. Padri atasema na kupaza sauti kubwa hivi (Irinika):*

**PADRI***:* Kwa amani, tumwombe, Bwana.

*Msomaji atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

**PADRI***:* Kwa ajili ya amani kutoka juu, na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya amani ya dunia yote, ya kusimama kuzuri kwa Ekklezia Takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya nyumba hii Takatifu, na ya wanaoingiamo kwa imani, kwa hesima na kwa kumcha Mungu, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya Arkiepiskopo wetu. . *(jina lake)*, ya Upresbiteri uheshimiwa, ya Ushemasi katika Kristu, ya Wateule wote na ya Watu wote, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya mji huu na inchi hii, kila mji na inchi, na ya waaminifu wanaoishi humo, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya kutupewa na hema tamu, na manenevu ya arzi, na nyakati za amani, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya sawafiri hewani, baharini na nchini, ya wagonjwa, ya wachoshwa, ya mateka, na kwa ajili ya wokovu wao, tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa ajili ya kutuokoa na kila sikitiko, gazabu, hatari na uhitaji, tumwombw Bwana.

**PADRI***:* Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utufazilie, ee Mungu kwa neema yako.

**PADRI***:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, Asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenywe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.

**MSOMAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa utukufu wote, na heshima na usujudu ni haki yako, ya Baba, na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha* ***WAIMBAJI*** *wanaimba:* Bwana ndiwe Mungu. . (*mara Ine*). na mashairi (Zaburi 118, 29, 10, 23) yake kwa sauti ya Tropari ya Juma Bwana. Kisha wanaimba*:* Utukufu kwa Baba. . Tropari ya Mtakatifu ya hii siku na kisha*:* Sasa na siku zote. . **T**heotokion ya Mzazi Mungu.

*Kisha padri atasema Ektenia kidogo:*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa utawala ni kwako, na ufalme na uwezi na utukufu ni wako wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

*Kisha Waimbaji wanaimba Kathisma wa Ufufuo ya Kristu. Kisha Mahimidi ya Ufufuo ya Kristu. Kisha Padri atasema:*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa jina lako limehimidiwa, ufalme wako umetukuzwa, wa Baba na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MSOMAJI***:* Amina. *Na anasoma Ipakoi ya sauti ya ile Juma.*

*Kisha Waimbaji wanaimba Anavathmi ya hii sauti ya Juma na kisha Prokimenon. Kisha wanaimba Kanuni ya Ufufuo ya Kristu na Mtakatifu ya siku.*

*Kisha Ode wa tatu padri atasema Ektenia Kidogo.*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa u Mungu wetu, na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata. . . .

*Kama tunashangilia Mtkatifu Mukubwa mu Juma na mu Ibada yake iko Kontakion na Ikos, mbele ya kuimba Waimbaji Kathisma, watasoma Kontakion na Ikos ya Ufufuo ya Kristu. Kisha wataimba Kundi moja wa kwanza Kathisma ya Mtakatifu wa leo na kundi wa mbili atasema:* **Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .** *Theotokion ya Mtakatifu. Kama hakuna Mtakatifu Mkubwa ya hii siku ya Mungu na hakuna Kontakion na Ikos yake, Waimbaji watasoma Kontakion na Ikos ya Ufufuo ya Kristu, kisha Ode wa sita.*

*Nikusema kisha Ode wa sita padri atasema Ektenia Kidogo:*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa Wewe u Mfalme wa amani tena Mwokozi wa roho zetu, na Kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

*Msomaji anasoma Kontakion na Ikos ya Ufufuo ya Kristu. Kisha Sinaksarion ya Watakatifu. Kisha wanasoma ma Ode nyingine. Kisha wanaomba Katavasies ya hii wakati na Siku Kuu. Shemasi anasimama mbele ya Mulango Bora na anasema:*

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa u Mtakatifu, ee Mungu wetu na kuwakalia watakatifu, na kwako tunauotoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Ropo Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina. Kila mwenye pumuzi, na amsifu Bwana (mara mbili). Na amsifu Bwana, kila mwenye pumuzi.

**SHEMASI***:* Na tumusihe Bwana Mungu wetu atustahilize, kusikiliza Evangelio Takatifu.

WAIMBAJI*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

**SHEMASI***:* Hekima, inukeni tusikilize Evangelio takatifu. Amani kwa wote.

ASKOFU ao **PADRI***:* Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**PADRI***:* Somo ya Evangelio takatifu ilioandikwa na *(jina la Mwevangelizaji).* Tusikilize.

**WAIMBAJI***:* Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

***PADRI*** *anasimama pa fasi ya kuhume ya Meza Takatifu na anasoma Evangelio ya asubui (Eothinon). Kama ni Askofu inje pa kiti yake, ku mwisho ya Evangelion, anabariki taifa na Msalaba. Waimbaji wanaimba***:** **Ee Rabi miaka mengi».** *Kisha Askofu anasoma sla hii:* **«Tukiona ufufuo wa Kristu. . .** *». Kama hana Askofu, Padri mkubwa ao Msomaji moja atasoma hii sala. Kisha padri atatoka inje na Evangelion mikononi mwake na Waimbaji wataimba Zaburi 50 (51). Kama ni Askofu atabusu Evangelion na atabariki waaminifu. Hii saa Waimbaji wataimba***:** **«Ee Rabi, miaka mengi».** *Padri ku mwisho ataweka Evangelion pa fasi ya Proskinitarion Kiti ya ma Ikone ku mwanzo ya Kanisa na atarudia kwake.*

*Waimbaji, kisha Zaburi 50 (51), wataimba:* **Kwa maombezi ya Mitume. . . Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu. . . Unirehemu, ee Mungu, sawasawa. . . Yesu alifufuka kaburini vivi hivi alivyosema. . .**

*Shemasi atasimama inje ya Mulango Bora na atasema hii sala. Kama hana Shemasi, padri atasema hii sala ndani na mbele ya Meza takatifu.*

**PADRI** ao **SHEMASI***:* Ee Mungu uwaokoe watu wako ukaubarikie urizi wako. Agua dunia yako kwa huruma na rehema; paza pempe ya wakristu waorthodoksi, ukakunjua juu yetu mafazili yako tele; kwa ajili ya maombezi ya Maria Bibi yetu msiye na doa. Mzazi-Mungu na Bikira daima. Kwa nguvu ya Msalaba mheshimiwa na tukufu. Kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwa ya mbinguni yaliyo bila mwili. Kwa maombi ya Yoane Mtangulizi, Mbatizaji, Nabii, Mtukufu na Muheshimiwa, Ya Mitume Watakatifu Watukufu na Wasifiwa, ya Wapadri wetu ambao katika Watakatifu na Waaskofu na Walimu Wakubwa, Bazile Mkubwa, Grigori Mutheologo, Yoane Krisostomo, Athanasie na Kirilli, Yoane Mrahimu, wapatriarka wa Aleksandria, Nikola wa Mira, Spirido Askofu Trimithunta wa muujiza, ya Mashahidi Watakatifu watukufu na washindaji wazuri; ya wapadri Watawa na Wabebaji-Mungu; ya Mashahidi Watakatifu watukufu wakubwa, ya Yeorghi Mubebaji ya ushindi (Mtropeoforo), Dimitri mwenye kutosha manukato (Mirovliti), Theodoro Mukubwa wa askari na Theodoro Jemadari (Mstratilati); ya Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki Yoakimu na Anna; ya Mtakatifu *(anataja jina na majina ya kujulisha mtakatifu wa siku ile*) aliye tunakumbuka (tunamukumbuka) leo hata na Watakatifu wako wote pamoja, Tunakusihi, ee Bwana, uliye peke yako na huruma kubwa, usikie sisi watu wenye zambi tukikuomba na ukatuhurumie.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia *(mara 12).*

**PADRI***:* Kwa kurehemu, na huruma, na upendo-wanadamu wa Mwana wako wa pekee, pamoja naye Uhimidiwa, pamoja na Roho wako Mtakatifu kamili, Mwema, Mpaji-uhai, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** ao **SHEMASI***:* Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tukimheshimu kwa nyimbo, na kumtukuza.

Shemasi anatayarisha chetezo, Padri anaibariki, na anaanza Shemasi kufukiza pembeni Meza takatifu, kisha taifa yote ndani ya kanisa. Waimbaji wanaimba*:* **Uliye watamani. . . ».** Kama ni Askofu inje pa Kiti yake anaimba huyu pa fasi pahali ya kundi wa kwanza.

Kisha Ode wa tisa ya katavasia, padri ao Shemasi anasema Ektenio Kidogo*:*

**SHEMASI** AO **PADRI***:*

Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa yanakusifu majeshi yote ya mbinguni, na kuuleta utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

**WAIMBAJI***:* Amina. Bwana Mungu wetu ndiye Mtakatifu. . .

*Kama ni Askofu pa kiti yake, Msomaji atasimama mbele ya kiti yake na atapaza sauti nguvu kusema hivi:* **Ee Rabi Mtakatifu, hamuru**. *Sauti (fulani). Ma Kundi ya waimbaji wanaanza kuimba Masifu. Kama ataisha kuimba Kundi wa mbili, Askofu atashuka ya Kiti yake, atasimama ku mbele ya Ikonostasi, atabusu ma Ikone na atabariki taifa. Waimbaji wataimba:* **Miaka mengi, ee Rabi».** *Kama atafanya Liturgia Askofu atasimama kati ya Kanisa pamoja nama Shemasi yake na watabeba Keros. Ku mwisho yao, Askofu atabariki taifa na waimbaji wataimba:* « **Miaka mengi, ee Rabi».** *Askofu anaingia ndani ya Aktari Takatifu kuvaa manguo yake takatifu.*

*Ile wakati waimbaji wanaimba Doksologia Mkubwa ku mwisho yake, Askofu na mapadri na mashemasi yote watatoka inje kati ya Kanisa na mbele Ikonostasi. Shemasi atasema na sauti chini:*

**SHEMASI***:* Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tuakuomba, utusikilize na utuhurumie. Bwana hurumia *(mara tatu).*

Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu watawa waorthodoksi wote. Bwana hurumia *(mara tatu).*

Tena tunakuomba kwa ajili ya Arkiepiskopo wetu. *(jina yake)* na kwa ajili ya undugu wetu wote. Bwana hurumia *(mara tatu).*

**ASKOFU*:*** Kwa kuwa u Mungu mwenye huruma, tena Mpenda-wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele.

**SHEMASI MWINGINE*:***
Tumalize ombi letu la asubui kwa Bwana.
Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utufazile, ee Mungu kwa neema yako.
Siku hii kubwa kamila, takatifu, tulivu, bila zambi tuombe kwa Bwana.
Malaika wa amani, mwongozi mutumainifu, mulinzi wa roho na mwili yetu, tuombe. .
Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe. .
Vilivyo vyema na vifanyo kwa roho zetu kwa amani na toba ya dunia yote, tuombe. .
Kuimarisha maisha yetu inabaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.
Tuombe ili mwisho wetu uwe kikristu, kwa amani, bila maumivu, bila aibu, tena kutuona teto njema mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.
Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Bibi wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote; ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.

**ASKOFU***:* Kwa kuwa U Mungui wa huruma, wa rehema na kuwapenda wanadamu, kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**ASKOFU***:* Amani kwa wote.

**SHEMASI***:* Tuinamishe vichwa vyetu mbele ya Bwana.

*Askofu kwa siri anasoma hii sala:*

Ee Bwana, uliye ukikea, juuni, unavisimamisha vilivyo chini, tena kwa jicho lako lilio kuviona vyote unauangalia ulimwengu wote, tumekuinamia shingo la roho na la mwili, tunakyomba ewe Mtakatifu wa Watakatifu, Uunyoshe mkono wako juu ya sisi kuuona kutoka katika makao yako matakatifu, ukatubariki sisi wote, ukatusamehe kila kosa tuliikosa kwa kutaka wala si kwa kutaka, utupe sisi vyema vyako vilivyo hapa duniani na huku uliimwenguni wa kuja.

**SHEMASI***:* HEKIMA.

**ASKOFU***:* Aliye ahimidiwe Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**SHEMASI***:* Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu)*, Ee Rabi Mtakatifu barikia.

Aliye fufuka katika wafu Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mama Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuishaji, kwa matunzo ya Majeshi maheshimiwa ya mbinguni juu yasiyo na mwili; kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, Watukufu, Wasifiwa kamili, ya Mashahidi Watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapateri Watawa na wabebaji-Mungu (*ya Mutakatifu musimamizi wa Kanisa*), ya Yoakim na Anna Mababu-Mungu, watakatifu na wenye haki, (*ya mutakatifu wa ile siku*) makumbusho yake ya leo, hata ya watakatifu wote, atuhurumie, akatuokoe, ya Mungu Mwema, Mrahimu na Mpenda-wanadamu, Kwa maombazi ya Wapateri wetu watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

**PADRI** wa kwanza*:* Kwa maombezi ya Rabi Mutakatifu wetu, ee Bwana Yesu Kristu, utuhurumie na utuokoe.

## DESTURI YA MA SIKU KUU MAKUBWA YA BWANA YESU, MZAZI-MUNGU NA WATAKATIFU WAKUBWA.

*Kama Askofu atafanya Liturgia, lakini atavaa ma nguo yake inje kati ya kanisa, ku mwisho ya Doksologia takatifu, waimbaji wataimba na wakati pole-pole kabisa hivi:* **Ee Bwana umulinde**

**Rabi na Askofu wetu, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi».** *Hii saa Askofui atabeba Keros pamoja na ma Shemasi yake. Kisha atavaa Askofu ma nguo yake Takatifu inje. Watamusaidia ma padri wote.*

*Ku mwisho Shemasi wa kwanza atasema:* **«Vivyo hivyo nuru yenu iangaze mbele ya watu, waone matendo yenu mazuri, watukuze Baba yenu aliye mbingu».**

*Shemasi wa mbili atasema***: «Daima, sasa na siku zote, hata milele, na milele. Amina».**

*Kisha Shemasi wa kwanza atakaribia kwa Askofu atamupatie Dikirotrikiron (Ma taa wa wili). Askofu atabeba na atabariki taifa. Waimbaji wataimba:* **«Miaka mengi, ee Rabi**».

*Hapa sasa, kama ni mapenzi ya Askofu, yeye anasoma sala ya kufanya mtu moja Msomaji ao Ipodiakono (Sude Shemasi).*

*Kisha kundi wa mbili wataimba:* «Leo wokovu ulifanyika duniani. . . ».

**SHEMASI** *anasema:* «Sasa ni wakati kwa Mungu».

ASKOFU*:* Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI***:* Omba kwa Mungu kwa ajili yangu.

ASKOFU*:* Bwana amiongoze mwendo wenu.

**SHEMASI***:* Utukumbuke, ee Rabi.

ASKOFU*:* Bwana Mungu amikumbuke upadri na ushemasi wenu.

*Kisha ma padri na ma shemasi wote wanabusi mukono wa kuhume ya Askofu yao ya kusema:* Bwana Mungu amikumbuke cheo ya upandirisho wenu.

*Kisha padri wa kwanza ataingia mu Altari takatifu, lakini Shemasi wa kwanza atasimama mbele ya Mlango Bora kusema:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, himidi.

**PADRI***:* Mhimidiwa ufalme wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu. . . *vile inaanza Liturgia takatifu.*

*Kama hana Askofu, ile wakati waimbaji wanaimba Doksologia Mkubwa, padri anasimama ku mbele ya Altari takatifu na shemasi pa kuhume yake na Shemasi anasema na sauti chini hivi:*

**SHEMASI***:* Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na utuhurumie.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Askofu wetu. . *(jina yake).* na kwa ajili ya wandugu wote.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu watawa waorthodoksi wote.

Tena tunakuomba kwa ajili zetu wapresviteri, washemasi, Watawa na ndugu zetu wote katika Kristu.

Tena tunakuomba kwa ajili ya watumishi wa Mungu wakristu waorthodoksi wanaokaa ao kupita mji na inchi hii, waparishyoni, wasimamizi, wasaidizi, wanaoweka sadaka katika nyumba hii takatifu, ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, kuzuru, masameo na maondoleo ya zambi.

Tena tunakuomba kwa ajili ya warehemu wajengazi wa nyumba hii Takatifu na heshimiwa kamili, wakichoka, wakiimba, na ya watu wote wanaosimama hapa, na kuingojea wapewe huruma yako kubwa na kitajiri.

**PADRI***:* Kwa kuwa U Mungu Mrahimu na Mpenda-Wanadamu, na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI** ao **PADRI***:*

Tumalize ombi letu la asubui kwa Bwana.

Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utufazile, ee Mungu kwa neema yako.

Siku hii kubwa kamila, takatifu, tulivu, bila zambi tuombe kwa Bwana.

Malaika wa amani, mwongozi mutumainifu, mulinzi wa roho na mwili yetu, tuombe. .

Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe. .

Vilivyo vyema na vifanyo kwa roho zetu kwa amani na toba ya dunia yote, tuombe. .

Kuimarisha maisha yetu inabaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Tuombe ili mwisho wetu uwe kikristu, kwa amani, bila maumivu, bila aibu, tena kutuona teto njema mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Bibi wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote; ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.

**PADRI***:* Kwa kuwa U Mungu wa huruma, wa rehema na kuwapenda wanadamu, kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Amani kwa wote.

**SHEMASI***:* Tuinamishe vichwa vyetu mbele ya Bwana.

*Padri kwa siri anasoma hii sala:*

Ee Bwana, uliye ukikea, juuni, unavisimamisha vilivyo chini, tena kwa jicho lako lilio kuviona vyote unauangalia ulimwengu wote, tumekuinamia shingo la roho na la mwili, tunakyomba ewe Mtakatifu wa Watakatifu, Uunyoshe mkono wako juu ya sisi kuuona kutoka katika makao yako matakatifu, ukatubariki sisi wote, ukatusamehe kila kosa tuliikosa kwa kutaka wala si kwa kutaka, utupe sisi vyema vyako vilivyo hapa duniani na huku uliimwenguni wa kuja.

Kwa kuwa kutuhurumia na kutuokoa ni kwako, ee Mungu wetu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI** ao **PADRI***:* Hekima.

**PADRI***:* Aliye ahimidiwe Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote. . .

Bwana Mungu aiimarishe imani takatifu isiyo na lawama ya wakristu watawa waorthodoksi, katika Kanisa Takatifu milele na milele.

Utukufu kwako, ee Mungu, Matumaini yetu, utukufu kwako.

**PADRI***:*

Uliye umefufuka katika wafu, Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mama Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuishaji, kwa matunzo ya Majeshi maheshimiwa ya mbinguni juu yasiyo na mwili; kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, Watukufu, Wasifiwa kamili, ya Mashahidi Watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapateri Watawa na wabebaji-Mungu (*ya Mutakatifu musimamizi wa Kanisa*), ya Mtakatifu Baba watu Yoane Askofu Mkubwa ya Konstantinupoli, na Liturgia yake leo tutafanya *(Ao ya Mt. Baba wetu Bazile. . . )* ya Yoakim na Anna Mababu-Mungu, watakatifu na wenye haki, (*ya mutakatifu wa ile siku*) makumbusho yake ya leo, hata ya watakatifu wote, atuhurumie, akatuokoe, ya Mungu Mwema, Mrahimu na Mpenda-wanadamu.

Kwa maombazi ya Wapateri wetu watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

*Kama itaisha wimbo:* «Leo wokovu ulifanyika duniani. . . » *Shemasi atakamata pa midole ya mukono wake wa kuume, atakaribia padri, atainamisha kichwa mbele yake na atasema:*

**SHEMASI***:* Sasa ni wakati kwa Mungu. Ee Rabi Mtakatifu, himidi.

*Padri ataweka mukono wake wa kuhume pa kichwa ya Shemasi na atasema:* Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote. . .

**SHEMASI***:* Ee Rabi, omba kwa ajili yangu.

**PADRI***:* Bwana akuongoze mwendo yako kwa kila kazi vema.

**SHEMASI***:* Ee rabi mtakatifu, unikumbuke.

**PADRI***:* Bwana Mungu akukumbuke katika ufalme wake, daima, sasa na siku zote, hata milele.

*Shemasi aasema Amina. Kisha atatoka inje, atasimama mbele ya Mulango Bora, lakini padri atasimama mbele ya Meza takatifu, atapika magoti mara tatu kusema na sauti chini hivi:*

**«Utukufu kwa Mungu juu pia; amani katika inchi mapendo kwa wanadamu».** *(mara mbili).* **«Ee Bwana, ufungue midomo yangu na kinywa changu kitaonyesha sifa zako».** *Vile inaisha matayarisho ya kuingia mu Ibada ya Liturgia Takatifu.*

*Kama, kwa mfano, tunashangilia Siku Kuu moja mkubwa ya Bwana Yesu Kristu ao Mzazi wake Mtakatifu kamili Maria, desuri ni hivi:*

*Kisha wimbo ya Kathisma ndani ya Orthros Waimbaji wanaimba Antifonon ya kwanza ya sauti ya inne, ni kusema:*

Toka ujana wangu, tamaa mbaya mingi inanigombanisha. Lakini ewe Mwokozi wangu, unilinde na uniokoe *(Mara mbili)*

Enyi muliochukia Sayuni, mupate haya toka Bwana. Kwani kama majani mbele ya moto, mutakuwa wakikauka *(Mara mbili).*

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na Kwa Roho Mutakatifu.

Katika Roho Mutakatifu, kila nafsi inakuwa hai, na kwa usafisho inanyanyuliwa, inaangazwa, katika Utatu Umoja, kwa siri Takatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Katika Roho Mutakatifu, maji ya neema inayotelemuka inatoka, ikinywesha kiumbe kiote, kusudi kiwe na uzima.

*Kisha wataimba na Prokimenon ya hii Siku Kuu. Kisha shemasi atasema nguvu:*

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**MSOMAJI***:* Bwana hurumia.

**PADRI***:* Kwa kuwa U Mtakatifu, ee Mungu wetu, na kuwakalia watakatifu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Waimbaji wanaimba Shairi hii:*

Kila mwenye pumuzi, na amsifu Bwana. Kila mwenye pumuzi, ma amsifu Bwana. Na amsifu Bwana, kila mwenye pumuzi.

**PADRI***:* Na tumusihi pumuzi Mungu wetu atustahilize, kusikiliza Evangelio Takatifu.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia, Bwana, hurumia, Bwana hurumia.

**PADRI***:* Hekima; inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote. *(anabariki watu).*

**MSOMAJI***:* Na kwa roho yako.

**PADRI***:* Somo ya Evangelio Takatifu ilioandikwa na. . . *(Jina la Mwevangelizaji).* Tusikilize.

**MSOMAJI***:* Utukufu kwako. ee Bwana, utukufu kwako.

*Padri anasoma Evangelion ya asubui. Kisha Padri mkubwa ao Msomaji anasoma Zaburi 50 (51) bila kuiimba. Waimbaji wanaimba: Wainmbaji wanaimba:* Utukufu kwa Baba. . Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu. . . Ao wimbo ingine ya Bwana Yesu Kristu.

*Kama tunashangilia Siku Kuu mkubwa ya Bwana Yesu ao Mzazi wake hatuimbe Ode wa tisa: ni kusema:* **Uliye wa tamani. . . »** *lakini tunaimba Ode wa tisa. Kisha Shemasi atasema Ektenia Kidogo hivi:*

**SHEMASI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa yanakusifu majeshi yote ya mbinguni, na kuuleta utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

*Kisha tunaimba Eksapostilarion. Kama tunafanya Mashangilio ya Yesu Kristu ao Mzazi wake tunaimba hii mwimbo mara tatu. Kama tukona Mtakatifu moja mkubwa tunaimba Eksapostilarion moja, kisha:* **Utukufu. . . Sasa. . .** *Theotokion yake. Kisha waimabaji wanaimba Masifu. Wimbo wa inne ya hii Shangilio ao ya Mtakatifu wa hii siku. Kisha tunaimba Doksastikon na Theotokion. Kisha*

*Doksologia Mkubwa. Ku mwisho yake tunaiumba Apolitikion ya Siku Kuu ao ya hule Mtakatifu ya ile siku. Vile tunaingia mu Ibada ya Liturgia Takatifu.*

## DESTURI YA IBADA YA ASUBUI YA KILA SIKU

*Kama tunafanya Ibada ya Mtakatifu moja ya kila siku desturi ya Ibada ya Asubui itakuwa hivi:*

*Kisha:* **«Bwana ndiwe Mungu. . . »** *tunaimba Apolitikion ya Mtakatifu ya hii siku na Theotokion ya Mzazi-Mungu. Kisha Shemasi aoPadri atasema Ektenia Kidogo, hivi:*

**SHEMASI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa ni kwako uwezo na utawala na nguvu nma utukufu ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha waimbaji wataimba ma Kathisma ya hile siku. Kisha wanasoma Zaburi 50 (51). Kisha wanasoma ao wanaimba Ma Kanuni ya Paraklitiki na Mineon. Kisha ode wa tatu Shemasi ao padri anasema Ektenia Kidogo, hivi:*

**SHEMASI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa Wewe ni Mungu wetu na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. .

*Kisha Ode wa tatu waimbaji wanaimba Kathisma ya hule Mtakatifu ya hii siku. Kisha* « **Utukufu. . . Sasa nasiku zote. . . »** *Theotokion. Kisha wasomaji wanasoma Ode wa inne, tano na sita na mara ingine Shemasi atafanya Ektenia kidogo, hivi:*

**SHEMASI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa wewe u Mfalme wa amani tena mwokozi wa roho zetu na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

*Kisha Msomaji anasoma Kontakion na Ikos ya Mtakatifu ya hii siku na Sinaksarion ya Watakatifu wa leo. Kisha, katika Desturi, tunasoma ma Ode wa saba na mnane na tunaimba Irmosi ya Ode wa mnane. Kisha Shemasi ao Padri anasema:*

**SHEMASI***:* Mzazi-Mungu na Mama wa Nuru, tukimheshimu kwa nyimbo na kumutukuza.

*Kisha shemasi ao padri atafanya Ektenia Kidogo:*

**SHEMASI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa yanakusifu majeshi yote ya mbinguni na kuuleta utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha waimbaji wanaimba Eksapostilarion ya Mutakatifu ya hii siku, ao, kama hakuna, anaimba Eksapostilarion ya ile siku pamoja na Theotokion. Kisha Msomaji anasoma Doksologia Kidogo. Kisha Padri anamaliza maombi ya asubui, hivi:*

**PADRI***:* Tumalize ombi letu la asubui kwa Bwana. . . . . . *(Ona yulu).*

*Kisha Waimbaji wanaimba Apostika ya Paraklitiki na padri ku mwisho yao anasema hii sala:*

**PADRI***:* Ni neno jema kushukuru Bwana na kuimba sifa kwa jina lako, ee wewe uliye juu; kuonyesha wema wako asubui na uaminifu wako kila usiku. (Zab. 92, 1).

**MSOMAJI***:* Trisagion*:* Mungu Mutakatifu. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa. . .

*Kisha waimbaji wanaimba Apolitikion ya Mtakatifu na Theotokion. Kisha inaanza Ibada ya Liturgia Takatifu.*

*Kama hasitakufuata Litirgia, Mosomaji anasoma Saa ya Kwanza na sala hii:* Kristu, Nuru wa kweli, aliyeangaza na kutakasa kila mutu. . . *(Ona mu Kitabu Saa Mukubwa). Kisha Msomaji ata soma Matendo ya Mitume (Apostolos) na Padri atasoma Evangelion ya hii siku. Msomaji atasema:* Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako. *Na padri ataanza kusema hivi:*

**PADRI***:* Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.

**MSOMAJI** *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

Bwana mwenyezi. Mungu wa mababu, tunakuomba, utusikie na ukatuhurumie.

Utuhurumie, ee Mungu, katika huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wa madini na wakristu waorthodoksi wote.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu. . . *(jina lake)*

Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristu.

Tena tunakuomba kwa ajili ya kupata rehema, uzima, amani, afya, wokovu, ulinzi, usamehe na maondoleo ya zambi za watumishi wa Mungu, wadini wote na wakristu waorthodoksi ambao wanakaamo na wanakutana katika muji huu (ao nyumba wa watawa), wa parokia, na walakini na wapotani wa hekalu hii takatifu.

Tena tunakuomba kwa ajili ya watulivu na wenye heri, wajengaji wa hekalu hii takatifu, kwa ajili ya Baba na ndugu zetu wanaofariki ambao wanaolala kwa madini na kwa ajili ya waorthodoksi wanaolala hapa na popote.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wafazili wa hekalu hii takatifu na heshima kwa ajili ya wapaji, kwa ajili ya wote wanaotumikamo na wanaoimbamo na kwa ajili ya watu wote walipo hapa ambao wanakujongea kwa rehema kubwa na nyingi.

Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mpenda wanadamu na tunakutukuza. Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Kisha Padri anasema Kuaga na inaanza Liturgia Takatifu.*

## DESTURI WAKATI YA KWAREZIMA YA PASKA

*Kisha Eksapsalmos padri atasema Irinika:* **Ku amani tumwoimbe Bwana. .** *. na sala ya mwisho:* **Kwa kuwa ni Kwako uwezo na utawala na nguvu na Utukufu ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote. . .**

*Pa fasi ya wimbo: Bwana ndiwe. . . » Waimbaji wanaimba ma Shairi nyingine. Ni ndani ya Kitabu Saa Mkubwa. Na kisha ma shairi Aliluia mara tatu. Kisha wanaimba Wimbo ya Utatu Mutakatifu. Kisha Padri atafanya Ektenia Kidogo:*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa utawala ni kwako na ufalme na uwezi, na utukufu ni wako wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha waimbaji wanaimba ma Kathisma ya sauti ya ile siku. Wanasoma Zaburi 50(51) na kisha padri anasema hivi:*

**PADRI***:* Ee Bwana, okoa watu wako na bariki urizi wako. . . *(Ona yulu, mu ukurasa. . . . . )*

Kisha waimbaji wanasoma ma Kanuni ya Triodio na Mineon. Kisha Ode wa tatu padri atafanya Ektenia Kidogo*:*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa wewe ni Mungu wetu na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

*Kisha waimbaji wanaimba ma Kathisma na Theotokion ya Mineon. Wanasoma kisha ma Ode wa inne, wa tano na wa sita na Shemasi ao padri atafanya Ektenia ingine Kidogo.*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa wewe Mfalme wa amani tena Mwokozi wa roho zetu na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

*Kontakion na Ikos ya Mineon hatusome, lakini pa fasi yao tunasoma Wimbo ya Mashahidi (Martirikon). (Tafuta hii ku mwisho ya Triodio mu fasi ya sauti ya ile siku). Kisha Msomaji anasoma Sinaksarion ya Watakatifu ya ile siku. Na kisha wanasoma ma Ode wa saba na mnane na tisa ya Mineon na Triodio, kama iko. Kisha shemasi atasema:*

**SHEMASI***:* Mzazi-Mungu na Mama wa Nuru, tukimheshimu kwa nyimbo na kumutukuza.

Waimbaji wanaimba mara wa sita*:* Uliye watamani pamoja na ma shairi yao.

Kisha Kundi wa kwanza ya waimbaji wanaimba Irmos ya Ode wa tisa na Kundi ya mbili anaimba*:* «Ni wajibu kweli. . . ». Padri anafanya Ektenia Kidogo*:*

**PADRI***:* Tena na tena. . .

Utusaidie, utuokoe. . .

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili. . .

Kwa kuwa yanakusifu majeshi yote ya mbinguni na kuuleta utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata. . . . . . . . . .

*Kisha waimbaji wanaimba pa fasi ya Eksapostilarion Wimbo ya Mwangaza (Fotagogikon). mara tata. Tafuta hii ku mwisho ya Kitabu ya Triodion na sauti ya hii Juma. Ma Zaburi wa tatu ya Masifu, kisha wanasoma Doksologia Kidogo. Kisha padri atasema Ekteni Mkubwa:* «**Tumalize ombi letu la asubui kwa Bwana. . . »**

*Ksiah Waimbaji wanaimba Apostika na padri ku mwisho yao atasema hii sala:*

**PADRI***:* Ni neno jema kushukuru Bwana na kuimba sifa kwa jina lako, ee wewe uliye juu; kuonyesha wema wako asubui na uaminifu wako kila usiku. (Zab. 92, 1).

**MSOMAJI***:* Trisagion*:* Mungu Mutakatifu. . .

**PADRI***:* Kwa kuwa. . .

*Kisha Msomaji anasoma hii wimbo:*

Ewe Mzazi-Mungu, mlango wa mbingu, tunaposimama hekaluni kwa utukufu wako, tunazani ya kama tunasimama mbele ya mbingu, basi, utufungulie mlango ya huruma yako.

Msamoaji*:* Bwana hurumia *(makumi ine*), Uliye wa thamani. , , Kwa jina la Bwana bariki, ee Padri.

**PADRI***:* Aliye ahimidiwe Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Ee Mfalme wa mbinguni, sabitisha imani, tuliza mataifa, leta amani duniani, linda hii Kanisa Takatifu (Mission ao Monasteri), weka katika makao ya wenye haki baba zetu na ndugu zetu waliyolala tena pokea toba yetu na kukiri kwetu, kwani ndiwe mwema tena mpenda wanadamu.

*Kisha tunafanya Metania (kupika magoti) tatu na kusema kwa kila metania moja-moja sala ya ile inafwatayo ya Mtakatifu Efremi wa Siria*

Ee Bwana na Rabi wa uzima wangu, ondoa mbali nami roho ya uvivu, ya utawanyiko, ya kutawala wengine na maneno ya bure.

Unipe roho ya usafi, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo, mimi mtumishi wako.

Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi zangu tena nisimuhukumu ndugu yangu, kwani umehimidiwa milele na milele. Amina.

*Kisha tunafanya Metania kidogo Kumi na mbili na kisha moya Metania mukubwa na kusema:*

Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi.

*Padri anafanya Kuaga ( Apolisis).*

**SHEMASI** ao **PADRI***:* Hekima.

*Padri mkubwa ao waimbaji:* Bwana Mungu aiimarishe imani takatifu isiyo na lawama ya wakristu watawa waorthodoksi, katika Kanisa Takatifu milele na milele.

**PADRI***:* Utukufu kwako, ee Mungu, Matumaini yetu, utukufu kwako.

**WAIMBAJI***:* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele, Amina. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia, Rabi Mutakatifu barikia.

**PADRI***:*

Uliye umefufuka katika wafu, (*paka siku ya Posho*) Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mama Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuishaji, kwa matunzo ya Majeshi maheshimiwa ya mbinguni juu yasiyo na mwili; kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume

Watakatifu, Watukufu, Wasifiwa kamili, ya Mashahidi Watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapateri Watawa na wabebaji-Mungu (*ya Mutakatifu musimamizi wa Kanisa*), ya Yoakim na Anna Mababu-Mungu, watakatifu na wenye haki, (*ya mutakatifu wa ile siku*) makumbusho yake ya leo, hata ya watakatifu wote, atuhurumie, akatuokoe, ya Mungu Mwema, Mrahimu na Mpenda-wanadamu, Kwa maombazi ya Wapateri wetu watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**Kisha ni desturi kusoma Saa ya Kwanza, ya Tatu na ya Sita. Saa ya Tisa tunaisoma mbele ya Ibada ya Mangaribi.**

*Mwisho ya desturi ya ibada ya asubui*

## DESTURI YA IBADA YA LITURGIA TAKATIFU

*Kama ni Askofu, kisha somo ya Ode wa sita, pamoja na ma padri na ma shemasi yake atasima ma mbele ya Ikonostasi kufanya Ibada ya Keros. (Maana ya Keros ni wakati; nikusema matayarish ya roho yetu mbele ya wakati ya mwanzo ya Liturgia Takatifu).*

### IBADA YA KEROS

**SHEMASI***:* Ee Rabi, himidi.

**ASKOFU AO PADRI***:* Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele. . .

**SHEMASI***:* Amina.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mfalme wa mbinguni, wewer Mfariji, Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema we.

Mungu Mutakatifu. . . (*mara tatu)* Utatu Mtakatifu kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, Mtakatifu utukaribie na utuponye magonjwa wetu. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**B**aba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje mapenzi yako ya- timizwe hapa duniani kama kule mbinguni. Utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu, kama

sisi vilevile tunavyosamehe wadeni wetu. Na usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

**PADRI**: **K**wa kuwa ufalme, uwezo na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**PADRI**: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwa kuwa sisi watu wenye zambi, hatuna teto yoyote kukuileta, ila ombi huu tunakutolea kwako, uliye Rabi, utuhurumie.

**SHEMASI**: Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Ee Bwana, utuhurumie, kwa kuwa tunategemea kwako. Usituazibu sana, wala kuzikumbuka zambi zetu. Lakini hata sasa utangalie, kama mwenye huruma, ukatuokoe na maadui wetu. Kwa kuwa wewe u Mungu wetu, tena sisi watu wako. Sisi zote viumbe vya mikono yako; jina lako tunaliita.

**PADRI**: Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utufungulie mulango wa huruma, ewe Muzazi-Mungu mubarikiwa. Tukikutumaini wewe, tutakuwa bila kuanguka. Kwako tutaziepuka taabu; Kwa kuwa wewe wokovu wa muzao wa wakristu.

*Kisha Askofu ku mbele ao Padri wanaanza kubusu ma Ikone ya Watakatifu pa Ikonostasi. Mbele ya Picha (Ikone) ya Bwana Yesu kristu wanasema hii Apolitikion yake:*

Tunaabudu Ikone wako safi kabisa, ee Mwema, na tunaomba rehema ya makosa yetu, ee Kristu Mungu. Ulipanda Msalabani kwa kutaka kwako mwilini mwako sababu ya kuokoa ku utumwa wa adui hawa ulioumba. Ndiyo maana tunakushukuru tukipaza sauti: Ulijaza vitu vyote na furaha, ee Mwokozi wetu, ulipokuja kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu.

*Mbele ya Picha ya Mzazi-Mungu wanasema hii wimbo:*

Chemchem ya mapendo, , utustahilishe ku huruma yako, ee Mzazi-Mungu; tazama taifa wawa waliotenda zambi, onyesha daima uwezo wako; maana tunajaa na matumaini yako, tunakupazia sauti: Salamu! Kama alivyofanya zamani Gabrieli, Jemadari wa majeshi ya Wabila mwili.

*Mbele ya Picha ya Mtakatifu Yoane Mbatizaji na Mutangulizi tunaimba Apolitikion yake hii:*

Makumbusho ya mwenye haki yanafanyiwa kwa masifa; lakinio kwako, ewe Mtangulizi, utatosha ushahidi wa Bwana. sababu umeonyeshwa kweli kati ya manabii muheshimiwa zaidi; kwani ulistahilishwa hata kumubatiza majini Yeye aliyehubiriwa. Uliposhindania ukweli, uliwahubiri na furaha evangelio wale walio kuzimuni, maana Mungu anafunuliwa mwilini, anachukua zambi ya dunia, akatupatia huruma kubwa.

*Kisha wataenda kubusu Picha ya Mtakaitifu ya kanisa na watasema Apolitikion yake.*
*Kwa mfano, Apolitikion ya Mtakatifu Mshahidi Georgie ni hii:*

## APOLITIKION YA MT. MSHAHIDI GEORGIE.

Ewe George shahidi mukubwa, muletaji ushindi. Kwa wewe ni uhuru wa wafunga na musaada wa masikini. Mungaga wa wagonjwa na mushindi wafalme. Umuombe Kristu Mungu wetu, aokoe nafsi yetu.

## APOLITIKION YA ASKOFU NEKTARIOS

Enyi Waaminifu tunamusifu Nektariow, kama Mutumishi Mungu wa Kristu, huyu alionekana katika miaka ya mwisho. Aliyezaliwa katika mji wa Silivria na aliyekuwa askofu wa Egina na akawa rafiki wa kweli wa fazila. Anatirikiza maponyesho yote kwa wale wenye kutukuza na heshima. Utukufu kwake huyu aliyemutukuza, utukufu kwake huyu aliyemuvika taji, utukufu kwake huyu anayetenda katika wewe, kwa kuponyesha wote.

## APOLITIKION YA ASKOFU

Haki ya matendo yako ilikufanya wewe kuwa kanuni ya imani ya kundi lako la kondoo, mfano wa upole, rabi wa kiasi; ndiyo maana katika unyenyekevu wako ulipata utukufu na katika umasikini wako ulipata utajiri. Baba Mtakatifu. . *(jina lake)*. . . umuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

## APOLITIKION YA SHAHIDI

Shahidi wako, . . . *(jina lake)*, ee Bwana, kwa mashindano aliyoshindana alipokea kwako. Mungu wetu, taji ya milele; aliposukumwa na nguvu yako, uliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yake okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

## APOLITIKION YA MASHAHIDI WENGI

Mashahidi wako, ee Bwana, kwa ajili ya mashindano walioshindana walipokea kwako. Mungu wetu, taji ya milele, waliposukumwa na nguvu yako waliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

## APOLITIKION YA PADRI NA SHAHIDI (Ieromartis)

Ulipokuwa na hali ya uzima wa Mitume na ulipokuwa halifa wa kiti yao, ulipata katika zoezi ya fazila njia yenye kwenda ku mawazo ya umungu; ndio maana, ulipoeneza na ibada neno la ukweli, ulishindana mpaka ku damu sababu ya ulinzi wa imani. . *(jina lake)*. . Shahidi Mutakatifu umwombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

## APOLITIKION YA MUTAKATIFU MUTAWA

Jangwa ilikuwa mji wako, katika mwili ulikuwa Malaika, miujiza yako yamekushuhudia. Baba yetu. . *(jina lake)*, Mubebaji-Mungu. Kwa kufunga, kukesha na sala ulipokea vipaji vya mbinguni sababu ya kuponya wagonjwa na roho za waaminifu wenye kukimbilia kwako. Utukufu kwa huyu aliyekupa hii uwezo, utukufu kwa huyu aliyekutukuza, utukufu kwa huyu anayetenda matunzo kwa wote katika maombezi yako.

**Ingine*:***

Kwa mawimbi ya machozi yako ulistawisha jangwa kavu, kwa maombolezo yako ya ndani ulitoa ku mateso yako matunda mara mia moja na kupita, kwa miujiza yako ya ajabu umekuwa taa yenye kuangaza ulimwengu wote*:* Mutawa Baba yetu. . *(jina lake)*, umuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

**Ingine*:***

Katika wewe. Baba, sura ya umungu ilionekana kabisa, kwa kufanana nayo ulichukuwa msalaba wako na ulimufwata Kristu; na kwa uzima wako ulifundisha kuzarau mwili kwa sababu ni ya kupotea, kwa kushurulika na roho isiyokufa hata milele. Ni hivi roho yako inafurahiwa, ewe Mtawa. . *(jina lake)*, pamoja na malaika.

## APOLITIKION YA MUTAKATIFU MWANAMUKE MUTAWA

Katika wewe Mama, sura ya umungu ilionekana kabisa, kwa kafanana nayo ulichukua msalaba wako na ulimufwata Kristu; na kwa uzima wako ulifundisha kuzarau mwili, kwa sababu ni ya kupotea, kwa kushurulika na roho isiyokufa hata milele; ni hivi roho yako inafurahiwa, ewe Mutawa. . *(jina lake)*, pamoja na Malaika.

## APOLITIKION YA MWANAMUKE SHAHIDI

Kondoo wako, ee Yesu analia nguvu na sauti yake; ni wewe napenda Bwana arusi wangu, ni wewe natafuta ninaposindana, nimesulubiwa na nimezikwa kwa ubatizo wako, na nateswa kwa ajili yako, ili niishi pia ndani yako; lakini pokea sawa sadaka yasipo kosa huyu mwenye kujitoa kwa kutaka kwake kwa ajili yako kwa maombezi yake, ee Mungu wa huruma okoa roho zetu.

### APOLITIKION YA MT. MTHEOLOGO.

Mwogozi wa Orthodoksi, mwalimu wa imani na mupole, taa ya Kanisa, pambo kimungu ya watawa, mwenye hekima. . *(jina lake),* uliangaza wote kwa mafundisho yako kwa sababu ulikuwa kiumbe cha Roho Mtakatifu. Umwombe Kristu Mungu wetu ili aokoe roho zetu.

### APOLITIKION YA MUTUME MOJA

Mutakatifu Mutume. . *(jina lake),* umuombe Mungu wa huruma, ili alete ku roho zetu maondoleo ya zambi zetu.

*Maelezo: Kama Mutume eko tena Mwevangelisti, tanaimba ivi:*

Ee Mutakatifu Mutume na Mwevangelizaji. . *(jina lake),* umuombe Mungu wa huruma. .

*Kama Mitume weko mengi tunaimba ivi:*

Enyi Watakatifu Mitume, mumwombee Mungu wa huruma. . .

### APOLITIKION YA NABII

Ee Bwana, tunashangilia leo makumbusho ya Nabii wako. . *(jina lake)* na tunakuomba katika huyu aokoe roho zetu.

*Kisha Askofu ao Padri pamoja na mapadri wengine na ma shemasi watasimama mbele ya Ikonostasi na Askofu ao padri mkubwa atasema hii sala:*

Ee Bwana, nyosha mkono wako toka juu ya makao yako, na unisabitishe kwa hii kazi ili nionekane mbele ya Meza yako ya ajabu bila kuhukumiwa, na kutimiza sadaka isiyochafuka. Kwa kuwa ufalme, uwezo na utukufu ni Wako, hata nmilele na milele.

Shmeasi*:* Amina.

**SHEMASI***:* Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Rabi Mtakartifu bariki*:*

*Askofu ao padri atafanya Kuaga kidogo:*

Kristu ukweli Mungu wetu, kwa maombi ya Mama wake asiye na doa wala sina lawama kamili; ya wa padri wetu Mtakatifu Yoane Krisostomo Mwarkiepiskopo wa Konstantinopoli, aliye miongoni mwa Watakatifu, ya. . . . *(anataja jina ya Mtakatifu ya hii siku),* hata wa Watakatifu wote, atuhurumie, na kutuokoe kama Mungu mwema na mupenda wanadamu.

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

*Kisha wote ma padri pamoja wanamisha ma kichwa yao kidogo ya kuomba hurumia ya waaminifu na wanaingia ndani ya Altari Takatifu. Kila padri ao shemasi hii wakati ya kuingia anasema ndani ya akili yake hivi:*

Nitaingia nyumbani mwako, nitasujudu mbele ya Hekalu yako Takatifu, mwenyi kujaa na woga.

*Wenye kuongoza Ibada watapiga magoti mara tatu mbele ya Meza takatifu na padri atabusu Evangelio na Meza, na shemasi atabusu paka Meza, kisha wataenda ku Rala (Diakonikon) ya Kanisa. Shemasi atamugongea Padri akikamata ku mukono wa kuume stikari (Kanzo) na Orario (Sitola) zenyi kukunjwa; atainamisha kichwa na atasema:*

**SHEMASI***:* Bariki, ee Rabi, Stikari na Orari.

*Padri, pa kubariki, atasema:*

Mhimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote. . .

**SHEMASI***:* Amina.

*Shemasi atavala Stikari yake akisema:*

Roho yangu itashangilia katika Bwana, kwani amenifuka nguo ya wokovu na amenivika kanzu ya furaha. Amenivika taji kama bwana-arusi, amenipamba kwa mapambo kama bibi-arusi. Sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Atabusu Orario na ataiweka pa bega ya kushoto. Vivyo hivyo ataweka epimaniko (Nguo ya ku Mukono) ku mukono wa kuume na atasema:*

Mukono wako wa kuume, ee Bwana, umetukuzwa katika uwezo; mukono wako wa kuume, ee Bwana, umewavunja maadui, na kwa sifa kuu ya utukufu wako, umewavunja washindani.

*Anapovala epimaniko ya mbili ku mukono wa kushoto atasema:*

Mikono yako imenifanya na kunitengeneza; unipe akili nitajifunza maagizo yako.

*Padri atabariki Stikari yake:* Mhimidiwa ni Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Pa kuvaa Stikari atasema:* Roho yangu itashangilia katika Bwana, kwani amenifunika nguo ya wokovu na amenivika kanzu ya furaha. Amenivika taji kama bwana-arusi, amenipamba kwa mapambo kama bibi-arusi. Sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Anapobariki Epitrakili ao Sitola yake padri, atasema:*

Mhimidiwe Mungu aliyemimina neema yake juu ya mapadri, kama mafuta kichwani, iteremukayo ndevuni, ndevu ya Aroni na ishukayo mpaka upindo wa mavazi yake.

*Akivaa mshipi, atasema:*

Mhimidiwa ni Mungu anayezizungusha na nguvu; amefanya njia yangu bila kosa. Amefanya miguu yangu sawasawa na ile ya jike la swala na ameniweka katika pahali pa juu, daima, sasa na siku zote, hata milele.

*Anapobariki maepimaniko atasema kama shemasi:*

Mukono wako wa kuume, ee Bwana, umetukuzwa katika uwezo; mukono wako wa kuume, ee Bwana, umewavunja maadui, na kwa sifa kuu ya utukufu wako, umewavunja washindani.

*Anapovala epimaniko ya mbili ku mukono wa kushoto atasema:*

Mikono yako imenifanya na kunitengeneza; unipe akili nitajifunza maagizo yako.

*Kisha kubariki na kubusu Epigonati (Juu-Goti), (kama eko nayo daraja), ataivaa akisema:*

Ewe shujaa, weka pajani upanga wako; ndio urembo wako na pambo lako. Nenda ukafanikiwe kuipigania uaminifu na haki, na mkono wako wa kuume utende mambo ya sifa, daima sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Padri atabariki Feloni (kazula), kisha kuibusu ataivaa akisema:*

Mapadri wako, ee Bwana, watavaa haki watakatifu wako watashangilia shangwe, daima sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Kisha, waongozi wa Ibada watanawa mikono wakiimba zaburi:*

Nitanawa mikono yangu katika mwenye-usafi na nitaizunguka Altare yako, ee Bwana, ili nitangaze waziwazi ya sifa yako, na kuyaeleza maajabu yako yote. Ee Bwana, napenda nzuri wa nyumba yako, na pahali unapokaa utukufu wako. Usiondoe roho yangu pamoja na wenye zambi, wala uzima wangu pamoja na watu wa damu. Walio na makosa mikononi mwao, mkono wao wa kuume umejaa rushwa mikononi za uovu. Lakini mimi nilikwenda safi; uniopoe, ee Bwana, na unihurumie. Mguu wangu umesimama katika njia sawa, katika Eklezia mikutano nitakutukuza Bwana.

# IBADA YA MATAYARISHO (PROSKOMIDI)

*Kisha waongozi wa Ibada wataenda ku Altare ya Matayarisho (Prothesis) na watasujudu mara tatu, wakisema:*

Ee Mungu, uniwe razi, na unihurumie mimi mwenye zambi *(mara tatu).*

*Watatayarisha vyombo vitakatifu vya Liturgia wakiweka Sahani kushoto na Kikombe kuume. Vivyo hivyo manguo (Kalimata), Nyota na Mukuki, Mikate divai na maji. Wakizipanga, watasema:*

Jitayarishe, Bethlehemu, Edeni ni wazi wote; jipambe Efratha, kwani mti wa uzima ilimaa katika pango kwa Bikira; tumbo lake limekuwa Paradizo ya kufikiri humo mumeshipuka mumea wa kimungu, huko tutakula na tutaishi wala hatutakufa kama Adamu; Kristu amezaliwa duniani kusudi ainushe Sura ilioanguka.

Umetukomboa ku laana ya Sheria kwa Damu yako ya heshimiwa. Ulisulubiwa msalabani na kuchomwa mkuki umejifanya kwa watu chemchem ya kutokufa, ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

*Shemasi atasema:* Ee Rabi, himidi.

*Padri atainua prosforo (mukate)na atasema:*

Mhimidiwe ni Mungu wetu daima, sasa na siku zote. . .

*Tena padri atakamata Mkuki Mtakatifu ku mkono wake wa kuume na prosforo ku mkono wa kushoto. Na mkuki atafanya mara tatu alama ya msalaba katikati ya Prosforo, akisema:*

Kwa ukumbusho wa Bwana, Mungu na Mwokozi wetu yesu Kristu *(mara tatu).*

*Atapasua Prosforo kandokando ya alama sababu ya kukata ile sehemu ya kati iitwayo «Mwana-Kondoo».*

*Shemasi atainua orario ku mkono wa kuume atasema kwa kila mkato:*

Tumwombe Bwana.

*Padri kisha ataweka mkuki upande wa kuume, atakata atasema:*

Kama Kondoo aliyepelekwa pahali pa machinjo.

*Kisha atakata upande wa kushoto atasema:*

na kama Mwana-Kondoo asiye na doa, anyamazaye mbele ya mwenye kumukata manyonya, hivi hafugue kinywa.

*Atakata upande wa juu, akisema:* Katika unyenyekevu wake hukumu yake iliondolewa.

*Mwisho atakata upanda wa chini, atasema:* Nani atausimlia uzazi wake?

**SHEMASI***:* ee rabi, inua.

*Padri, kwa mukuki, ataondoa lile sehemu la Mwana-Kondoo kisha kuindoa ku upande wa chini wa Prosforo atampanda Mkate Mtakatifu, atasema:*

Kwani uzima wake uliinuwa duniani.

**SHEMASI***:* Ee Rabi, sadaka.

*Padri ataweka Mwana-Kondoo Mtakatifu mwenyi kupindua pa Sahani takatifu alama chini. Atakata mwili mu alama ya Msalaba, akisema:*

Anatolewa sadaka, Mwana-Kondoo wa Mungu anayeondoa zambi ya dunia, kwa ajili ya uzima na wokovu wa dunia.

**SHEMASI***:* Ee Rabi, sulubisha.

*Padrti tena atapindua Mwana-Kondoo, alama juu, atamweka katikati ya sahani, na mkuki atapasua ku upande wa kuume wa Mwana-Kondoo (chini ya alama) IC, akisema:*

Mmoja wa askari aliuchoma ubavu wake kwa mkuki palepale ikatoka damu na maji. Naye aliyeona akashuhudia, ushuhuda wake ni wa kweli.

*Shemasi ataweka divai na maji katika kikombe kitakatifu kadiri inavyofaa, kisha atasema:*
ee Rabi, uubarikie, mchanganyo mtakatifu.

*Padri atabariki na akisema:*
Ubarikiwe Mchanganyo wa vitu Vitakatifu, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Padri atakamata tena Prosforo ya mbili, kama iko, na atasema:*
Kwa heshima na makumbusho ya Bibi wetu Mutakatifu, Mubarikiwa, zaidi Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima Maria. Kwa maombezi yake, ee Bwana, pokea sadaka hii katika altare yako ya juu mbinguni.

*Atachukua sehemu ya Mzazi-Mungu atiweka kuume kwa Mwana-Kondoo, akisema:*
Malkia amesimama mkono wako wa kuume, amevaa mapambo ya zahabu ya ofiri.

*Padri atakamata Prosforo ya tatu ambako atatoa sehemu za majeshi 9 Watakatifu, mfano hivi katika mistari tatu (lakini ndogo sana) ataziweka kushoto kwa mwana-Kondoo mbele (makabala) ya Mzazi-Mugu. Ataanza ku mstari wa kwanza, akisema:*

Kwa heshima na makumbusho ya Mikaeli na Gabrieli, majemadari wakubwa kamili, na ya Majeshi yote ya mbinguni ya Wabila-mwili.

*Kisha atachukua sehemu ya mbili na ataiweka chini ya ile ya kwanza, akisema:*
Kwa heshima na makumbusho ya Muhehsimiwa na Mtukufu Nabii na Mtangulizi na Mbatizaji Yoane. Ya Manabii Watakatifu na watukufu Musa na Aaroni, Elia na Elizeo, Isaya, Daudi na Yesse, ya Vijana wa tatu na Nabio Danieli na ya Manabii Watakatifu wote.

*Kisha atachukua sehemu ya tatu na ataiweka chini ya ile ya mbili, akisema:*
Ya Mitume Watakatifu, watukufu na Wasifiwa Petro na Paulo, ya kumi na wa wili na makumi saba, hata ya Mitume Watakatifu wote.

*Hıvi atahukua sehemu ya inne ataiweka upande wa ile ya kwanza hivi unaanza kiwima wa mbili, na atasema:*
Ya Wapadri wetu kati ya watakatifu, Waaskofu Wakubwa tena Walimu wa ulimwengu Bazili Mkuu, Grigorio Mtheologo na Yoane Krisostomo, Atnanasio na Kirilo, Nikola wa Mira, Spiridon wa mji Trimithunta na ya Waaskofu Watakatifu wote.

*Atachukua sehemu ya tano ataiweka chini ya ile ya inne, akisema:*
Ya Stefano Shemasi Mkuu, Mtume Mtakatifu na Shahidi wa kwanza, ya watakatifu na Mashahidi wakuu Dimitri, Georges, Theodoro na ya mashahidi wote wanaume na wanawake.

*Atachukua sehemu ya sita ataiweka ku mwisho ya mstari kilima wa mbili, akisema:*
Ya Watawa watakatifu wabebaji-Mungu Antonio, Eftimio, Pakomio, Sava, Onufrio, Musa wa Ethiopia, Petro na Athanasio wa Mulima Takatifu Athos ya Grekia na ya Watawa Watakatifu wote wanaume na wanawake.

*Atachukua sehemu ya saba na ataanza mstari wa tatu kiwima, akisema:*
Ya watakatifu, watukufu na wafanyaji alamu na wabila feza Kosmas na damianos, Kiro na Yoane, Panteleimoni na Ermolao, Sapsoni na Dimidi, Thaleleo na Trifoni na ya wabila-feza Watakatifu wote.
*Atachukua sehemu ya nane ataiweka chini ya ile ya saba, akisema:*

Ya Yoakimu na Anna Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki, (*Ya mtakatifu wa siku),* na ya watakatifu wote; kwa maombezi yao ututazame, ee Mungu.

*Atachukua sehemu ya mwisho ataiweka pa fasi tisa, akisema:*

Ya Mpateri wetu Yoane Krisostomo, Mwarkiaskofu wa Konstantinopoli, aliye miongoni mwa Watakatifu *(wala Bazili Mkuu kama liturgia yake yanafanyika).*

*Atachukua Prosforo hii atakatako sehemu moja ataiweka chini ya mwana-Kondoo ku upande wa kushoto wa Sahani, akisema:*

Kumbuka, ewe Rabi Mpenda-wanadamu, Waaskofu wote wa Orthodoksi, askofu Mkubwa wetu *(jina lake),* Upadri uheshimiwa, ushemasi katika Kristu, na kila jeshi ia wateule, ndugu na wenzetu katika fumbo takatifu, hata wote hawa umewaita kuwa kwako, kwa huruma yako, ewe Rabi Mwema-kamili.

*Kisha ataweka sehemu zingine kwa ajili ya hule askofu aliyemupa upandirisho kama yupo mzima na kwa ajili ya wote waorthodoksi apendao walio hai kadiri ya daftari ya parokia na zile zimeletwa na waaminifu.*

*Kishaatakamata Prosforo hii atakatako sehemu kidogo-kidogo ataiweka chini ya kuume wa Sahani ya ile udyako wa Eklezia, akisema:*

Kwa makumbusho na maondoleo ya zambi za marehemu wajengazi wa hekalu takatifu hii (ao monasteri).

*Anaendelea kuweka sehemu na kusema. Kisha anakumbuka majina wale wa ndugu waorthodoksi walilala katika Kristu na jina ya askofu aliyemupatia upandirisho kwake, kama asipokuwa miongoni mwa wenye uzima.*

*Ku mwisho anasema:* Na kwa ajili ya Wapateri na ndugu zetu waorthodoksi waliolala kwa matumaini ya ufufuo na ya uzima wa milele kwa maungano wako, ewe Bwana mpenda-wanadamu.

*Vivyo hivyo shemasi atataja majina ya walio hai na ya wafu anataka, na padri ataondoa sehemu kwa ajili yao. Kisha, padri, atachukua sehemu ya mwisho kwa ajili yake mwenyewe akisema:*

Kumbuka pia, ee Bwana, kutosyahili kwangu na unisamehe uhalifu wote niliyofanya wa kutaka na wasiokutaka.

*Hivi yamepatikana katika Sahani Eklezia yote yenye kukusanyika karibu ya mwana-Kondoo.*

*Halafu Shemasi atakamata chetezo, atawekamo ubani, akasema:*

Ee Rabi, bariki ubani. Tumwombe Bwana.

*Padri anapobariki atasema hii sala ya ubani:*

Tunakutolea ubani, ee Kristu Mungu wetu, kama manukato ya harafu ya kiroho; ukiopokea ku Altare yako ya juu mbinguni, ututumie kisha neema ya Roho yako Mtakatifu kamili.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana. Ee Rabi, imarisha.

*Padri atafukiza nyota na ataiweka pa Sahani, juu ya Mwana-Kondoo na sehemu zingine, akisema:*

Nayo Nyota ikafika na ikasimama juu pahali alipokuwa Mtoto.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

*Pasri atafukiza cha kwanza kitambaa-Funiko (kalimata) ambayo atafunika Sahani.*

Bwana ni mufalme, amevaa utukufu; Bwana amevaa uwexo, amejifunga kiunoni, aliuimarisha ulimwengu nao hautatikisika.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana. Ee Rabi funika.

*Padri atafunika ku kitambaa-ufuniko cha pili ambayo atafunika Kikombe, akisema:*

Mbingu zimefunikwa na fazila yako, ee Kristu, na dunia imejaa na sita yako.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana. Ee Rabi funika.

*Padri atafunika Kitambaa-funiko Kikumbwa (Aera), tena atafunika Sahani na Kikombe, akisema:*

Utulinde sisi kwa kivuli cha mabawa yako; tenga mbali nasi kila adui na mshindani; amarisha maisha yetu, ee Bwana, utuhurumie sisi na dunia yako, na okoa roho zetu, kwa kuwa wewe ni Mwema na Mpenda-wanadamu.

*Padri atafukiza mara tatu Altare ya Matayarisho akisema kwa kila mara:*

Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, aliyependezwa hivi; utukufu kwako.

*Shemasi kisha kila mara akisema:* Daima, sasas na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Shemasi atakamata chetezo na atasema:* Kwa ajili ya vipaji viheshimiwa, tumwombe Bwana.

*Padri atasema sala ya matayarisho:*

Ee Mungu, Mungu wetu, wewe uliyetutumia, chakula cha dunia yote, Bwana Mungu wetu Yesu Kristu, ili awe, Mwokozi, Mkombozi na Mfazili akitubariki na kututakasa; wewe mwenyewe, bariki hii sadaka na uipokee ku altare yako ya mbinguni. Kumbuka wewe Mwema na Mpenda-wanadamu, hawa ambao walioileta na hawa waliiletea, tena utulinde sisi bila kuhukumiwa katika ibada ya mafumbo yako ya kimungu. Kwa kuwa jina lako liheshimiwa na tukufu kamili limetakaswa na kutukuzwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina

*Padri atamaliza Ibada ya matayarisho, kusema hivi:*

Utukufu kwako, ee Kristu Mungu, kitumaini wetu, utukufu kwako.

**SHEMASI***:* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Rabi mtakatifu, bariki.

*Padri anafanya Kuaga (Apolisis)*

Huyu aliyezaliwa kwa ajili ya wokovu wetu ndani ya pango na kulalishwa katika sanduku ya kulishia wa nyama *(siku ya Mungu ataongeza: na aliyefufuka katika wafu),* Kristu Mungu wetu wakweli, kwa maombezi ya Mama wake asiye na doa, kwa maombezi ya Mpadri wetu Yoane Krisostomo Mwarkiaskofu wa Konstantinopoli, aliye katika watakatifu *(Kama Liturgia ni ya bazili Mkuu, tunasema hivi: Kwa maombezi ya Mpadri wetu Bazili Mkuu, Mwarkiaskofu wa Kesaria ya Kapadokia, aliye katika Watakatifu)* na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani Yeye ni mwema na Mpenda-wanadamu.

**SHEMASI***:* Amina.

*Watainama mara tatu na watabusu vipaji, hapo padri atasema:*

Mugu Mtakatifu, Baba wa milele; mweza Mtakatifu, mwana aliye wa milele, Msiyekufa Mtakatifu, Roho Mtakatifu kamili, Utatu Mtakatifu, utukufu kwako.

*Tena Shemasi atafukiza altare yq Matayarisho na pande zote akisema kwa siri:*

Ulikuwa kaburini na Mwili wako, kuzimuni na roho kama Mungu, Paradizoni pamoja na Mnyanganyi, Ulikaapa kiti cha pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, ee Kristu, Wewe unayevijaza vitu vyote.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Iliyo kweli ya samani kuipita Paradizo, ya kuangaa zaidi kuliko makao yote ya mfalme, ee Kristu, ni hivi ilionekana kwetu kaburi yako yenye kuleta uzima; ni chemchemi ya ufufuo wetu.

Sasa na siku zote. . .

Salamu, makao yenye kutakaswa, Hekalu kimungu ya aliyejuu, ee Mzazi-Mungu, ni katika wewe furaha imepewa kwa sisi na tunapaza sauti*:* Mbarikiwa qwewe katika wanawake, malkia bila doa kamili.

# LITURGIA KIMUNGU YA PADRI WETU YOANE KRISOSTOMO ASKOFU MKUBWA YA KONSTANTINOPOLI

## LITURGIA YA WAKATIKUMENO

*Elezo: Mbele ya Meza takatifu, wenye kuongoza Ibada watapiga magoti mara tatu wakisema:*

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

Utukufu kwa Mungu juu pia, amani katika inchi mapendo kwa wanadamu. *(mara tatu. )*
Bwana, utafungua midomo yangu na kinywa changu kitatangaza sifa yako. *(mara mbili).*
Ee Bwana, utufungulie mulango wa huruma yako.

*Kisha padri atabusu Evangelion na shemasi atabusu paka Meza takatifu. Shemasi atainamisha kichwa mbele ya Padri na akiinua orarion na mkono wa kuume. Kisha kupokea baraka ya mwongozi wa Ibada, Shemasi atatoka ku Altare Takatifu kwa mlango wa kaskazini, atasimama mbele ya mlango Bora na atainamisha kichwa atapaza sauti kusema:*

**SHEMASI:** Ee Rabi, himidi.
*Padri atasimama mbele ya Meza, atakamata pa mikono yake Evangelio Takatifu, atafanya alama ya msalaba juu ya Antiminsio(nguo takatifu nyekundu) na atapaza sauti kusema:*

**PADRI**: Mhimidiwe ufalme wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
**WAIMBAJI***:* Amina.
*Shemasi atapaza sauti atasema Irinika (maombi ya amani), hivi:*
*Waimbaji watajibu kwa kila ombi:* Bwana hurumia.
**SHEMASI***:*
Kwa amani tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya amani kutoka juu na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya amani ya dunia yote, na kusimama imara kwa maeklezia Matakatifu ya Mungu, na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya nyumba hii takatifu na ya wanaoingiamo imani na ibada na kumwogopa Mungu, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya wakristu waabudu na waorthodoksi, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya Mwarkiaskofu wetu (jina lake), ya ukasisi uheshimiwa, ya ushemasi katika Kristu, ya wateule wote na ya watu wote, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya taifa letu, ya wale wanaoitawala, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya muji huu *(ao Monasteri, inchi ao Kisanga)* kila muji na kila inchi na ya wanaoishimo kwa imani, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya majira mema ya mwaka, ya wingi wa matunda duniani na ya wakati za amani, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya walio baharini, ya wasafiri, ya wagonjwa, ya wafungwa, ya wale wote wanaoteseka, na kwa ajili ya wokovu wa wote, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya kuokolewa ku kila sikitiko, kila uadui, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.
Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.
Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na Watakatifu wote, sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu, Mungu wetu.

**WAIMBAJI***:* kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Antifonon ya kwanza (Kiitikio).*

Ee Bwana, Mungu wetu, mwenye enzi yote na utukufu kupita kila ufahamu, uliye na huruma sana, tena na mapendo kwa wanadamu yasiyoelezeka, wewe mwenyewe, ee Rabi, katika huruma yako, utuangalie sisi na hekalu hii takatifu na utupe sisi pamoja na hawa wanaosali pamoja nasi, huruma yako ya utajiri na rehema yako.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa utukufu wote, na heshima na usujudu ni haki yako ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Halafu Waimbaji wanaimba Antifonon ya kwanza:*

**ANTIFONON WA KWANZA**

Shairi*:* Umsifu Bwana, ee roho yangu, na yote yaliyo ndani yangu yasifu Jina lako takatifu.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Umsifu Bwana, ee roho yangu, wala usisahau mema yake yote.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Bwana amesimika kiti chake mbinguni, na ufalme wake unatawala vitu vyote.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

*Kama Liturgia inafanyika katikati ya Juma tunaimba hii Antifonon wa kwanza:*

Shairi*:* Ni vema kumwungama Bwana, na kuliimbia jina lako, ewe uliye-juu

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Ni vema kutangaza huruma wako asubui, na uaminifu wako nyakati za usiku.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Maana Bwana ni mwenye Haki na hakuna uzulumu ndani yake.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

*Shemasi atasema Ektenia Kidogo:*

Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na Watakatifu wote, sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu, Mungu wetu.

**WAIMBAJI***:* kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Antifonon wa mbili.*

Ee Bwana, Mungu wetu, okoa taifa wako na bariki uriti wako; ulinde jamii ya Eklezia yako, na takasa hawa wanaopenda uzuri wa nyumba yako; uwape utukufu kwa uwezo wako wa umungu, na usituache sisi tunaotumaini wewe.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa utawala ni kwako, na ufalme, na uwezi na utukufu ni wako wa Baba, na wa Mwana, na

wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

***WAIMBAJI****:* Amina.

*Halafu Waimbaji wanaimba Antifonon wa mbili:*

**ANTIFONON WA MBILI**

*Shairi:* Umsifu Bwana, ee roho yangu, nitamsifu Bwana maisha yangu yote, nitamwimbia Mungu wangu zaburi mimi ningali mzima.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Shairi*:* Heri mtu anayesaidiwa na Mungu wa yakobo, anayemtumainia Bwana, Mungu wake.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Shairi*:* Bwana anatawala milele. Mungu wako, ee Sayuni, kizazi hata kizazi.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Uliye Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, ukiwa msiyekufa ukakubali kwa ajili ya wokovu wetu kupata mwili kwa Maria Mzazi-Mungu, tena Bikira daima, ukawa mtu bila kujigeuza; hata kusulubiwa, ewe Kristu Mungu, na kukikanyanga kifo kwa kifo; ukiwa mumoja na Utatu Mtakatifu, na kutukuzwa pamoja na Baba, na Roho Mtakatifu, utuokoe.

*Kama Liturgia inafanyika katikati ya Juma tunaimba hii Antifonon wa mbili:*

*Shairi:* Bwana ni Mfalme, amevaa utukufu, Bwana amevaa uwezo, amejifunga ezi kiunoni.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye Watakatifu ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Shairi:* Amekaza ulimwengu usitikisike.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye Watakatifu ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Shairi:* Nyumba yako imajaa utakatifu, ee Bwana, muda wa siku nyingi sana.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye Watakatifu ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Uliye Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, . . . . . . . . . . .

*Shemasi atasema Ektenia Kidogo:*

Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu, Mungu wetu.

**WAIMBAJI***:* kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Antifonon wa tatu:*

Wewe uliyetupatia neema ya kuunganisha masauti yetu kwa kukutolea sala hizi za pamoja na uliyeahidi kusikiliza maombi ya watu wawili hata watu watatu wanaokusanyika katika jina lako, wewe mwenyewe, sasa utimize maombi ya watumishi wako, kwa faida yetu, ukitupatia katika wakati huu kamili ukweli wako, tena uzima wa milele katika ulimwengu utakaokuja.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu, na kwako tunakutolea utukudu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**ANTIFONON YA TATU**

*Waimbaji wanaimba Apolitikion ya Ufufuo, kama ni mu Juma ao ya Mtakatifu fulani kama ni siku ingine shangilio yake.*

Shairi*:* Hii ndiyo siku aliyofanya Bwana tunashangilia na tunafurahiwa nayo.

*Apolitikion ya Ufufuo. Kama ni Liturgia katikati ya Juma tunaimba Apolitikion ya hule Mtakatifu, bila shairi.*

*Wakati wa hii wimbo padri atakamata Evangelio Takatifu atamupa Shemasi. Kisha, watatoka ku Altare Takatifu kwa mlnago wa kaskazini na watatanguliwa kwa watoto wenye kubeba taa. Watasimama mbele ya mlango Bora, pahali pa kuwaida. Watainamisha vichwa vyao. Shemasi kwa sauti ya chini:* Tumwombe Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya kuingia ndogo (Mikra Isodos).*

Ee Rabi na Bwana Mungu wetu, uliyeweka mbinguni makundi na majeshi ya malaika, na malaika majemadari kwa kazi ya utukufu wako; ufanye kuingia kwetu kuwe pamoja na malaika watakatifu, wanaotumika na kuutukuza pamoja nasi wema wako.

Kwa kuwa utukufu wote, heshima na usujudu ni haki yako kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Shemasi kwa sauti ya chini atamwambia padri:*

Ee Rabi, bariki Kuingia Kitakatifu.

*Kwa sauti chini padri ataibariki hivi:*

Kubarikiwa kuingia kwa Patakatifu pako, daima sasa na siku zote hata milele nma milele.

*Shemasi atapeleka Evangelio Takatifu kwa padri ataibusu, kisha kama wimbo itaisha Shemasi atapaza sauti:*

Hekima. Simameni.

*Padri na Shemasi wataingia ndani ya Altare takatifu katika Mlango Bora na Shemasi ataweka Evangelio Takatifu juu ya Antiminsion.*

*Waimbaji wataimba wimbo wa Kuingia:*

Njooni, tumwabudu na kumwangukia Kristu. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Siku ya katikati ya Juma tunaimba*:*

Njooni tumwabudu na kumwangukia Kristu. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye katika watakatifu wa ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Kisha Waimbaji wataimba Apolitikion ya sauti ni siku ya Mungu. Kisha Apolitikion ya Mtakatifu wa siku, ya Mtakatifu ya Kanisa na Kontakion.*

*Kama wanafanya Liturgia wa padri wawili na juu, hawa wataimba Kontakion. Lakini kama anafanya Liturgia mpaka padri moja, Kontakio wataiimba Waimbaji.*

*Kama hakuna Siku Kuu kubwa, mapadri wanaimba:*

**KONTAKION YA MZAZI-MUNGU***:*

Ee Mulinzi usiyepatisha wakristu haya, na mupatanishi wa Muumba usiyeweza kubadilika, usizarau sauti ya kusihi ya wenye-zambi. Lakini fika kama mwema, kwa kutusaidia sisi, tunaokuita

na imani*:* Ujiharikishe kwa upatanisho, na ukimbie kwa kutuomba, ewe Muzazi-Mungu unayelinda, wanaokuheshimu daima.

*Kila padri, kama ni Siku Kuu mkubwa, ataweza kutafuta Kontakio ya hii Siku Kuu ku mwisho ya hii Kitabu. Ukurasa:*

*Shemasi atapaza sauti anasema inje ya Mlango Bora:*

Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI**: Bwana hurumia.

*Padri atasema kwa siri sala ya Trisayo:*

Ee Mungu Mtakatifu, unayekaa katika watakatifu, unayeimbwa kwa sauti Takatifu tatu na Wa Serafi, na kutukuzwa na Wakeruvi, na kusijudiwa na nguvu zote za mbinguni! Uliyefanya vitu vyote kwa bure, vikawa, uliyemwaumba mwanadamu kwa sura na mfano wako, tena kumpamba kwa vipaji vyako vyote; wewe unayempa yoyote anayekuomba hekima na busara na usiyemzarau mwenye zambi kumwacha apotee, lakini umeweka kutubu kama njia ya wokovu; Wewe uliyetustahilisha, sisi watumishi wako wanyenyekevu na wasiostahili, kusimama hata wakati huu mbele ya utukufu wa Altare yako takatifu na kukuletea usujudu na sita iliyo haki yako; wewe mwenyewe, ee Rabi, pokea pia ku midomo yetu zambi Wimbo wa takatifu tatu na utufikie kwa wema wako; utusamehe kila kosa tumefanya wala ya kutaka, wala yasiokutaka, utakasa roho zetu na miili yetu tena utupe kukuabudu katika utakatifu siku zote za maisha yetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu mtakatifu na ya watakatifu wote waliokupendeza tangu milele.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa Wewe ni Mtakatifu, ee Mungu wetu na kwako tunautoa, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote,

**SHEMASI***:* Hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Waimbaji wanaimba Trisayo:*

Mungu Mtakatifu, Mweza Mutakatifu, Msiyekufa Mutakatifu, utuhurumie *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Msiyekufa Mutakatifu, utuhurumie.

**SHEMASI***:* Nguvu (Dinamis).

**WAIMBAJI***:* Nguvu (Dinamis). Mungu Mtakatifu, Mweza Mutakatifu, Msiyekufa Mutakatifu, utuhurumie.

*Wakati wa wimbo wa Trisayo Padri na Shemasi watasali kwa siri* «Mungu Mtakatifu. . . . » *Kisha wataenda ku Altare ya Matayarisho (Prothesis) na Shemasi atamwambia Padri na sauti ya chini:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, amuru.

*Padri atasema na sauti ya chini:* Mhimidiwe Yeye anayekuja kwa jina la Bwana.

*Tena, Padri na Shemasi wataenda «pahali pa juu», pahali pa kiti cha askofu wala kwa msulubiwa, iliyo nyuma ya Altare na Shemasi atamwambia Padri na sauti ya chini.*

**SHEMASI***:* Ee Rabi himidi kiti cha enzi kilicho juu.

**PADRI***:* Uhimidiwe, wewe katika kiti cha enzi cha Ufalme wako, unayekaa juu ya Wakeruvi, daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha wimbo wa Trisayo, msomaji atasoma Shairi ya kwanza ya Prokimenon yenye kutangulia somo la Barua ya Matendo ya Mitume (Apostolos).*

**SHEMASI***:* Tusikilize.

*Msomaji atasoma shairi ya mbili ya prokimenon.*

**SHEMASI***:* Hekima.

*Msomaji atasoma kipindi cha somo la barua ya matendo (Apostolos).*

**SHEMASI***:* Tusikilize.

*Wakati wa somo ya Apostolos, Shemasi atafukiza Altare, Meza ya Matayarisho (Prothesis). Kingio kubwa, na tangu milango bora, ikone na watu wote. Akiisha, Shemasi atainamisha kichwa mbeletya Padri na atamwambia na saudi chini:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, bariki msomaji wa Evangelio Takatifu, kama ilivyoandikwa na Mtuma Mtakatifu tena Mwevangelizaji *(jina lake).*

*Padri atasema kwa siri:*

Kwa maombi ya Mtume Mtakatifu, Mtukufu na Mwevangelizaji *(jina lake*), Mungu akupe neno ya kutangaza Habari Njema na nguvu nyingi, kwa kutimiza Evangelio ya mwana wake Mpendwa, Bwana wetu Yesu Kristu.

*Shemasi kwa sauti chini atasema:*

Amina. Amina. Amina. Iwe kwangu sawasawa na neno lako.

*Padri atamupa Shemasi Evangelio. Huyu atapanda pa Ambon (Kiti ya Muhubiri) akitanguliwa kwa taa.*

*Padri kwa siri atasoma, mbele ya Altare, hii sala:*

Ee Rabi, Mpenda-wanadamu, wangaze mioyoni mwetu na nuru isiyokufa ya kujua umungu wako, tena fungua macho ya akili yetu ili tusikie mahubiri ya Evangelio yako. Weka ndani yetu woga wa amri zako, ili tuishi uzima wa kiroho tukikanyanga tamaa yote mbaya ya kimwili, tukiwaza na kutenda vitu vyote vinavyokupendeza.

Kwa kuwa Wewe ni mwangaza wa roho zetu na miili yetu, ee Kristu Mungu, na kwako tunautoa utukufu, pamoja na Baba yako wa milele, na Roho wako Mtakatifu kamili, Mwema na Mpaji wa uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Ku mwisho ya somo la Apostolos Padri atasimama ku mlango bora atambariki msomaji akipaza sauti:*

**PADRI**: Amani kwako, ee Msomaji.

**WAIMBAJI***:* Aliluia, Aliluia, Aliluia.

**PADRI***:* Hekima. Simameni. Tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Somo katika Evangelio takatifu iliyoandikwa na *(jina ya: Matayo, Marko, Luka, Yoane).*

**PADRI***:* Tusikilize.

**WAIMBAJI***:* Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Shemasi atasoma Evangelio. Ku mwisho ya somo padri atasema kwake:*

**PADRI***:* Amani kwako, ee Mwevangelizaji.

**WAIMBAJI***:* Utukufu Kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Shemasi atarudi ku mlango bora na atamupa Padri Evangelio. Padri atarudi mu Altare Takatifu na ataweka Evangelio pa Meza. Kwa hii wakati askofu wala padri atafasiria maandiko ya somo ya Evangelio wala ya barua (APOSTOLOS), tena atawafundisha watu wa Mungu.*

*Shemasi atasimama pahali paka pa desturi mbele ya Mlango Bora, atapaza sauti atasema Ektenia Kubwa.*

Tuseme sisi wote kwa roho yetu na kwa akili yetu, tuseme.

*Waimbaji watasema kisha kila maombi:* Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Ee Bwana mwenyezi, Mungu wa Baba zetu, tunakuomba utusikilize na kutuhurumia.

Utuhurumia, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na kutuhurumia.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Wakristu, wenyi ibada na Waorthodoksi wote.

tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiaskofu wetu *(jina lake). . .*

Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, Watawa, mashemasi, hata ya ndugu wetu wote katika Kristu.

Tena tunakuomba kwa ajili ya watumishi wa Mungu, wakristu wote, wenyi ibada na waorthodoksi, wanaokaa katika mji huu na ya jamii ya parokia hii, ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, msaada, usamehe na maondoleo ya zambi.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wenye heri wajengaji wa hekalu hii takatifu, ya Baba na ndugu zetu waorthodoksi ambao wamelela hapa na ibada na pahali popote.

Tena tunakuomba kwa ajili yao wanaotenda matendo mema katika hekalu hii takatifu na heshimiwa, kwa ajili yao wanaoleta zawadi, wanaotumikiamo, wanaoimbiamo hata ya watu wote wanaosimama hapa, wakingoja huruma yako kubwa na ya utajiri.

*Padri kwa siri atasoma hii sala.*

Ee Bwana, Mungu wetu, pokea maombi marefu haya ya watumishi wako na utuhurumie kadiri ya wingi wa huruma yako; tena utupatie rehema zako, sisi na watu wako hawa wanaongoja huruma yako kubwa na ya utajiri.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa Wewe ni Mungu wa huruma na Mpenda-wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Shemasi atapaza sauti ataanza maombi kwa ajili ya Wakatikumeno. Waimbaji watajibu kwa kila maombi:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Enyi Wakatikumeno, ombeni kwa Bwana.

Hata sisi tulioamini, kwa ajili ya wakatikumeno, tumwombe Bwana.

Ili Bwana awahurumie.

Awafundishe neno la ukweli.

Awafundishe Evangelio ya haki.

Awafundishe ku Eklezia yake takatifu, Katholiki *(wa dunia mzima*) na Apostoliki (*wa Mitume*).

Uwaokoe, uwahurumie, uwasaidie, uwalinde, ee Mungu, kwa neema yako.

Enyi wakatikumeno, inamisheni vichwa vyenu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya wakatikumeno:*

**PADRI***:* Ee Bwana, Mungu wetu, unayekaa juu mbinguni na kuona viymbe vinyenyekevu, uliyetuma Mwana wako wa pekee, Mungu na Bwana wetu Yesu Kristu, aliye wokovu wa wanadamu, uwaangalie watumishi wako, wakatikumeno, wanaoinamisha vichwa vyao mbele yako. Uwastahilishe kuzaliwa mara ya mbili, na kupewa maondoleo ya zambi na vazi lisioharikia, uwaunganishe ku Eklezia yako Takatifu, Katholiki *(wa dunia mzima)* na Apostoliki *(wa Mitume)*, na uwahesabie katika kundi la wateule wako.

*Padri atapaza sauti:*

Ili hata hawa pamoja nasi walitukuze jina lako lenye kustahili heshima yote na utukufu wote, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri atakunjua Antiminsio pa Altare, wakatipo Shemasi atapaza sauti akisema:*

**SHEMASI***:* Walio Wakatikumeno tokeni. Enyi Wakatikumeno, tokeni. Walio wakatikumeno, tokeni. Mtu mkatikumeno asikae ndani.

## LITURGIA YA WAAMINIFU

**SHEMASI***:* Sisi tulio waaminifu, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Hekima.

*Padri atasoma sala ya kwanza ya Waaminifu*

**PADRI***:* Tunakushukuru, ee Bwana Mungu wa majeshi, uliyetustahilisha hata sasa kusimama mbele ya Altare yako Takatifu na kusujudu mbele yako tukiomba huruma yako kwa ajili ya zambi zetu na ya makosa yakutojua watu. Upokee, ee Mungu, ombi letu. Utustahilishe kukuletea sala zetu, maombi na sadaka bila damu kwa ajili ya watu wako wote. Utupe nguvu, sisi uliotuweka katika utumishi huu, ya kukuomba wakati wote na pahali pote, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, bila hukumu wala laumu na zamiri safi, ili ukisikiliza sala zetu, utuhurumie kadiri ya wingi wa wema wako.

*Padri atapaza sauti kusema:*

Kwa kuwa Utukufu wote, na heshima, na usujudu ni haki yako ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**SHEMASI***:* Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Hekima.

*Padri kwa siri atasema sala ya mbili ya Waaminifu:*

Tena na tena tunasujudu mbele yako na tunakuomba Wewe Uliye Mwema na mpenda-wanadamu, wangalie ombi letu, usafishe roho zetu na miili yetu kwa kila aibu ya mwili na ya roho. Tena utupe tusimame mbele ya Altare yako Takatifu, bila laumu, wala hukumu. Uwape, ee Mungu, hawa wanaosali pamoja nasi maendeleo ya maisha, imani na hekima ya kiroho; uwajalie kukutumikia daima safi na woga na mapendo bila hukumu ku Mafumbo yako Matakatifu na wastahilishwe kuingia katika Ufalme wako wa juu mbinguni.

*Padri atapaza sauti:*

Ili sisi tukilindwa daima kwa uwezo wako, tukutolee utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Wainmbaji wataimba wimbo ya **KHERUVIKON** pole-pole na vizuri.*

Sisi tunaofanana kwa siri na wakeruvi na tunaoimbia Utatu Mpaji-uzima wimbo wa takatifu Tatu, tuache sasa shuruli zote za dunia hii. Kwa kupokea Mfalme wa vitu vyote.

*Hii wakati ya wimbo ya Keruvikon Padri atasoma kwa siri sala mbele ya Meza, hivi:*

Mtu hata mmoja wa wale wenye kufungwa kwa tamaa na furaha za mwili anayestahili kuja Kwako, kukujongea na kukuabudu ee Mfalme wa utukufu. Kwani kukutumikia ni kituki kubwa na cha kuogopa sana hata kwa majeshi ya mbinguni. Lakini katika mapendo Yako isiyokaairika ya isiyohesabika kwa ajili ya mwanadamu, umejifanya mtu bila kujigeuza wa ukawa Kuhani wetu mkuu; tena, ee Rabi wa vitu vyote, umetupatia utimizo wa sadaka hii isiyo na damu. Peke Yako, ee Bwana Mungu wetu, unatawala mbinguni na duniani, umekaa katika kiti cha enzi cha wakheruvi, ee Bwana wa Maserafi, Mfalme wa Israeli, uliye peke yako Mtakatifu na kupumzika katika Watakatifu. Basi, nakusihi, Wewe peke Mwema na mfazili, uniangalie mimi mutumishi, mwenyi zambi na msiyestahili, u takase roho na moyo wangu kwa kila wazo baya tena unipe nguvu, kwa uwezo wa Roho yako Mtakatifu, ili nikivaa neema ya upadri nisimame mbele ya Meza yako hii takatifu, kutolea Mwili Wako Takatifu safi na damu yako ya samani. Nakuja Kwako nikiinamisha kichwa tena nakusihi*:* Usinifiche Uso wako na usinikatae kuwa katikati ya watumishi wako, unistahilishe, mimi mwenye zambi na mtumishi nisiyestahili kukutolea zawadi hizi. Kwani ndiwe unayetoa na kutolewa unapokea na kugawanya, ee Kristu Mungu wetu; na kwako tunautoa utukufu, pamoja na Baba yako asiye na mwanzo na Roho yako Mtakatifu kamiliMwema na Mpaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha padri atainua mikono akisema kwa siri wimbo wa Wakeruvikon:*

Sisi tunaofanana, kwa siri na Wakeruvi na tunaoimbia Utatu Mpaji-uzima, wimbo wa takatifu tatu, tuache sasa shuruli zote za dunia hii.

**SHEMASI** (*kwa siri*)*:* Kwa kumpokea mfalme wa vitu vyote, mwenye kusindikizwa bila kuonekana na majeshi ya Malaika. Aliluia, Aliluia, Aliluia.

*Tena ataisema mara tatu.*

*Kisha Padri atakamata chetezo na akisema, siku ya Mungu:* «Tukiona Ufufuo. . . na Zaburi 50 *(51). na siku za Juma atasema:* Njooni tumwabudu. . . *(mara tatu)* na Zaburi 50 (51*). Atafukiza Altare, Meza ya Matayarisho (Prothesis) na waaminifu wotwe.*

*Kisha, padri na Shemasi watainama mara tatu watabusu Antiminsio na Meza Takatifu, watageuka upenda wa watu, watainamisha kichwa wataenda ku Meza ya Matayarisho.*

*Shemasi kwa sauti ya chini atamwambia padri:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, inua.

*Padri atakamata* Aera *(Nguo ya kufunika Vitu Vitakatifu) pa mabega ya Shemasi akisema:*

Inueni mikono yenu patakatifu na kukuzeni Bwana.

*Shemasi atapokea kwa Padri Sahani. Padri mwenyewe atakamata Kikombe. Kisha wimbo:* **Kwa kumpokea mfalme wa vitu vyote».** *Hapo watatoka patakatifu katika mlango wa kaskazini, wakitanguliwa kwa taa chetezo, watafanya kuingia kubwa.*

*Shemasi atapaza sauti nguvu:*

**SHEMASI***:* Bwana Mungu, atukumbuke sisi wote katika ufalme wako daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina. Mwenye kusindikizwa bila kuonekana na majeshi ya malaika. Aliluia, Aliluia, Aliluia.

*Padri na Shemasi watarudi Patakatifu katika Mlango Bora kisha kuweka Kikombe pa Antiminsion, Padri atakamata Sahani kwa Shemasi, ataiweka pia pa Antiminsion akisema kwa siri:*

Muheshimiwa Yosefu aliposhusha Mwili wako safi kamili Msalabani, akaufunika na sanda safi, akaupakaa manukato, alauweka katika kaburi mupya.

Ulikuwa kaburini na Mwili wako, kuzimuni na roho kama Mungu, Paradizoni pamoja na Mnyanganyi, ulikaapa kiti cha pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, ee Kristu wewe uneyevijaza vitu vyote.

Iliyo kweli ya samani kuipita Paradizo, ya kuangaa zaidi kuliko makao yote ya mfalme, ee Kristu, ni hivi ilionekana kwetu kaburi yako yenye kuleta uzima; na chemchemi ya Ufufuo wetu.

*Padri atatosha vitambala-funiko (Kalimata) pa sahani na Kikombe, ataviweka vyenye kukunjwa pa Meza. Kisha atakamata Aera ku mabega ya Shemasi, ataifukiza na atafunika Sahani na Kikombe. Kisha atafukiza vipaji Vitakatifu, tena Shemasi atasema kwa sauti ya chini:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, utende mema.

**PADRI***:* Hapo watatolea ngombe juu ya Altare yako *(mara tatu).*

*Padri atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Unikumbuke, ee ndugu na mshirika wangu.

*Shemasi atamwambia Padri:*

**SHEMASI***:* Bwana Mungu akumbuke upadriwako katika Ufalme wake daima, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

*Shemasi, akiinamisha kichwa na kukamata Orario na vidole tatu vya mkono wa kuume, atamwambia padri:*

**SHEMASI***:* Uniombee, ee Rabi, mtakatifu.

**PADRI***:* Roho Mtakatifu atashuka juu yako, na nguvu zake aliye-juu zitakufunika kama kivuli.

**SHEMASI***:* Roho Mtakatifu huyu atatenda pamoja nasi siku zote za maisha yetu. Unikumbuke, ee Rabi mtakatifu.

**PADRI***:* Bwana Mungu akukumbuke katika Ufalme wake, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**SHEMASI***:* Amina.

*Shemasi atatoka inje ya Patakatifu, atasimama pa fasi ya kawaida. Aliluia ya wimbo ya Keruvikon ikimalizika, Shemasi atapaza sauti kusema Ektenia kubwa.*

*Waimbaji watajibu kisha kila maombi ya Shemasi, hivi:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:*

Tumalize ombi letu kwa Bwana.

Kwa ajili ya vipaji viheshimiwa vilivyowekwa mbele, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya nyumba hii takatifu na ya wanaoingiamo kwa imani, na ibada, na kumwogopa Mungu, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya kuokolewa na kila sikitiko, uadui, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

*Kwa hii wakati Padri anayesimama wima mbele ya Meza takatifu atasoma kwa siri hii sala ya sadaka:*

**PADRI** *(kwa siri):*

Ee Bwana Mungu Mwenyezi, uliye peke yako Mtakatifu, unayepokea sadaka ya sifa ya hawa wanaokuomba kwa moyo wao wote, pokea pia ombi letu sisi wenye zambi uilete jju ya Altare yako Takatifu. Utupe sisi kukutolea vipaji na sadaka za roho kwa ajili ya zambi zetu na ya makosa ya kutojua ya watu wako. Tena utustahilishe kupata neema kwako, iliupendezwemna sadaka yetu, na Roho yako Mwema wa neema yako ashuke juu yetu sisi, juu ya hivi vipaji na juu ya taifa zako zote

*Shemasi ataendelea kusema:*

Siku hii yote iwe kamili, takatifu, tulivu na bila zambi, tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji watajibu kisha kila ombi ya Shemasi hivi:* Utupe, ee Bwana.

Malaika wa amani, Mwongozi ya kweli, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu, tuombe kwa Bwana.

Vilivyo vyema na vinavyofaa ku roho zetu na amani ya dunia yote, tuombe kwa Bwana.

Kumaliza maisha yetu yanayobaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Mwisho wa maisha yetu uwe kikristu, bila maumivu, bila aibu, wa amani, tnea tuone neno njema mbele ya kiti chake cha kuogopa, tuombe cha Kristu.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa mbarikiwa kushinda, Malkia wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na Watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Padri atapaza sauti:*

**PADRI***:* Kwa huruma ya Mwana wako wa pekee ambaye umehimidiwa pamoja naye, na Roho yako Mtakatifu kamili, mwema na mpaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Tupendane sisi kwa sisi, ili kwa nia moja tuungame.

**WAIMBAJI***:* Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Utatu wa asili moja na usiyotengana.

*Padri atainama mara tatu atabusu Sahani, Kikombe na Meza takatifu, akisema kwa siri:*

**PADRI** *(kwa siri):* Nitakupenda, ee Bwana, nguvu yangu; Bwana ni imara yangu msaada wangu, kimbilio changu na Mwokozi wangu. *(mara tatu).*

*Shemasi atapaza sauti:*

Milango, Milango tusikilize kwa hekima.

*Padri atakamata Aera ataitikisa juu ya vipaji Vitakatifu akisema kwa siri Simvolo(Fundisho) ya Imani.*

*Waaminifu na waimbaji wanasema pamoja Simvolo ya Imani.*

**N**asadiki Mungu mmoja Baba mwenyezi, mwumba wa mbingu na wa dunia, hata vyote vilivyoonekana na visivyoonekana, tena Bwana mmoja Yesu Kristu. Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa na Baba mbele ya wakati wowote. Nuru toka Nuru. Mungu ukweli toka Mungu ukweli, aliyezaliwa, si umbwa mwenye asili moja (omousion) na Baba, aliye kwake vyotevilifanywa, aliye kwa ajili yetu wanadamu na ya wokovu wetu alishuka mbinguni, akapata mwili kwa Roho Mtakatifu na kwa Bikira Maria, na akawa mtu. Aliye sulibiwa kwa ajili yetu wakati wa Pontio Pilato. Akateswa, akawekwa kaburini, Na aliyefufuka katika siku ya tatu, kama ya navyo maandiko. Na akapanda mbinguni ndipo anapokaa kuume kwa Baba. Na atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio na hai na waliokufa. Ufalme wake utakuwa bila mwisho. Tena Roho Mtakatifu yu Bwana yu Mwumba hai, aliyetoka na Baba, aliyesujudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii, kwa Eklezia moja Takatifu, Katholiki na Apostoliki. Naungama kwa ubatizo moja kwa maondoleo ya zambi. Natumaini ufufuo wa wafu hata uzima wa milele utakapokuja. Amina.

*Shemasi atapaza sauti:*

**SHEMASI***:* Tusimame vizuri! Tusimame na woga! Tusikilize kwa kutolea sadaka takatifu kwa amani.

**WAIMBAJI***:* Huruma ya amani, zabihu ya sifa.

**PADRI***:* Neema ya Bwana wetu Yesu kristu, na mapendo ya Mungu, na Baba na ushirika wa Roho Mtakatifu, uwe nanyi nyote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

*Padri atainua mikono na atasema:* Tuweke mioyo juu.

**WAIMBAJI***:* Tunayo kwa Bwana.

*Padri atageuka ku Altare, akisema:* Tumsukuru Bwana.

**WAIMBAJI***:* Ni wajibu na haki.

*Padri atasali kwa siri sala ya matoleo:*

Ni wajibu na haki kukuimbia, kukutukuza kukusifu, kukushukuru na kukusujudu pahali popote pa utawala wako. Kwani ndiwe Mungu usiyeelezeka, usiyewajika, usiyeonekana, usiyesikitikana, uliye wa milele, uliye sawasawa nyakti zote. Wewe na Mwana wako wa pekee, na Roho yako Mtakatifu. Ulitufanya kwa bure, tukawa ukatusimamisha sisi tulioanguka, na ulifanya vyote mpaka kutuinua mbinguni na kutupatia Ufalme wako utakaokuja. Kwa ajili ya hivi vyote tunakushukuru Wewe, na Mwana wako wa pekee, na Roho yako Mtakatifu; kwa ajili ya mema yote yakujulikana na yasiyojulikana kwa sisi, ya kuonekana na yasiyoonekana uliyotutendea. Tunakushukuru pia kwa ajili ya Liturgia hii uliyokubali kuipokea kwa mikono yetu, hatakama una mbele yako maekfu ya Malaika majemadari, na makumi maelfu ya malaika, Wakeruvi na Waserafi, wenye mabawa sita, macho mengi, wakirukaruka kwa kukutumikia.

*Padri atapaza sauti:*

Wakiiimba, wakilia, wakipaza sauti, na kusema wimbo wa shangwe.

*Wakati wa hii tangazo ya padri, Shemasi atakamata Nyota ku mkono wa kuume atafanya alama ya msaada juu ya sahani, kila chongo ya Nyota itagusa Sahani. Ataweka Nyota juu ya Meza kisha kuikumbatia*

**WAIMBAJI***:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana Savaothi. Mbingu na inchi zimejazwa kwa utukufu wako. Hosana juu pia, mhimidiwa yeye anayekuja kwa jina la Bwana! Hosana uliye juu pia.

*Padri atasema kwa siri:*

Hata sisi pamoja nao majeshi heri hawa, ee Rabi Mpenda-wanadamu, tunapaza sauti tukisema*:* Wewe ni Mtakatifu, Mtakatifu kamili, Wewe na Mwana wako wa pekee, na Roho yako Mtakatifu. Wewe ni Mtakatifu, Mtakatifu kamili, utukufu wako na karimu. Wewe uliyeupenda ulimwengu wako, hata ukamtoa Mwana wako wa pekee, ili kila mtu akimwamini asipotee, lakini awe na uzima wa milele. Alikuja akatimiza kwa ajili yetu. Usiku ule alipotolewa, na zaidi alijitoa mwenyewe kwa ajili ya uzima wa ulimwengu. Alikamata mkate mikononi mwake mitakatifu, akaumega akawapa Wafwasi na Mitume wake Watakatifu, akisema*:*

*Padri ataonyesha mkate na mkono wa kuume akipaza sauti:*

**PADRI***:* Twaeni, kuleni, huu ni mwili wangu unaomegwa kwa ajili yenu, kwa maondoleo ya zambi.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** *(kwa siri):* Vilevile alikamata Kikombe kisha kula, akisema*:*

*Padri ataonyesha Kikombe akipaza sauti:*

**PADRI***:* Nyweni ninyi wote, hii ni Damu yangu ya Agano Jipya, inayomwangika kwa ajili yenu na ya wengi, kwa maondoleo ya zambi.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** *(kwa siri):* Kwa hivyo tukikumbuka amuri hii ya kuokoa, tena vyote vilivyofanywa kwa ajili yetu*:* Msaada, kaburi, ufufuo wa siku ya tatu, kupanda mbinguni, kukaa kuume na kuja mara ya mbili kwa utukufu.

*Padri akipakata mikono, kwa alama ya Msalaba, atakamata sahani ku mkono wa kuume na Kikombe ku mkono wa kushoto, atazipandisha akisema:*

**PADRI***:* Vilivyo vyako kutoka vilivyo vyako, tunakutolea kadiri ya vyote na kwa ajili ya vyote.

**WAIMBAJI***:* Tunakuimbia, tunakuhimidi, tunakushukuru, ee Bwana, na tunakuomba, ee Mungu wetu.

**PADRI** *(kwa siri):* Tena tunakutolea ibada hii ya akili na bila damu, tunakuomba na kukusihi na kukuronga. Utume Roho yako Mtakatifu juu yetu sisi na juu ya vipaji hivi vilivyo mbele hapa.

*Shemasi akionyesha mkate na Orario yake atasema kwa siri:*

**SHEMASI** *(kwa siri):* Kristu ufanye mkate huu kuwa Mwili mheshimiwa wa Kristu wako. Amina.

*Akionyesha Kikombe na Orario yake, atasema:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, bariki Kikombe Kitakatifu.

*Padri anapobariki Kikombe atasema:*

Na iliyo ndani ya Kikombe hiki kuwa, Damu heshimiwa ya Kristu wako.

**SHEMASI***:* Amina.

*Anapoonyesha vyote viwili, anasema:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi bariki Vitakatifu vyote viwili.

*Padri ataibariki vyote viwili akisema:* Ukivigeuza kwa Roho yako Mtakatifu.

**SHEMASI***:* Amina. Amina. Amina.

*Padri ataendelesha sala ya Ukaristia:*

**PADRI***:* Ili viwe kwao wanaovipokea, makesha ya roho, maondoleo ya zambi, ushirika wa Roho yako Mtakatifu, utimilifu wa Ufalme wa mbinguni, matumaini kwako, kutohukumiwa wala kuapizwa. Tena tunakutolea ibada hii ya akili kwa ajili ya wala waliopumzika katika imani*:*

Mababu, Wababa, Wapatriarkhe, Manabii, Mitume, Wahubiri, Waevangelizaji, Mashahidi, Waungamizi, Watawa na kila roho ya mwenye haki aliyefariki katika imani.

*Padri atafukiza vipaji viheshimiwa, atapaza sauti:*

Hasa Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Malkia wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Maria Bikira daima.

*Shemasi anafukiza pembeni Meza Takatifu na kukumbuka kwa siri, ma jina ya ndugu zake waorthodoksi, walikufa ao wanazima.*

*Waimbaji wanaimba Wimbo (Megalinarion) ya Mzazi-Mungu.*

**WAIMBAJI***:* Ni wajibu kweli kukuita, ee Mzazi-Mungu, mwenyi heri daima na usiye na doa tena Mama wa Mungu wetu. Uliye wa thamani kuwashinda Wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno, bila kuharabika, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.

*Wakati wa wimbo huu Padri atasema hii sala:*

**PADRI***:* Ya Yoane Mtakatifu, Mbatizaji, Nabii na Mtangulizi; ya Mitume Watakatifu watukufu na wasifiwa kamili; ya *(jina la Mtakaatifu wa siku hii)* tunayemukumbuka hata ya Watakatifu wako. Kwa maombi yao, ee Mungu, utuangalie. Na ukumbuke, wote hawa waliolala katika matumaini ya ufufuo wa uzima wa milele *(hapa padri atawataja wafu)* na uwapumzishe pahali pa mwangaza wa nuru ya uso wako. Tena tunakusihi*:* Ukumbuke, ee Bwana, kila uaskofu wa Waorthodoksi unaoeneza imara neno la ukweli wako, uapadri wote, ushemasi katika Kristu, hata kila jeshi la upadri na la utawa. Tena tunakutolea ibada hii ya akili kwa ajili ya ulimwengu, ya Eklezia yako Takatifu, Katholiki *(wa dunia mzima*), Apostoliki (*wa Mitume*); ya wale wanaoishi katika usafi na mwenendo wa kiasi, ya inchi yetu na ya watawala wetu; uwape kutawala katika amani, ili hata sisi tuweze kuishi katika utulivu wanaotulea, amani na ukimya, kwa ibada ya upole na mwenendo mwema.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Ee Bwana, ya kwanza umkumbuke Mwarkiaskofu wetu *(jina lake),* umlinde katika Eklezia yako Takatifu ili aishi miaka mengi mu amani uzima, mheshimiwa, mwenye afya aeneze imara neno wako la ukweli.

*Shemasi katika Mlango Bora atasoma Daftari akipaza sauti:*

**SHEMASI***:* Hata wale walio ndani ya akili ya kila mmoja; tena wanaume na wanawake wote.

**WAIMBAJI***:* Na wanaume na wanawake wote.

**PADRI** *(kwa siri):* Ukumbuke, ee Bwana, mji huu *(ao inchi hii, ao Monasteri, ao Kisanga),* pahali tunapokea, hata kila mji na inchi, na hawa wanaokaa humo kwa imani. Uwakumbuke, ee Bwana, wasafiri baharini, hewani na inchini kavu, wagonjwa wafungwa na wale wote wanaoteswa na kwa ajili ya wokovu wao. Uwakumbuke, ee Bwana, wale wanaoleta zawadi na wanaotenda matendo mema katika maeklezia yako Matakatifu, wanaowakumbuka maskini na utupe sisi wote huruma yako *(Hapa Padri atataja wazima).*

**PADRI** *(na sauti nguvu):*

Na utuwezesha ili sisi kwa kinywa na moyo mmoja kututukuze na kusifu jina lako liheshimiwa na litukufu la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu, sasa na siku zote.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri akibariki Waaminifu atasema:*

**PADRI***:* Rehema za Mungu wetu mkubwa na Mwokozi Yesu Kristu, jitakuwa pamoja nanyi nyote.

**WAIMBAJI***:* Hata na roho yako.

*Shemasi atatoka inje ya Patakatifu, ataenda pa fasi yake ya kuwaida atapaza sauti akisema:*

**SHEMASI***:* Tukiwakumbuka watakatifu wote, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

*Waimbaji kwa kila ombi watajibu:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:*

Kwa ajili ya vipaji viheshimiwa vilivyotolewa na kutakaswa tumwombe Bwana.

Ili Mungu wetu, Mpenda-wanadamu, aliyevipokea katika Altare yake Takatifu, ya mbinguni na isiyoonekana, kama manukato ya harufu ya kiroho, aturudishie neema, kimungu na zawadi ya Roho Mtakatifu, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya kuokolewa na kila sikitiko, uadui, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

*Katika hii wakati padri atasema kwa siri hii sala ifwatayo:*

**PADRI***:* Ee Rabi, mpenda-wanadamu, tunaweka maisha yetu yote na matumaini yetu mikononi mwako. Tunakuomba na kutusihi*:* Utustahilishe kushiriki katika fumbo zako za mbinguni na ajabu za Meza hii ya kiroho kimungu, na zamiri safi, kwa maondoleo ya zambi, usamehe wa makosa, ushirika wa Roho Mtakatifu na uriti wa ufalme wa mbinguni, ili tuwe na matumaini ya kuja mbele yako, bila hukumu wala kuapizwa.

*Shemasi ataendelea akisema:*

**SHEMASI***:* Siku yote iwe kamili, takatifu, tulivu na bila zambi tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji kisha kila ombi watajibu:* Utupe, ee Bwana. .

Malaika wa amani, Mwongozi ya kweli, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na makosa yetu, tuombe kwa Bwana.

Vilivyo vyema na vinavyofaa kwa roho zetu na amani ya dunia yote, tuombe kwa Bwana.

Kumaliza maisha yetu yanayobaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Mwisho wa maisha yetu uwe kikristu, bila maumivu, bila aibu, wa amani, tena tuone neno njema mbele ya kiti chake cha kuogopa tombe kwa Kristu.

Tukiomba umoja wa imani, na ushirika wa Roho Mtakatifu sisi na kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Na utustahilishe, ee Rabi, kusubutu na matumaini na bila hukumu, kukuita Baba, wewe Mungu wa mbinguni, na kusema;

*Waaminifu, Waimbaji na wasomaji watasema pamoja sala ya Rabi:*

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

**PADRI***:* Kwa kuwa na ufalme, na uwezo, na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakaitfu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI** *(kwa siri):* Tunakushukuru, ee Mfalme usiyeonekana, wewe kwa nguvu yako isiyopimika, umeviumba vyote, tena kwa wingi wa huruma yako umevitoa vyote toka bure vikawa. Wewe mwenyewe, ee Rabi, utazame toka mbinguni juu ua hawa wanaoinamisha kwako vichwa vyao, kwani hawakuinamisha kwa mwili na damu, ila kwako, uliye Mungu wa kuogopesha. Basi wewe, ee Rabi, utupatie, vipaji hivi vifae kila mmoja wetu kadiri ya uhitaji wake; safiri pamoja nao wanaosafiri baharini, hewani na inchini, uponyesha wagonjwa, wewe Mganga wa roho ya miili yetu.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Kwa neema, na rehema na mapendo kwa wanadamu ya Mwana wako wa pekee ambaye, umehimidiwa pamoja naye, na Roho yako Mtakatifu kamili, Mwema na mpaji uzima sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** *(kwa siri):* Usikilize, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, toka makao yako matakatifu na toka kiti cha utukufu wa Ufalme wako utujie ututakase, wewe unayekaa mbinguni pamoja na Baba, tena uliye hapa pamoja nasi bila kuonekana. Ukubali kutugawanyia ku mkono wako wa uwezo, Mwili wako Safi na Damu yako heshimiwa, na kwa mikono yetu wote.

*Padri na Shemasi watainama mara tatu wakisema kwa siri:*

Ee Mungu, uniwe razi, mimi mwenye zambi. *(mara tatu).*

**SHEMASI** *(na sauti nguvu):* Tusikilize.

*Pasdri atapandisha na mikono miwili mkate juu ya sahani akisema:*

Vitu Vitakatifu kwa watu watakatifu.

**WAIMBAJI***:* Mtakatifu ni mmoja peke yake, Bwana ni mmoja peke yake. Yesu Kristu, katika utukufu wa Mungu Baba. Amina.
*Shemasi atarudi Patakatifu na Waimbaji wataimba wimbo wa ushirika wa siku wala wa siku Kuu. Kila siku ya Mungu tunaimba:*
Msifuni Bwana kutoka mbinguni; msifuni katika pahali pa juu pia. Alliluia.
*Wakati wanaimba wimbo huu Padri na Shemasi watashiriki katika roho kadiri ya Ibada ifwatayo na yenye kufanyika kwa siri.*
**SHEMASI***:* Ee Rabi, mega mkate Mtakatifu.

*Padri ataumega mkata ataweka sehemu mbalimbali pa Sahani akisema:*
Anamegwa na kugawanyika Mwana-Kondoo wa Mungu kila mara anakatwa bila kutengana; anayeliwa kila mara bila kumalizwa, lakini anawatakasa washirika wake.

*Shemasi ataonyesha Kikombe na Orario yake akisema:*
Ee Rabi, jaza Kikombe Kitakatifu.
*Padri atakamata sehemu ya Mwili Mtakatifu iliyo na alama IC ataiweka mu Kikombe akisema.*

Kujazwa kwa Kikombe, kwa imani na Roho Mtakatifu.
**SHEMASI***:* Amina.
*Kisha Shemasi atakamata chombo chenye maji ya moto (Zeon), ataipeleka kwa padri akisema:*
**SHEMASI***:* Ee Rabi, bariki maji ya moto.
*Padri anapobariki maji ya moto atasema:*

Ubarikiwa umoto wa Watakatifu wako, daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Hapo Padri na Shemasi watasema sala za Komonyo Takatifu.*

Nasadiki, ee Bwana, na kuungama ya kama kweli Wewe Kristu, Mwana wa Mungu mzima, uliyekuja duniani kwa ajili ya kuokoa wenye zambi, ambao mimi ni wa kwanza. Nasadiki tena ya kama huu ni Mwili wako safi na hiyi ni Damu yako heshimiwa. Nanakuomba*:* Unihurumie na kunisamehe makosa yangu yakutaka na yakutotaka, kwa maneno ao kwa matendo, yakuja wala yakutokuja, unistahilishe kushiriki katika fumbo zako za bila doa, kwa ajili ya maondoleo ya zambi na uzima wa milele. Amina.

Angalia sasa najongea karibu ya Komonyo yako Takatifu, ee Mwumba wangu, usiniunguze ku ushariki huo. Sababu Wewe ni moto unaounguza wasiyostahili. Lakini unitakase ku aibu hiyi.

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho*:* Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Akionapo Damu Kimungu, atetemeke, ee Mwanadamu, kwa sababu ni makala ya moto ilunguzayo wasiostahilivu. Mwili Kimungu unageuzwa kimungu na unalisha, unatakasa na unalisha mawazo namna isiosikilizwa

Ee Kristu, kwa mapendo yako ulinipeleka ku furaha na kwa ulinzi wako ulinigeuza kuwa mtu mwengine*:* Choma zambi zangu kwa moto usiyo vyombo na kubali kunijaza na furaha zako, sababu nikiwa tele na furaha, nitasifu majio zako mawili, ee Wewe mjaliwa na wema.

Nitaingia je, mimi msiye stahili, katika ukuu wa watakatifu wako? Nikisubutu kwingia katika nyumba ya arusi, nguo langu litanitoa, maana hayuko ya arusi na nikifwatane, malaika watanifukuza. Bwana, safisha basi mataka ya moyo wangu na uniokoe, wewe mpenda wanadamu.

*Na pia Sala hii:*

Rabi, rafiki ya wanadamu, Bwana Yesu Kristu, Mungu wangu, vipaji vyako vitakatifu visiwe nami hukumu sababu ya maovu yangu*:* Lakini utakaso wa moyo na wa mwili na rahani ya uzima na ya ufalme wa milele. Ni vizuri kwangu kwa kumshika Mungu na kuweka tumaini la wokovu wangu katika Bwana.

*Na tena tunasoma hii:*

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako. . . .

*Padri, kwa mkono wa kushoto, atakamata sehemu moja ataiweka mu mkono wake wa kuume, akisema:*

Tazama, namjongea Kristu, Mfalme msiyekufa, Mungu wetu. Mimi (atataja jina lake) padri, napewa Mwili Mheshimiwa Mtakatifu na mwenye kuleta uzima, wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Hivi Padri anakuja Mkate Mtakatifu na woga wa Mungu na utaratibu.*

*Kisha atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Ee Shemasi, jongea.

*Shemasi atajongea akisema:*

**SHEMASI***:* Tazama, namjongea Kristu, Mfalme msiyekufa, Mungu wetu. Ee Rabi, unipe mimi *(atataja jina lake),* Shemasi, Mwili mheshimiwa Mtakatifu na mwenye kuleta uzima wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi zangu na uzima wa milele.

*Padri atamupa pa mkono wa kuume wenyi kuwekwa juu ya wa kushoto sehemu ya Mwili Mtakatifu, akisema:*

Kwa *(jina lake),* Shemasi, anapewa Mwili wa samani, Mtakatifu na bila doa kamili wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Shemasi akipokea Mwili Mtakatifu atabusu mkono wa padri ataenda nyuma ya Meza Takatifu huko ataukula kwa utaratibu sawasawa na padri.*

*Kisha padri atakamata Kikombe Kitakatifu pamoja na kitambaa-kifuniko atasema:*

**PADRI***:* Tazama, namjongea tena Kristu Mfalme msiyekufa na Mungu wetu. Mimi (*jina lake),* mutumishi wa Mungu na Padri napewa Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Na atakunwa mara moja. Kisha atapanguza midomo yake vilevile upande wa midomo ya Kikombe na atakibusu akisema.*

Hii imegusa midomo yangu; maovu yangu yataondolewa na zambi zangu zitatakaswa.

*Atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Ee Shemasi, jongea tena.

*Shemasi atajongea atapanguza kwa utaratibu mkono wake wa kuume na Musa akisema:*

Tazama, namjongea tena Kristu Mfalme msiyekufa na Mungu wetu. Ee Rabi, unipe Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Akimpa Kikombe mara moja, padri atasema:*

Mtumishi wa Mungu na Shemasi *(jina lake*), anapewa Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Kisha, wakati Shemasi atabusu midomo ya Kikombe, Padri atasema:*

Hii imegusa midomo yako, maovu yako yataondolewa, na zambi zako zitatakaswa.

*Kisha, Shemasi atakamata Sahani juu ya Kikombe ataweka sehemu katika Kikombe akipanguza vizuri Sahani na Musa (Yoga ya bahari). Anapofanya hivi, atasema:*

Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye peke yake bila zambi. Tunausujudu msalaba wako, ee Kristu, tena tunausifu na kuutukuza ufufuo wako takatifu. Kwa kuwa wewe Mungu wetu, la wewe peke yako hatumjui mwengine, jina lako tunaliita. Njoni enyi waaminifu wote, tuusujudu ufufuo takatifu wa Kristu. Kwa kuwa. je! Kwa ajili ya msalaba umefika furaha katika dunia mzima. Tukimhimidi Bwana daima, tunasifu ufufuo wako; kwa sababu akiuvumilia masalaba kwa ajili yetu, aliangamiza kifo kwa kifo chake.

*Padri ataweka mu Kikombe Kitakatifu vipande vyote ya Mkate ya wale watu waliokuta ao wanaoishi akisema:*

Ee Bwana, kwa Damu yako takatifu na kwa maombi ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu wako wote, zima zambi za hawa waliokumbushwa hapa. Amina.

*Kisha, atafunika Kikombe na Kitambaa (Kalimata). Kun mwisho ya wimbo wa Ushirika (Kinonikon), Shemasi atapokea Kikombe ku mikono ya padri na kukionyesha kwa watu, atapaza sauti akisema.*

Kwa woga wa Mungu, na imani, na mapendo, gongeeni.

*Padri atakamata Kikombe na akimupa kila Mwaminifu Komonyo, atasema:*

Mtumishi wa Mungu *(jina lake)* anapewa Mwili na Damu heshimiwa na takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu kwa maondoleo ya zambi zake na uzima wa milele. Amina.

*Wakati huu wa Kukomunika watu, waimbaji wataimba wimbo hii:*

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho*:* Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

*Kisha Komonyo ya Waaminifu Padri atawabariki watu na Kikombe Kitakatifu akipaza sauti:*

Ee Mungu, okoa taifa yako na bariki uriti wako.

**WAIMBAJI***:* Tumeona nuru wa kweli, tumepokea Roho wa mbinguni, tumepata imani ya kweli, tukiusujudu Utatu usiotengwa, kwani Huu umetuokoa.

*Kama Kanisa yetu inashangilia Siku Kuu moja ya Bwana Yesu Kristu, pa fasi ya wimbo:* (Tumeona nuru wa kweli. . . » *tunaimba Apolitikion ya hii Siku Kuu.*

*Padri ataweka Kikombe Kitakatifu juu ya Meza takatifu, atafukiza akisema kwa siri.*

Ee Mungu, utukuzwe juu mbinguni na utukufu wako uwe duniani yote.

*Hapo, padri atampa Shemasi Sahani, huyu atageuka ku upande wa watu kisha ataenda ku Meza ya Matayarisho (Prothesis), ataiweka huko. Padri mwenyewe atakamata Kikombe Kitakatifu atasema kwa siri.*

**PADRI***:* Ahimidiwe Mungu wetu.

*Kisha Padri atapinduka kwa watu, atawaonyesha Kikombe Kitakatifu akipaza sauti:*

Daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Shemasi atatoka pa fasi yake ya kuwaida na atapaza sauti:*

Simameni. Tukishiriki Fumbo za ajabu za Kristu, Fumbo za umungu, takatifu bila doa, za kutokufa, za mbinguni na zenyi kuleta uzima, tumshukuru Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie na utulinda, ee Mungu kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Tukimaliza kuomba siku hii yote iwe kamilifu, takatifu, tulivu na bila zambi; sisi na kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

*Na atarudi Patakatifu. '*

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Shukrani.*

Tunakushukuru, ee Rabi Mpenda-wanadamu, mfazili wa roho zetu, kwa kutustahilisha tena leo ku Fumbo zako za mbinguni na za kutokufa. Utuimarishe njiani sawasawa, utusabirishe sisi zote katika woga wako, ulinda maisha yetu, ukaze hatua zetu, kwa sala na maombi ya Maria Mzazi-Mungu na Bikira daima mtukufu na ya watakatifu wako wote.

*Kisha kukunja Antiminsion, Padri atafanya alama ya Msalaba, na Evangelion juu ya Meza akipaza sauti:*

Kwa kuwa wewe ni utakaso wetu na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha Padri ataweka Evangelion juu ya Antiminsion.*

***WAIMBAJI****:* Amina.

*Padri atageuka ku upande wa watu, atapaza sauti akisema:*

Twendeni na amani.

**WAIMBAJI***:* Kwa jina la Bwana.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia *(mara tatu)*, ee Rabi mtakatifu barikia.

*Padri atatoka inje ya Mlango Bora, atasimama mbele ya Ikone ya Kristu na atapaza sauti akisema:*

Ee Bwana, unayewabariki wale wanaokuhimidi na kuwatakasas wale wanaokutumainia, okoa taifa wako na bariki uriti wako. Ulinde Waaminifu wa Eklezia yako, uwatakase wale wanaopenda uzuri wa nyumba yako; uwarudishe utukufu kwa uwezo wako wa umungu. Usituache sisi tunaokutumainia. Uipatie dunia yako amani, ma Eklezia yako, mapadri, wakubwa wa inchi wetu na watu wako wote. Kwani kila neema na kila kipaji kamilifu kinatoka Kwako juu, uliye Baba wa nuru. Tunakushukuru na kukuabudu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Kisha waimbaji wataimba:*

Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa, na mupaka milele. *(mara tatu).*

*Padri ataenda ku Meza ya Matayarisho ana tasoma kwa siri hii sala ifwatayo:*

Ee Kristu Mungu wetu, uliye ukamilifu wa Sheria na wa manabii, Wewe uliyetimiza matengenezo yote ya Baba kwa ajili ya wokovu wetu, ujaze mioyo yetu na furaha na shangwe daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

*Padri ao Askofu atawabariki Waaminifu hivi:*

Baraka ya Bwana na huruma yake iwe nanyi, kwa neema yake na mapendo yake kwa ajili ya wanadamu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu, matumaini yetu, utukufu kwako.

**MSOMAJI***:* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milelena milele. Amina. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia, ee Padri mtakatifu barikia.

*Padri atapinduka ku upande wa Waaminifu, atafanya Kuaga hivi:*

Aliyefufuka katika wafu, *(kama ni Siku ya Mungu)* Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mama yake Mtakatifu asiye na doa, kwa nguvu na msaada mheshimiwa na wenyi kuleta uzima, kwa ulinzi wa majeshi maheshimiwa ya mbinguni yasiyo na mwili, kwa maombezi ya Yoane, Nabii Mtangulizi na Mbatizaji, mheshimiwa na mtukufu, ya Mitume Watakatifu, watukufu na waifiwa, *(ya Mtakatifu wa Kanisa kama ni Nabi, Mtume, wala askofu),* ya Mashahidi Watakatifu, watukufu na wasindaji, *(ya Mtakatifu wa Kanisa kama ni Shahidi),* ya wababa wetu Watakatifu na wabebaji-Mungu, *(ya Mtakatifu wa Kanisa kama ni Mtawa),* ya Baba wetu Mtakatifu Yoane Krisostomo, Mwarkiaskofu wa Kontantinopoli, ya YOakimu na Anna, Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki, ya Mtakatifu wa hii siku *(jina yake)* tunayekumbuka leo, na ya Watakatifu wote, atuhurumie na kutuokoa, kwani Yeye ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu na Mrahimu.

Kwa maombezi ya wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

*Kama ni Askofu Padri atasema hivi:* Kwa maombezi ya Askofu wetu Mtakatifu, ee Bwana Yesu Kristu. . .

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri atawabariki waaminifu akisema:*

Utatu Mtakatifu uwalinde ninyi wote.

**WAIMBAJI***:* Anayetubariki na kututakasa, ee Bwana, umlinde miaka mengi.

*Kama Liturgia anafanya Askofu waimbaji wataimba hivi:*

Ee Bwana, umulinde Rabi na Askofu wetu, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi.

*Kisha Askofu ao Padri atagawanya mkate wenyi kubarikiwa uitwao Antidoron akisema kwa kila mwaminifu.*

Baraka ya Mungu na huruma yake iwe nawe.

# LITURGIA KIMUNGU YA MTAKATIFU BAZILE MKUBWA ASKOFU MKUBWA WA KESARIA YA KAPADOKIA

## LITURGIA YA WAKATIKUMENO

*Elezo: Mbele ya Meza takatifu, wenye kuongoza Ibada watapiga magoti mara tatu wakisema:*

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

Utukufu kwa Mungu juu pia, amani katika inchi mapendo kwa wanadamu. *(mara tatu)*
Bwana, utafungua midomo yangu na kinywa changu kitatangaza sifa yako. *(mara mbili).*
Ee Bwana, utufungulie mulango ya huruma yako.

*Kisha padri atabusu Evangelion na shemasi atabusu paka Meza takatifu. Shemasi atainamisha kichwa mbele ya Padri na akiinua orarion na mkono wa kuume. Kisha kupokea baraka ya mwongozi wa Ibada, Shemasi atatoka ku Altare Takatifu kwa mlango wa kaskazini, atasimama mbele ya mlango Bora na atainamisha kichwa atapaza sauti kusema:*

**SHEMASI:** Ee Rabi, himidi.

*Padri atasimama mbele ya Meza, atakamata pa mikono yake Evangelio Takatifu, atafanya alama ya msalaba juu ya Antiminsio(nguo takatifu nyekundu) na atapaza sauti kusema:*

Mhimidiwe ufalme wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Shemasi atapaza sauti atasema Irinika (maombi ya amani), hivi:*

*Waimbaji watajibu kwa kila ombi:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:*

Kwa amani tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya amani kutoka juu na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya amani ya dunia yote, na kusimama imara kwa maeklezia Matakatifu ya Mungu, na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya nyumba hii takatifu na ya wanaoingiamo imani na ibada na kumwogopa Mungu, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya wakristu waabudu na waorthodoksi, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya Mwarkiaskofu wetu (jina lake), ya ukasisi uheshimiwa, ya ushemasi katika Kristu, ya wateule wote na ya watu wote, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya taifa letu, ya wale wanaoitawala, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya muji huu *(ao Monasteri, inchi ao Kisanga)* kila muji na kila inchi na ya wanaoishimo kwa imani, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya majira mema ya mwaka, ya wingi wa matunda duniani na ya wakati za amani, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya walio baharini, ya wasafiri, ya wagonjwa, ya wafungwa, ya wale wote wanaoteseka, na kwa ajili ya wokovu wa wote, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya kuokolewa ku kila sikitiko, kila uadui, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na Watakatifu wote, sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu, Mungu wetu.

**WAIMBAJI***:* kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Antifonon ya kwanza (Kiitikio).*

Ee Bwana, Mungu wetu, mwenye enzi yote na utukufu kupita kila ufahamu, uliye na huruma sana, tena na mapendo kwa wanadamu yasiyoelezeka, wewe mwenyewe, ee Rabi, katika huruma yako, utuangalie sisi na hekalu hii takatifu na utupe sisi pamoja na hawa wanaosali pamoja nasi, huruma yako ya utajiri na rehema yako.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa utukufu wote, na heshima na usujudu ni haki yako ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Halafu Waimbaji wanaimba Antifonon ya kwanza:*

**ANTIFONON WA KWANZA**

Shairi*:* Umsifu Bwana, ee roho yangu, na yote yaliyo ndani yangu yasifu Jina lako takatifu.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Umsifu Bwana, ee roho yangu, wala usisahau mema yake yote.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Bwana amesimika kiti chake mbinguni, na ufalme wake unatawala vitu vyote.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

*Kama Liturgia inafanyika katikati ya Juma tunaimba hii Antifonon wa kwanza:*

Shairi*:* Ni vema kumwungama Bwana, na kuliimbia jina lako, ewe uliye-juu

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Ni vema kutangaza huruma wako asubui, na uaminifu wako nyakati za usiku.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Shairi*:* Maana Bwana ni mwenye Haki na hakuna uzulumu ndani yake.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ee Mwokozi utuokoe.

*Shemasi atasema Ektenia Kidogo:*

Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na Watakatifu wote, sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu, Mungu wetu.

**WAIMBAJI***:* kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Antifonon wa mbili.*

Ee Bwana, Mungu wetu, okoa taifa wako na bariki uriti wako; ulinde jamii ya Eklezia yako, na takasa hawa wanaopenda uzuri wa nyumba yako; uwape utukufu kwa uwezo wako wa umungu, na usituache sisi tunaotumaini wewe.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa utawala ni kwako, na ufalme, na uwezi na utukufu ni wako wa Baba, na wa Mwana, na

wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

***WAIMBAJI**:* Amina.

*Halafu Waimbaji wanaimba Antifonon wa mbili:*

**ANTIFONON WA MBILI**

*Shairi:* Umsifu Bwana, ee roho yangu, nitamsifu Bwana maisha yangu yote, nitamwimbia Mungu wangu zaburi mimi ningali mzima.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Shairi*:* Heri mtu anayesaidiwa na Mungu wa yakobo, anayemtumainia Bwana, Mungu wake.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Shairi*:* Bwana anatawala milele. Mungu wako, ee Sayuni, kizazi hata kizazi.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Uliye Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, ukiwa msiyekufa ukakubali kwa ajili ya wokovu wetu kupata mwili kwa Maria Mzazi-Mungu, tena Bikira daima, ukawa mtu bila kujigeuza; hata kusulubiwa, ewe Kristu Mungu, na kukikanyanga kifo kwa kifo; ukiwa mumoja na Utatu Mtakatifu, na kutukuzwa pamoja na Baba, na Roho Mtakatifu, utuokoe.

*Kama Liturgia inafanyika katikati ya Juma tunaimba hii Antifonon wa mbili:*

*Shairi:* Bwana ni Mfalme, amevaa utukufu, Bwana amevaa uwezo, amejifunga ezi kiunoni.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye Watakatifu ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Shairi:* Amekaza ulimwengu usitikisike.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye Watakatifu ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Shairi:* Nyumba yako imajaa utakatifu, ee Bwana, muda wa siku nyingi sana.

Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye Watakatifu ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Uliye Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, . . . . . . . . . . .

*Shemasi atasema Ektenia Kidogo:*

Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu, Mungu wetu.

**WAIMBAJI***:* kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Antifonon wa tatu:*

Wewe uliyetupatia neema ya kuunganisha masauti yetu kwa kukutolea sala hizi za pamoja na uliyeahidi kusikiliza maombi ya watu wawili hata watu watatu wanaokusanyika katika jina lako, wewe mwenyewe, sasa utimize maombi ya watumishi wako, kwa faida yetu, ukitupatia katika wakati huu kamili ukweli wako, tena uzima wa milele katika ulimwengu utakaokuja.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu, na kwako tunakutolea utukudu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**ANTIFONON YA TATU**

*Waimbaji wanaimba Apolitikion ya Ufufuo, kama ni mu Juma ao ya Mtakatifu fulani kama ni siku ingine shangilio yake.*

Shairi*:* Hii ndiyo siku aliyofanya Bwana tunashangilia na tunafurahiwa nayo.

*Apolitikion ya Ufufuo. Kama ni Liturgia katikati ya Juma tunaimba Apolitikion ya hule Mtakatifu, bila shairi.*

*Wakati wa hii wimbo padri atakamata Evangelio Takatifu atamupa Shemasi. Kisha, watatoka ku Altare Takatifu kwa mlnago wa kaskazini na watatanguliwa kwa watoto wenye kubeba taa. Watasimama mbele ya mlango Bora, pahali pa kuwaida. Watainamisha vichwa vyao. Shemasi kwa sauti ya chini:* Tumwombe Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya kuingia ndogo (Mikra Isodos).*

Ee Rabi na Bwana Mungu wetu, uliyeweka mbinguni makundi na majeshi ya malaika, na malaika majemadari kwa kazi ya utukufu wako; ufanye kuingia kwetu kuwe pamoja na malaika watakatifu, wanaotumika na kuutukuza pamoja nasi wema wako.

Kwa kuwa utukufu wote, heshima na usujudu ni haki yako kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Shemasi kwa sauti ya chini atamwambia padri:*

Ee Rabi, bariki Kuingia Kitakatifu.

*Kwa sauti chini padri ataibariki hivi:*

Kubarikiwa kuingia kwa Patakatifu pako, daima sasa na siku zote hata milele nma milele.

*Shemasi atapeleka Evangelio Takatifu kwa padri ataibusu, kisha kama wimbo itaisha Shemasi atapaza sauti:*

Hekima. Simameni.

*Padri na Shemasi wataingia ndani ya Altare takatifu katika Mlango Bora na Shemasi ataweka Evangelio Takatifu juu ya Antiminsion.*

*Waimbaji wataimba wimbo wa Kuingia:*

Njooni, tumwabudu na kumwangukia Kristu. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

Siku ya katikati ya Juma tunaimba*:*

Njooni tumwabudu na kumwangukia Kristu. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliye katika watakatifu wa ajabu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Kisha Waimbaji wataimba Apolitikion ya sauti ni siku ya Mungu. Kisha Apolitikion ya Mtakatifu wa siku, ya Mtakatifu ya Kanisa na Kontakion.*

*Kama wanafanya Liturgia wa padri wawili na juu, hawa wataimba Kontakion. Lakini kama anafanya Liturgia mpaka padri moja, Kontakio wataiimba Waimbaji.*

*Kama hakuna Siku Kuu kubwa, mapadri wanaimba:*

**KONTAKION YA MZAZI-MUNGU***:*

Ee Mulinzi usiyepatisha wakristu haya, na mupatanishi wa Muumba usiyeweza kubadilika, usizarau sauti ya kusihi ya wenye-zambi. Lakini fika kama mwema, kwa kutusaidia sisi, tunaokuita na imani*:* Ujiharikishe kwa upatanisho, na ukimbie kwa kutuomba, ewe Muzazi-Mungu unayelinda, wanaokuheshimu daima.

*Kila padri, kama ni Siku Kuu mkubwa, ataweza kutafuta Kontakio ya hii Siku Kuu ku mwisho ya hii Kitabu. Ukurasa:*

*Shemasi atapaza sauti anasema inje ya Mlango Bora:*

Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI**: Bwana hurumia.

*Padri atasema kwa siri sala ya Trisayo:*

Ee Mungu Mtakatifu, unayekaa katika watakatifu, unayeimbwa kwa sauti Takatifu tatu na Wa Serafi, na kutukuzwa na Wakeruvi, na kusijudiwa na nguvu zote za mbinguni! Uliyefanya vitu vyote kwa bure, vikawa, uliyemwaumba mwanadamu kwa sura na mfano wako, tena kumpamba kwa vipaji vyako vyote; wewe unayempa yoyote anayekuomba hekima na busara na usiyemzarau mwenye zambi kumwacha apotee, lakini umeweka kutubu kama njia ya wokovu; Wewe uliyetustahilisha, sisi watumishi wako wanyenyekevu na wasiostahili, kusimama hata wakati huu mbele ya utukufu wa Altare yako takatifu na kukuletea usujudu na sita iliyo haki yako; wewe mwenyewe, ee Rabi, pokea pia ku midomo yetu zambi Wimbo wa takatifu tatu na utufikie kwa wema wako; utusamehe kila kosa tumefanya wala ya kutaka, wala yasiokutaka, utakasa roho zetu na miili yetu tena utupe kukuabudu katika utakatifu siku zote za maisha yetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu mtakatifu na ya watakatifu wote waliokupendeza tangu milele.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa Wewe ni Mtakatifu, ee Mungu wetu na kwako tunautoa, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote,

SHEMASI*:* Hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Waimbaji wanaimba Trisayo:*

Mungu Mtakatifu, Mweza Mutakatifu, Msiyekufa Mutakatifu, utuhurumie *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Msiyekufa Mutakatifu, utuhurumie.

**SHEMASI***:* Nguvu (Dinamis).

**WAIMBAJI***:* Nguvu (Dinamis). Mungu Mtakatifu, Mweza Mutakatifu, Msiyekufa Mutakatifu, utuhurumie.

*Wakati wa wimbo wa Trisayo Padri na Shemasi watasali kwa siri* «Mungu Mtakatifu. . . . » *Kisha wataenda ku Altare ya Matayarisho (Prothesis) na Shemasi atamwambia Padri na sauti ya chini:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, amuru.

*Padri atasema na sauti ya chini:* Mhimidiwe Yeye anayekuja kwa jina la Bwana.

*Tena, Padri na Shemasi wataenda «pahali pa juu», pahali pa kiti cha askofu wala kwa msulubiwa, iliyo nyuma ya Altare na Shemasi atamwambia Padri na sauti ya chini.*

*SHEMASI:* Ee Rabi himidi kiti cha enzi kilicho juu.

**PADRI***:* Uhimidiwe, wewe katika kiti cha enzi cha Ufalme wako, unayekaa juu ya Wakeruvi, daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha wimbo wa Trisayo, msomaji atasoma Shairi ya kwanza ya Prokimenon yenye kutangulia somo la Barua ya Matendo ya Mitume (Apostolos).*

**SHEMASI***:* Tusikilize.

*Msomaji atasoma shairi ya mbili ya prokimenon.*

**SHEMASI***:* Hekima.

*Msomaji atasoma kipindi cha somo la barua ya matendo (Apostolos).*

**SHEMASI***:* Tusikilize.

*Wakati wa somo ya Apostolos, Shemasi atafukiza Altare, Meza ya Matayarisho (Prothesis). Kingio kubwa, na tangu milango bora, ikone na watu wote. Akiisha, Shemasi atainamisha kichwa mbeletya Padri na atamwambia na saudi chini:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, bariki msomaji wa Evangelio Takatifu, kama ilivyoandikwa na Mtuma Mtakatifu tena Mwevangelizaji *(jina lake).*

*Padri atasema kwa siri:*

Kwa maombi ya Mtume Mtakatifu, Mtukufu na Mwevangelizaji *(jina lake*), Mungu akupe neno ya kutangaza Habari Njema na nguvu nyingi, kwa kutimiza Evangelio ya mwana wake Mpendwa, Bwana wetu Yesu Kristu.

*Shemasi kwa sauti chini atasema:*

Amina. Amina. Amina. Iwe kwangu sawasawa na neno lako.

*Padri atamupa Shemasi Evangelio. Huyu atapanda pa Ambon (Kiti ya Muhubiri) akitanguliwa kwa taa.*

*Padri kwa siri atasoma, mbele ya Altare, hii sala:*

Ee Rabi, Mpenda-wanadamu, wangaze mioyoni mwetu na nuru isiyokufa ya kujua umungu wako, tena fungua macho ya akili yetu ili tusikie mahubiri ya Evangelio yako. Weka ndani yetu woga wa amri zako, ili tuishi uzima wa kiroho tukikanyanga tamaa yote mbaya ya kimwili, tukiwaza na kutenda vitu vyote vinavyokupendeza.

Kwa kuwa Wewe ni mwangaza wa roho zetu na miili yetu, ee Kristu Mungu, na kwako tunautoa utukufu, pamoja na Baba yako wa milele, na Roho wako Mtakatifu kamili, Mwema na Mpaji wa uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Ku mwisho ya somo la Apostolos Padri atasimama ku mlango bora atambariki msomaji akipaza sauti:*

Amani kwako, ee Msomaji.

**WAIMBAJI**: Aliluia, Aliluia, Aliluia.

**PADRI***:* Hekima. Simameni. Tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Somo katika Evangelio takatifu iliyoandikwa na *(jina ya: Matayo, Marko, Luka, Yoane).*

**PADRI***:* Tusikilize.

**WAIMBAJI***:* Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Shemasi atasoma Evangelio. Ku mwisho ya somo padri atasema kwake:*

**PADRI***:* Amani kwako, ee Mwevangelizaji.

**WAIMBAJI***:* Utukufu Kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Shemasi atarudi ku mlango bora na atamupa Padri Evangelio. Padri atarudi mu Altare Takatifu na ataweka Evangelio pa Meza. Kwa hii wakati askofu wala padri atafasiria maandiko ya somo ya Evangelio wala ya barua (APOSTOLOS), tena atawafundisha watu wa Mungu.*

*Shemasi atasimama pahali paka pa desturi mbele ya Mlango Bora, atapaza sauti atasema Ektenia Kubwa.*

Tuseme sisi wote kwa roho yetu na kwa akili yetu, tuseme.

*Waimbaji watasema kisha kila maombi:* Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Ee Bwana mwenyezi, Mungu wa Baba zetu, tunakuomba utusikilize na kutuhurumia.

Utuhurumia, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na kutuhurumia.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Wakristu, wenyi ibada na Waorthodoksi wote.

tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiaskofu wetu *(jina lake).* . .

Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, Watawa, mashemasi, hata ya ndugu wetu wote katika Kristu.

Tena tunakuomba kwa ajili ya watumishi wa Mungu, wakristu wote, wenyi ibada na waorthodoksi, wanaokaa katika mji huu na ya jamii ya parokia hii, ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, msaada, usamehe na maondoleo ya zambi.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wenye heri wajengaji wa hekalu hii takatifu, ya Baba na ndugu zetu waorthodoksi ambao wamelela hapa na ibada na pahali popote.

Tena tunakuomba kwa ajili yao wanaotenda matendo mema katika hekalu hii takatifu na heshimiwa, kwa ajili yao wanaoleta zawadi, wanaotumikiamo, wanaoimbiamo hata ya watu wote wanaosimama hapa, wakingoja huruma yako kubwa na ya utajiri.

*Padri kwa siri atasoma hii sala.*

Ee Bwana, Mungu wetu, pokea maombi marefu haya ya watumishi wako na utuhurumie kadiri ya wingi wa huruma yako; tena utupatie rehema zako, sisi na watu wako hawa wanaongoja huruma yako kubwa na ya utajiri.

*Padri atapaza sauti:*

Kwa kuwa Wewe ni Mungu wa huruma na Mpenda-wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Shemasi atapaza sauti ataanza maombi kwa ajili ya Wakatikumeno. Waimbaji watajibu kwa kila maombi:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Enyi Wakatikumeno, ombeni kwa Bwana.

Hata sisi tulioamini, kwa ajili ya wakatikumeno, tumwombe Bwana.

Ili Bwana awahurumie.

Awafundishe neno la ukweli.

Awafundishe Evangelio ya haki.

Awafundishe ku Eklezia yake takatifu, Katholiki *(wa dunia mzima*) na Apostoliki (*wa Mitume*).

Uwaokoe, uwahurumie, uwasaidie, uwalinde, ee Mungu, kwa neema yako.

Enyi wakatikumeno, inamisheni vichwa vyenu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya wakatikumeno:*

**PADRI***:* Ee Bwana, Mungu wetu, unayekaa juu mbinguni na kuona viymbe vinyenyekevu, uliyetuma Mwana wako wa pekee, Mungu na Bwana wetu Yesu Kristu, aliye wokovu wa wanadamu, uwaangalie watumishi wako, wakatikumeno, wanaoinamisha vichwa vyao mbele yako. Uwastahilishe kuzaliwa mara ya mbili, na kupewa maondoleo ya zambi na vazi lisioharikia, uwaunganishe ku Eklezia yako Takatifu, Katholiki *(wa dunia mzima)* na Apostoliki *(wa Mitume),* na uwahesabie katika kundi la wateule wako.

*Padri atapaza sauti:*

Ili hata hawa pamoja nasi walitukuze jina lako lenye kustahili heshima yote na utukufu wote, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri atakunjua Antiminsio pa Altare, wakatipo Shemasi atapaza sauti akisema:*

**SHEMASI***:* Walio Wakatikumeno tokeni. Enyi Wakatikumeno, tokeni. Walio wakatikumeno, tokeni. Mtu mkatikumeno asikae ndani.

# LITURGIA YA WAAMINIFU

**SHEMASI***:* Sisi tulio waaminifu, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Hekima.

*Padri atasoma sala ya kwanza ya Waaminifu*

**PADRI***:* Tunakushukuru, ee Bwana wa majeshi, uliyetustahilisha hata sasa kusimama mbele ya Altare yako Takatifu na kusijudu mbele yako tukiomba huruma yako kwa ajili ya zambi zetu na ya makosa ya kutojua watu. Upokee, ee Mungu, ombi letu. Utustahilishe kukuletea sala zetu, maombi na sadaka bila damu kwa ajili ya watu wako wote. Utupe nguvu, sisi uliotuweka katika utumishi huu, ya kukuomba wakati wote na pahali pote, kwa uwezo wa Roho Mutakatifu, bila hukumu wala laumu, na zamiri safi, ili ukisikiliza sala zetu, utuhurumie kadiri ya wingi wa wema wako.

*Padri atapaza sauti kusema:*

Kwa kuwa Utukufu wote, na heshima, na usujudu ni haki yako ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**SHEMASI***:* Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Hekima.

*Padri kwa siri atasema sala ya mbili ya Waaminifu:*

Ee Mungu, Wewe mwenye kutazama na rehema na huruma unyenyekevu wetu, Wewe uliyetuweka mbele ya utukufu wako takatifu, sisi wenye zambi wako wanyenyekevu na watumishi wasiostahili, kwa kazi ya Altare yako Takatifu, utusabitishe kwa ajili ya ibada hii kwa uwezo wa Roho yako Mutakatifu, na utupe, tukifungua kinywa, manenp ya kufaa sababu ya kuomba Neema ya Roho yako Mtakatifu juu ya zawadi zitatolewa kwako.

*Padri atapaza sauti:*

Ili sisi tukilindwa daima kwa uwezo wako, tukutolee utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Wainmbaji wataimba wimbo ya* ***KHERUVIKO*** *pole-pole na vizuri.*

Sisi tunaofanana kwa siri na wakeruvi na tunaoimbia Utatu Mpaji-uzima wimbo wa takatifu Tatu, tuache sasa shuruli zote za dunia hii. Kwa kupokea Mfalme wa vitu vyote.

*Hii wakati ya wimbo ya Keruvikon Padri atasoma kwa siri sala mbele ya Meza, hivi:*

Mtu hata mmoja wa wale wenye kufungwa kwa tamaa na furaha za mwili anayestahili kuja Kwako, kukujongea na kukuabudu ee Mfalme wa utukufu. Kwani kukutumikia ni kituki kubwa na cha kuogopa sana hata kwa majeshi ya mbinguni. Lakini katika mapendo Yako isiyokaairika ya isiyohesabika kwa ajili ya mwanadamu, umejifanya mtu bila kujigeuza wa ukawa Kuhani wetu mkuu; tena, ee Rabi wa vitu vyote, umetupatia utimizo wa sadaka hii isiyo na damu. Peke Yako, ee Bwana Mungu wetu, unatawala mbinguni na duniani, umekaa katika kiti cha enzi cha wakheruvi, ee Bwana wa Maserafi, Mfalme wa Israeli, uliye peke yako Mtakatifu na kupumzika katika Watakatifu. Basi, nakusihi, Wewe peke Mwema na mfazili, uniangalie mimi mutumishi, mwenyi zambi na msiyestahili, u takase roho na moyo wangu kwa kila wazo baya tena unipe nguvu, kwa uwezo wa Roho yako Mtakatifu, ili nikivaa neema ya upadri nisimame mbele ya Meza yako hii takatifu, kutolea Mwili Wako Takatifu safi na damu yako ya samani. Nakuja Kwako nikiinamisha kichwa tena nakusihi*:* Usinifiche Uso wako na usinikatae kuwa katikati ya watumishi wako, unistahilishe, mimi mwenye zambi na mtumishi nisiyestahili kukutolea zawadi hizi. Kwani ndiwe unayetoa na kutolewa unapokea na kugawanya, ee Kristu Mungu wetu; na kwako tunautoa utukufu, pamoja na Baba yako asiye na mwanzo na Roho yako Mtakatifu kamiliMwema na Mpaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha padri atainua mikono akisema kwa siri wimbo wa Wakeruvikon:*

Sisi tunaofanana, kwa siri na Wakeruvi na tunaoimbia Utatu Mpaji-uzima, wimbo wa takatifu tatu, tuache sasa shuruli zote za dunia hii.

**SHEMASI** (*kwa siri*)*:* Kwa kumpokea mfalme wa vitu vyote, mwenye kusindikizwa bila kuonekana na majeshi ya Malaika. Aliluia, Aliluia, Aliluia.

*Tena ataisema mara tatu.*

*Kisha Padri atakamata chetezo na akisema, siku ya Mungu:* «Tukiona Ufufuo. . . na Zaburi 50 *(51). na siku za Juma atasema:* Njooni tumwabudu. . . *(mara tatu)* na Zaburi 50 (51*). Atafukiza Altare, Meza ya Matayarisho (Prothesis) na waaminifu wotwe.*

*Kisha, padri na Shemasi watainama mara tatu watabusu Antiminsio na Meza Takatifu, watageuka upenda wa watu, watainamisha kichwa wataenda ku Meza ya Matayarisho.*

*Shemasi kwa sauti ya chini atamwambia padri:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, inua.

*Padri atakamata* Aera *(Nguo ya kufunika Vitu Vitakatifu) pa mabega ya Shemasi akisema:*

Inueni mikono yenu patakatifu na kukuzeni Bwana.

*Shemasi atapokea kwa Padri Sahani. Padri mwenyewe atakamata Kikombe. Kisha wimbo:* Kwa kumpokea mfalme wa vitu vyote»*. Hapo watatoka patakatifu katika mlango wa kaskazini, wakitanguliwa kwa taa chetezo, watafanya kuingia kubwa.*

*Shemasi atapaza sauti nguvu:*

**SHEMASI***:* Bwana Mungu, atukumbuke sisi wote katika ufalme wako daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina. Mwenye kusindikizwa bila kuonekana na majeshi ya malaika. Aliluia, Aliluia, Aliluia.

*Padri na Shemasi watarudi Patakatifu katika Mlango Bora kisha kuweka Kikombe pa Antiminsion, Padri atakamata Sahani kwa Shemasi, ataiweka pia pa Antiminsion akisema kwa siri:*

Muheshimiwa Yosefu aliposhusha Mwili wako safi kamili Msalabani, akaufunika na sanda safi, akaupakaa manukato, alauweka katika kaburi mupya.

Ulikuwa kaburini na Mwili wako, kuzimuni na roho kama Mungu, Paradizoni pamoja na Mnyanganyi, ulikaapa kiti cha pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, ee Kristu wewe uneyevijaza vitu vyote.

Iliyo kweli ya samani kuipita Paradizo, ya kuangaa zaidi kuliko makao yote ya mfalme, ee Kristu, ni hivi ilionekana kwetu kaburi yako yenye kuleta uzima; na chemchemi ya Ufufuo wetu.

*Padri atatosha vitambala-funiko (Kalimata) pa sahani na Kikombe, ataviweka vyenye kukunjwa pa Meza. Kisha atakamata Aera ku mabega ya Shemasi, ataifukiza na atafunika Sahani na Kikombe. Kisha atafukiza vipaji Vitakatifu, tena Shemasi atasema kwa sauti ya chini:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, utende mema.

**PADRI***:* Hapo watatolea ngombe juu ya Altare yako *(mara tatu).*

*Padri atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Unikumbuke, ee ndugu na mshirika wangu.

*Shemasi atamwambia Padri:*

**SHEMASI***:* Bwana Mungu akumbuke upadriwako katika Ufalme wake daima, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

*Shemasi, akiinamisha kichwa na kukamata Orario na vidole tatu vya mkono wa kuume, atamwambia padri:*

**SHEMASI***:* Uniombee, ee Rabi, mtakatifu.

**PADRI***:* Roho Mtakatifu atashuka juu yako, na nguvu zake aliye-juu zitakufunika kama kivuli.

**SHEMASI***:* Roho Mtakatifu huyu atatenda pamoja nasi siku zote za maisha yetu. Unikumbuke, ee Rabi mtakatifu.

**PADRI***:* Bwana Mungu akukumbuke katika Ufalme wake, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**SHEMASI***:* Amina.

*Shemasi atatoka inje ya Patakatifu, atasimama pa fasi ya kawaida. Aliluia ya wimbo ya Keruvikon ikimalizika, Shemasi atapaza sauti kusema Ektenia kubwa.*

*Waimbaji watajibu kisha kila maombi ya Shemasi, hivi:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:*

Tumalize ombi letu kwa Bwana.

Kwa ajili ya vipaji viheshimiwa vilivyowekwa mbele, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya nyumba hii takatifu na ya wanaoingiamo kwa imani, na ibada, na kumwogopa Mungu, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya kuokolewa na kila sikitiko, uadui, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

*Kwa hii wakati Padri anayesimama wima mbele ya Meza takatifu atasoma kwa siri hii sala ya sadaka:*

**PADRI** *(kwa siri):*

Ee Bwana Mungu wetu, Wewe uliyetuumba na kutuleta ku uzima huu, Wewe uliyetuonyesha njia za wokovu, Wewe uliyetupatia Ufufuo wa FUmbo za mbinguni, Wewe uliyetuweka kwa kazi hii katika uwezo wa Roho yako Mtakatifu, Wewe peke, ee Bwana, fanya ili tuwe watumishi wa Agano lako Jipya, waongozi wa Fumbo zako takatifu; utupokee, kadiri ya huruma yako kubwa, wakati tunapojongea ku Altare yako Takatifu, ili tustahili kukutolea Ibada hii ya roho yasiyo damu kwa ajili ya zambi zetu na ujinga wa watu; uipokee ku Altare yako Takatifu, ya mbinguni na ya kiroho kama manukato nzuri ya kiroho, ututumie Neema ya Roho yako Mtakatifu. Ututazame ee Mungu: Tazama sadaka yetu na uipokee kama ulivyopokea zawadi za Abeli, zabihu za Noa, sadaka za Abrahamu, sadaka za Musa na Aroni, matoleo ya amani ya Samueli. Vivyo hivyo, kama ylivyokubali Ibada ya Mitume wako watakatifu, pokea pia, ee Bwana, ku mikono yetu ya zambi; vipaji hivi, ili, tukistahili kutumika bila lawama ku Altare yako takatifu, tupate tuzo ya wasimamizi waamini na wenye hekima siku ya ajabu ya Hukumu yako ya haki.

*Shemasi ataendelea kusema:*

Siku hii yote iwe kamili, takatifu, tulivu na bila zambi, tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji watajibu kisha kila ombi ya Shemasi hivi:* Utupe, ee Bwana.

Malaika wa amani, Mwongozi ya kweli, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu, tuombe kwa Bwana.

Vilivyo vyema na vinavyofaa ku roho zetu na amani ya dunia yote, tuombe kwa Bwana.

Kumaliza maisha yetu yanayobaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Mwisho wa maisha yetu uwe kikristu, bila maumivu, bila aibu, wa amani, tnea tuone neno njema mbele ya kiti chake cha kuogopa, tuombe cha Kristu.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa mbarikiwa kushinda, Malkia wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na Watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Padri atapaza sauti:*

**PADRI***:* Kwa huruma ya Mwana wako wa pekee ambaye umehimidiwa pamoja naye, na Roho yako Mtakatifu kamili, mwema na mpaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Tupendane sisi kwa sisi, ili kwa nia moja tuungame.

**WAIMBAJI***:* Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Utatu wa asili moja na usiyotengana.

*Padri atainama mara tatu atabusu Sahani, Kikombe na Meza takatifu, akisema kwa siri:*

**PADRI** *(kwa siri):* Nitakupenda, ee Bwana, nguvu yangu; Bwana ni imara yangu msaada wangu, kimbilio changu na Mwokozi wangu. *(mara tatu).*

*Shemasi atapaza sauti:*

Milango, Milango tusikilize kwa hekima.

*Padri atakamata Aera ataitikisa juu ya vipaji Vitakatifu akisema kwa siri Simvolo(Fundisho) ya Imani.*

*Waaminifu na waimbaji wanasema pamoja Simvolo ya Imani.*

**N**asadiki Mungu mmoja Baba mwenyezi, mwumba wa mbingu na wa dunia, hata vyote vilivyoonekana na visivyoonekana, tena Bwana mmoja Yesu Kristu. Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa na Baba mbele ya wakati wowote. Nuru toka Nuru. Mungu ukweli toka Mungu ukweli, aliyezaliwa, si umbwa mwenye asili moja (omousion) na Baba, aliye kwake vyotevilifanywa, aliye kwa ajili yetu wanadamu na ya wokovu wetu alishuka mbinguni, akapata mwili kwa Roho Mtakatifu na kwa Bikira Maria, na akawa mtu. Aliye sulibiwa kwa ajili yetu wakati wa Pontio Pilato. Akateswa, akawekwa kaburini, Na aliyefufuka katika siku ya tatu, kama ya navyo maandiko. Na akapanda mbinguni ndipo anapokaa kuume kwa Baba. Na atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio na hai na waliokufa. Ufalme wake utakuwa bila mwisho. Tena Roho Mtakatifu yu Bwana yu Mwumba hai, aliyetoka na Baba, aliyesujudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii, kwa Eklezia moja Takatifu, Katholiki na Apostoliki. Naungama kwa ubatizo moja kwa maondoleo ya zambi. Natumaini ufufuo wa wafu hata uzima wa milele utakapokuja. Amina.

*Shemasi atapaza sauti:*

**SHEMASI***:* Tusimame vizuri! Tusimame na woga! Tusikilize kwa kutolea sadaka takatifu kwa amani.

**WAIMBAJI***:* Huruma ya amani, zabihu ya sifa.

**PADRI***:* Neema ya Bwana wetu Yesu kristu, na mapendo ya Mungu, na Baba na ushirika wa Roho Mtakatifu, uwe nanyi nyote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

*Padri atainua mikono na atasema:* Tuweke mioyo juu.

**WAIMBAJI***:* Tunayo kwa Bwana.

*Padri atageuka ku Altare, akisema:* Tumsukuru Bwana.

**WAIMBAJI***:* Ni wajibu na haki.

*Padri atasali kwa siri sala ya matoleo:*

Ee Rabi, Bwana, Mungu, Baba Mwenyezi na mwabudiwa, Wewe uliye uzima, kweli nyafaa na ni haki kukutukuza ku Utakatifu wako mkuu, kukuimbia, kukuhimidi, kukuhabudu, kukushukuru, kuimbia utukufu wako, peke yako Mungu kweli; na kukutolea na moyo wa sikitiko na roho ya unyenyekevu, Ibada ya roho, kwani ndiwe uliyetufanyia neema ya kujua ukweli yako. Nani anaweza kuhadisia uwezo wako? Nani anaweza kusikilizisha sifa zote zenye kukuelekea? Nani ataweza kuhadisia maajabu yote uliyofanya, ee Rabi wa vitu vyote, Bwana wa mbingu na dunia, wa viumbe vyote vyenye kuonekana na visionekana, Wewe unayekaa pa kiti cha utukufu, Wewe unayevumbua kuzimuni, Wewe uliye wa milele, msiyeonakana, msiyesikilikana, msiyehadisiwa, imara, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristu, Mungu Mkuu na Mwokozi, matumaini yetu? Ni sura ya wema wako,

Muhuri wenye kufanana nawe, unayejionyesha katika yeye, wewe Baba yake; Yeye kweli ni Neno hai, Mungu kweli, Hekima ya mbele ya nyakati, Uzima, Utakaso, Uwezo, Nuru ya kweli. katika Yeye Roho Mtakatifu amefunuliwa, Roho ya ukweli, kipaji cha upokeleo, Ahadi ya urisi utakaokuja Malimbuko ya mema ya milele, Nguvu yenye kuleta uzima, Chemchem ya utakaso, yaliposabitishwa kwa Yeye, kiumbe chote cha akili na Majeshi yote ya Wabila-mwili wanakuimbia wimbo huu wa milele, kwani wote wamekutumikia Wewe. Umetukuzwa na malaika, Malaika wakuu, Wafalme, Utawala, usultani, Majeshi na Wakheruvi wa macho mengi; ni wewe wanazunguka waserafi, mmoja wa mabawa sita, mwingine wa mabawa; wawili wao wamefunika uso wao, wawili miguu yao, wawili wameruka: Mmoja kwa mwingine na sauti yao yasiyochoka, kwa wimbo wasipo mwisho:

*Padri atapaza sauti:*

Wakiiimba, wakilia, wakipaza sauti, na kusema wimbo wa shangwe.

*Wakati wa hii tangazo ya padri, Shemasi atakamata Nyota ku mkono wa kuume atafanya alama ya msaada juu ya sahani, kila chongo ya Nyota itagusa Sahani. Ataweka Nyota juu ya Meza kisha kuikumbatia*

**WAIMBAJI***:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana Savaothi. Mbingu na inchi zimejazwa kwa utukufu wako. Hosana juu pia, mhimidiwa yeye anayekuja kwa jina la Bwana! Hosana uliye juu pia.

*Padri atasema kwa siri:*

Hata sisi pamoja nao Majeshi heri hawa, ee Rabi Mpenda-wanadamu, tunapaza sauti tukisema: Wewe ni Mtakatifu kweli, Mtakatifu kamili, utakatifu wako mkuu hauna kipimo; Wewe ni Mtakatifu katika matendo yako yote, ulifanya yote na haki kwa ajili yetu. Ulipomuumba mwanadamu kwa udongo, ulipomupa sura yako, Wewe Mungu wake, ukamuweka katika Paradizo ya furaha ukimuahidia umilele na wake, ukamuweka katika utimizo wa mapenzi yako. Lakini, alipodanganywa na nyoka na alipouawa kwa tamaa zake, akavunja amri yako Wewe Mungu wa kweli, Muumba wake, ni hapo, ee Mungu wa haki yote. Ukamufukuza Paradizoni, ukamutuma duniani yetu hii na ukamurudisha udongoni alikotoka, umamutayarishia wokovu akizaliwa mara ingine katika Kristu wako. Kwani haukukataa milele kiumbe ulichoumba kwa wema wako, na hakusahau kazi ya mikono yako, lakini ukamulinda namna yote kwa rehema yako kubwa. Ulituma Manabii, katika kila kizazi, ulifanya maajabu katika mateule waliokupendeza; Ulinena nasi kwa kinywa cha Manabii watumishi wako sababu ya kututangazia wokovu utakaokuja: Ukatupatia amri kama msaala wetu; Ukaweka Malaika kwa kutulinda. Ulipofika ukamilifu wa nyakati, ukanena nasi katika Mwana wako, katika Yeye ukafanya umilele. Ni Yeye Nuru ya utukufu wako, Muhuri wa hali yako ambaye, alipochukua kitu yote kwa neno lake ya uwezo akazania ya kama kuwa kama Wewe ni uwizi, ee Mungu Baba yake. lakini, japo Mungu ni wa milele. Akaonekana duniani na akaishi pamoja na wanadamu, akachukua mwili kwa Bikira Mtakatifu akajishusha alipotwaa hali ya mtumwa, akachukua mwilini mwake hali ya uzaifu wetu ili tufanane na utukufu wake. Lakini, wakati katika mtu zambi ilipoingia duniani, na kwa zambi lufu, Mwana wako wa pekee. Huyu aliye kifwani mwako Wewe Baba yake, Mwana wako wa pekee aliyezaliwa kwa mwanamuke Maria Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili na Bikira daima, aliyepata mwili chini ya amri, akakubali kuhukumu zambi kwa mwili wake ili wale waliokufa katika Adamu wapate uzima katika Yeye, Kristu wako. Alipokuwa mkaaji wa dunia hii, alipotupatia mafundiosho ya wokovu, alipotuondoa ku udanganyifu wa sanamu, akatuleta ku maarifa yako, ewe Mungu kweli na Baba, kisha kutununua Yeye mwenyewe kama watu, ukohani wa ufalme, kabila takatifu. Kisha kutusafisha na maji na kututakasa na Roho Mtakatifu, akajitoa mwenyewe ku lufu ambako tulifungwa tulipouzwa ku zambi. Aliposhuka kuzimuni toka msalabani kwa kutimiza yote kwa yeye mwenyewe, akavunja woga wa lufu. Alipofufuka siku ya tatu, alipomfungulia mwanadamu wote njia ya Ufufuo (kwani haikuwezekana kwa Chemchem ya uzima atawaliwe na uwovu), akawa malimbuko ya wale walilala Msaliwa wa kwanza kati ya wafu, ili awe wa kwanza kwa vyote. Alipopanda mbinguni, amekaa kuume kwa Ukuu wako, juu mbinguni, huko atakaporudi kumulipa kila mmoja kadiri ya matendo yake. Akatuachia pia hii makumbusho ya mateso yake ya wokovu, makumbusho tuliotolea kama

yalivyo amri zake mwenyewe. Kwani, kama alivyokuwa tayari kwenda kwa kutaka kwake ku lufu yenye kuleta uzima na makumbusho ya milele, usiku ule alipojitoa mwenyewe kwa ajili ya uzima wa ulimwengu, akakamata mukate mikononi mwake mitakatifu na safi, akauonyesha kwako wewe Mungu Baba, akashukuru, akaubariki, akautakasa, akaumega.

Akawapa Wafwasi na Mitume wake Watakatifu, akisema:

*Padri ataonyesha mkate na mkono wa kuume akipaza sauti:*

**PADRI***:* Twaeni, kuleni, huu ni mwili wangu unaomegwa kwa ajili yenu, kwa maondoleo ya zambi.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** *(kwa siri):* Vivyo hivyo, akamata Kikombe cha matunda ya mzabibu, akachanga na maji, akashukuru, akabariki, akaitakasa.

*Padri ataonyesha Kikombe na atasema:* Akawapa Wafwasi na Mitume wake Watakatifu, akisema:

**PADRI***:* Kunyweni ninyi wote, hii ni Damu yangu ya Agano Jipya, inayomwangika kwa ajili yenu na ya wengi, kwa maondoleo ya zambi.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** *(kwa siri):* Fanyeni hii kwa kunikumbuka, kwani kila mara munapokula Mkate huu na Kunywa Kikombe hiki munatangaza kifo changu na kuungama Ufufuo wangu. Sisi pia, ee rabi, tunapokumbuka mateso yake ya wokovu, ya Msalaba wake wenye kuleta uzima, ya Maziko yake ya siku tatu, ya Ufufuo wake katika wafu, ya kupanda kwake mbinguni, ya kukaa kwake kuuma Kwako, Mungu Baba, ya kurudi kwake na utukufu na kwa ajabu.

*Padri akipakata mikono, kwa alama ya Msalaba, atakamata sahani ku mkono wa kuume na Kikombe ku mkono wa kushoto, atazipandisha akisema:*

**PADRI***:* Vilivyo vyako kutoka vilivyo vyako, tunakutolea kadiri ya vyote na kwa ajili ya vyote.

**WAIMBAJI***:* Tunakuimbia, tunakuhimidi, tunakushukuru, ee Bwana, na tunakuomba, ee Mungu wetu.

*Padri na Shemasi watapiga magoti mara tatu wakisema:*

Ee Mungu, uwe Mwema na unihurumie mimi mwenye zambi.

*Padri atainua mkono akisema:*

**PADRI**: Ee Bwana, pa saa ya tatu ukawashusia Mitume wako Roho yako Mtakatifu kamili, usituondoleeyo, lakini katika wema wako utufanye wapya sisi tunaokuomba.

SHEMASI: Ee Mungu, umba moyo safi ndani yangu, tengeneza roho imara kifwani mwangu.

*Watapiga magoti mara moja. Padri atasema tena mara ya pili:*

**PADRI**: Ee Bwana, pa saa ya tatu ukawashusia Mitume wako Roho yako Mtakatifu kamili, usituondoleeyo, lakini katika wema wako utufanye wapya sisi tunaokuomba.

SHEMASI: Usinitupe mbali ya Uso wako, usiniondolee Roho yako Mtakatifu.

**PADRI**: Ee Bwana, pa saa ya tatu ukawashusia Mitume wako Roho yako Mtakatifu kamili, usituondoleeyo, lakini katika wema wako utufanye wapya sisi tunaokuomba.

*Watapiga magoti. Padri ataendelesha sala ya matoleo:*

**PADRI**: Ndiyo maana, ee Rabi Mtakatifu kamili, sisi pia watumishi wako wasiostahili, sisi tuliostahili kutumikia ku Altare yako takatifu, si kwa ajili ya matendo yetu, maana hatukufanya kitu nzuri duniani, lakini kwa huruma na rehema unayutumwangia sisi tunaojongea na matumaini ku Altare yako takatifu, na tunapokutolea Mifano ya Mwili na Damu Takatifu ya Kristu wako, tunakuomba na kukusihi, Mtakatifu wa Wataaktifu, kwa mapendo yako kubwa: Ututumie sisi na juu ya Vipaji hivi Roho yako Mtakatifu ili avibariki, abitakase na aufanye.

*Shemasi atainamisha kichwa, ataonyesha mkate takatifu na Orarion yake. Padri ataubariki Mkate takatifu akisema:*

**PADRI**: Mukate huu kuwa Mwili Mheshimiwa wa Bwana, Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu.

**SHEMASI:** Amina.

*Shemasi atainamisha kichwa, ataonyesha Kikombe takatifu na Orarion yake. Padri ataibarikiKikombe akisema:*

**PADRI**: Na Kikombe hiki kuwa Damu heshimiwa yenyewe ya Bwana, Mungu na Mwokozi wetu yesu Kristu.

**SHEMASI:** Amina.

**PADRI**: Iliyomwangika kwa ajili ya uzima wa dunia.

**SHEMASI**: Amina, amina, amina.

*Padri ataendelea:*

**PADRI**: Na sisi wote tunaosharikia ku Mkate huu Moja na ku Kikombe hiki Moja ituunganishe katika Muungano wa Roho Moja Mtakatifu na ifanye ili mtu hata mmoja kati yake asishariki ku Mwili Takatifu na ku Damu takatifu ya Kristu wako juu ya hukumu yake, lakini ili tupate huruma na neema pamoja na watakatifu wote waliokupendeza tangu mwanzo wa nyakati: Ma babu, wapatriarche, Manabii, Mitume, Wahubiri, Waevangelizaji, Mashahidi, Waungamizi, Waalimu na roho zote za haki zilizokufa katika imani.

*Padri atafukiza vipaji viheshimiwa, atapaza sauti:*

Hasa Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Malkia wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Maria Bikira daima.

*Shemasi anafukiza pembeni Meza Takatifu na kukumbuka kwa siri, ma jina ya ndugu zake waorthodoksi, walikufa ao wanazima.*

*Waimbaji wanaimba Wimbo (Megalinarion) ya Mzazi-Mungu.*

**WAIMBAJI***:* Ewe Mujaliwa neema wewe Kiumbe yote, Majeshi ya malaika na wanadamu wanafurahi. Wewe ni hekalu lenye kutakaswa, Paradizo ya roho, utukufu wa mabikira; ni kwako Mungu alipata mwili na akawa Mtoto mchanga, yeye Mungu wetu wa milele. Akaweka kiti chake tumboni mwako na akafanya Mwili wako kuwa pana kuliko mbingu. Ewe Mjaliwa neema, katika Wewe kiumbe yote inafurahiwa. Utukufu Kwako.

*Wakati wa wimbo huu Padri atasema hii sala:*

**PADRI***:* Na Yoane Mtakatifu, Mbatizaji, Nabii na Mtangulizi; ya Mitume Watakatifu, Watukufu na Wasafiwa kamili; ya. . . (jina la Mtakatifu wa siku) tunayemukumbuka hata Watakatifu wako wote. Kwa maombi yao, ee Mungu, utulinde.

Na ukumbuke, ee Bwana, wote hawa walilala katika matumaini ya ufufuo wa uzima wa milele *(hapa padri atawataja wafu),* ma uwapumuzishe pahali pa mwangaza wa nuru ya Uso wako.

Tena tunakuomba: Ukumbuke, ee Bwana, Aklezya yako Takatifu, Katholiki (wa dunia mzima) na Apostoliki (wa Mitume) inayotawanyika duniani kote. Leta amani kwa hii uliopata kwa Damu Heshimiwa ya Kristu wako. Sabirisha pia nyumba hii takaitfy mpaka mwisho wa nyakati.

Uwakumbuke, ee Bwana, wale wanaokutolea matunda na wenye kutenda mema katika Maeklezya yako takatifu pia na wale wenye kuwatendea maskini mema. Uwarudishie Neema zako kubwa za mbinguni; uwape mema ya mbinguni pahali pa mema ya dunia, mema ya milele pahali pa mema ya wakati, mema isiyoweza kupevusha pahali pa mema ya uovu.

Uwakumbuke, ee Bwana, wale walio jangwani, milimani na walio mbali.

Uwakumbuke, ee Bwana, wale wanaoishi katika ubikira, ibada, utawa na uwaminifu.

Uwakumbuke, ee Bwana, watawala wetu yliyopatia utawala wa dunia; uwatuze na ukweli na wema, funika kichwa yao siku ya vita, zidisha nguvu ya mkono yao, inua mkono wao wa kuume, sabitisha utawala wao, weka chini yao wale wote wanaotaka vita, uwape amani ya ndani isiyoweza kupotea, sikilizisha moyoni mwao mashauri mema kwa ajili ya Aklezya yako ya watu wako ili watuimarishe katika amani, tuishi katika ibada na utakatifu.

Uwakumbuke, ee Bwana, Wakubwa wote na mamlaka yote, ndugu zetu walio katika serkali na askari jeshi; sabitisha watu wema katika wema wako, watu wabaya katika fazili yako.

Uwakumbuke, ee Bwana, watu hawa wanaotuzunguka hana na wale hawapo juu ya kisha ya kweli; uwahurumie na sisi pia kadiri ya wingi wa mapendo yako; jaza hazina zao na mema yote, linda umoja wao katika amani na mapatano, lea watoto wao na adibisha vijana wao; leta nguvu ku uzee, subutisha wenye woga, kusanya wenye kutawanyika, rudisha wenye kupotea na uwaunganishe ku Eklezya yako Takatifu katholiki (wa dunia muzima) na Apostoliki (wa Mitume), okoa wale wanaolemezwa na pepo wachafu, safiri na wasafiri baharini, hewani na inchini kavu, uwe Mlinzi wa wajane, uwe ngao wa mayatima, opoa wagonjwa; uwakumbuke, ee Mungu, wale wote wanaohukumiwa, wanaokimbilia katika inchi ya ugeni, wanaoteseka kwa huzuni, uhitaji na hatari na wale wote wanaoitaji rehema yako kubwa, wale wenye kutupenda na wale wenye kutuchukiwa, wale waliotuomba sisi tusiostahili kuwaombea, na watu wako wote. Uwakumbuke wote, ee Bwana Mungu wetu, na uwamwangie wote huruma yako kubwa, ukiwapa wote, maombi wanaofanya kwa ajili ya wokovu wao. Kama kwa kutokujua wala kusahau ya majina mengi hatukuweza kuwakumbuka wengine uwakumbuke wewe Mwenyewe, ee Mungu, Wewe mwenye kujua miaka ya kila mmoja na jina lake, wewe mwenye kujua kila mutu tangu tumboni mwa mama yake. Kwani, ee Bwana, wewe ni msaada wa wale wasiyo na msaada, Matumaini ya wenye kukata matumaini, Mwokozi wa wale walio katika tufani, bandari ya wasafiri, Mganga wa wagonjwa. Uwe wewe mwenyewe wote kwa ajili ya wote, Wewe mwenye kujua kila mmoja na maombi yake, jamaa yake na mahitaji yake. Kinga, ee Bwana, muji huu, muji wote na inchi yote ku njaa, magonjwa, mtetemeko wa dunia, mafuriko ya maji, moto, ushambulio wa wageni na ku vita kati ya wa kaaji wa inchi moja.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Ee Bwana, ya kwanza umkumbuke Mwarkiaskofu wetu *(jina lake),* umlinde katika Eklezia yako Takatifu ili aishi miaka mengi mu amani uzima, mheshimiwa, mwenye afya aeneze imara neno wako la ukweli.

*Shemasi katika Mlango Bora atasoma Daftari akipaza sauti:*

**SHEMASI***:* Hata wale walio ndani ya akili ya kila mmoja; tena wanaume na wanawake wote.

**WAIMBAJI***:* Na wanaume na wanawake wote.

**PADRI** *(kwa siri):* Ukumbuke, ee Bwana, Waarkiepiskopo, Waorthodoksi wote unaoenezea na imani neno la ukweli wako. Ukumbuke, ee Bwana, kutostahili kwangu kadiri ya rehema yako kubwa. Unihurumie kwa kosa yote ya kutaka na yasiyokutaka, na kwa sababu ya zambi zangu; usitenge mbali na vipaji hivi Neema ya Roho yako Mtakatifu. Ukumbuke, ee Bwana, ukasisi na ushemasi uheshimiwa katika Kristu; usikatae hata mmoja kati yetu tunaozunguka Altare yako Takatifu. Utulinde, ee Bwana, katika wema wako. Onekana kwa sisi katika rehema yako kubwa. Utupe wakati wa utulivu na wa kufaa, leta ku udongo mvua ya lazima juu ya ustawi wake mingi, na katika wema wako, bariki nyakati za mwaka huu. Kwa uwezo wa Roho yako Mtakatifu achisha magawanyiko ya Maeklezya zimisha majivuno ya mataifa, ujiharikishe kumaliza maasia ya fitina ya dini. Utupokee katika Ufalme wako kisha kutufanya waana wa nuru, waana wa Jua; Utupe amani yako na mapendo yako, ee Bwana Mungu wetu; kwani ni Wewe uliyetupatia vyote.

Na utupe tutukuze na tuimbe kwa sauti moja na moyo Jina lako heshimiwa na karimu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Padri akibariki Waaminifu atasema:*

**PADRI***:* Rehema za Mungu wetu mkubwa na Mwokozi Yesu Kristu, jitakuwa pamoja nanyi nyote.

**WAIMBAJI***:* Hata na roho yako.

*Shemasi atatoka inje ya Patakatifu, ataenda pa fasi yake ya kuwaida atapaza sauti akisema:*

**SHEMASI***:* Tukiwakumbuka watakatifu wote, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

*Waimbaji kwa kila ombi watajibu:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya vipaji viheshimiwa vilivyotolewa na kutakaswa tumwombe Bwana.

Ili Mungu wetu, Mpenda-wanadamu, aliyevipokea katika Altare yake Takatifu, ya mbinguni na isiyoonekana, kama manukato ya harufu ya kiroho, aturudishie neema, kimungu na zawadi ya Roho Mtakatifu, tumwombe Bwana.

Kwa ajili ya kuokolewa na kila sikitiko, uadui, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.

*Katika hii wakati padri atasema kwa siri hii sala ifwatayo:*

**PADRI***:* Ee Mungu wetu. Mungu wa wokovu wetu, utufundishe kukushukuru na heshima kwa ajili ya mema uliyotupatia na unayotupatia tena. Ee Mungu wetu, wewe uliyepokea Vipaji hivi, ututakase ku uchafu wote wa mwili na wa roho, na utufundishe kuishi na utakatifu katika woga wako ili tukipokea na ushuhuda wa zamiri safi sehemu yetu ya Vipaji vilivyotakaswa, tuungane na Mwili takatifu na Damu Takatifu ya Kristu wako, na kisha kuvipokea na heshima, tuwe na Kristu mioyoni mwetu tena tuwe Hekalu la Roho yako Mtakatifu. Ndiyo, ee Mungu wetu, usihukumu hata mmoja wetu sababu ya Fumbo hizi zajabu na za mbinguni, wala usiregeze roho na mwili sababu ya kuyashariki bila kustahili. Lakini utupe, mpaka mwisho wa pumuzi yetu, kupokea na heshima sehemu yetu ya Vipaji vyako takatifu kama komonyo kwa ajili ya uzima wa milele na ulinzi mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu wako, tuwe nasi pia pamoja na watakatifu wote waliokupendeza tangu mwanzo wa nyakati, washariki ku mema yako ya milele uliyowatayarishia wenye kukupenda, ee Bwana.

*Shemasi ataendelea akisema:*

**SHEMASI***:* Siku yote iwe kamili, takatifu, tulivu na bila zambi tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji kisha kila ombi watajibu:* Utupe, ee Bwana. .

Malaika wa amani, Mwongozi ya kweli, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na makosa yetu, tuombe kwa Bwana.

Vilivyo vyema na vinavyofaa kwa roho zetu na amani ya dunia yote, tuombe kwa Bwana.

Kumaliza maisha yetu yanayobaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Mwisho wa maisha yetu uwe kikristu, bila maumivu, bila aibu, wa amani, tena tuone neno njema mbele ya kiti chake cha kuogopa tombe kwa Kristu.

Tukiomba umoja wa imani, na ushirika wa Roho Mtakatifu sisi na kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Na utustahilishe, ee Rabi, kusubutu na matumaini na bila hukumu, kukuita Baba, wewe Mungu wa mbinguni, na kusema;

*Waaminifu, Waimbaji na wasomaji watasema pamoja sala ya Rabi:*

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

**PADRI***:* Kwa kuwa na ufalme, na uwezo, na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakaitfu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI** *(kwa siri):* Ee Rabi na Bwana, Baba wa huruma na Mungu wa utulizo, bariki hawa wanaoinamisha kichwa mbele yako; uwatakase, uwalinde, uwape nguvu, uwasabitishe, uwatayarishe ku tendo lote njema na uwastahilishe kushariki bila hukumu ku fumbo zako takatifu

na zenye kuleta uzima, kwa ajili ya maondoleo ya zambi zao na ya muungano wa Roho Mtakatifu.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Kwa neema, na rehema na mapendo kwa wanadamu ya Mwana wako wa pekee ambaye, umehimidiwa pamoja naye, na Roho yako Mtakatifu kamili, Mwema na mpaji uzima sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** *(kwa siri):* Usikilize, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, toka makao yako matakatifu na toka kiti cha utukufu wa Ufalme wako utujie ututakase, wewe unayekaa mbinguni pamoja na Baba, tena uliye hapa pamoja nasi bila kuonekana. Ukubali kutugawanyia ku mkono wako wa uwezo, Mwili wako Safi na Damu yako heshimiwa, na kwa mikono yetu wote.

**SHEMASI** *(na sauti nguvu):* Tusikilize.

*Padri atapandisha na mikono miwili mkate juu ya sahani akisema:*

Vitu Vitakatifu kwa watu watakatifu.

**WAIMBAJI***:* Mtakatifu ni mmoja peke yake, Bwana ni mmoja peke yake. Yesu Kristu, katika utukufu wa Mungu Baba. Amina.

*Shemasi atarudi Patakatifu na Waimbaji wataimba wimbo wa ushirika wa siku wala wa siku Kuu. Kila siku ya Mungu tunaimba:*

Msifuni Bwana kutoka mbinguni; msifuni katika pahali pa juu pia. Alliluia.

*Wakati wanaimba wimbo huu Padri na Shemasi watashiriki katika roho kadiri ya Ibada ifwatayo na yenye kufanyika kwa siri.*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, mega mkate Mtakatifu.

*Padri ataumega mkata ataweka sehemu mbalimbali pa Sahani akisema:*

Anamegwa na kugawanyika Mwana-Kondoo wa Mungu kila mara anakatwa bila kutengana; anayeliwa kila mara bila kumalizwa, lakini anawatakasa washirika wake.

*Shemasi ataonyesha Kikombe na Orario yake akisema:*

Ee Rabi, jaza Kikombe Kitakatifu.

*Padri atakamata sehemu ya Mwili Mtakatifu iliyo na alama IC ataiweka mu Kikombe akisema.*

Kujazwa kwa Kikombe, kwa imani na Roho Mtakatifu.

**SHEMASI***:* Amina.

*Kisha Shemasi atakamata chombo chenye maji ya moto (Zeon), ataipeleka kwa padri akisema:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, bariki maji ya moto.

*Padri anapobariki maji ya moto atasema:*

Ubarikiwa umoto wa Watakatifu wako, daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Hapo Padri na Shemasi watasema sala za Komonyo Takatifu.*

Nasadiki, ee Bwana, na kuungama ya kama kweli Wewe Kristu, Mwana wa Mungu mzima, uliyekuja duniani kwa ajili ya kuokoa wenye zambi, ambao mimi ni wa kwanza. Nasadiki tena ya kama huu ni Mwili wako safi na hiyi ni Damu yako heshimiwa. Nanakuomba*:* Unihurumie na kunisamehe makosa yangu yakutaka na yakutotaka, kwa maneno ao kwa matendo, yakuja wala yakutokuja, unistahilishe kushiriki katika fumbo zako za bila doa, kwa ajili ya maondoleo ya zambi na uzima wa milele. Amina.

Angalia sasa najongea karibu ya Komonyo yako Takatifu, ee Mwumba wangu, usiniunguze ku ushariki huo. Sababu Wewe ni moto unaounguza wasiyostahili. Lakini unitakase ku aibu hiyi.

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho*:* Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Akionapo Damu Kimungu, atetemeke, ee Mwanadamu, kwa sababu ni makala ya moto ilunguzayo wasiostahilivu. Mwili Kimungu unageuzwa kimungu na unalisha, unatakasa na unalisha mawazo namna isiosikilizwa

Ee Kristu, kwa mapendo yako ulinipeleka ku furaha na kwa ulinzi wako ulinigeuza kuwa mtu mwengine*:* Choma zambi zangu kwa moto usiyo vyombo na kubali kunijaza na furaha zako, sababu nikiwa tele na furaha, nitasifu majio zako mawili, ee Wewe mjaliwa na wema.

Nitaingia je, mimi msiye stahili, katika ukuu wa watakatifu wako? Nikisubutu kwingia katika nyumba ya arusi, nguo langu litanitoa, maana hayuko ya arusi na nikifwatane, malaika watanifukuza. Bwana, safisha basi mataka ya moyo wangu na uniokoe, wewe mpenda wanadamu.

*Na pia Sala hii:*

Rabi, rafiki ya wanadamu, Bwana Yesu Kristu, Mungu wangu, vipaji vyako vitakatifu visiwe nami hukumu sababu ya maovu yangu*:* Lakini utakaso wa moyo na wa mwili na rahani ya uzima na ya ufalme wa milele. Ni vizuri kwangu kwa kumshika Mungu na kuweka tumaini la wokovu wangu katika Bwana.

*Na tena tunasoma hii:*

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako. . . .

*Padri, kwa mkono wa kushoto, atakamata sehemu moja ataiweka mu mkono wake wa kuume, akisema:*

Tazama, namjongea Kristu, Mfalme msiyekufa, Mungu wetu. Mimi (atataja jina lake) padri, napewa Mwili Mheshimiwa Mtakatifu na mwenye kuleta uzima, wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Hivi Padri anakuja Mkate Mtakatifu na woga wa Mungu na utaratibu.*

*Kisha atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Ee Shemasi, jongea.

*Shemasi atajongea akisema:*

**SHEMASI***:* Tazama, namjongea Kristu, Mfalme msiyekufa, Mungu wetu. Ee Rabi, unipe mimi *(atataja jina lake),* Shemasi, Mwili mheshimiwa Mtakatifu na mwenye kuleta uzima wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi zangu na uzima wa milele.

*Padri atamupa pa mkono wa kuume wenyi kuwekwa juu ya wa kushoto sehemu ya Mwili Mtakatifu, akisema:*

Kwa *(jina lake)*, Shemasi, anapewa Mwili wa samani, Mtakatifu na bila doa kamili wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Shemasi akipokea Mwili Mtakatifu atabusu mkono wa padri ataenda nyuma ya Meza Takatifu huko ataukula kwa utaratibu sawasawa na padri.*

*Kisha padri atakamata Kikombe Kitakatifu pamoja na kitambaa-kifuniko atasema:*

**PADRI***:* Tazama, namjongea tena Kristu Mfalme msiyekufa na Mungu wetu. Mimi (*jina lake),* mutumishi wa Mungu na padri napewa Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Na atakunwa mara moja. Kisha atapanguza midomo yake vilevile upande wa midomo ya Kikombe na atakibusu akisema.*

Hii imegusa midomo yangu; maovu yangu yataondolewa na zambi zangu zitatakaswa.

*Atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Ee Shemasi, jongea tena.

*Shemasi atajongea atapanguza kwa utaratibu mkono wake wa kuume na Musa akisema:*

Tazama, namjongea tena Kristu Mfalme msiyekufa na Mungu wetu. Ee Rabi, unipe Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Akimpa Kikombe mara moja, padri atasema:*

Mtumishi wa Mungu na Shemasi *(jina lake*), anapewa Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Kisha, wakati Shemasi atabusu midomo ya Kikombe, Padri atasema:*

Hii imegusa midomo yako, maovu yako yataondolewa, na zambi zako zitatakaswa.

*Kisha, Shemasi atakamata Sahani juu ya Kikombe ataweka sehemu katika Kikombe akipanguza vizuri Sahani na Musa (Yoga ya bahari). Anapofanya hivi, atasema:*

Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye peke yake bila zambi. Tunausujudu msalaba wako, ee Kristu, tena tunausifu na kuutukuza ufufuo wako takatifu. Kwa kuwa wewe Mungu wetu, la wewe peke yako hatumjui mwengine, jina lako tunaliita. Njoni enyi waaminifu wote, tuusujudu ufufuo takatifu wa Kristu. Kwa kuwa. je! Kwa ajili ya msalaba umefika furaha katika dunia mzima. Tukimhimidi Bwana daima, tunasifu ufufuo wako; kwa sababu akiuvumilia masalaba kwa ajili yetu, aliangamiza kifo kwa kifo chake.

*Padri ataweka mu Kikombe Kitakatifu vipande vyote ya Mkate ya wale watu waliokuta ao wanaoishi akisema:*

Ee Bwana, kwa Damu yako takatifu na kwa maombi ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu wako wote, zima zambi za hawa waliokumbushwa hapa. Amina.

*Kisha, atafunika Kikombe na Kitambaa (Kalimata). Kun mwisho ya wimbo wa Ushirika (Kinonikon), Shemasi atapokea Kikombe ku mikono ya padri na kukionyesha kwa watu, atapaza sauti akisema.*

Kwa woga wa Mungu, na imani, na mapendo, gongeeni.

*Padri atakamata Kikombe na akimupa kila Mwaminifu Komonyo, atasema:*

Mtumishi wa Mungu *(jina lake)* anapewa Mwili na Damu heshimiwa na takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu kwa maondoleo ya zambi zake na uzima wa milele. Amina.

*Wakati huu wa Kukomunika watu, waimbaji wataimba wimbo hii:*

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho*:* Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

*Kisha Komonyo ya Waaminifu Padri atawabariki watu na Kikombe Kitakatifu akipaza sauti:*

Ee Mungu, okoa taifa yako na bariki uriti wako.

**WAIMBAJI***:* Tumeona nuru wa kweli, tumepokea Roho wa mbinguni, tumepata imani ya kweli, tukiusujudu Utatu usiotengwa, kwani Huu umetuokoa.

*Padri ataweka Kikombe Kitakatifu juu ya Meza takatifu, atafukiza akisema kwa siri.*

Ee Mungu, utukuzwe juu mbinguni na utukufu wako uwe duniani yote.

*Hapo, padri atampa Shemasi Sahani, huyu atageuka ku upande wa watu kisha ataenda ku Meza ya Matayarisho (Prothesis), ataiweka huko. Padri mwenyewe atakamata Kikombe Kitakatifu atasema kwa siri.*

**PADRI***:* Ahimidiwe Mungu wetu.

*Kisha Padri atapinduka kwa watu, atawaonyesha Kikombe Kitakatifu akipaza sauti:*

Daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Shemasi atatoka pa fasi yake ya kuwaida na atapaza sauti:*

Simameni. Tukishiriki Fumbo za ajabu za Kristu, Fumbo za umungu, takatifu bila doa, za kutokufa, za mbinguni na zenyi kuleta uzima, tumshukuru Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie na utulinda, ee Mungu kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Tukimaliza kuomba siku hii yote iwe kamilifu, takatifu, tulivu na bila zambi; sisi na kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

*Na atarudi Patakatifu.*

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya Shukrani.*

**PADRI:** Tunakushukuru, ee Bwana Mungu wetum, sababu ya ushariki huu ku Fumbo zako takatifu, safi, za milele na za mbinguni ulizotupatia kwa ajili ya mema, utakaso na uponyesho wa roho zetu na wa miili yetu. Wewe, ee Rabi wa vitu vyote, fanya ili Ushirika ku Mwili takatifu na ku Damu takatifu ya Kristu wako uwe ndani yetu imani yasiyo haya, mapendo yasipo mzunguko. ukamilifu wa hekima, uponyesho wa roho yetu na wa mwili wetu, ushindi juu ya adui wote, utimizo wa amri zako na ulinzi wa nguvu mbele ya kiti cha uhkumu cha Kristu wako.

*Kisha kukunja Antiminsion, Padri atafanya alama ya Msalaba, na Evangelion juu ya Meza akipaza sauti:*

Kwa kuwa wewe ni utakaso wetu na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha Padri ataweka Evangelion juu ya Antiminsion.*

**WAIMBAJI**: Amina.

*Padri atageuka ku upande wa watu, atapaza sauti akisema:*

Twendeni na amani.

**WAIMBAJI***:* Kwa jina la Bwana.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia *(mara tatu)*, ee Rabi mtakatifu barikia.

*Padri atatoka inje ya Mlango Bora, atasimama mbele ya Ikone ya Kristu na atapaza sauti akisema:*

Ee Bwana, unayewabariki wale wanaokuhimidi na kuwatakasas wale wanaokutumainia, okoa taifa wako na bariki uriti wako. Ulinde Waaminifu wa Eklezia yako, uwatakase wale wanaopenda uzuri wa nyumba yako; uwarudishe utukufu kwa uwezo wako wa umungu. Usituache sisi tunaokutumainia. Uipatie dunia yako amani, ma Eklezia yako, mapadri, wakubwa wa inchi wetu na watu wako wote. Kwani kila neema na kila kipaji kamilifu kinatoka Kwako juu, uliye Baba wa nuru. Tunakushukuru na kukuabudu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Kisha waimbaji wataimba:*

Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa, na mupaka milele. *(mara tatu).*

*Padri ataenda ku Meza ya Matayarisho na atasoma kwa siri hii sala ifwatayo:*

Tazama, ee Kristu Mungu wetu, tumetimiza na kumaliza kama ulivyoweza, Fumbo ya Mapendo yako. Tulikumbuka Kifo chako, tumeona mfano wa Ufufuo wako,, tumejazwa na uzima wa milele, tumepata heri isiyomalizika ambayo tunakuomba utustahilishe wote, katika wakati utakaokuja, kama tulivyo, kwa neema ya baba yako wa milele na ya Roho Mtakatifu, mwema na Mletaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI:** Bwana hurumia.

*Padri ao Askofu atawabariki Waaminifu hivi:*

Baraka ya Bwana na huruma yake iwe nanyi, kwa neema yake na mapendo yake kwa ajili ya wanadamu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu, matumaini yetu, utukufu kwako.

**MSOMAJI***:* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milelena milele. Amina. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia, ee Padri mtakatifu barikia.

*Padri atapinduka ku upande wa Waaminifu, atafanya Kuaga hivi:*

**PADRI:** Aliyefufuka katika wafu, *(kama ni Siku ya Mungu)* Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mama yake Mtakatifu asiye na doa, kwa nguvu na msaada mheshimiwa na wenyi kuleta uzima, kwa ulinzi wa majeshi maheshimiwa ya mbinguni yasiyo na mwili, kwa maombezi ya Yoane, Nabii Mtangulizi na Mbatizaji, mheshimiwa na mtukufu, ya Mitume Watakatifu, watukufu na waifiwa, *(ya Mtakatifu wa Kanisa kama ni Nabi, Mtume, wala askofu),* ya Mashahidi Watakatifu, watukufu na wasindaji, *(ya Mtakatifu wa Kanisa kama ni Shahidi),* ya wababa wetu Watakatifu na wabebaji-Mungu, *(ya Mtakatifu wa Kanisa kama ni Mtawa),* ya Baba wetu Mtakatifu Yoane Krisostomo, Mwarkiaskofu wa Kontantinopoli, ya YOakimu na Anna, Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki, ya Mtakatifu wa hii siku *(jina yake)* tunayekumbuka leo, na ya Watakatifu wote, atuhurumie na kutuokoa, kwani Yeye ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu na Mrahimu.

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

*Kama ni Askofu Padri atasema hivi:* Kwa maombezi ya Askofu wetu Mtakatifu, ee Bwana Yesu Kristu. . .

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri atawabariki waaminifu akisema:*

Utatu Mtakatifu uwalinde ninyi wote.

**WAIMBAJI***:* Anayetubariki na kututakasa, ee Bwana, umlinde miaka mengi.

*Kama Liturgia anafanya Askofu waimbaji wataimba hivi:*

Ee Bwana, umulinde Rabi na Askofu wetu, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi.

*Kisha Askofu ao Padri atagawanya mkate wenyi kubarikiwa uitwao Antidoron akisema kwa kila mwaminifu.*

Baraka ya Mungu na huruma yake iwe nawe.

# LITURGIA KIMUGU YA WENYE KUTAKASWA (PROIGISMENI)

*Liturgia Takatifu ya Proigiasmeni inafanyika:*

*-Kila siku ya Mu kazi Tatu na Mu Kazi Tano ya Kwarezima Mkubwa ya Paska.*

*-Mu Kazi Inne ya Juma ya Tano ya Kwarezima ya Kanuni Mkubwa.*

*-Mu Kazi Moja, Mu Kazi Mbili na Mu Kazi Tatu ya Juma Mkubwa na Takatifu.*

*-Siku Kuu ya Washahidi Wakubwa Makumi Inne (Tarehe 9 Martie).*

*-Mpaka ku Siku Kuu zingine, kama zikiangukia mu siku ya kwanza ya Kwarezima kufika mu kazi Tano mkubwa.*

*-Ku Siku Kuu ya kutangaza Habari Njema ya Maria ikiangukia mu siku yoyote wanafanya Liturgia Takatifu ya Mt. Yoane Krosostomo.*

*Kila mara Liturgia Takatifu ya Proigiasmeni inafanyika kisha Saa ya Tisa pamoja na Esperinow. (Kutoka minuit ya jana usiku kufika saa ya Proigiasmeni Padri anamupashwa kufunga pasipo kula ao kunywa). Siku zote ni Padri anaiganya yeye mwenyewe hii Liturgia. Pamoja na Shemasi anaifanya kama iko siku mkubwa ya Mtakatifu ao Juma Mkubwa kwa sababu hii wakati tunasoma Evangelio.*

*Ndani ya Kanisa apana kuwakisha moto mingi, nguo ya Kanisa iko sawa ya kilio. Sauti ya Waimbaji ya pole-pole na chini. Kwa hii sala kusoma na mingi lakini kuimba ni kidogo.*

### *IBADA YA KEROS YA KUFANYA LITURGIA PROIGIASMENI*

*Wakati Waimbaji wataimba wimbo wa Heri ya Saa Tisa, Padri atakamata Keros sawa siku zote, lakini hii wakati atasimama mbele ya mlango Bora ao wakati anabusu ikona hatasema sala ingine ya Keros. Atasema mpaka mara nyingi: «***Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe».**

*Kama wanaingia ndani ya ALtare takatifu, watabusu Meza Takatifu na watavaa ma nguo yao bila kuvaa Msalaba ao Epigonation.*

*Padri atatia muhuri na kubusu paka amfia Takatifu yake, hatasema kitu kingine paka* **«Tumwombe Bwana» ao «Kwa maombezi. . . . »** *na Shemasi atasema pamoja wakati anavaa ma nguo yake. Kama hii siku iko na Arkiaskofu ndani ya kanisa, atakaa pa Kiti yake pasipo Mandia. Atavaa mpaka Epanokalimafko na Egolpio na atakamata na Bakora ku mkono yake.*

*Inawezekana kufanika Liturgia na Askofu pamoja, ambayo Arkiaskofu atafanya akivaa Amfia (Ma nguo takatifu) yake yasipo pambo na pasipo mitra (Kofya) na Omoforio mkubwa. Inawezekana kama kuiko lazima kufanika upadirisho mpaka wa shemasi, kisha Kuingia Mkubwa. Na wanapadirisha hata washemasi wadogo kisha mwisho wa Saa Tisa na mbele ya Esperinow kwa Arkiaskofu mwenye kuvaa Epitrakilio na Omoforio kidogo.*

### *KIPANDE YA MATAYARISHO*

*Ni vizuri Liturgia takatifu ya Proigiasmen ifanyiwe ku ile masiku tulisema ku mwanzo, ku Proskomidi ya siku ya Mungu ao siku ya Posho, sawa vile Padri atatia muhuri, kukata, kuweka na atatwaga mkate ya ile siku ya Liturgia, atatia muhuri na kukata mikate ingine wingi wa Liturgia ya Proigiasmeni watakayofanya mu masiku za juma na kusema kwa kila mumoja: «***Kwa makumbusho ya Bwana».** *na ifwatayo:*

**«Sawa Kondoo anapelekwa kuchinjwa» na**

**«Kondoo wa Mungu anatolewa» na:**

**«alitwangiwa mkuki ku ubavu kwa askari***» na ataweka vipande vya Amnos yulu ya Sahani. Kisha ataweka ndani ya Kiombe takatifu vinyo na maji na kusema: «***Ubarikiwe mchanganyiko. . .**

**»** *tena ataendelesha mpaka mwisho wa Proskomidi. Kwa kwendelea watafanya Liturgia Takatifu ya Mta. Bazili Mkubwa ao ya Mt. Yoane Krosostomo sawa zoezo.*

*Katika Liturgia wakati wa mchanganyiko wa vitu Vitakatifu, atasema:* **Ufanye mkate huu»** *(Tunaita mkate apana mikate kwani Mwili wa Kristu ni Moja tu hata unaona vipande viwili ao vitatu). Wakati itakuwa lazima kwa kuinyanyua katikati ya Liturgia, atanyanyua yote Amnos pamoja, na atavunja vipande inne vua mwili wa kwanza (ingine mwili wa Proigiasmeni itabakia mzima). Kisha atakamata moja ya vipande hivi inne yulu yake panaandikwa YESU ataweka ndani ya Kikombe Takatifu na ataongeza maji ya Zeon (moto). Kisha atakamata lavida takatifu (lupau)) ku mkono wa kuume na ku mkono wa kushoto atakamata yulu ya Musa (Yoga ya bahari) mkate takatifu moja na ataimwangia ku lavida (Lupau) Damu Takatifu yulu ya Mwili takatifu kwa alama ya msalaba.*

*Mwisho ya Liturgia inapaswa kukausha hii mwili ndani ya Sahani takatifu moja karibu ya babula. Kisha ataweka ndani ya Artoforion ya Proigiasmeni na ataichunga yulu ya Meza Takatifu na hii siku Mwili iko yulu ya Meza Kandili ya kuwaka saa yote.*

*Hakuna namna kufanya Liturgia na kipande moja ya Mwili Takatifu, inapaswa yote ine mzima. Inapaswa padri kujua ya kama hakuna namna yakutosha Mwili Takatifu ya Proigiasmeni ya Kanisa moja kupeleka na kufanya nayo Liturgia ku Kanisa ingine.*

## SALA YA MANGARIBI PAMOJA NA LITURGIA YA WENYE KUTAKASWA

*Elezo: Padri na Shemasi watasimama mbele ya Meza takatifu, watapiga magoti mara tatu na watasema:* **«Mungu uniwe na unihurumie mimi mtu mwenye zambi».** *Shemasi atabusu Meza Takatifu na mkono wa kuume ya padri, ksiha atatokea ku mlango kaskazini na atasimama katikati ta mlango Bora. Atasujudu ku kiti cha Arkiaskofu, atakamata Orarion na vidole tatu na atasema:*

**SHEMASI***:* Ee Rabi, himidi.

*Elezo: Hii wakati Padri atafanya metania tatu (Kupiga magoti), atabusu Evangelio Takatifu, ataikamata ku mikono wake na atainyangula, na kisha «***Ee Rabi, himidi»,** *ya Shemasi, atabariki Antiminsion mu alama ya Msalaba, atasema:*

**PADRI***:* Uhimidiwe ufalme wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele

*Elezo: Wakati Msomaji anasoma kipande cha kwanza cha Kathisma 18, Padri atakamata Evangelio atafanya alama ya Msalaba yulu ya Andiminsion, kisha ataweka Evangelion mbele ya Artoforio mukongo ya Evangelio itangalia ku mangaribi, kisha atafungua Antiminsion na atasoma sala ya Antifonon wa kwanza:*

SALA I

Ee Bwana mwenyi huruma, aendaye polepole kwa hasira na mwenye tele na huruma, usikie ombi letu, sikiliza sauti ya maombi yetu. Utufanyizie kuwa alama ya wema; utuongoze katika njia zako, ili tutembee katika wema wako; Furahisha moyo wetu katika woga wa jina lako takatifu, kwani u Mkuu na unafanya maajabu; u Mungu wa pekee, hakuna afananaye nawe miongoni mwa wakuwako kimungu. Ee Bwana, mwenyezi katika rehema na mwema katika uwezo kwa kusaidia kufariji na kuokoa wao ambao wanatumainia katika jina lako takatifu. Kwa kuwa kwako tunautoa utukufu wote, heshima na uabudu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA II

Ee Bwana, usituajibu katika hasira yako nyingi, usitutwalii tena katika ukali wako; lakini ututendee kadiri ya wema wako, ewe mganga na mponya wa roho zetu; utuongoze bandarini ya mapenzi yako, angaza macho ya moyo wetu ili tupate kujua ukweli wako; utupe kuisha masalio ya siku hii na ya uzima wetu, katika amani na bila zambi; kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi Mungu,

na ya watakatifu wote. Kwani kwako tunakutoa nguvu, utawala, uwezo, na utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA III

Ee Bwana Mungu wetu, utukumbuke sisi watumishi wako, watenda zambi na batilifu; tukipokumbuka jina lako takatifu, usituchanganya katika ungojezi wetu wa rehema yako; lakini utupatie, ee Bwana, wema wote tunaokuomba kwa ajili ya wokovu wetu; uturudishe kuwa wastahilivu wa kukupenda na roho yetu yote, wa kukuogopa na wa kutenda katika vyo vyote mapenzi yako. Kwani u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na tunakutukuza. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA IV

Ee Wewe unaye tukuziwa kwa nyimbo bila kuachilia na nyimbo ya utukuzo wa mfululizo, ya uwezo takatifu, ikipojazwa kinywa chetu na sifa zako, ili tuweze kutukuza jina lako takatifu, utupe sisi fungu na uriti pamoja na wao wote wanaokuogopa katika ukweli, a wanaochunga amri zako; kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi-Mungu, na ya watakatifu wote. Kwani kwako tunautoa utukufu wote, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA V

Ee Bwana, unayeshika ulimwengu mikononi mwako bila doa; u mvumilivu kwetu, na unajitesa kwa vitendo vyetu vibaya; ukumbuke huruma yako na rehema, utuangalie katika wema wako; utupe, kwa neema yako, kwa kukimbia pia, kwa wakati wa masalio ya siku hii, kwa fitina mbalimbali ya mwovu; zuia uzima wetu ku makimbilio ya mitego yoyote kwa neema ya roho yako mtakatifu unapobarikiwa naye, kama vile roho yako mtakatifu kamili. Kwa rehema na upendo kwa ajili ya wanadamu wa mwana wako wa pekee, unapobarikiwa naye, kama vile roho yako mtakatifu kamili, mwema na muletauhai, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA VI

Ee Mungu, mkuu na mwenye maajabu, unatawala na unaongoza ulimwengu na wema usiyoweza kusema na tuzo kubwa; umetupa mali ya ulimwengu huu, na ulipotuongoza kwa mali uliyotupa, unatupa rahani ya ufalme uliyotuhaidia majira ya siku hii mkosama uliyotupa, umetuepusha ubaya wo wote; utupe sisi kwa kuishi bila magombezi, katika ukuwapo wa utukufu wako takatifu, na kwa kukuimba, ewe Mungu wa pekee, mwema kamili na mpenda wanadamu. Kwani u Mungu wetu na tunakutukuza Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA VII

Ee Mungu mkuu na uliye juu, u peke uliye umilele, a unayekaa nuru kutokaribika; na hekima ukafanya kiumbe cho chote, ukatenganisha nuru na giza ukiweka jua kutawala mchana, mwezi na nyota kutawala usiku, isipokuwa zambi zetu, ukatuhukumu wastahilivu, na kusimama, wakati huu, mbele ya uso wako, wa kutangaza jina lako na kukutolea sifa ya mangaribi; ee Bwana rafiki wa watu, peleka wewe mwenyewe sala yetu kama uvumba mbele yako, na uyapokee sawa sawa manukato ya arufu nzuri. Utupe mangaribi na usiku tulivu, utuvike silaha za mwangaza; utuokoe kwa woga kubwa wa usiku na kwa werevu wo wote unaotupeleka gizani; utupe usingizi ambao ulitupatia kama pumziko kwa uregevu wetu, ukipofukuza mbali nao sura yo yote ya kishetani. Ndiyo, ee Rabi, mgawanyi wa wema yo yote, fanya, ili katika usiku huu, ukipenywa na juto la zambi kitandani mwetu, tukumbuke jina lako takatifu na tukiangaziwa kwa usimamizi wa amri zako, tukisimama, roho ikipojazwa tele na furaha, kwa kutukuza wema wako, na kutolea ku huruma yako maombi na sala zetu kwa ajili ya zambi zetu na kwa ajili ya yale ya watu wako; katika rehema yako, utulinde kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi-Mungu, Kwani u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI***:* Kwa amani, tumuombe, Bwana.

***MSOMAJI*** *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya amani kutoka juu, na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya amani ya dunia yote, ya kusimama kuzuri kwa Eklezia Takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya waKristu watawa wa Orthodoksi wote, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya Arkiepiskopu wetu. . *(jina lake)*, ya upresbyteri uheshimiwa, ushemasi katika Kristu, ya wateule wote na ya watu wote, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya mji hii na inchi hii, kila mji na inchi, na ya waaminifu ya wanaoishimo, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya kutupewa na hewa tamu, na manenevuya arzi, na nyakati za amani, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya wasafiri hewani, baharini na nchini, ya wagonjwa, ya wateswa, ya mateka, na kwa ajili ya wokovu wao, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Kwa ajili ya kutuokolewa na kila sikitiko, gazabu, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

**SHEMASI***:* Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.

**SHEMASI***:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtukufu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmojamwenye we, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.

**MSOMAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa utukufu wote ni wako, heshima na uabudu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MSOMAJI***:* Amina.

Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu na Mungu Mfalme wetu.

Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

ZABURI IO4*: Uwezo wa Bwana katika viumbe.*

Bariki Bwana, ee nafsi yangu, ee Bwana Mungu, . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Elezo: Msomaji kisha maombi ya Irinika ya Shemasi atasimama katikati ya Kanisa ataanza kusoma Kathsima 18 ya Zaburi. Kisha somo ya kipande wa kwanza, msomaji atasema:* **Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Alliluia, Utukufu kwako, ee Mungu *(mara tatu)*. Bwana hurumia *(mara tatu)*. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote, hata milele na milele**. *Asitaseme: Amina. Amina atasema wakati ataanza Kipande ya mbili ya Kathisma wa zaburi 18.*

*Shemasi atasema Ektenia Kidogo, kisha kipande ya kwanza ya Zaburi:*

**SHEMASI***:* Tena na tena kwa amani, tumwombe Bwana.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtakatifu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili nasi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.

**MSOMAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa kwako ni nguvu, utawala, uwezo na utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Elezo*: Hii saa Msomaji anasoma kipande ya kwanza ya Kathsima wa zaburi, padri anasoma Antifonon ya kwanza*

**ANTIFONON YA KWANZA**

Ee Bwana mwenyi huruma, aendaye polepole kwa hasira na mwenye tele na huruma, usikie ombi letu, sikiliza sauti ya maombi yetu. Utufanyizie kuwa alama ya wema; utuongoze katika njia zako, ili tutembee katika wema wako; Furahisha moyo wetu katika woga wa jina lako takatifu, kwani u Mkuu na unafanya maajabu; u Mungu wa pekee, hakuna afananaye nawe miongoni mwa wakuwako kimungu. Ee Bwana, mwenyezi katika rehema na mwema katika uwezo kwa kusaidia kufariji na kuokoa wao ambao wanatumainia katika jina lako takatifu. Kwa kuwa kwako tunautoa utukufu wote, heshima na uabudu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**MSOMAJI***:* Amina. *Mara moja ataanza kuendelesha ya kusoma Kipande wa mbili ya Kathisma. Shemasi Kisha somo ya kipande wa mbili atafanya ektenia kidogo:*

**SHEMASI***:* Tena na tena kwa amani, tumwombe Bwana.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtakatifu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili nasi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.

**MSOMAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa u Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu na kwako tunakutolea utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Elezo*: Hii saa Msomaji anasoma kipande ya mbili ya Kathsima wa zaburi, Padri anasoma Antifonon hii:*

**ANTIFONON YA MBILI**

Ee Bwana, usituajibu katika hasira yako nyingi, usitutwalii tena katika ukali wako; lakini ututendee kadiri ya wema wako, ewe mganga na mponya wa roho zetu; utuongoze bandarini ya mapenzi yako, angaza macho ya moyo wetu ili tupate kujua ukweli wako; utupe kuisha masalio ya siku hii na ya uzima wetu, katika amani na bila zambi; kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi Mungu, na ya watakatifu wote. Kwani kwako tunakutoa nguvu, utawala, uwezo, na utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Elezo: Wakati ataisha kusoma Msomaji Kathisma yote Shemasi atafanya Ektenia ingine Kidogo:*

**SHEMASI***:* Tena na tena kwa amani, tumwombe Bwana.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.

**MSOMAJI***:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtakatifu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili nasi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.

**MSOMAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI***:* Kwa kuwa wewe ni Mungu wetu, Mungu mwenye kurehemu na kuokoa, na kwako tunautoa utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Zaburi I4I*:*

Bwana, nimekuita, unisikilize, Unisikilize, ee Bwana. Bwana nimekuita, unisikilize; usikie sauti ya kusihi kwangu. Wakati ninapokuita, unisikilize, ee Bwana.

Maombi yangu ya elekezwe, kama uvumba mbele yako. Kunyanyua kwa mikono yangu, kama zabihu ya mangaribi, unisikilize, ee Bwana.

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Kisha Waimbaji wataimba Wimbo ya Triodio na Mineon. Kisha:* **«Utukufu kwa Baba. . . . . Sasa siku zote. . . »**

*Wakati waimbaji wanaimba «***Ututuku kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . »** *Shemasi na Padri bila Evangelio, paka na chetezo, (Evangelio shemasi atakamata, kama ni Siku Kuu mkubwa kati ya wakati ya Kwarezima), watatoka inje na mlago ya kaskazini watasimama kati ya Kanisa na Shemasi atasema na sauti chini mbele ya padri:*

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana*:*

*Hii saa padri, anasema kwa siri Sala ya Kuingia. Ni hii:*

**PADRI***:* Mangaribi, asubui na azuhuri tunakusifu, tunakubariki, tunakushukuru na tunakukililia, ee Rabi wa ulimwengu. Bwana mpenda wanadamu. Pokea sala yetu kama uvumba mbele yako, usiinamishe roho yetu kwa sauti ao kwa mawazo mabaya lakini utuokoe kwa wale wanasakaroho yetu. Kwako, ee Bwana, kunanyanyuka macho yetu; katika wewe tunatumaini, ee Mungu wetu, fanya kusudi tusichanganywi. Kwa kuwa kwako tunautoa utukufu wote, heshima na kuabudu. Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI***:* Bariki, ee Rabi kuingina huku Takatifu.

*Padri atabariki na kusema kwa sauti ya upole:*

**PADRI***:* Kubarikiwe kuingia kwa watakatifu wako, wakati wowote, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Shemasi anafukiza na kusema kwa kupaza sauti:*

**SHEMASI***:* Hekima. Tusimameni.

Mwandamano wa kwingia.

*Kisha watarudia mu Altare Takatifu, na waimbaji wataimba:* **«Mwangaza upole (ilaron). . . »**

**SHEMASI***:* Mangaribi ao Njioni.

*Msomaji anasoma Somo ya Kitabu ya Mwanzo ya Biblia Takatifu.*

**SHEMASI:** *Hekima. Tusikilize.*

*Ku mwisho ya hii somo, Msomaji atasema:*

Amuru.

*Padri atakamata Mshumaa (bougie) yenye kuwaka ku mukono ya kuume ku vidole vya chini vya hii mkono atakamata chetezo kwa hii chetezo na mshumaa pamoja atabariki Meza Takatifu kwa alama ya Msalaba na pa hiio fasi atasema kwa sauti nguvu:*

**Hekima. Simameni. Mwangaza wa Kristu uwangazie wote.**

*Padri atabarikia watu kwa alama ya Msalaba na hii saa anasema hii sala ya yulu.*

*Msomaji atasoma somo ya Mezali.*

**SHEMASI***:* Hekima. Tusikilize.

*Kama itaisha somo ya Mezali Padri atasimama mbele ya Meza Takatifu na atafukiza, ataimba hivi:*

**PADRI***:* Maombi yangu ya elekezwe kama uvumba mbele yako. Kunyanyua kwa mikono yangu, kama zabihu ya Mangaribi.

***PADRI*** *atasoma Shairi:*

Bwana nimekuita, unisikilize. Unisikilize, ee Bwana. Bwana nimekuita unisikilize; usikie sauti ya kusihi kwangu. Wakati ninapokuita, unisikilize, ee Bwana.

**MWIMBAJI***:* Maombi yangu ya elekezwe. .

**PADRI***:* Uniweke mulinzi, ee Bwana, mbele ya kinywa changu uchunge mulango wa midomo yangu.

**MWIMBAJI***:* Maombi yangu ya elekezwe. .

**PADRI***:* Usisukume moyo wangu kwa kitu kibaya, nifanye matendo ya uovu.

**MWIMBAJI***:* Maombi yangu ya elekezwe. .

**PADRI***:* Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. .

*(Sasa anasimama mbele ya Meza ya Proskomidi).*

**MWIMBAJI**. Maombi yangu ya elekezwe. .

**PADRI** *anaimba peke yake:* Maombi yangu ya elekezwe" *mupaka:* "kwa mikono yangu"

***MWIMBAJI*** *ataendelesha:* Kama zabihu ya Mangaribi.

*Shemasi anasimama mbele ya Milango Takatifu na sauti kubwa anasema maombi yafwatayo:*

**SHEMASI***:* Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.

**MSOMAJI** *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.

**SHEMASI***:* Bwana mwenyezi. Mungu wa mababu, tunakuomba, utusikie na ukatuhurumie.

**SHEMASI***:* Utuhurumie, ee Mungu, katika huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.

**SHEMASI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya wa madini na wakristu waorthodoksi wote.

**SHEMASI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu. . . *(jina lake)*

*Kisha padri atasoma hii sala:*

**PADRI***:* Ee Bwana, Mungu wetu, uyapokee maombi haya ya watumishi wako, ukatuhurumie kadiri wa wingi wa huruma yako; utushikie rehema yako yulu yetu na yulu ya waaminifu wako wote, wanaopokea huruma yako ya kitajiri.

Kwa kuwa u Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu na kwako tunakutolea utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Shemasi atapaza sauti ataanza maombi kwa ajili ya Wakatikumeno. Waimbaji watajibu kwa kila maombi:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Enyi Wakatikumeno, ombeni kwa Bwana.

Hata sisi tulioamini, kwa ajili ya wakatikumeno, tumwombe Bwana.

Ili Bwana awahurumie.

Awafundishe neno la ukweli.

Awafundishe Evangelio ya haki.

Awafundishe ku Eklezia yake takatifu, Katholiki *(wa dunia mzima*) na Apostoliki (*wa Mitume*).

Uwaokoe, uwahurumie, uwasaidie, uwalinde, ee Mungu, kwa neema yako.

Enyi wakatikumeno, inamisheni vichwa vyenu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Padri atasema kwa siri sala ya wakatikumeno:*

**PADRI***:* Ee Bwana, Mungu wetu, Mjengaji na Muumbaji wa vyote, unayetaka wote waokolewe na waje ku maarifa ya ukweli, tazama watumishi wako wakatekumeno na uwakomboe ku udanganyifu wa zamani na ku mfano wa adui; na kuwaalika ku uzima wa milele, angazia roho zao, na miili na uwahesabie katika kundi la kondoo wa akili, ambako kunaitwa Jina lako Takatifu.

*Padri atapaza sauti:*

Ili hata hawa pamoja nasi walitukuze jina lako lenye kustahili heshima yote na utukufu wote, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri atakungua Antiminsio pa Altare, wakatipo Shemasi atapaza sauti akisema:*

**SHEMASI***:* Walio Wakatikumeno tokeni. Enyi Wakatikumeno, tokeni. Walio wakatikumeno, tokeni. Mtu mkatikumeno asikae ndani.

**SHEMASI***:* Sisi tulio Waaminifu, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

*Hii Sala tunasoma hapa nyuma tunaisoma kufika paka Mu kazi Mbili ya Juma ya Inne ya Kwarezima. Kisha « Bwana hurumia» ya waimbaji iko hapa juu padri ataanza kusema sala ya*

*Waaminifu «Wewe Mungu Mkubwa na Msifiwa. . . » (Angalia hii sala kidogo chini). Na ataendelesha kule na mbele Liturgia. Kama sasa hii Liturgia tunafanya iko kisha MU Kazi Tatu ya Juma wa Inne na Kwarezima tutaongeza katikati ya sala « Ili hata hawa. . . » (angalia yulu) na «Wewe Mungu Mkubwa. . . »*

*Sasa tunaongeza maombi ya wale wanatayarishwa Ubatizo Takatifu:*

**SHEMASI***:* Walio wakatikumeno, tokeni. Enyi wakatikumeno, tokeni. Ninyi mutangaziwa, tokeni. Enyi mutaangaziwa ombeni.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia *(kwa kila maombi).*

Sisi waaminifu, tumwombe Bwana kwa ajili ya wao wanaotayarishiwa kwa mwangaza takatifu na kwa wokovu wao.

Ili Bwana Mungu wetu awasimamishe na awape nguvu, tumwombe Bwana.

Awaangazie na mwangaza wa maarifa na wa Ibada, tumwombe Bwana.

Awastahilishe ku wakati mzuri wa kuoga kuzaliwa kwao kwa mara ya mbili, na kwa maomdoleo ya zambi, na kuwavika nguo isiyoharibika, tumwombe Bwana.

Awape kuzaliwa kwa mara ya mbili kwa maji na kwa Roho Mtakatifu, tumwombe Bwana.

Awape zawadi na imani kamili, tumwombe Bwana.

Awahesabie ku kundi la Watakatifu wake, tumwombe Bwana.

Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utufazie, ee Mungu kwa neema yako.

Ninyi munaokuja ku mwangaza, inamisheni vichwa vyenu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

Hii wakati Shemasi anaomba, Padri anasoma sala yake mbele ya Meza takatifu*:*

**PADRI***:* Onyesha uso wako, ee Rabi, kwa wao wanaotayarishwa kwa kwangaza, na wanataka kutupa uchafu wa zambi; angazia kabisa akili yao; uwastahilishe kwa imani; uwasimamishe mu matumaini; kamilisha mapendo yao; uwafanye washariki wema wa Kristu wako, aliyejitoa mwenyewe pa fasi ya ukombozi wa roho yetu.

Kwa kuwa wewe ni mwangaza wetu na tunautoa Utukufu kwako kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**SHEMASI***:* Tokeni, wenye kuja ku mwangaza, na wenye kuja ku mwangaza, tokeni.

-Enyi walio wakatikumeno, tokeni. Hata mumoja asikae ndani. Na wenye kuamini.

-Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

Elezo*: Hapa panamalizikia hii ongezo ya wenye kwangaziwa. Na hiki kipande cha waangaziwa kiko hapa juu katika mistari miwili tunakisoma paka kisha juma ya Inne ya Kwarezima.*

*Sala ya kwanza ya waaminifu ambayo Padri atasoma kisha kutandiwa kwa Antiminsion.*

## SALA YA WAAMINIFU YA KWANZA

Wewe Mungu mkubwa na msifiwa, kwa lufu ya Kristu wako Mletaji-uzima, unatuondosha ku hali ya kuharibika, tosha mahasa yetu yote ku lufu ya mawazo mabaya, na weka yulu yao akili mwema ya ndani sawa mkubwa; na saidia licho kione kila kitu cha uovu, na sikio lisikie mazungumuzo ya bure, na ulimi ubaki safi ku neno mbaya. Ee Bwana, safisha midomo yetu, inayokusifu; fanya mikono yetu, ijitenge mbali na matendo mabaya, ifanye paka ile inayokufurahisha, viungo vyetu vyote, na akili yote, uvichunge kwa neema yako.

**SHEMASI***:* Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utudazie, ee Mungu kwa neema yako.

**PADRI***:* Kwa kuwa utukufu wote na heshima na usujudu ni haki yako ya Baba na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**SHEMASI***:* tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

## SALA YA WAAMINIFU YA MBILI

**PADRI***:* Ee Rabi Mtakatifu, mwema kamili, tunakuomba, wewe mtajiri wa rehema, uwe na huruma wa sisi wenye zambi, na utustahilishe kwa upokeo wa Mwana wako wa pekee, na Mungu wetu, Mfalme wa utukufu. Kwani tazama Mwili wake takatifu, na Damu yenyi kuleta uzima, kwa hii saa vitaingia, wataviweka yulu ya Meza ya siri, na pempeni yao majeshi ya mbinguni wanazunguka bila kuwaona, utupe Komonyo bila hukumu; kwani kwa wao kunaangaziwa macho ya akili yetu, na tuwe wana wa nuru na mwanga.

**SHEMASI***:* Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utudazie, ee Mungu kwa neema yako.

**PADRI***:* Kwa zawadi ya kristu wako, pamoja naye unabarikiwa, na Roho Mtakatifu kamili, Mwema na Muumba uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Elezo: Hii saa Shemasi ataingia ku mlango wa kusini mu Altare Takatifu. waimbaji waanza kuimba pole-pole Kheruvikon. Padri paka hii wimbo ataisoma mara tatu mbele ya Meza takatifu na kusujudu mara tatu na atabusu Meza takatifu pamoja na Shemasi;*

## KHERUVIKON

Sasa enzi za mbinguni bila kuwaona, wanaabudu pamoja nasi. Kwani tazama Mfalme wa utukufu anaingia.

*Elezo: Hii wakati waikbaji wataimba, Padri atafukiza Meza na Prothesis na atasimama pa mlango Bora. Atafukiza ma Ikone na Waaminifu sawa zoezo. Atasema moyoni wake:*

Njooni tumwinamie. . . . . Zaburi 50 (51).

*Kama atafika pa:* Halafu utafurahi kwa zabihu za haki. . . » *na atakuja ku Meza Takatifu, ataibusu mara tatu pamoja na Shemasi, akisema kwa sauti chini:*

Hee Mungu uniuwe razi, mimi mwenye zambi na unihurumie *(mara tatu).*

*Kisha wataangalia waaminifu pa mlango Bora na wataomba huruma na wataenda ku Prothesis kusujudu Vitu Vitakatifu na kusema paka:* **«Kwa maombezi. . . »** *kutakuwa ukimya kubwa na wote watapiga magoti chini na uso wao utaangalia chini, kila mumoja atasema moyoni mwake:* **«Kwa maombezi. . . »***watatokea ku Altare takatifu ku mlango wa kaskazini na Shemasi atatangulia na mshuma na chetezo atafukiza pole-pole, naye padri ataweka aera juu ya kichwa na atabamba ku mkono wa kuume yulu ya kichwa Sagani Takatifu na ku mkono wa kushoto Kikombe Takatifu mbele ya kilari yake. Padri hatasema kitu kingine paka:* **«Kwa maombezi. . . »**

*Watangia ndani ya Altare Takatifu ku mlnago Bora. padri ataweka Vitu Vitakatifu yulu ya Meza Takatifu na atatosha yulu yake Vifuniko na ataiweka ku ngambo ya kuume. Padri atakamata Aera ku mikono yake na Shemasi atafukiza. Kisha ataifunika pa Vitu Vitakatifu. tena ataifukiza mara tatu na hii saa atafukiza ataendelesha mwisho wa zaburi 50 (51):* **«Halafu watatoa ngombe dume. . . »,** *na atabusu Vitu Vitakatifu na kusema:* **« Kwa maombezi. . . ».** *Waimbaji wataendelea kuimba kipande kilibakia ku wimbo:* **«Sasa enzi. . . ».**

**WAIMBAJI***:* Tazama matoleo ya siri, ni kamili wanaisindikiza. Tukaribie na imani ya juhudi, ili tusharikie ku uzima wa milele. Alliluia.

*Kisha kuweka Vitu Vitakatifu yulu ya Meza takatifu Padri atasema hii sala:*

**PADRI***:* Ee Mungu wa siri isiyokadirika na isiyoonekana, kunakotoka hazina ya hekima na maarifa ya siri, huyu anayetufunulia utimizi wa ibada hii na unayetuweka wenye zambi kwa mapendo yako mingi juu ya wanadamu, kwa kukutolea Zawadi na sadaka kwa ajili ya zambi zetu, na ya makosa ya Waaminifu; Wewe peke, Mfalme Msiyeonekana, mwenye kufanya vitu vikubwa visivyosikilika, vitukufu vya ajabu visiyo hesabiwa, tazama sisi watumishi wako wasiyostahili, tunaosimama mbele ya hii Altare yako Takatifu, sawa Wakeruvi mbele ya Kiti chako, yulu panapumzikia Mwana wako wa pekee na Mungu wetu, kwa hii siri ya woga iliyo mbele yetu; na ulete uhuru kwa sisi na kwa Waaminifu wako wote ku uchafu wote, ututakase sisi wote ku roho na miili, na utakaso usiyoondoshwa; kwani, zamiri safi pasipo yaha ku uso, na moyo wa kuangaziwa, tukomunike ku vitu vitakatifu vyenyi kutakaswa, na kwa hii tunakuwa wenyiuzima, tuna muungamia Yeye Kristu wako, Mungu wetu wa kweli, aliyesema*:* Anayekula Mwili wangu, na kuinywa Damu

yangu anakaa ndani yangu nami ndani yake; juu ya kukaa ndani yetu na kutembea Neno lako, ee Bwana, tunakuwa hekalu ya Roho yako Takatifu na iaabudiwa, waliokombolewa ku mayele yote ya Shetani, ya kufanya ao ya kusema ao ya kuwaza mu akili; na tupate mema yote aliosema kwa sisi, pamoja na watakatifu wako wote, wale wanaokufurahisha milele.

*Shemasi ila wakati atatoka ku Altare Takatifu ku mlango wa kaskazini na atasimama pa fasi yake inje na atasema:*

**SHEMASI***:* Tumalize ombi letu ya mangaribi kwa Bwana.

**WAIMBAJI***: Watasema kwa kila ombi ya Shemasi:* Bwana hurumia

Kwa ajili ya Vipaji Viheshimiwa, vilivyoletwa na kutakaswa mbele, tumwombe Bwana.
Ili Mungu wetu, Mpenda-wanadamu, aliyevipokea katika Altare yake Takatifu, ya mbinguni na isiyoonekana, kama manukato ya harufu ya kiroho, aturudishie neema, kimungu na zawadi ya Roho Mtakatifu, tumwombe Bwana.
Kwa ajili ya kuokolewa na kila sikitiko, uadui, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.
Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utulinde, ee Mungu, kwa neema yako.
*Shemasi ataendelea akisema:*
**SHEMASI***:* Mangaribi hii mzima kamili, takatifu, iwe ya amani na bila zambi tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji kisha kila ombi watajibu:* Utupe, ee Bwana. . . .
Malaika wa amani, Mwongozi ya kweli, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana.
Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na makosa yetu, tuombe kwa Bwana.
Vilivyo vyema na vinavyofaa kwa roho zetu na amani ya dunia yote, tuombe kwa Bwana.
Kumaliza maisha yetu yanayobaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

Mwisho wa maisha yetu uwe kikristu, bila maumivu, bila aibu, wa amani, tena tuone neno njema mbele ya kiti chake cha kuogopa tombe kwa Kristu.

Tukiomba umoja wa imani, na ushirika wa Roho Mtakatifu sisi na kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Na utustahilishe, ee Rabi, kusubutu na matumaini na bila hukumu, kukuita Baba, wewe Mungu wa mbinguni, na kusema;

*Waaminifu, Waimbaji na wasomaji watasema pamoja sala ya Rabi:*

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

**PADRI***:* Kwa kuwa na ufalme, na uwezo, na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakaitfu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Amani kwa wote.

**WAIMBAJI***:* Na kwa roho yako.

**SHEMASI***:* Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

**PADRI** *(kwa siri):* Wewe Mungu, peke yako mwema na mwenye rehema, unayekaa juu, na kuangalia chini, tazama na macho ya huruma taifa lako mzima na ulilinde; utustahilishe sisi wote, pasipo hukumu kukomunika ku siri hii yenyi kuumba uzima; kwani Kwako tunakukomunika ku

siri hii yenyi kuumba uzima; kwani Kwako tunainamisha vichwa vyetu, tunapokea Kwako rehema yako ya utajiri.

**PADRI** *(na sauti nguvu):* Kwa neema, na rehema na mapendo kwa wanadamu ya Mwana wako wa pekee ambaye, umehimidiwa pamoja naye, na Roho yako Mtakatifu kamili, Mwema na mpaji uzima sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI** *(kwa siri):* Usikilize, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, toka makao yako matakatifu na toka kiti cha utukufu wa Ufalme wako utujie ututakase, wewe unayekaa mbinguni pamoja na Baba, tena uliye hapa pamoja nasi bila kuonekana. Ukubali kutugawanyia ku mkono wako wa uwezo, Mwili wako Safi na Damu yako heshimiwa, na kwa mikono yetu wote.

*Padri na Shemasi watainama mara tatu wakisema kwa siri:*

Ee Mungu, uniwe razi, mimi mwenye zambi. *(mara tatu).*

*Hii saa Aera inafunika Vitu Vitakatifu, padri ataweka mikono chini ya Aera. Atakamata mwili Takatifu yulu ya Sahani atanyangula na atafanya alama ya Msalaba na hii wakati atasema:*

**SHEMASI** *(na sauti nguvu):* Tusikilize.

Vitu Vitakatifu venye kubarikiwa mbele kwa watu watakatifu.

**WAIMBAJI***:* Mtakatifu ni mmoja peke yake, Bwana ni mmoja peke yake. Yesu Kristu, katika utukufu wa Mungu Baba. Amina.

*Shemasi atarudi Patakatifu na Waimbaji wataimba wimbo wa ushirika wa siku. Ni hii:*

## USHIRIKA (KINONIKONI)

**WAIMBAJI***:* Onjeni na tazamani, kwani Bwana ni Mwema. Alliluia.

*Hii Saa wanaimba waimbaji Ushirika, padri anaisha kufungua Vitu Vitakatifu na ataanza kumega mukate mu vipande inne na ataweka pa Sahani na alama ya msalaba. Na atasema:*

«Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

*Shemasi ataonyesha kwa Orarion Kikombe Kitakatifu na atasema:* **« Ee Rabi, kamilisha Kikombe Kitakatifu».** *Padri atachukua kipande kile cha juu IC atafanya alama ya msalaba yulu ya Kikombe kisha ataweka ndani. Atasema:* **«Kwa maombezi. . .** »*Shemasi atajibu:* «**Amina».** *Na atabeba maji ya moto akisema mbele ya padri:* **« Hee Rabi ubarikie maji ya moto»**. *Padri ataibarikia atasema: «***Kwa maombezi. . . »** *Shemasi atamwanga maji ndani ya Kikombe na padri atasema:* **Kwa maombezi. . . »**

*Hapo Padri na Shemasi watasema sala za Komonyo Takatifu.*

Nasadiki, ee Bwana, na kuungama ya kama kweli Wewe Kristu, Mwana wa Mungu mzima, uliyekuja duniani kwa ajili ya kuokoa wenye zambi, ambao mimi ni wa kwanza. Nasadiki tena ya kama huu ni Mwili wako safi na hiyi ni Damu yako heshimiwa. Nanakuomba*:* Unihurumie na kunisamehe makosa yangu yakutaka na yakutotaka, kwa maneno ao kwa matendo, yakuja wala yakutokuja, unistahilishe kushiriki katika fumbo zako za bila doa, kwa ajili ya maondoleo ya zambi na uzima wa milele. Amina.

Angalia sasa najongea karibu ya Komonyo yako Takatifu, ee Mwumba wangu, usiniunguze ku ushariki huo. Sababu Wewe ni moto unaounguza wasiyostahili. Lakini unitakase ku aibu hiyi.

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho*:* Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Akionapo Damu Kimungu, atetemeke, ee Mwanadamu, kwa sababu ni makala ya moto ilunguzayo wasiostahilivu. Mwili Kimungu unageuzwa kimungu na unalisha, unatakasa na unalisha mawazo namna isiosikilizwa

Ee Kristu, kwa mapendo yako ulinipeleka ku furaha na kwa ulinzi wako ulinigeuza kuwa mtu mwengine*:* Choma zambi zangu kwa moto usiyo vyombo na kubali kunijaza na furaha zako, sababu nikiwa tele na furaha, nitasifu majio zako mawili, ee Wewe mjaliwa na wema.

Nitaingia je, mimi msiye stahili, katika ukuu wa watakatifu wako? Nikisubutu kwingia katika nyumba ya arusi, nguo langu litanitoa, maana hayuko ya arusi na nikifwatane, malaika watanifukuza. Bwana, safisha basi mataka ya moyo wangu na uniokoe, wewe mpenda wanadamu.

*Na pia Sala hii:*

Rabi, rafiki ya wanadamu, Bwana Yesu Kristu, Mungu wangu, vipaji vyako vitakatifu visiwe nami hukumu sababu ya maovu yangu*:* Lakini utakaso wa moyo na wa mwili na rahani ya uzima na ya ufalme wa milele. Ni vizuri kwangu kwa kumshika Mungu na kuweka tumaini la wokovu wangu katika Bwana.

*Na tena tunasoma hii:*

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako. . . .

*Padri, kwa mkono wa kushoto, atakamata sehemu moja ataiweka mu mkono wake wa kuume, akisema:*

Tazama, namjongea Kristu, Mfalme msiyekufa, Mungu wetu. Mimi (atataja jina lake) padri, napewa Mwili Mheshimiwa Mtakatifu na mwenye kuleta uzima, wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Hivi Padri anakuja Mkate Mtakatifu na woga wa Mungu na utaratibu.*

*Kisha atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Ee Shemasi, jongea.

*Shemasi atajongea akisema:*

**SHEMASI***:* Tazama, namjongea Kristu, Mfalme msiyekufa, Mungu wetu. Ee Rabi, unipe mimi *(atataja jina lake)*, Shemasi, Mwili mheshimiwa Mtakatifu na mwenye kuleta uzima wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi zangu na uzima wa milele.

*Padri atamupa pa mkono wa kuume wenyi kuwekwa juu ya wa kushoto sehemu ya Mwili Mtakatifu, akisema:*

Kwa *(jina lake)*, Shemasi, anapewa Mwili wa samani, Mtakatifu na bila doa kamili wa Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Shemasi akipokea Mwili Mtakatifu atabusu mkono wa padri ataenda nyuma ya Meza Takatifu huko ataukula kwa utaratibu sawasawa na padri.*

*Kisha padri atakamata Kikombe Kitakatifu pamoja na kitambaa-kifuniko atasema:*

**PADRI***:* Tazama, namjongea tena Kristu Mfalme msiyekufa na Mungu wetu. Mimi (*jina lake)*, mutumishi wa Mungu na padri napewa Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Na atakunwa mara moja. Kisha atapanguza midomo yake vilevile upande wa midomo ya Kikombe na atakibusu akisema.*

Hii imegusa midomo yangu; maovu yangu yataondolewa na zambi zangu zitatakaswa.

*Atamwambia Shemasi:*

**PADRI***:* Ee Shemasi, jongea tena.

*Shemasi atajongea atapanguza kwa utaratibu mkono wake wa kuume na Musa akisema:*

Tazama, namjongea tena Kristu Mfalme msiyekufa na Mungu wetu. Ee Rabi, unipe Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Akimpa Kikombe mara moja, padri atasema:*

Mtumishi wa Mungu na Shemasi *(jina lake*), anapewa Damu Heshimiwa na Takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa maondoleo ya zambi na uzima wa milele.

*Kisha, wakati Shemasi atabusu midomo ya Kikombe*, *Padri atasema:*

Hii imegusa midomo yako, maovu yako yataondolewa, na zambi zako zitatakaswa.

*Kisha, Shemasi atakamata Sahani juu ya Kikombe ataweka sehemu katika Kikombe akipanguza vizuri Sahani na Musa (Yoga ya bahari).*

*Padri atasema hii sala:*

**PADRI***:* Tunakushukuru Wewe Mwokozi na Mungu wa wote, kwa mema yote uliotupatia sisi, na komonyo ya Mwili Takatifu na Damu ya kristu wako; na tunaomba Kwako, Rabi Mpenda-wanadamu, utulinde chini ya kivuli cha mabawa yako; na utupe sisi mpaka mwisho wa pumzi yetu, tupokee Vitu Vitakatifu sawa wenye kustahili, kwa kuangazia roho na mwili, na kuriti Ufalme wa mbinguni.

*Padri atakamata Kikombe na akimupa kila Mwaminifu Komonyo, atasema:*

**PADRI***:* Kwa woga wa Mungu, na imani, na mapendo muje.

**WAIMBAJI***:* Amina. Abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana, Bwana ndiye Mungu amefunuliwa kwetu.

*Padri ataanza kukomunika Waaminifu kusema hivi:*

Mtumishi wa Mungu *(jina lake)* anapewa Mwili na Damu heshimiwa na takatifu ya Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu kwa maondoleo ya zambi zake na uzima wa milele. Amina.

*Wakati huu wa Kukomunika watu, waimbaji wataimba wimbo hii:*

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho*:* Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

*Kisha Komonyo ya Waaminifu Padri atawabariki watu na Kikombe Kitakatifu akipaza sauti:*

Ee Mungu, okoa taifa yako na bariki uriti wako.

**WAIMBAJI***:* Nitamutukuza Bwana kila wakati, sifa yake kinywani mwangu siku zote; mkate wa mbinguni na kilauri cha uzima wa kuonja na muone kama Bwana ni mwema. Alliluia, Alliluia, Alliluia.

*Padri ataweka Kikombe Kitakatifu juu ya Meza takatifu, atafukiza akisema kwa siri.*

Ee Mungu, utukuzwe juu mbinguni na utukufu wako uwe duniani yote.

*Hapo, padri atampa Shemasi Sahani, huyu atageuka ku upande wa watu kisha ataenda ku Meza ya Matayarisho (Prothesis), ataiweka huko. Padri mwenyewe atakamata Kikombe Kitakatifu atasema kwa siri.*

**PADRI***:* Ahimidiwe Mungu wetu.

*Kisha Padri atapinduka kwa watu, atawaonyesha Kikombe Kitakatifu akipaza sauti:*

Daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Shemasi atatoka pa fasi yake ya kuwaida na atapaza sauti:*

Simameni. Tukishiriki Fumbo za ajabu za Kristu, Fumbo za umungu, takatifu bila doa, za kutokufa, za mbinguni na zenyi kuleta uzima, tumshukuru Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Utusaidie, utuokoe, utuhurumie na utulinda, ee Mungu kwa neema yako.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

**SHEMASI***:* Mangaribi hii yote, kamili, takatifu, ya amani na bila zambi tukiomba; sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.

*Na atarudi Patakatifu. '*

**WAIMBAJI***:* Kwako, ee Bwana.

*Kisha kukunja Antiminsion, Padri atafanya alama ya Msalaba, na Evangelion juu ya Meza akipaza sauti:*

Kwa kuwa wewe ni utakaso wetu na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Kisha Padri ataweka Evangelion juu ya Antiminsion.*

**WAIMBAJI**: Amina.

*Padri atageuka ku upande wa watu, atapaza sauti akisema:*

Twendeni na amani.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia *(mara tatu),* ee Rabi mtakatifu barikia.

*Padri atatoka inje ya Mlango Bora, atasimama mbele ya Ikone ya Kristu na atapaza sauti akisema:*

**PADRI***:* Ee rabi Mwenyezi, uliyeumba dunia nzima na hekima; kwa maongozi yako isiyoweza kuhadisiwa na rehema yako kubwa, uliyetuletea ku siku hizi ziheshimiwa, sababu ya utakaso wa roho na miili, kadiri ya makosa, juu ya matumaini ya ufufuo; ambaye katika siku makumi inne, uliweka mikononi mwa Mtumishi wako Musa Maandiko aliyoandika Mungu, utupe na sisi Wewe Mwema ushindano mwema, tutimize njia ya kwarezima, tuchunge imani bila kuigawanya, tuvunje vichwa vya nyama ya ajabu, tuwe washindi wa zambi, na tufika bila kuhukumiwa na kuabudu Ufufuo takatifu. Kwani jina lako kuu na nzuri linabarikiwa na kusifiwa, la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Kisha waimbaji wataimba:*

Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa, na mupaka milele. *(mara tatu).*

*Padri ataenda ku Meza ya Matayarisho atasoma kwa siri hii sala ifwatayo:*

Ee Bwana, Mungu wetu, uliyetuletea ku siku hizi ziheshimiwa na uliyetusharikisha ku siri za woga, utuunganishe ku kundi la Kondoo wa akili, na utufanye wariti wa Ufalme wako, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI***:* Bwana hurumia.

*Padri atatokea ku mlango Bora, atawabariki Waaminifu hivi:*

Baraka ya Bwana na huruma yake iwe nanyi, kwa neema yake na mapendo yake kwa ajili ya wanadamu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI***:* Amina.

**PADRI***:* Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu, matumaini yetu, utukufu kwako.

**MSOMAJI***:* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milelena milele. Amina. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia, ee Padri mtakatifu barikia.

*Padri atapinduka ku upande wa Waaminifu, atafanya Kuaga hivi:*

Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mama yake Mtakatifu asiye na doa, kwa nguvu na msaada mheshimiwa na wenyi kuleta uzima, kwa ulinzi wa majeshi maheshimiwa ya mbinguni yasiyo na mwili, kwa maombezi ya Yoane, Nabii Mtangulizi na Mbatizaji, mheshimiwa na mtukufu, ya Mitume Watakatifu, watukufu na waifiwa, ya Mashahidi Watakatifu, watukufu na wasindaji, ya wababa wetu Watakatifu na wabebaji-Mungu, *(* ya Baba wetu Mtakatifu Grigorio Dialogo, askofu

mkubwa wa Roma, ya Yoakimu na Anna, Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki, ya Mtakatifu wa hii siku *(jina yake)* tunayekumbuka leo, na ya Watakatifu wote, atuhurumie na kutuokoa, kwani Yeye ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu na Mrahimu.

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Tunasoma zaburi hii:*

Zaburi 34 (35)

Nitabariki Bwana wakati wote; sifa yake itakuwa kinywani mwangu daima. Nafsi yangu itajisifu katika Bwana; Wapole watasikia na watafurahi. Musifu Bwana pamoja nami, na tutukuze jina lake pamoja. Nilitafuta Bwana, naye alinijibu, na kuniponyesha toka woga zangu zote. Wakamutazama, na walitiwa nuru; Na nyuso zao hazitaona haya milele. Masikini huyu akalia, Bwana akamusikia, akamwokoa toka taabu zake zote. Malaika ya Bwana anapiga kambi kuzunguka wale wanaomwogopa, na anawaokoa. Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni Mwema; Heri mutu anayemuwekea tumaini lake. Ogopeni Bwana, ninyi watakatifu wake; Kwa sababu wale wanaomwogopa hawahitaji kitu. Wana-simba wanahitaji, wanaona njaa; Lakini wao wanaotafuta Bwana hawatakosa kitu cho chote kilicho chema. Njooni, ninyi watoto, munisikilize; nitawafundisha ninyi woga wa Bwana. Ni nani mutu yule anayetaka uzima, na anayependa siku nyingi ili apate kuona mema*?* Uzuize ulimi wako na ubaya, na midomo yako na kusema hila. Uache mabaya ukatende mema; Tafuta salama, na kuifuata. Macho ya Bwana yanatazama wenye haki, na masikio yake ni wazi kwa kusikia kilio chao. Uso wa Bwana ni juu yao wanaotenda mabaya, aondoshe ukumbusho wao duniani. Wenye haki walilia, na Bwana alisikia, na kuwaponyesha toka taabu zao zote. Bwana ni karibu na wenye moyo wa kuvunjika, na anaokoa wenye roho ya toba. Mateso ya mwenye haki ni mengi; Lakini Bwana anamuponyesha nayo yote. Anachunga mifupa yake yote; haukuvunjika hata mumoja. Uovu utawa mwovu; nao wanaochukia wenye haki watahukumiwa. Bwana anakomboa nafsi ya watumishi wake; wala hawatahukumiwa wote wanaomuwekea yeye kimbilio lao.

Zaburi 145

Nitakutuka, Mungu wangu, ee Mufalme; na nitabariki jina lako milele na milele. Nitakubariki kila siku; na nitasifu jina lako milele na milele. Bwana ni mukubwa na mwenye kusifiwa sana; na ukubwa wake hauwezi kutafutikana. Kizazi kimoja kitasifu kazi zako kwa kingine, na kitatangaza matendo yako ya uwezo. Nitafikili enzi ya utukufu ya heshima yako na kazi zako za ajabu nitafikili. Na watu watataja uwezo wa matendo yako ya kuogopesha; nami nitasimulia ukubwa wako. Wao watasema ukumbusho wa wema wako mukubwa na wataimba haki yako. Bwana ni mwenye neema na anajaa rehema, pole-pole kwa kukasirika na mwenye rehema nyingi. Bwana ni mwema kwa watu wote; Na rehema zake ni juu ya kazi zake zote. Kazi zako zote zitakushukuru, ee Bwana; na watakatifu wako watakubariki. Watasema juu ya utukufu wa ufalme wako na kuzungumuza juu ya uwezo wako; kujulisha wana wa watu matendo yake ya uwezo na utukufu wa enzo ya ufalme wake. Ufalme wako ni ufalme wa milele, na mamlaka yako ni ya vizazi vyote. Bwana anategemeza wote wanaoanguka na kuwanyanyua wanaoinama chini. Macho ya watu wote yanakungojea; Nawe unawapa chakula chao kwa wakati wake. Unafungua mukono wako, na kushibisha hamu ya kila kitu kilicho hai. Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote, na mwenye neema katika kazi zake zote. Bwana ni karibu nao wanaomwitia, nao wanaomwitia kwa kweli. Atatimiza hamu yao wanaomwogopa; atasikia kilio chao na kuwaokoa. Bwana anachunga wote wanaomupenda; lakini waovu wote atawaharibu. Kinywa changu kitapasha sifa ya Bwana; na miili yote wabariki jina lake takatifu milele na milele.

**MSOMAJI***:* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Bwana hurumia *(mara tatu).* Rabi Mtakatifu bariki.

**PADRI***:* Kwa maombezi ya wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

*Kama ni Askofu Padri atasema hivi:* Kwa maombezi ya Askofu wetu Mtakatifu, ee Bwana Yesu Kristu. . .

**WAIMBAJI***:* Amina.

*Padri atawabariki waaminifu akisema:*

Utatu Mtakatifu uwalinde ninyi wote.

**WAIMBAJI***:* Anayetubariki na kututakasa, ee Bwana, umlinde miaka mengi.

*Kama Liturgia anafanya Askofu waimbaji wataimba hivi:*

Ee Bwana, umulinde Rabi na Askofu wetu, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi, miaka mengi, ee Rabi.

*Kisha Askofu ao Padri atagawanya mkate wenyi kubarikiwa uitwao Antidoron akisema kwa kila mwaminifu.*

Baraka ya Mungu na huruma yake iwe nawe.

*Kama ni Siku Kuu mkubwa Mapadri ndani ya Altare Takatifu wanaimba moja Kontakion ya hii ni hapa chini:*

**KONTAKION YA KUZALIWA KRISTU.** *Sauti ya tatu*

Leo Bikira amezaa Mungu Mkuu na dunia pango inapokea msiye karibika. Malaika na wachungaji-Kondoo wanatukuza. Majusi pamoja na nyota wanatembea. Kwani kwa ajili yetu alizaliwa, Mtoto Mchanga, Mungu wa mbele ya nyakati.

**KONTAKION YA EPIFANIA YA KRISTU** *Sauti ya Ine.*

Leo siku ya Epifania ulimwengu umeona mwangaza wako, kwani, ee Bwana, ulijifunua na nuru yako inatuangaza; ndio maana na ufahamu wetu tunakuimbia*:* Ulikuja na ulijifunua, Nuru isiyokaribika.

## SIKU KUU YA KUPOKELEWA KWA BWANA YESU KRISTU MIKONONI MWA MWENYI HAKI SIMEONI

**Kontakion** Sauti ya Kwanza.

Katika kuzaliwa kwako ulitakasa tumbo la Bikira, katika kutolewa kwako ulibariki mikono ya Simeoni, sawa ilivyofaa, ulikuja sasa na ulituokoa ee Kristu Mungu wetu. Leta mu wakati wetu amani ku uzima wetu, na sabitisha wafalme wetu, wale uliyopenda, wewe peke Mpenda-wanadamu.

## SIKU KUU YA MUNGU YA MATAWI NA UFUFUO WA LAZARO

**Kondakion**. Sauti ya Sita.

Ewe Kristu Mungu wetu, unashuka toka kiti cha mbinguni na unatembea katika inchi juu ya punda, unapokea wimbo wa Malaika na wale watoto wa wayuda, wote wanakupazia sauti*:* Ndiwe Mbarikiwa anayekuja kumurudisha Adamu.

## SIKU KUU YA PASKA

**Kondakion**. Sauti ya Mnane.

Ewe Msiyekufa, ulishuka kaburini na uliharibu nguvu ya Hadeze, Kristu Mungu wetu, ulifufuka kama Mshindi ukawaambia wanawake Wabebaji-manukato*:* Furahini! Uliwapa Mitume wako amani, na wale walioanguka uliwafufua.

## SIKU KUU YA KUPANDA MBINGUNI

Kondakion. Sauti ya Sita.

Ulipotimiza kwa ajili yetu tendo lako la wokovu, kisha kuunganisha mbingu na dunia, watu na Mungu, katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukapanda mbinguni bila kutwacha, lakini umekaa siku zote katikati yetu na ukawaambia wale wanaochunga mapendo yako*:* Mimi ni pamoja nanyi siku zote na mutu hata mumoja hawezi kufanya chochote juu yenu.

### SIKU KUU YA PENTEKOSTI

**Kondakion**. Sauti ya Mnane.

Alipochanganya lugha za ulimwengu, Bwana wa juu mbinguni akasambaza mataifa; lakini alipogawanya ndimi za moto, anawalika watu wote ku umoja na wote pamoja tunamutukuza Roho Mtakatifu kamili.

### SIKU KUU YA MAGEUZO SURA YA YESU KRISTU MWOKOZI WETU

**Kondakion**. Sauti ya Saba.

Mlimani ulijigeuza, na kama inavyowezekana wanafunzi wako waliona, ewe Kristu Mungu, utukufu wako; wakati walikuona Msalabani, na walisikia mateso yako kwa mapenzi yako na, watahubiri duniani, ya kama ndiwe kweli Mtukufu wa Baba.

## KONDAKIA ZA SIKU KUU ZA MZAZI-MUNGU

### SIKU KUU YA KUZALIWA KWA MAMA MZAZI-MUNGU

**Kondakion**. Sauti ya Ine

Yoakimu na Anna ku utasa wa haya, Adamu na Eva ku mauti ya uharibifu waliombolezwa Bikira Safi, kwa ajili ya kuzaliwa kwako; hivi mataifa yake wanakushangilia, kwa maana walikombolewa ku utumwa wa zambi na wanaimbia tasa aliyezaa Mzazi-Mungu na mlinzi wa uzima wetu.

### SIKU KUU YA KUINGIA KWAKE MZAZI-MUNGU HEKALUNI

**Kondakion**. Sauti ya Ine.

Leo ameingia nyumbani mwa Bwana Hekalu safi ya Mwokozi, chumba tukufu na Bikira, zahabu takatifu ya utukufu wa Mungu na neema ya Roho Mtakatifu pamoja naye huyu, mwenye kuimbiwa na Malaika wa Mungu, kwani yeye ni hema ya mbingu.

### SIKU KUU YA HABARI NJEMA YA BIKIRA MARIA MZAZI-MUNGU

**Kondakion**. Sauti ya Ine.

Masauti yetu ya ushindi yavume kwa ajili ya heshima yako, ewe Malkia msiyeweza kushindwa, wewe mwenye kutuokoa ku hatari ya vita, Mzazi-Mungu. Bikira Mkuu. Sifa zetu na nyimbo zetu za shukrani zinapanda kwako. Simika pembeni yetu moja ya maboma imara na mkono wako wa uwezo, utuokoe ku hatari yote ujiharikishe kuwasaidia waaminifu wanaokuimbia*:* Salamu, Bibi-arusi usiyeolewa.

### SIKU KUU YA KULALA KWAKE MZAZI-MUNGU

**Kondakion. Sauti ya mbili.**

Ee Mzazi-Mungu usiyechoka kutuombea kamwa kwa ulinzi wako hauwezi kuacha kuwa matumaini yetu, uwakamate kaburi na lufu kwani ndiwe Mama wa Uzima aliyeikaa tumboni mwa bikira daima na kukupandisha.

### SIKU YA MUNGU YA APOKREO

**KONTAKION.Sauti wa kwanza.**

Wakati utakapokuja na utukufu duniani, ee Mungu wetu, viumbe vyote vitatetemeka, mto ya moto itapita mbele ya baraza yako ya hukumu, vitabu vitafunguliwa na siri zitafunuliwa; kwa hii siku uniokoe toka moto ya milele, na unistahilishe nisimame kuume kwako, ee Mwamuzi mwenyi haki.
Siku ya Mungu ya Tirofagi (Jivini)
KONTAKION Sauti wa sita.

Ee Mwongozi wa hekima tena Rabi wa uwezo, mwalimu mwenye kutufundisha mlinzi wa maskini, sabitisha na kufundisha roho yangu, unipe neno, ee Neno la Mungu, maana siwezi kuzuia midomo yangu kukuimbia*:* Ee Mungu wa mapendo unihurumie mimi maskini mkosefu.

*Wakati ya Kwarezima Siku ya Mungu mu juma wa kwanza, wa mbili, wa tatu, wa inne na wa tano tunaimba*

**KONTAKION YA WIMBO AKATHISTE YA MZAZI-MUNGU**.

Sauti ya mnane**.**

Kwako jemadari kunilinda nina deni
kukushukuru kwa wokovu na kushinda wangu
mimi mji wako, ee Mzazi Mungu.
Tena kwa mamlaka yakosi kushindwa,
na hatari kila namna niepuwe kukuimba,
kwa kelele kuu*:* Salamu, Bibi Arusi, usiolewa.

# SIKU KUU YA WATAKATIFU WOTE TUNAIMBA:

## KONTAKION YA MASHAHIDI Sauti ya Mnane

Ee Bwana, ulimwengu inakutoa, kama mwanzo ya inchi, kwa Muumba ya dunia, Washahindi Wabebaji-Mungu; basi, ewe Mwenye huruma kamili, katika maombi wao, chunga Kanisa wako katika amani mingi kwa maombezi ya Mzazi-Mungu.

***Kama tunafanya Liturgia kwa mapumziko ya Wafu tunaimba Kontakion yao. Ni hii:***
**KONTAKION YA WAFU. Sauti ya Mnane**
Pamoja na watakatifu, pumzisha, ee Kristu, roho za watumishi wako, pahali pasipo umivu, bila sikitiko, bila muchoko, lakini uzima wa milele.

*Kama tunafanya Siku Kuu ya Kunyanyua Msalaba ya Kristu, nikusema 14 Mwezi ya Tisa*

## KONTAKION YA MSALABA

Ewe Kristu Mungu, uliyeinuliwa kusudi msalabani, uipe jamii ile jipya iliyo na jina lako, rehema yako. Uwafurahishe wafalme wetu waaminifu na nguvu yako, ukiwatunza na kushinda juu ya washindanao, wakifurahiwa kwa agano lako jipya, silaha, ya amani, alama isioshindika.

## ASUBUI SIKU YA KOMONYO TAKATIFU

*Asubui mapema sema hii sala:*

Mungu Mutakatifu, mweza Mutakatifu, msiye kufa Mutakatifu, utuhurumie *(mara tatu).*
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. .
Utatu Mutakatifu. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Baba yetu uliye mbinguni. . . Bwana hurumie (kumi na pili).
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu Yeye Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu.

***ZABURI 23***

Bwana ni mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu. Ananilalisha katika malisho ya majani mabichi; ananiongoza kando ya maji matulivu. Anarudisha nafsi yangu; ananiongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Ndiyo, hata nikipita kati ya bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa mabaya;

kwa maana wewe ni pamoja nami; Gongo lako na fimbo yako zinanifariji. Unanitengenezea meza mbele ya adui zangu; Umenipakalia mafuta kichwani; kikombe changu kinafurika. Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu; na nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.

***ZABURI 24***

Inchi na kujaa kwake ni mali ya Bwana; Dunia, nao wanaokaa ndani yake. Kwa maana ameweka misingi yake juu ya bahari, na kuisimamisha juu ya garika. Nani atakayepanda mulimani mwa Bwana? Na nani atakayesimama katika pahali pake patakatifu? Mtu aliye na mikono safi, na moyo mweupe; asiyenyanyua nafsi yake kwa uwongo, wala hakuapa kwa hila. Yeye atapokea baraka kwa Bwana, na haki kwa Mungu wa wokovu wake. Hiki ni kizazi chao wanaomutafuta, wanaotafuta uso wako, ee Mungu wa Yakobo. Nyanyueni vichwa vyetu, ee ninyi malango; na munyanyuliwe, ninyi milango ya milele; na mfalme wa utukufu ataingia. Nani aliye mfalme wa utukufu? Bwana mwenye nguvu na uwezo. Bwana mwenye uwezo vitani. Nyanyulisheni vichwa vyenu, ee ninyi malango, ndiyo, muvinyanyue, ninyi milango ya milele, na mfalme wa utukufu ataingia, Ni nani huyu mfalme wa utukufu? Bwana ya majeshi, yeye ni Mfalme wa utukufu. Sela.

***ZABURI 116. 10-19***

Ninaamini, kwa maana nitasema*:* Niliteswa sana*:* Nikasema katika haraka yangu*:* Watu wote ni wawongo. Nitamupa Bwana nini kwa ukarimu wake wote alionitendea? Nitapokea kikombe cha wokovu, na kuitia jina la Bwana. Nitalipa Bwana naziri zangu, ndiyo, mbele ya watu wake wote. Ni ya damani machoni mwa Bwana mauti ya watakatifu wake. Ee Bwana, kweli mimi ni mtumishi wako*:* Mimi ni mtumishi wako, mwana wa kijakazi chako; umefungua vifungo vyangu. Nitakutolea zabihu ya kushukuru, na kuita jina la Bwana. Nitalipa naziri zangu kwa Bwana, ndiyo, mbele ya watu wake wote; katika viwanja vya nyumba ya Bwana, katikati yako, ee Yerusalema. Musifu Bwana.

Utukufu. . . Sasa. . Alliluia *(mara tatu).* Utukufu kwako, ee Mungu. Bwana hurumia *(mara tatu).*

*Kiisha anza kusoma nyimbo zifuatavyo: Sauti ya sita*

Zarau wovu wangu, ee Mungu wewe uliyezaliwa kwa Bikira, takasa roho yangu, ulifanye hekalu ya mwili na damu yako kuwa takatifu, kwa hasira yako usinitupe mbali ya uso wako, wewe mwenyi huruma usiyokadirikana kisilani mbele ya uso wako, wewe uliyekuwa na huruma yasiyo kipimo.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Nitasubutu je, mimi mwovu, kujongea mafumbo yako Takatifu? Nikijaribu kujongea pamoja na wenye kustahili nguo yangu itanitoa maana haiko ya arusi. Na nitavuta mbegu ya hukumu kwa moyoni mwangu mtenda zambi nyingi. Ee Bwana, takasa roho yangu yenyi kuchafuka na uniponye kwani wewe ni mwema na Mpenda wanadamu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**THEOTOKION**

Ee Mama wa Mungu, zambi zangu zinapita wingiu; ninakimbilia kwako Mtakatifu kwa kutafuta wokovu. Angalia moyo wangu wenye kushikwa na ugonjwa na uniombee kwa mwana wako. Mungu wetu, anisamehe mabaya yote niliofanya kwako, ewe Mbarikiwa.

*Paka siku kubwa ya kazi Ine Takatifu wanaongeza kusoma: Sauti ya Mnane.*

Mitume watukufu waliangazwa, wakati walioshwa miguu ku karamu ya mwisho, kwa ile wakati Yudasi kafiri, kwa tamaa yake mbaya, akaingia gizani na akakutoa wewe mwamuzi wa kweli, kwa mwamuzi waovu. Ee mnyanganyi, tazama ni kwa sababu ya hii amejitundika*:* Epuka tamaa iliyomuongoza kutendee Rabo wake maovu ya hii namna. Ee Bwana mwema wa wote, utukufu kwako.

Bwana hurumia (Mara 40)

## NAMNA YA KUKARIBIA KOMUNYO TAKATIFU.

### SIMEONI MFASIRI

Ee Wewe menyi lujitayarisha kuwa kuonja mwili wa Bwana, karibia na woga kusudi usiungue*:* Ni moto. Kwa kunywa Damu ya ushirika, mbele ya upatano vema na wao walikukosea, kisha jongeo uonje chakula cha fumbo.

### INGINE VILEVILE

Mbele ya kukomunika sadaka ya woga, mwili wa Rabi, wenye kuleta uzima, sala hivi namna yafuatayo na matetemeko*:*

### SALA 1 YA MTAKATIFU BAZILE MKUBWA

Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, chemchem ya uzima na ya uzima usiyo kufa. Muumba wa ulimwengu unaoonekana na usiyoonekana. Mwana wa milele pamoja na Baba bila mwanzo na Wewe Mwenyewe usiye mwanzo*:* Wewe ambao katika ziada ya wema, ulikamata mwili, wewe ulisulubiwa na kuwekwa kaburini kwa ajili yetu sisi wasio shukrani na wapotevu ambao kwa ajili ya damu yako ulitupatanisha na hali yetu ya zambi, wewe mwenyewe. Mfalme wa milele, ulikubali majuto yangu, mimi mukosefu; inamisha sikio lako kwangu na usikie chochote ninapotaka kusema. Nilikosea mbingu na Wewe Mwenyewe na sistahili tena kunyanyua macho yangu juu kulio sifa yako, kwani nilikasirikisha wema wako nilipovunja amri zako na kukataa kutii amri zako. Lakini, ee Rabi, uko mvumilivu na mwenye huruma; tena wakati unapogonja ubadilisho wangu, haukuniacha kupotea na zambi zangu. Wewe, ee rafiki wa binadamu, uliyesema mwenyewe kwa kinywa cha manabii wako*:* Hakuna hata kamwe ginsi yangu mimi kuachilia mukosefu, lakini ninataka abadilike na awe hai, hautaki, ee Rabi, kupoteza kazi ya mikono yako na haukupenda uharibifu wa wanadamu, lakini unataka kama wote waokolewe na wafike kwa kujuwa ukweli. Tena mimi ninapokuwa mwovu, wa mbingu, wa dunia na wa maisha ya kidunia, mimi ninayetii kamili ku zambi na kuwa mtumwa wa tamaa zangu, mimi nilichafusha sura yako, nikuwapo lakini jambo la mkono wako na muumbwa wako, sikukati tumaini ya wokovu wangu, mimi maskini mzima, kwani mimi niko mtumaini katika rehema yako yasiyo mpaka na ninakukaribia. Unipokee basi, ee Kristu, rafiki wa wanadamu, sawa bibi mkosefu, mwivi, mtenda zambi na mtoto mpotevu na uniokoe ku zambi zangu zote. Wewe unaondoa zambi za dunia na kuponya magonjwa ya wanadamu, wewe unaoita na kutuliza wao wanaoteswa na wanaolemewa, wewe ulikuja kuwaita ku majuto, hapana wenye haki, lakini wakosefu, unitakase uchafu wa mwili na wa roho. Unifundishe kutenda vitendo vitakatifu katika oga yako. Ninapokua na ushahidi mwema wa zamiri, na ninapokea upaji wako takatifu, nitaungana na mwili na damu, utakuwa ndani yangu mkaaji na Baba na Roho Mtakatifu, ndiyo, ee Bwana Yesu Mungu wangu, ushiriki huo ku mistiri zako takatifu na zileta uhai zisiwe nami upatilivu wala hukumu na nisiwe munyonge wa moyo na wa mwili kwa kuyashariki bila ustahilivu. Lakini unipatie kuyapokea daima mpaka mwisho wa pumzi yangu vipaji vyako vitakatifu, bila kupatikana na upatilivu; uwe nami upasho wa Roho Mtakatifu, ukaristia wa mwisho ku uzima wa milele, uhakikisho unaokubaliwa mbele ya hukumu yako ya hofu, kusudi pamoja na wateule wako wote, niwe nami mshariki wa mali isiyo wovu uliotengenezea wao wanaokupenda. Bwana, uhimidiwe katikati yao milele na milele. Amina.

### SALA 2 YA MTAKATIFU BAZILE MKUBWA

Ninajua, Bwana, ya kuwa ninakomunika nisio mstahilivu mwili wako Takatifu na Damu yako yenye bei, niko mukosefu ninakula na ninakunywa uhukumu yangu, ninapokosa kutambua Mwili na Damu yako, lakini ninapoamini ukarimu wako ninakujongea wewe uliyesema*:* Ye yote anayekula mwili na damu anakaa ndani yangu nami ndani yake. Unirehemu Bwana, usiniaibishe, mimi mukosefu, lakini unitendee kadiri ya rehema yako*:* Aina hiyo takatifu iwe nami matunzo, utakaso na mwangaza, ulinzi na wokovu, utakaso wa moyo na wa mwili wangu, ifukuze mbali nami sanamu na vitendo vyote vya shetani zinapojizoeza na roho yangu mpaka na maungu yangu yote; uniongezee kitumaini na mapendo kwangu, ilinde na kutengeneza uzima wangu, iniendeleshe mbele katika njia

ya fazila na ukamilifu; nipate kutimiza amri zako na kushariki Roho yako Takatifu, iwe nami chakula changu cha uzima nitapoingia nacho katika uzima wa milele; iwe nami katazo mbele ya hukumu yako; isiwe nami maamzi ao hukumu. Amina.

### SALA 3 YA MTAKATIFU YOANNE KRISOSTOMO

Ee Rabi Mungu wangu, ninajua ya kama sistahili uingie rohoni mwangu kwa sababu niko mtupu na mharibifu na ndani yangu hauna fasi nzuri wewe kustarehe kichwa chako. Lakini vile kwa sababu ya ajili yetu sisi ulishuka mbinguni na shuka sasa karibu na udogo wangu. Tena ulitaka kuwekwa katika pango na katika sanduku ya kulisha nyama bila sababu, uliingia ndani ya sanduku yakulisha nyama ya roho yangu mupiswa na ya mwili wangu mchafu. Ulipenda kuingia na kula pamoja na wakosefu ndani ya nyumba ya Simoni mukoma kubali kuingia ndani ya nyumba ya moyo wangu mimi mkoma na mkosefu. Haukutupa hata moja anafanana nami, mimi mkosefu, wakati alikujongee na kukugusa wala haukuchukia kinywa chake mchafu na laanifu wakati alikubusu, usichukie vilevile kinywa changu kichafu na laanifu sawasawa chake hata midomo yangu michafu na mikufuru na hata ulimi wangu mchafu pia. Lakini makala ya moto yaliyo katika Mwili wako Takatifu na Damu yenye bei yiwe nami utakaso, mwangaza na afya ya moyo na ya mwili wangu ili itulize makosa mengi mno na kunikinga kwa shetani; ifukuze zoezo zangu mbaya, izuie na kuharibu tamaa, kutimiza amri zako, kuzizidisha na neema yako ya kimungu na kuzikaribisha katika ufalme wako wa milele kwani, ee Mungu, nisikaribie karibu nawe na boka. Lakini na kitumaini katika wema wako nisikose nawe ushirikisho na nishikwe na mnyanganyi mbwa wa mwitu. Ninakuomba kwani uko Mtakatifu mmoja. Bwana, na utakase moyo, roho na mwili wangu, mafigo na matumbo yangu unifanye mpya kamili, tia oga wako katika maungu yangu na utakaso wako ukae ndani yangu. Uwe msaada na mkingaji wangu, kiongozi wa uzima na salama yangu, unifanye mstahilivu wa kuwa mkono wako wa kuume pamoja na Watakatifu wako kwa usimamizi na maombezi ya Mama wako bila doa na nguvu yasiyo mwili Takatifu inaokutumikia na kwa Watakatifu wote walikupendeza tangu mwanzo wa milele na milele. Amina.

### SALA 4 YALEYALE YA MTAKATIFU YOANNE KRISOSTOMO

Ee Rabi na Bwana, sistahili uingie rohoni mwangu, kwa sababu unataka, sawa rafiki ya wanadamu, kukaa ndani yangu mimi ninapokukaribia na uhodari. Uamuru nifunguwe milango iliyo paka wewe peke uliumba kwa kuingia na mapendo yako imara. Utaingia na kwangaza mawazo yangu mabaya, ninasadiki kweli haukufukuza muke mtenda zambi aliyekuja kwako na machozi mbele yako, haukusukuma nyuma mkosefu anaotubu, wala haukumkatalia mwivi wakati walipotambua ufalme wako; ama haukumzarau aliyekuja kutubu haukumwacha, lakini wote waliyekuja kwako kutubu, uliwaweka fasi ya warafiki wako, wewe mbarikiwa pekee wakati wowote, sasa na milele bila mwisho. Amina.

### SALA 5 YALEYALE YA MTAKATIFU YOANNE KRISOSTOMO

Bwana Yesu Kristu, unisafishe mimi mkosefu na mtumishi mwovu. Sahau na unisamehe makosa na zambi niliyokutukana nayo tangu utoto wangu mpaka siku ya leo na saa hii*:* Isipokuwa kwa akili ao kwa upiswa, kwa sauti kwa vitendo ao kwa mawazo, kwa zoezo ao maana yangu yote. Kwa maombezi ya yule aliyekuzaa bila mbegu, Bikira Maria Mama yako, yeye peke kitumaini chetu kisichochanganyikwa, msaada na wokovu wangu; unirudishe mstahilivu nikomunike bila hukumu ku maisha yasiyo mwisho, yenye uzima na maumbo ya maondoleo ya zambi zangu, na uzima wa milele kwa utakaso, mwangaza, utunzo na afya ya moyo na mwili wangu kwa maondoleo na maangamizi ya mawazo yangu mabaya, ya kusudi na kwa mawazo yangu ya ngiza ililetwa na roho za ngiza na kali. Kwa kuwa kwako ni utawala, uwezo na sifa; Utukufu na ibada kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

## SALA 6 YA MTAKATIFU YOANNE DAMASCENI.

Ee Rabi, Bwana wetu Yesu Kristu, Mungu wetu, wewe peke una uwezo wa kuondoa zambi, wewe rafiki wa wanadamu, unisamehe zambi zangu zote ninazofahamu na nisizofahamu, nistahili bila kuhukumiwa, niungane na mafumbo yako Matakatifu ya bumungu yenye kuleta uzima. Bila kuvuta azabu, masumbuko na kuongeza zambi zangu, nitakaswe na niwe rahani ya uzima wa ufalme utakayokuja, ukingo na msaada zitawanye wadui zangu na ziondoe zambi zangu nyingi. Kwa sababu uko Mungu Mwema, wa huruma na wa mapendo ya wanadamu na tunakushukuru na Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## SALA 7 YA SIMEONI MUTHEOLOGO MUPYA

Kwa midomo iliochafuka, kwa roho mubaya, kwa ulimi ulioambukizwa, kwa moyo muchafu, kamata sala, ee Kristu wangu, usinifukuze mbali nawe, kwa vitendo na mifano yangu mibaya, hata kwa ukosefu wangu wa haya, unisaidie niseme kwa uhodari, ee Kristu wangu, yote yaliyo ndani ya roho yangu, lakini ni vizuri zaidi unifundishe, yaliyo ya kutenda na yaliyo yakunena. Nilifanya zambi kuliko zile za mzinifu, ambaye aliposikia wapi unapoikala, alinunua manukato, alipofika akapakaa kwa uhodari, miguu yako, Kristu wangu, ya Rabi na ya Mungu wangu.

Kama vile haukumufukuze yule, aliyejikaribia kwa haraka kwa haraka. Pamoja nami mwana, usinifukuze mbali nawe, unipe miguu yako nitakayogusa na kuyabusu, na kwa mitoni mingi ya machozi, kama manukato ya bei mingi, nitakuja kwa uhodari kukupakaa. Kwa machozi yangu unisafishe mwana, unitakase, ee Bwana. Uniachilie ukosefu wangu; unipe rehema yako. Unapojua idadi ya zambi zangu, unajua madonda yangu; na unajua maumivu yangu; lakini unapojua imani yangu, unajua haraka yangu, na unasikia kite langu, bila kufichwa. Mungu wangu. Muumba wangu. Mwokozi wangu hata tone ya machozi, hata sehemu ya tone.

Kwa jambo la ugumu wangu, macho yako yaliona; kitabuni chako, hata zambi zangu zote nitakazo fanya, zinandikizwa. Angalia unyenyekevu wangu, unaona mchoko wangu, ee Bwana Mungu, uniachilie ukosefu wangu; ili roho yangu isafishwe, kwa hofu ya akili, na moyo nyenyekevu, nikamate kwa bila doa, siri zako takatifu, ambako atekukamata uzima na atekugeuzwa Mungu, yeyote atakayekula na atakaye kunywa, na roho ya ukweli. Kwani, ee Rabi wangu, ndivyo ulivyo sema, Yeye mwenye kula mwili wangu, na kunywa damu yangu, nami ndani yake, neno la Rabi Mungu wangu ni kweli japo lolote. Akamataye vipaji Takatifu na neema ya vitu kimbingu, habaki pekee lakini pamoja nawe, ee Kristu wangu, nuru ya Utatu Mtakatifu, yaletayo mwangaza duniani.

Basi ili nisibaki peke. Mbali nawe mwenye kutoa uzima, pumzi yangu, uzima wangu, furaha yangu, wokovu wa dunia, kwa hiyo ninakukaribia kama unanipoona na machozi na moyo wenye sikitiko ninakuomba unipe fidia ya makosa yangu, yaleta uzima na mistiri safi, kuyashariki bila kulaumu ili ibaki sawasawa ulivyosema, karibu nami mukosefu; ili nisipate pasipo neema yako yenye kudanganyika, kusudi nikamate mwenye udanganyi abembelezaye kwa kunikamata neno lako kimungu. Kwa hiyo ninakusujudia, na kwa uvuguto ninakulilia; sawasawa uliyemupokea mupotevu na kahaba aliyekukaribia, pamoja unipokee nami kahaba na mupotevu, ewe mwenye huruma, na moyo wenye sikitiko, ninapokukaribia hapa sasa.

Mwengine alifanya kosa kuliko mimi, na kufanya yaliyo mabaya, sawasawa niliotenda mimi. Lakini kwa hiyo ninajuwa mara ingine kuomba hakuna unene wa kosa, na idadi ya zambi kupita kwa Mungu wangu, wingi wa uvumilivu na mapendo ya wanadamu yasiyo na mwisho; lakini kwa mafuta ya pendeleo, ya watu wanaotubu kwa uvuguto unawasafisha na kuwaangarisha, na kuwasharikisha mwangaza yako, wenzi ya umungu wako. Unawaleteya neema yako mingi mno; na jambo hilo la ajabu na la malaika, na akili ya binadamu. Unaposumulia na wale mara nyingi, sawa marafiki zako za kweli na mambo haya yote yananipatia uhodari. Na mambo haya yote yananipa mabaya Kristu, na ninapata uhodari wa neema ya utajiri wako, ya furaha na kutetemeka pamoja, ninakomunika moto yako, ninapokuwa majani na muujiza ya ajabu! Ninashikwa na baridi jinsi isiyoweza kusema sawasawa kijiti cha zamani kiliwaka lakini hakikuteketei. Basi, uniwe razi ya

wazo langu, uniwe razi ya roho yangu, uniwie razi ya vipindi vya mwili wangu, ya roho na ya mwili wangu, ninakubusu kwa mazidisho, na ninakukuza wee Mungu wangu, sawa mhimidiwa kweli sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

### SALA 8 YA SIMEONI MFASIRI

Ee Bwana, wewe peke mtakatifu na bila doa, uliye na rehema na mapendo kwa wanadamu, uliyechukua hali yetu nzima na damu yako takatifu na ya ubikira wa yule alikuzaa kwa usimamizi wa Roho Mtakatifu na kwa ukubali wa Baba wa milele. Kristu Yesu akili ya Mungu, amani yake na nguvu yake aliyependa kuongeza kujifanya mtu, mateso yako yenye uzima na ya ukombozi, msalaba, musumari, mukuki, kifo, ziharibu, tamaa mbaya inaouwa roho yangu. Wewe uliyetwalia ufalme wa shetani kwa maongezi yako mema na kukuza roho zangu chafu. Wewe, kwa ufufuko wako siku ya tatu, uliinua jiwe letu lililoanguka; nilianguka katika zambi, unishimamishe unipatie majuto, wakati uliopanda mbinguni, uliwapatia wanadamu maisha kuchukuliwa kwako juu na kuituza kwa makao yako mkono wa kuume wa Baba. Nistahili ku komonyo na kupata fazi mkono wa kuume kati ya wenye kuokoka. Kwa ukoo wa Roho Mtakatifu. Mfariji, ulishukuru mitume wako kwa chombo cha heshima, unifanye niwe makao mastahilivu ya kuja kwako. Wewe utakaokuja tena kuhukumu ulimwengu na uhaki wote, uniruhusu nami kuja mbele yako mwamzi na mwumba wangu. Kwa Baba yako na kwa Roho Mtakatifu, Mwema na Mpaji wa roho na uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

### SALA 9 YA YOANNE DAMASCENI

Ninasimama mbele ya milango ya hekalu yako na mawazo mabaya yanaokataa kunitoka. Lakini wewe Kristu Mungu ulihakikisha mtoza ushuru aliyemhurumia mkanana moja aliyemfungulia mwivi milango ya mbinguni, unifungulie basi nami matunbo ya mapendo ya binadamu na unipokee nami ninakukaribia na kukugusa sawa yule mwanamke kahaba na mbawasiri, mmoja alipogusa kanzu yako*:* Na alipata sasa hivi kupona, na mwengine aliposhika miguu yako takatifu, aliondolewa zambi zake zote. Na vilevile nami mkosefu, wakati ninaposubutu kupokeya mwili wako kamili nisiteketezwe. Lakini unipokee sawa wale wawili na angazia makosa ya moyo wangu unaonguza uinamizi wa zambi kwa maombezi ya yule bila doa alikuzaa kwa nguvu ya mbinguni, kwa sababu uko mbarikiwa milele na milele.

## SHUKRANI YA NEEMA IBADA YA KOMONYO KIMUNGU

### SALA 1

Unapokamata vizuri komonyo, siri hizi zinaleta uzima. Unisifu na unishukuru. Mkuu, na sema kwa rafla rohoni mwako na uvuguto Kimungu, (utukufu kwako, ee Mungu); *(mara tatu).*

Ninakushukuru, ee Bwana Mungu wangu kwa sababu haukunifukuze mimi mtenda zambi, lakini ulinistahilisha mimi mwovu, kwa kushariki kusiri zako takatifu za mbingu, lakini, wewe Rabi, rafiki wa wanadamu, uliyekufa na kufufuka kwa ajili yetu na uliyetupa siri za uzima kwa mema na utakaso wa moyo na wa mwili; fanya ili ziponye roho na mwili wangu, zifukuze adui yeyote, yangazie macho na roho yangu, zilete salama moyoni mwangu, kitumaini yasio haya, mapendo ya kweli, hekima kubwa, utii wa amri zako, uzindisho wa neema ya Mungu ndani yangu na upatanisho wa ufalme wako. Nitakumbuka siku zote neema yako uliyeweka katika utakaso wako, halafu sitaishi tena mimi mwenyewe, lakini na wewe Bwana na mkarimu wangu. Nikipoishi katika kitumaini ya uzima wa milele, nitafika halafu katika mapumziko yasiyo mwisho, kutapokuwapo furaha yasio mpaka, ya wao wataostajabu uzuri wa uso wako kukamwa, Kwa sababu uko kweli kweli yeye

ambako tunaokwenda kuvuta pumzi na furaha yasio alama ya wao wanaokupenda, ee Kristu Mungu*:* viumbe vyote vinakuimbia milele na milele. Amina.

**SALA 2 YA MTAKATIFU BAZILE MKUBWA**

Ee Rabi, Kristu Mungu Mfalme wa karini na muumba wa vitu vyote, ninakushukuru kwa wema wako wote uliyenipatia na kwa Komonyo ya siri zako takatifu, ninakuomba, ee Mungu wangu mwema na mpenda wanadamu, unilinde chini ya kivuli ya mabaya yako*:* Unifanyizie mpaka siku zangu za mwisho, nistahili kupokea mafumbo yako na ufahamu mwema kwa maondoleo ya zambi na ya uzima wa milele. Kwa sababu uko mkate wa uzima, chemchem takatifu, mgawanya wa mema na tunakutukuza pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SALA 3 YA SIMEONI MFASIRI**

Wewe uliyenipa kwa masudi, mwili wako mu chakula, wewe unaokua moto unaonguza waovu usinichome, ee Mwumba wangu; Lakini ingia katika maungu yangu, mu vingo vyangu vyote, mu utumbo wangu na mu roho yangu. Choma miiba ya makosa yangu. Safisha roho yangu, takasa mawazo yangu. Sabitisha viungo na mifupa yangu. Angazia vifungu vyangu tano vya mwili. Unilinde siku zote, unikinge na unilinde ku vitendo vyote ao ku sauti ya mauti juu ya roho yangu, unisafishe na unioshe, unipambe, unitengeneze, unifundishe na uniangaze. Unifanye makao ya roho moja tu, na isiokua makao ya zambi. Na, ninapokua nyumba yako ulipoingia kwa komonyo, roho mubaya na ya tamaa inikimbiye sawa moto, ninaomba usimamizi ya wale wote wanaotakaswa, majeshi ya wasio mauti, Mtangulizi wako, Mitume wako wa arifa, na hata kuliko vyote, Mama wako Mtakatifu na bila doa, Ee Kristu wangu, kubali kupokea na huruma maombi yao, na fanyizia Mwana wako kwa mtumishi wa mwangaza. Kwa sababu uko Mungu mwema Mtakasa wa pekee na mwangazaji wa mioyo zetu na wote tunakukuza namna inayofaa, wewe Mungu wetu na Rabi wetu. Amina.

**SALA 4**

Mwili wako na damu yako, ee Bwana Yesu Kristu, inipe uzima wa milele, na damu yako ya bei iwe nami maondoleo ya zambi. Na ukaristia huo unijalie furaha, afya na heri. Wakati wa ujio wako wa pili wenye hatari, unistahilishe, mimi mkosefu, kukaa kuume kwako kutukufu, kwa maombezi ya Mama wako Mtakatifu kabisa na ya Watakatifu wote. Amina.

**SALA 5 KWA BIKIRA MZAZI-MUNGU.**

Ee Malkia Mtakatifu kamili, Mama wa Mungu, Mwangaza wa moyo wangu uliotiliwa gizani, tumaini langu, tegemeo yangu, kimbilio langu; faraja na heri zangu, ninakushukuru pakunistahilisha mimi mwovu kwa kukumunika mwili takatifu na damu heshimiwa ya Mwana wako. Wewe uliyezaa nuru ya kweli, angazia macho ya kiroho ya moyo wangu. Wewe uliyezaa chemchem ya uzima wa milele, unirudishiye uzima, mimi niliyeuwawa na zambi. Wewe Mama wa Mungu wa huruma moyoni mwangu, unihurumie, huzunisha na sikitisha moyo wangu, unyenyekevu ndani ya mawazo yangu na ufikiri katika akili yangu. Unistahilishe mpaka siku yangu ya mwisho, kwa kupokea bila hukumu utakaso wa siri zako takatifu, kwa uponya wa moyo wangu na wa mwili wangu. Unipe machozi ya majuto na ya ungamo, ili nikuimbie na kukusifu siku zote za uzima wangu, (kwa sababu uko mbarikiwa na mjaliwa na utukufu milele. Amina). *(mara tatu).*

*Padri atasoma wimbo wa Simeoni.*

Sasa, ee Rabi, uruhusu mtumishi wako aende kwa utulivu kama ulivyosema, kwa sababu macho yangu yameona wokovu wako ulioweka tayari mbele ya macho ya watu wote; Nuru ya kwangazia mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli (Luka 2, 29).

**SHEMASI** ao **MSOMAJI**: Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Utatu Mtakatifu kamili utuhurumie. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Baba yetu uliye mbinguni. . .

**Apolitikion ya Mtakatifu Yoane Krisostomo.** Sauti ya mnane

Kwa kinywa chako kama taa, neema imechuruzika na ulimwengu uliangaziwa, umevumbua hazina ya uadili, umetuonyesha ukuu wa unyenyekevu. Utafundisha kwa kinywa chako, ewe Baba wetu Yoane Krisostome, utuombee kwa Bwana, Kristu Mungu, aokoe mioyo yetu.

**Kontakion Sauti ya sita**

Utukufu kwa Baba. .

Kwa mbingu, umepokea neema kimungu, na kwa midomo yako wote tunafunza kumwabudu Mungu moja katika Utatu, ee Yoane Krisostomo, Mtakatifu mwenye heri, tunakusifu kwa ustahilivu, kwani hauishe kutufundisha, unatuangazia vitu takatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Sasa na siku zote. .

Kwa maombezi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, ee Bwana, utupe amani yako na utuhurumie, kwani Wewe peke yako mwenye huruma.

**Apolitikion ya mtakatifu Bazili askofu ya Kesaria wa Kapadokia**
**Sauti ya kwanza**

Sifa yako imeenea duniani kote kumepokelewa neno lako. Kwa neno lako, umetufundisha elimu umetufunulia hali ya viumbe, umenyosha desturi za wanadamu. Baba mtukufu, Kohani mfalme, umusihi Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

**Kontakion Sauti ya ine**

Utukufu kwa Baba. . .

Umeonakana kama msingi imara wa Eklezya yote, ukawapa wenyi mauti wote uwezo wako kama makimbilio na ukawatilia muhuri wa mafundisho yako, ee Baasile mtukufu, Baba wa mayatima.

Sasa na siku zote. . .

Kwa maombezi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, ee Bwana, utupe amani yako na utuhurumie, kwani Wewe peke yako mwenye huruma.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Bwana hurumia *(kumi na pili).* Uliye wa thamani. . Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . Kwa jina la Bwana, Padri mtakatifu, bariki.

*Padri atafanya kuaga.*

Utukufu kwako, ee Mungu, matumaini yetu, utukufu kwako.

Uliye umefufuka katika wafu Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombezi ya Mama wako Mtakatifu asiye na doa wala na lawama kamili. Kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapadri wetu Watawa na wabebaji-Mungu, ya Yoakimu na Anna Mababu-Mungu, Watakatifu, na wenye haki, hata ya Watakatifu wote, utuhurumie, ukatuokoe sawa Mungu Mwema, marahimu na mpenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

*Kisha kunawa mikono Padri na Shemasi watapiga magoti mara tatu mbele ya Altare, wataibusu. watatoka Hekaluni wakimutukuza na kumushukuru Mungu kwa vyote.*

## NYIMBO ZA KUINGIA KATIKA SIKU KUU

***KUZALIWA KWA KRISTU***

Nimekuzaa tumboni mwangu mbele ya nyota ya asubui. Bwana ameapa wala hatageuka. Wewe ni kuhani hata milele, kwa namna ya Melkisedeki (zab. 109 (110). Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyezaliwa kwa Bikira, tunaokuimbia, Alliluia.

***KU TOHARA.***

Kujeni, tumwabudu na tumsujudu Kristu. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, wewe uliyetahiriwa katika mwili, tunaokuimbia. Alliluia.

***EPIFANIA.***

Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana; Bwana ni Mungu naye ameonekana kwetu. (Zab. 117 (118). Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyebatizwa na Yoane, katika Yordani, tunaokuimbia. Alliluia.

***KUKUTANA KWA BWANA.***

Bwana amefunua wokovu wake mbele ya mataifa yote (Zab; 97 (98), 2). Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyebabwa mikononi mwa mwenye haki Simeoni, tunaokuimbia. Alliluia.

***HABARI NJEMA YA BIKIRA.***

Siku kwa siku tangazeni wokovu wa Mungu wetu (Zab. 95 (96), 2). Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyepata mwili kwa Bikira, tunaokuimbia. Alliluia.

***KUGEUZA SURA.***

Tabori na Hermoni inafurahia jina lako (Zab. 88(89), 13). Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyegeuza sura mlimani wa Tabori, tunaokuimba. Alliluia.

***KUPAZWA KWA MSALABA MTAKATIFU.***

Tukuzeni Bwana Mungu wetu, na msujudu mbele ya miguu yake, kwani Yeye ni Mtakatifu. Utuokoe, wewe uliyesulubiwa mwilini, tunaokuimbia. Alliluia.

***SIKU YA MUNGU YA MATAWI.***

Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana! Bwana ni Mungu naye ameonekana kwetu (Zab. 117 (118), 26). Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, Wewe uliyepanda mwana-punda, tunaokuimbia. Alliluia.

***SIKU YA MUNGU YA PASKA.***

Katika makusanyo yenu, mtukuzeni Mungu, mtukuzeni Bwana, enyi wazao wa Israeli (Zab. 67(68), 27). Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

***KUPANDA MBINGUNI.***

Mungu amepanda kwa mashangilio, Bwana kwa mlio wa baragumu (Zab. 46, 6). Utuokoe, ee Bwana wa Mungu, Wewe uliyepanda kwetu na utukufu mbinguni, tunaokuimbia. Alliluia.

***SIKU YA MUNGU YA PENTIKOSTI NA SIKU YA ROHO MTAKATIFU.***

Simama, ee Bwana, kwa enzi yako, nasi tutaimba na kutukuza nguvu yako (Zab. 20 (21), 14). Utuokoe, ee Mfariji Mwema kamili, tunaokuimbia. Alliluia.

# KUAGA KATIKA SIKU KUU ZA BWANA

***KUZALIWA KWA KRISTU***

Yeye aliyezaliwa kwa ajili ya wokovu wetu katika pango na kulalishwa katika sanduku ya kulishia wa nyama, Kristu, Mungu wetu kweli. . .

***TOHARA.***

Yeye aliyekubali kutahiriwa mwilini siku ya nane kwa ajili ya wokovu wetu, Kristu Mungu wetu kweli. . .

***EPIFANIA.***

yeye aliyekubali kubatizwa ya Yoane katika Yordani kwa ajili ya wokovu wetu, Kristu Mungu wetu kweli. . .

***KUPELEKEWA KWA KRISTU HEKALUNI.***

Yeye aliyekubali kubebwa mikononi mwa mwenye haki simeoni kwa ajili ya wokovu wetu, Kristu mungu wetu kweli. . .

***KUGEUZA SURA.***

Yeye aliyegeuza Sura kwa utukufu mlimani wa Tabori, mbele ya Wafrwasi na Mitume wake Watakatifu, Kristu Mungu wetu kweli. . .

***SIKU YA MUNGU YA MATAWI.***

Yeye aliyekubali kupanda mwana-punda kwa ajili ya wokovu wetu, Kristu Mungu wetu kweli. . .

***SIKU YA MUNGU ILE ILE MANGARIBI NA MPAKA SIKU YA TATU TAKATIFU***

Bwana alipoteswa kwa kutaka kwake kwa ajili ya wokovu wetu, Bwana Kristu Mungu kweli. . .

***SIKU YA INNE TAKATIFU.***

Yeye katika wema wake mkubwa, aliyeonyesha kwa kuwanawisha Wafwasi wake miguu ya kama unyenyekevu ulikuwa ni njia bora tena aliyejishusha kwa ajili yetu mpaka Msalabani na Kaburini, Kristu Mungu wetu kweli. . .

***IBADA YA ASUBUI YA SIKU YA TANO TAKATIFU***
***(IBADA YA MATESO YA KRISTU)***

Yeye, kwa ajili ya sisi wanadamu na kwa ajili ya wokovu wetu, alikubali kwa kutaka kwake kuteswa mwilini, Msalabani na hata Kaburini, Kristu Mungu wetu kweli. . .

***SIKU YA MUNGU TAKATIFU NA KUU YA PASKA, MPAKA MASINDIKIZO YA PASKA, NA KILA SIKU YA MUNGU YA MWAKA MZIMA.***

Aliyefufuka katika wafu, kristu Mungu wetu kweli. . .

***KUPANDA MBINGUNI.***

Yeye aliyepanda mbinguni katika utukufu tena anayekaa kuuma kwa Mungu Baba, Kristu, Mungu wetu kweli. . .

***SIKU YA MUNGU YA PENTIKOSTI.***

Yeye aliyewatumia Wafwasi na Mitume wake Watakatifu Roho Mtakatifu kamili toka mbinguni kama ndimi za moto, kristu Mungu wetu kweli. . .

***SIKU YA MUNGU ILI ILE KU ESPERINOS.***

Yeye ambaye, katika kifua cha Mungu Baba akajinyenyekeza, akashuka toka mbinguni hata duniani, akashukua hali yetu na akaifanya kuwa Mungu; yeye aliyepanda Mbinguni na kukaa kuume kwa Mungu Baba aliyewatumia Wafwasi Mitume wake Watakatifu Roho wa Mungu, Mtakatifu, wa asili moja na Baba, sawasawa naye kwa uwezo na utukufu na wa milele; yeye aliyewaangazia hivyo Nayo, na katika wao, ulimwengu wote, Kristu, Mungu wetu kweli, kwa maombi ya Mama yake asiye na doa, mtakatifu kamili, ya Mitume Watakatifu, watukufu na wasifiwa, wahubiri kimungu na wenye Roho Mtakatifu, na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani Yeye ni Mwema na Mpenda-wanadamu.

# WIMBO YA USHIRIKA WA SIKU ZA JUMA

***KILA SIKU YA MUNGU.***

Musifuni Bwana kutoka mbinguni, musifuni katika pahali pa juu pia. Alliluia.

***MUKAZI MOJA (WA MAJESHI YA SIYO NA MWILI)***

Unayefanya malaika wake kuwa roho, na watumishi wake kuwa ndimi za moto. Alliluia.

***MU KAZI MBILI (WA MBATIZAJI YOANE MHESHIMIWA)***

Mutu mwenye haki atakumbuka milele. Alliluia.

***MU KAZI TATU )WA MZAZI-MUNGU MTAKATIFU KAMILI).***

Nitaita Kikombe cha wokovu, nitaliomba jina la Bwana. Alliluia.

***MU KAZI INNE (WA MITUME WATAKATIFU).***

Lakini uvumi wao waenea duniani kota na maneno yao hata mipaka ya ulimwengu. Alliluia.

***MU KAZI TANO (WA MSALABA).***

Ee Bwana, uinue mwanga wa uso wako juu yetu. Alliluia. Ao*:* Ee Kristu Mungu ulifanya katika inchi matendo ya wokovu. Alliluia.

***MUPOSHO (WA WAFU).***

Heri wale uliowachagua na kuwapokea, ee Bwana; tena ukumbusho wago mpaka kizazi kwa kizazi. Alliluia.

# USHIRIKA ZA SIKU KUU WA MUNGU YESU KRISTU

***KUZALIWA KWA KRISTU.***

Bwana, amewapelekea taifa lake ukombozi. Alliluia.

***EPIFANIA.***

Neema ya wokovu wa Mungu ilionekana ku watu wote. Alliluia.

***USUJUDU WA MSALABA MTAKATIFU.***

Ee Bwana, uinue mwanga wako juu yetu. Alliluia.

***SIKU YA MUNGU YA MATAWI.***

Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana. Alliluia.

***SIKU MU KAZI INNE MKUBWA KWA JUMA YA MATESO YA MUNGU YESU KRISTU.***

Ee Bwana wa Mungu unipokee mimi leo, ku karamu yako ya fumbo*:* kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Mnyanganyi, na kuungamia*:* Ee Bwana unikumbuke, katika ufalme wako.

***SIKU MUPOSHO MKUBWA KWA JUMA YA MATESO.***

Hapo Bwana aliamka kama aliyelala usingizi akafufuka akituokoa. Alliluia.

***SIKU YA PASKA.***

Shirikeni Mwili wa Kristu, onjeni chemchem ya kutokufa. Alliluia.

***SIKU YA MUNGU YA MUTUME THOMAS.***

Umutukuze Bwana, ee Yerusalema, umusifu Mungu wako ee Siyoni. Alliluia.

***SIKU YA TATU KATIKATI YA PENTIKOSTI.***

Bwana akasema; anayekula mwili wangu na kunwa damu yangu anao uzima wa milele. Alliluia.

***SIKU YA KUPANDA MBINGUNI.***

Mungu amepanda kwa mashangilio, Bwana kwa mlio wa tarumbeta. Alliluia.

***SIKU YA PENTIKOSTI.***

Roho yako mwema aniogoze kwenye inchi sawa. Alliluia.

***SIKU YA MAGEUZO SURA YESU KRISTU.***

Ee Bwana, tutaendelea katika nuru ya utukufu wa Uso wako, tena tutafurahiwa kwa jina zako hata milele. Alliluia.

***KUPAZWA KU MSALABA MTAKATIFU.***

Ee Bwana, uinue muanga wako juu yetu. Alliluia.

## USHIRIKA ZA SIKU KUU YA MZAZI-MUNGU

***BWANA HABARI NJEMA YA MZAZI-MUNGU MARIA BIKIRA.***
Bwana ameichagua Siyoni; ametamani iwe makao yake. Alliluia.
***KWA WENGINE WOTE WA SIKU KUU YA MZAZI-MUNGU.***
Nitainua Kikombe cha wokovu, nitaliomba jina la Bwana. Alliluia.

## USHIRIKA YA WATAKATIFU WENGINE.

***KWA SIKU KUU ZA MALAIKA ZOTE.***
Anayefanya malaika wake kuwa roho na watumihsi kuwa ndimi za moto. Alliluia.
***KWA SIKU KUU YA MTAKATIFU YOANE MTANGULIZI NA MBATIZAJI.***
Mwenye haki atakumbuka milele. Alliluia.
***KWA KILA SIKU KUU YA WATAKATIFU WOTE.***
Ee wenye haki, shangilieni kwa Bwana, sifa ni haki ya wa sawa wao. Alliluia.
*Kwa siku kuu ya mitume Petro na Paulo ya makumi na mbili ya Waevangelizaji Inne, ya Mtakatifu Mtume Andrea, wa askofu wa tatu Wakuu na ya Watakatifu Konstantino na Elena.*
Ee wenye haki, shangilieni kwa Bwana, sifa ni haki ya wasawa wao.

## WIMBO YA KHERUVIKON PA FASI YA ILE TUNAIMBA KILA MU JUMA.

### KHERUVIKON YA LITURGIA WENYE KUTAKASWA (PROIGIASMENI)

Sasa ezi za mbinguni bila kuwaona, wanaabudu pamoja nasi. Kwani tazama Mfalme wa Utukufu anaingia. Tazama matoleo ya sisi, ni kamili wanaishindikiza. Tukaribie na imani na juhudi, ili tusharikie ku uzima wa milele. Alliluia

### KHERUVIKON YA MUKAZI INNE MKUBWA YA JUMA TAKATIFU

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho*:* Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia*:* Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

### KHERUVIKON YA MU POSHO MKUBWA YA JUMA TAKATIFU

Kila mwenye pumzi anyamaze, asimame na woga na atetemeke; aweke mbali wazo lote la dunia. Kwani Mfalme wa Wafalme na Bwana wa mabwana anajongea ili ajitoe mu sadaka na awe chakula cha Waaminifu. Makundi ya Malaika wanamutangulia na Watawala, wenye uwezo, Wakeruvi wenye macho mengi na Waserafi wenye mabawa sita wenyi kujifunika uso, wakiimba*:* Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu.

### MAJIBU YA PADRI KISHA YA KILA ODE YA KANUNI YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU

WIMBO 1
**PADRI***:* Kwa kuwa ni Kwako uwezo na utawala na nguvu na utukufu ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
WIMBO 3
**PADRI*:*** Kwa kuwa Wewe ni Mungu wetu, na Kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

**PADRI*:*** Kwa kuwa u Mungu Mwema na mpenda wanadamu na Kwako tunakutolea utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

WIMBO 5

**PADRI*:*** Kwa kuwa Jina lako liheshimiwa na utukufu kamili limetakaswa na kutukuzwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote. . .

WIMBO 6

**PADRI*:*** Kwa kuwa Wewe u Mfalme wa amani tena Mwokozi wa roho zetu na Kwako tutautoa utukufu, kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hate. . .

**PADRI*:*** Kwa kuwa uwezo ya ufalme wako ubarikiwa na utukuzwa ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu. . .

WIMBO 8

**PADRI*:*** Kwa kuwa imabarikiwa Jina lako na imetukuzwa Ufalme wako ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata. . .

WIMBO 9

**PADRI*:*** Kwa kuwa ya nakusifu majeshi yote ya mbinguni na kuleta utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata. . .

## FUNDISHO YA MT. BABA YETU YOANE KRISTOSTOMO.
## (Padri anaisoma hii Fundisho ku mwisho ya Liturgia wa Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu)

Mtu wowote mwabudu tena rafiki wa Mungu afurahiwe juu ya mwangaza huiwa siku kuu nzuri. Mtumishi wowote mwema awe na furaha kubwa kwa ajili ya Bwana wake! Yule alijitolea katika mafungo apate kupokea sasa mushahara wake! Yule alitumika tangu saa ya kwanza apokee sasa mushahara wake wa kweli kweli. Kama mumoja alikuja kisha saa ya tatu afurahiwe siku hiyi na kuyishukuru! Kama mumoja alichelewa mpaka saa sita, asikuwe na shaka, kwa sababu hapoteze kitu! Kama kuna mmoja aliongojea mpaka saa tisa, ajongee bila shaka! Kama kuna mmoja alichelewa mpaka saa kumi na moja, asiwe na haya ya ukosefu wa huhudi yake, kwa sababu Rabi ni mweme, anapokea wa mwisho kama vile wa kwanza. Anapokea ku mapumziko yule wa saa ya kumi na moja sawa mtumishi wa saa ya kwanza. Anahurumia wa mwisho tena anatunza wa kwanza. Analeta kwa huyu, na anahurumia mwengine. Anapokea ku mapumziko yule wa saa ya kumi na moja sawa mtumishi wa saa ya kwanza. Anahurumia wa mwisho tena anatunza wa kwanza. Analeta kwa huyu, na anahurumia mwengine. Anapokea matendo tena anakubali mwoyo mwema kwa mapendo. Anaheshimia tendo tena anasifu nia nzuri. Kwa hivi, muwe wote na furaha ya Bwana wenu; wa kwanza kama wa mbili, mutapokea tunzo lake. Watajiri sawa wamaskini, wenyi kukataa na wavivu muungane wote juu ya kusifu siku hiyi. Kama mulifunga ao hamukufunge, leo mufurahiwe. Meza iko tayari, kuleni wote; mwana ngombe eko tayari, hata mmoja asirudi na njaa. Mukubali wote ku karamu ya imani, ku hazina ya wema. Hata mumoja asisikitike juu ya umaskini wake, kwa sababu Ufalme unaonekana kwa ajili ya wote. Hata mumoja asilielie juu ya makosa yake, kwa sababu huruma unatokea kaburini. Hata mumoja asiogope lufu, kwa sababu kifo ya Bwana ilitukomboa wote; alimaliza lufu kisha kufa kwake. Yeye alishuka katika wafu, kwa kifo chake ameshinda mauti. Alijaza lufu na uchungu wakati mwili wake ulishuka kuzimu ya wafu. Na kwa hiyo Nabii Isaya alieleza ya kama*:* Lufu lulisirika wakati mulipatana ku udongo. Lufu ilizania ya kama ni mwili wa wanadamu, lakini alikuwa Mungu mbele yake; ilizania ya kama ni mwanadamu, lakini ni mtawala wa mbingu; ilikamata kile iliona, ilianguka kwa sababu haikujue umungu wake.

Ee lufu, wapi ushindi wako?

Kaburi, wapi ushindi wako?

Kristu amefufuka, lakini wewe unanguka chini. *(Taifa anajibu: Amefufuka)*

Kristu amefufuka, mashetani wanaanguka.

Kristu amefufuka, malaika wanafurahiwa.
Kristu amefufuka, tazama uzima unatawala.
Kristu amefufuka, hakuna wafu kaburini.
Kwa sababu Kristu amefufuka katika wafu waliotangulia kulala.
Kwa kuwa Utukufu na Uwezo ni kwake milele na milele. Amina.

**APOLITIKION YA MTAKATIFU YOANE Sauti ya Mnane**

Kwa kinywa chako kama taa, neema imechuruzika na ulimwengu uliangaziwa, umevumbua hazina ya uadili, umetuonyesha ukuu wa unyenyekevu. Utafundishe kwa kinwa chako, ewe Baba wetu Yoane Krisostome, utuombee kwa Mwana, Kristu Mungu, ili mioyo zetu ziokoke.

*Waimbaji awataimba:* Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa. . *lakini wataimba mara tatu:* Kristu alifufuka katika wafu. .

*Padri ku mwisho ya Liturgia atapaza sauti na msalaba pa mukono yake atasema mbele ya waaminifu wote:* Kristu alifufuka. *Waaminifu watajibu:* Kweli alifufuka. *(Vile watafanya mara tatu). Kisha padri atasema:* Utukufu kwa Ufufuo wake Takatifu wa siku tatu.

*Waaminifu watamujibu:* Tunasujudu Ufufuo wake wa siku tatu.

*Na kisha watu wote wataimba:* Kristu alifufuka katika wafu kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima.

## IBADA YA TRISAYO KWA WAFU

*Kisha Trisagio:* Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mtakatifu. . Baba yetu. .

*Kisha tunaimba Hii wimbo. sauti ya Ine.*

(Meta pnevmaton dikeon).

Pamoja na roho za wenyi haki kamilifu, ee Mwokozi, pumzisha roho ya watumishi wako na uichunge hii mu uzima wa heri uliyo karibu nawe, ewe rafiki ya wanadamu.

(Is tin katapafsin su).

Pa fasi ya ukimya, ee Bwana, kule watakatifu wote wanapumzika, pumzisha na roho ya watumishi wako, kwa sababu wewe ni msiye kufa.

Utukufu kwa Baba. .

(Si i o Theos imon).

Wewe Mungu wetu, ulishuka kuzimu na kufungua maumivu ya wafungwa, Ewe mpumzisha na roho ya watumishi wako, Mwokozi.

Sasa na siku zote (I moni Agni).

Wewe peke safi na asiye doa Bikira, uliyemzaa Mungu msiye kufa wa kusemwa, umuombe aokoe roho ya watumishi wake.

**PADRI***:* Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**PADRI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu, watawa na waorthodoksi wote.

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu (jina lake).

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**PADRI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya Raisi Mukubwa yetu (*jina lake*), ya watawala, Taifa, waaskari na watu wote.

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**PADRI** ai **SHEMASI***:* Tena tunakuomba kwa ajili ya wandugu wanaogombana vita kwa utukufu wa Taifa letu, wa tangu zamani ao wa sasa kwa ukumbusho wa pumziko ya heri ya mioyo yao milele na ya ondoleo ya zambi yao ya kusudi na yasiyo kusudi, ya hufahamu na yasiyofahamu.

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**PADRI***:* Tena tunakuomba mapumziko ya moyo wa watumishi wa Mungu tangu mwanzo ya dunia mupaka sasa na uwasamehe makosa yao yote ya kupenda na yasiyo kupenda.

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana.

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia.

**PADRI***:* Ee Mungu wa roho na wa mwili, uliyeshinda lufu na kumuharibu shetani, wewe uliyeleta uzima duniani, leta, ee Bwana, mapumuziko kwa roho ya watumishi wako pahali pa mwangaza, pa majani mazuri, pa mapumziko, kule kunakimbia maumivu, sikitiko na masumbuko. Uwasamehe zambi zao zote walitenda kwa sauti, kwa matendo na kwa mawazo, kwa sababu Wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu; kwani hakuna mutu hata moja, anakaa mu uzima huu pasipo kufanya zambi; kwa sababu wewe peke yako msiye zambi; haki yako, ni haki ya milele, na amri yako na ya kweli.

**SHEMASI***:* Tumwombe Bwana*:*

MWIMBAJI*:* Bwana hurumia.

**PADRI***:* Kwa kuwa wewe ni Ufufuo, uzima na mapumziko ya milele ua watumishi wako wamelala, Kristu Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu, pamoja na Baba yako wasipo mwanzo, na Roho Mtakatifu wako kamili, Mwema, Mpaaji wa uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MWIMBAJI*:* Amina. Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . .

### Kuaga (Apolisis).

**PADRI***:* Kristu Mungu ukweli wetu kwa wafu na wazima na aliyefufuka katika wafu, kwa maombezi ya Mama wake asiye doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuitaji. kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili. kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtakatifu, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume Watakatifu, Watukufu, wasifiwe kamili. *(kutaja jina la Mtakatifu wa Kanisa ile),* ya wapadri Watakatifu wetu na Waekumeniki Wakubwa, walimu na Waierarka, ya Washahidi, Watakatifu, watukufu, Washindaji Wazuri, ya Wapadri Wabebaji-Mungu, ya Yoakim na Anna, Mababu ya Mungu, Watakatifu na wenye haki (*Mtakatifu wa ile siku),* makubusho yake leo, hata ya watakatifu wote, atuhurumie, akatuokoe, Yu Mungu mwema, Mrahimu na Mpenda wanadamu.

Padri anaimba*:* Makubusho milele, makumbusho milele, makubusho milele yao.

MWIMBAJI*:* Makubusho milele. *(mara tatu).*

**PADRI***:* Makubusho milele. *(mara tatu).*

**PADRI***:* Kwa maombezi ya wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

MWIMBAJI*:* Amina.

### SALA YA WALE WATU WALIUNGAMA NA PADRI ANAWASOMA KWA USAMEHE WAO

Tumwombe Bwana

Padri: Ee Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu mwenyi muzima, Muchungaji na Mwana-Kondoo, uliyenyanyua zambi ya dunia na uliwapatia kwa wale wa mbili ndeni kwao na kwa yule mwanamuke ulumuapatia maondoleo ya ma zambi wake, wewe, ee Rabi, acha, samehe, hurumia ma zambi, mazulumu, makosa ya kuipenda na wasiyo kupenda, ya kuifamia na yasiyoifamia, walifanuikwa katika unyanganyi na bila utii kwa sheria wako ya watumishi hawa wako. Na, sababu weko watu na mwili na wanaikala ndani mu dunia, kama kwa ajili ya shetani walianguka ao walifingwa ya padri moja ao walikanyanga malako wao mbele Kwako, wewe, kama Rabi

Mwema na musiyechuki, hawa watumishi wako paka na neno wako uwafungulia na uwasamehe na malipizo wao na malako katika neema wako kubwa. Ndivyo, ee Rabi Bwana mpenda-wanadamu, utusikilize sisi, wenye tunaomba wema wako kwa hawa watumishi wako na kama mwenye huruma usione makosa wao yote, uwaokoe toka gehena ya milele, kwani wewe ulisema. ee Rabi: «Vitu vyo vyote munavyofungua duniani vitafungwa mbinguni, na vitu vyo vyote munavyofungua duniani, vitafunguliwa mbinguni» (Matayo 18, 18). Kwani wewe wa pekee uwe musiyezambi na kwako tunakutolea utukufu pamoja na Baba wako musiyemwanzo na Roho Mtakatifu kamili na Mwema na mmuletaji-uzima, daima, sasa na siku zote, hata milele. Amina.

### SALA INGINE

**PADRI**: Tumwombe Bwana.

Ewe Mungu, kama ulivyosamehe Nabii Daudi katika Nabii Natana na akatubu zambi zake zote na ukamsamehe Petro alipolia wakati alipomukana Yesu, na ukamsamehe kahaba alipolia mbele ya miguu ya Yesu Kristu, naukawasamehe mtoza kodi na mwana mupotevu, na sasa, ewe Mungu, usamehe katika mimi zambi zake zote alizotenda huyu, kwa hii wakati hata uzima wa milele, umuweke asimame mbele ya Kiti chako cha ezi bila hukumu. Kwa zambi zote ulizotubu, usiogope, nenda zako na amani.

### SALA YA KILA UGONJWA

Tumwombe Bwana. Bwana hurumia.

Ee Rabi Mwenyezi, mganga wa roho na wa miili, Wewe mwenye kunyenyekesha na kukuza, mwenyi kuazibu na kuponyesha, tazama kwa huruma yako ndugu (dada) yetu mgonjwa (jina lake). Nyosha mkono wako wenyi kuponyesha umutunze, umuamushe toka kitanda chake ukimuondoa toka ugonjwa. Tenga mbali yake mateso yote, ubaya wote na magonjwa yote yenyi kushika watu wengi, homa ao baridi yote. Ondolea, samehe, zima makosa yake yote kwa mapendo yako kwa wanadamu. Ndivyo, ee Bwana, hurumia kiumbe chako katika Yesu Kristu Bwana wetu, ambaye umetukuzwa naye, pamoja na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## SALA YA KOLIVA

Tumwombe Bwana. Bwana hurumia.

Ee Bwana, wewe ambaye kwa neno lako ulikamilisha ulimwengu na uliamuru udongo itoe matunda mbalimbali kwa ajili ya kinywaji na chakula chetu, wewe uliyewapa vijana watatu na Danieli afya njema kule Babiloni wakati walipokula mbegu, wewe mwenyewe, ee Rabi wa wema wote, bariki hii mchanganyo wa mbegu na matunda, takasa wale wataikula, kwa sababu hii imetolewa kwa watumishi wako kwa ajili ya utukufu wako na kwa heshima ya askari kijana mtakatifu shahidi mkuu Theodore, na sababu ya makumbusho ya marehemu waaminifu. Kwa wale walitayarisha hii chakula na kufanya hii makumbusho, uwape, kwa wema wako, ile wanaomba kwa ajili ya wokovu wao na furaha ya mema yako ya milele, kwa maombezi ya Maria Malkia wetu Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu na Bikira daima, ya shahidi mkuu mtakatifu Theodore askari kijana ambaye tunashangilia leo makumbusho yake, na ya watakatifu wote.

Kwa kuwa wewe ni Mungu mwenye kubariki na kutakasa vitu vyote, na tunakutolea utukufu, Baba wa milele, pamoja na Mwana wako wa pekee, na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji-uzima, daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## SALA YA KUBARIKI MATAWI

*Kisha Evangelion ya Asubui (kule katikati ya Kanisa mbele ya Ikone ya Siku Kuu), wakati wa somo la Zaburi 50 (51), padri akisindikizwa na Shemasi, atafukiza matawi yenye kutayarishwa katika sahani kubwa. Kisha Zaburi, Shemasi atasema:*

**PADRI:** Tumwombe Bwana. Bwana hurumia.

**PADRI**: Ee Bwana Mungu wetu mwenye kukaa juu ya waKheruvi, uliyeonyesha uwezo wako, na uliyetuma Mwana wako wa pekee, Bwana wetu Yesu Kristu, ili aokoe dunia kwa Msalaba, Maziko na Ufufuo wake uliyofanyika katika Yerusalema kwa mateso yake ya kutaka, taifa lililokaa katika giza na kivuli cha mauti limeshika alama ya ushindi, maana matawi ya miti na ngazi, kwa hii walionyesha Ufufuo wake. Ee Rabi, na sisi wenye kufananisha hii tendo lao hii siku Kuu, maana kushika matawa mikononi mwetu, utulinde kama wale watu wengi na watoto waliokuimbia Hosanna, utuokoe, hivi na sisi kwa hii wimbo wa mashangilio ya kiroho tutastahili kuufikia ufufuo wa siku ya tatu uletaji-uzima wa Bwana wetu Yesu Kristu, ambaye pamoja naye unatukuzwa pamoja na Roho Mtakatifu kamili na mletaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

# IBADA KWA SIKU WA KWANZA YA KILA MWAKA MUPYA

**SHEMASI:** Ee Rabi himidi.
**PADRI:** Ahimidiwe Mungu wetu daima sasa na siku zote, hata milele na milele.
**WAIMBAJI:** Amina.

### SIKU KUU YA TOHARA YA BWANA WETU YESU KRISTU NA SHANGILIO YA MWANZO YA MWAKA MUPYA

Apolitikion. Sauti ya Kwanza.

Ulichukuwa mwili wa ubinadamu bila ugeuzi, wewe uliye Mungu kwa hali yako. Bwana mwenyi huruma; kwa kutimiza kanuni ya sheria, ulitaka kutahiriwa mwilini sababu ya kuondoa giza na pazia kunakofichama tamaa zetu. Utukufu kwa wema wako kubwa, utukufu ku rehema yako, ee Neno la Mungu, utukufu ku mapendo isiyokaridika iliyokushusha mpaka kwa sisi.

### APOLITIKION YA MTAKATIFU BAZILI ASKOFU YA KESARIA WA KAPADOKIA

Sifa yako imeenea duniani kote kumepokelewa neno lako. Kwa neno lako, umetufundisha elimu umetufunulia hali ya viumbe, umenyosha desturi za wanadamu. Baba mtukufu, Kohani mfalme, umusihi Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

## Doksologia kubwa:

Utukufu kwako uliyeonyesha mwangaza, utukufu kwa Mungu juu pia; amani katika inchi mapendo kwa wanadamu.

Tukusifu, tukuhimidi, tukusujudu, tukutukuza, tukushukuru, maana utukufu wako ni mukubwa.

Ee Bwana Mufalmc Mungu wa yulu na mbinguni, Baba mwenyezi; Ee Bwana Mwana wa pekee Yesu Kristu, na wewe Roho Mutakatifu.

Ee Bwana Mungu we, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, unayezibeba zambi za dunia, utuhurumie, unayezibeba zambi za dunia.

Upokec ombi letu, Unayeketi kuume kwa Baba na kutuhurumia.

Kwa kuwa mutakatifu wa pekee, Bwana wa pekee Yesu Krtistu, katika utukufu wa Mungu Baba, Amina.

K ila siku nitakuhimidi, nitasifu jina 1ako la milele, hata milele na milele.

Ee Bwana, utujalie siku hii kutujilinda na zambi.

Umehimidiwa u, ee Bwana Mungu wa Baba zetu, jina lako Iimesifiwa na limetukuzwa milele. Amina

Ee Bwana, huruma yako iwe nasi, sawa tunakutumainia wewe.

Ee Bwana, umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako. *(mara tatu ).*

Ee Bwana wewe U kimbilio letu kizazi baada ya kizazi. Mimi nilisema: ee Bwana unihurumie, uiponye roho yangu, maana nimekutendea zambi.

Kwa sababu kwako iko chemchem ya uzima, katika mwangaza yako tutaona rnwangaza. Onyesha huruma yako kwa wao wakujuwa.

Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Musiye kufa Mutakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Musiye kufa Mutakatifu, hutuhurumie.

Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Musiye kufa Mutakatifu, utuhurumie.

**SHEMASI ao PADRI**: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na utuhurumie.

**WAIMBAJI**: Bwana hurumua. *(mara tatu).*

**SHEMASI:** Tena tunakuomba kwa ajili wa wakristu wakristiani waorthodoksi wote.

**WAIMBAJI**: Bwana uhurumia. *(mara tatu).*

**SHEMASI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo na Baba wetu (jina yake) na ya undugu wetu wote katika Kristu.

**WAIMBAJI**: Bwana hurumia . *(mara tatu).*

**SHEMASI:** Tena tunakuomba kwa agili ya Mukubwa wa Inchi yetu (jina lake), ya Taifa na waaskari na watu wote.

**WAIMBAJI**: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**SHEMASI:** Tena tunakuomba kwa ajili ya Nyumba hii Takatifu, kila muji na kila Bara zilindiwe ku njaa, tauni, matetemeko ya udongo, garika, moto, silaha, ushambulio ya watu wageni na vita ili itufazilie, mkarimu na wepesi kwa kwinamisha Mungu wetu mwema na mpenda wanadamu, kwa ajili ya kwepusha hasira yoyote yenye kutwelekea na ili tuokolewe ku vitisho adilifu vinavyokuwa juu yetu na atuhurumie.

**WAIMBAJI**: Bwana hurumia, *(mara makumi Ine*).

**PADRI**: Utusikilize, ee Mungu Mwokozi wetu, tumaini wao wanaokaa mpaka za inchi za dunia na ya wao wanao mbali baharini na hewani na utufazilie, ee Rabi, kwa ajili ya zambi zetu na utuhurumie. Kwani wewe ndiwe Mungu wa huruma na rafiki ya wanadamu na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata miolele na milele.

**WAIMBAJI**: Amina.

**SHEMASI:** Tumwombe Bwana.

**WAIMBAJI**: Bwana hurumia.

**PADRI**: Ee Bwana Mungu wetu, uliyeweka muda na wakati yote kwa mamlaka wako na ulitustahilisha katika wema na huruma yako kamili kuingia sisi ndani ya hii mwaka mupya ya wema Wako, Wewe uibariki huu mwaka na utulinde katika amani. Utuache na utuhurumie na utusamehe kwa kila kintu kibaya tulifanya hile wakati wa zamani na utuchunge katika huu mwaka mupya kuishi bila zambi. Utuangaziw katika mwangaza ya kweli na hamuri yako takatifu, simamisha ndani ya ma roho yetu mapenzi yako takatifu na utuongoze kwa kila kazi wema inayekufaruhisha. Kanisa yetu Takatifu, katika neema yake kimungu uichunge. Ee Bwana, kumbuka na inchi yetu na wakubwa wake. Tena ongoza vijana watoto kwa mapenzi yako; saidie wazee wetu na uwalinde wale walipotehsa imani yao. Wale walitoka mbali uwarudishe kwako na wale walipotesha imani yetu ukweli Orthodokse uwangazie kurudia kwako na uwapokee mu Kanisa yako. Funika inchi yetu katika nguvu yako, utupatie muda nzuri na matunda mengi toka bulongo yetu. Fungua roho ya wakubwa wetu na uwapatie nguvu yako na ma kundi ya askari wetu katika inchi, pepo na bahari uwasidie na uwachunge. Ee Bwana, tunakuomba kuja kwa sisi Ufalme wako, Ufalme ya mapendo, wema, amani, na haki na utustahilishe katika kinywa na roho moja tukuhimidi na kutukuza Jina yako wa sifa kamili na ukubwa wa Baba na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele, na milele. Amina.

**WAIMBAJI**: Amina. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* ee Rabi mtakatifu barikia.

**PADRI**: Kristu Mungu wetu wa kweli. kwa maombezi ya Mama wake asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa Msalaba uheshimiwa na uhuitaji, kwa matunzo ya majeshi

yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili. kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtakatifu, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume watakatifu, Watukufu, Wasifiwe kamili . . . (kutaja jina ya Mtakatifu wa Kanisa ile), ya Wapateri, Watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapateri Wabebaji-Mungu, ya Yoakim na Anna, Mababu Mungu, Watakatifu na wenye haki (Mtakatifu wa hii siku) makumbusho yake leo, hata ya watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe, yu Mungu mwema, Mrahimu na Mpenda wanadamu.

Kwa maombezi ya wapadri wetu. . .

**WAIMBAJI**: Amina.

## SYNAKSARI YA WATAKATIFU KATIKA MWAKA YA KANISA ORTHODOKSE

### IANUARIE

01 - Tunakumbuka Tohara ya Bwana wetu Yesu Kristu.
- Mt. Baba yetu Basile Mkuu, askofu wa Kesaria ya Kapadokia.

02 - Hii tarene, makumbusno ya Baba Silvestro, Papa wa Roma.
- Mt. shanidi Theagenis.

03 - Hii tarene, makumbusno ya Mt. Nabii Malahia.
- Mt. Gordios aliyekufa kwa kisu.

04 - Hii tarehe, makumbusho ya Baraza ya Mitume watakatifu 70.
- Mt. mtawa shahidi Zosimos na Athanasios Komendarisios.

05 - Hii tarene, makumbusho ya watakatifu mashahidi Theopemptos na Theonas, wenye walikwa ku mbele wafumu, walikufa kwa kisu, mwaka karibu 305.
- Mt. mwanamuke Shahidi Siglitiki, aliyekufa kwa kisu mu mji Aleksandria ya Misiri mwaka karibu 305.

06 - Hii tarene makumbusho ya kuonekana kwa Bwana na Mungu Mwokozi Yesu Kristu (Epifania).

07 - Hii tarehe, makumbusho ya baraza ya Mt. na Nabii Mtangulizi na Mbatizaji Yoane na tunakumbuka kwa kunamisha mukono wake kuupeleka ku Konstantinopoli.
- Mt. shahidi mupya Athanasios aliyekufa kwa kisu Smirni mu 1700.

08 - Hii tarene tunakumbuka Mt. mtawa mama yetu Dominika.
- Mtawa Baba yetu George Hozevitis, aliyekufa na amani mwaka karibu 600.

09 - Hii tarehe, makumbusho ya Mt. shahidi Poliefktos, aliyekufa mbele ya mwaka 260.
- Mt. Antonina, mwanamuke mushahidi, aliyekufa mu mji Nikomidia.

10 - Hii tarehe makumbusho ya Baba yetu Grigorios wa Nisa ndugu ya Mt. Basile, aliyekufa na amani mwaka 395.
- Mt. mtawa Baba yetu Dometianos, askofu wa Melitini ya Armenia mwaka karibu 500.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Theodosios mkubwa ya Monasteri yake (Kinoviarhis) na mwalimu mkubwa kwa wale waliishi mu jangwa.
- Baraza ya Malaika watakatifu inafanika katika siku Kuu ya Watakatifu wote na makumbusho ya Mt. Domninos, Stephanos wa Plakidini na Mt. Theodoros na Agapios archimandriti.

12 - Hii tarehe, makumbusho ya Mt. shahidi Tatiani.
- Mt. Petro wa Abesalamitis, mushahiidi, aliyekufa kwa moto.

13 -Hii tarehe, makumbusho ya watakatifu Washahidi Ermilos, shemasi na Stratonikos, murafiki yake, waliokufa ndani ya mtoni Dunavis ya Bulgaria karibu mwaka 323.
- Mt. mtawa Baba yetu Yakobo, askofu ya Nisivis. Alikufa na amani mwaka 338.

14 - Hii tarehe, tunakumbuka watakatifu watawa wote wa mulima Sinai waliouawa kwa Waturques.
- Watakatifu 33 ya Monasteri ya Mulima Sina na 38 watakatifu Watawa ya jangwa Raitho, wenye waliwauwa wapagano mwaka karibu 470.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Paulo ya jangwa Thivaida ya Misiri. , Alikufa na amani mu 341.
- Mtawa Mt. Baba yetu Yoane, mwenye anaitwa Kalivitis, masikini wa Kristu. Alikufa na amani mu Monasteri ya Akimiton ya Konstantinopoli, mwaka karibu 500.

16 - Hii tarehe, makumbusho ya usujudu wa monyororo ya Mt. mtukufu Mutume Petro.
- Watakatifu mashanidi wandugu : Pefsipos, Elasipos na Mesipos na Neonila, aliyekuwa mama wao. Walikufa na mateso mengi mwaka karibu 200 mu mji Kesaria ya kapadokia

17 - Hii tarehe, tunakumbuka Mt. mtawa Baba yetu mkubwa Antonios.
- Mt. mtawa Baba yetu Antonios mupya aliyeishi mjini Veria Grekia.

18 - Hii tarehe tunakumbuka watakatifu Baba zetu Athanasios na Kirilos patriarche ya Aleksandria.
- Mt. mwanamuke Theodouli.

19 - Hii tarehe, makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Makarios wa Misri, aliyekufa na amani mwaka 390. Tena na Mt. Mtawa makarios toka mji Aleksandria, aliyekufa na amani mwaka 394.

- Mt. shanidi na Bikira Efrasia, alikufa na mateso mengi, mwaka 304.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Efthimios mkubwa aliyeishi mu jangwa ya Yerusalema na alikufa na amani mu 473.

- Watakatifu mashahidi Vasos, Efsevios, Eftihios na Vasilidis, wenye aliwakokota mu imani ya Kristu Mt. Theopemtos mu mji Roma mbele ya mwaka 305.

21 - Hii tarehe makumbusho ya mtawa Baba yetu Maksimos, mkubwa musimamizi ya imani Orthodokse, aliyekufa na amani mu 662. .

- Mtawa Baba yetu Zosimos, askofu wa Sirakuses ya kisanga Sikelia, alikufa na amani mwaka karibu 680. .

22 - Hii tarehe, makumbusho ya Mtume Mt. Timotheos, mwanafunzi wa Mtume Mt. Paulo.

- Mt. Shahidi na mtawa Anastasios toka inchi Persia alikufa mwaka karibu 680.

23 - Hii tarehe, makumbusho ya shanidi mkubwa Klimis, askofu ya mji Agira ya Azia Kidogo, na shahidi Mt. Agathangelos, waliokufa mwaka karibu 305.

- Mt. mtawa Baba yetu Efsevios, aliyekufa na amani karibu mu 370.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mtawa mama yetu Kseni na watumishi wake wawili, waliokofa na amani mwaka karibu 480.

- Mashahidi watakatifu Paulo, Pafsirios na Theodotion, aliyekuwa zamani munyanganyi, walikufa na mateso mengi mwaka mbele ya 305.

25 - Hii tarehe, makumbusho ya Mt. Baba yetu Grigorio Mtheologo, askofu mkubwa ya mji Konstantinopoli. Ni mwalimu mkubwa na mpadri ya Kanisa wetu. Alikufa na amani mu 381.

- Mtawa Baba yetu Puplios, aliishi mu Mesopotamia mwaka karibu 360.

26 - Hii tarehe makumbusho ya mutawa Baba yetu Ksenofon na kundi lake Maria na watoto wake Arkadios na Yoane.

- Mtawa Baba yetu Simeon wa Zamani, alikufa na amani mwaka karibu 370.

27 - Hii tarehe makumbusho ya kuhamisha mifupa ya Mt. Baba yetu Yoane Krisostomos askofu wa Konstantinopoli mwaka 438.

- Mt. Markiani, mfalme mwanamuke, bibi ya mfalme Yustinos ya kwanza, aliyekufa na amani, mwaka 527.

28 - Hii tarehe, makumbusho ya Mt. Baba yetu Efrem wa Siros. (Toka inchi Siria). Mwalimu na mpadri mkubwa ya Kanisa yetu. Alikufa na amani mu 373.

- Mt. Baba yetu Paladios, aliyeishi na alikufa mu inchi Siria mu 380 karibu.

29 - Makumbusho ya kuhamisha mifupa ya Mt. shahidi Baba yetu Ignatios, kutoka Roma na kuipeleka mu mji Antiokia ya Siria.

- Watakatifu mashahidi saba wa ku Samosata : Filotheos, Iperehios, Avivos, Yulianos, Romanos, Yakovos na Parigorios walikufa mu mji Samosata karibu mwaka 270.

30 - Hii tarehe, makumbusho ya watakatifu na walimu wakubwa wa dunia, Baba yetu Vasile Mkuu, Grigorios Mtheologo na Yoane Krisostomo.

31 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu wa miujiza Anargiri Yoane toka mji Edesa ya Mesopotamia na Yoane toka mji Aleksandria, wanganga bila kukamata feza. Walikufa kwa kisu karibu mwaka 305.

- Mt. mwanamuke Athanasia na watoto wake watatu: Theodoti, Theoktisti na Evdoksia, walikufa kwa kisu, ile siku pamoja na washahidi Kiros na Yoane.

## F E B R U A R I

- Hii tarehe Makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Trifon wa miujiza, aliyekufa mwaka 251.

- Makumbusho ya Baba yetu Mt. Petro wa Galatia.

02 - Hii tarehe makumbusho ya kupokelewa kwa Bwana Yesu Kristu mikononi mwa mwenyi haki Simeoni.

- Mt. shahidi Agathodoros, aliyekufa mu mji Tiana ya Kapadokia.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Simeoni mwenyi Haki na Anna Nabii.

- Mt. shahidi Vlasios wa Voukolos toka Kesaria. .

- Watakatifu mashahidi Andrianos na Evulos, waliokufu mu Kesaria mbele ya mwaka 311.

04 - Hii tarehe makumbusho ya mtawa Baba yetu Isidoros wa Pilusiotis, aliyeishi na alikufa mu jangwa ya Misiri mwaka 440.

- Mt. mtawa Baba yetu Nikolaos, mwanafunzi ya Mt. Theodoros, alikuwa Igumeno mu Monasteri Studion na alikufa na amani mwaka 868.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Agathi, aliyekufa mwaka 251.

- Mt. Baba yetu Theodosios toka Kisanga Skopelos ya Grekia alikufa na amani mu ciecle ine.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Voukolos, askofu wa Smirni.

- Mt. shahidi Yulianos toka Emesa ya Siria, alikufa kwa kisu mu 284 karibu.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Parthenios askofu wa Lamsakos ya Azia Kidogo, alikufa na amani mu siecle ine.

- Mt. mtawa Baba yetu Luka wa mu Grekia, aliyekufa na amani mwaka 953.

08 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtukufu shahidi mkubwa Theodoros mkubwa ya wa sakasri, alikufa ma mateso mengi karibu mwaka 305 mu mji Frigia.

- Mt. Nabii Zakaria.

09 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Nikiforos, aliyekufa mu fasi ya Saprikios, mwenye alikataa Kristu mwaka 260.

- Mt. Baba yetu Romanos wa fasi Kilikia.

10 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Haralambos, aliyekufa na mateso mengi mwaka 211, mu Magnisia ya Azia Kidogo.

- Mashahidi watakatifu Vaptos na Porfirios waliokufa kwa kisu.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Vlasios askofu wa Sebastia ya Armenia, alikufa na mateso mwaka 324.

- Makumbusho ya watoto wawili na wanawake saba, waliokufa pamoja na Mt. Vlasios kwa kisu.

12 - Makumbusho ya Mt. Baba yetu Meletios askofu wa Antiohia, aliyekufa na amani mu 381. .

- Mt. Mtawa Maria, mwenye aliitwa Marinos, aliyeishi pamoja na baba wake Evgenios, walikufa na amani mu siecle sita.

13 - Hii tarehe makumbusho ya mtawa Martinianos, aliyeishi na alikufa na amani mu Kesaria ya Palestina mu siecle tano.

- Watakatifu Mitume na Mashahidi Akilas na bibi yake Priskila, wasaidizi ya Mtume Paulo, walikufa na mateso mu siecle ya kwanza.

14 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Afksentios wa kilima.

- Mt. mtawa Baba yetu Maron.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtume na shahidi Onisimos mwanafunzi wa Mt. Paulo.

- Mt. shahidi Mahior, alikufa kwa mukuki mwaka katikati ya 285-305.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Watakatifu mashahidi Pamfilos pamoja na yeye: Walis, Paulo, Selefkos, Elias, Yeremias, Yulianos, Isaya, Samueli na Danieli, waliokufa kwa kisu, mu mji Kesaria ya Palestina mwaka 290.

- Mt. Shahidi Theodulos aliyekufa msalabani.

17 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Theodoros wa Tyron, aliyekufa na mateso mengi, mwaka 313, mu mji Efkaita ya Azia Kidogo.

- Mt. mwanamuke Mariamni dada ya Mt. Filipo.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Leon, Papa wa Roma, aliyekufa mu 461.

- Watakatifu Leon na Parigorios walikufa kwa mateso mengi kwa Patara ya Likia.

19 - Hii tarehe makumbusho ya mitume Arhipos, Filimon na Apfia, wenye walikuwa wanafunzi ya Mtume Paulo.

- Mashahidi Maksimos, Isihios, Theodotos na mwanamuke Askliriodoti, waliokufa na mateso mengi mu mji Adrianupolis ya Traki ya Grekia mu kati ya 285-305.

20 - Hii tarehe makumbusho ya mtawa Mt. Baba yetu Leon wa miujiza, askofu ya mji Katani ya Kisanga Sikelia, aliyekufa na amani mu 785.

- Watakatifu padri na shahidi Sadok, askofu ya inchi Persia pamoja na wengine mia moja na makumi mawili na mnane waliokufa kwa kisu.

21 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Timotheo wa Symvolis, aliyeishi na alikufa mu siecle tisa.

- Mt. mtawa Baba yetu Efstathios, askofu mkubwa wa Antiokia mkubwa, aliyekufa na amani mu 360.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Baba yetu Mt. Athanasios ya Monasteri Pavlopetriu, aliyekufa na amani mu siecle tisa.

- Watakatifu mitume Andronikos na Yunia. Kupata na kutosha mifupa yao na ya mashahidi wengine.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mtakatifu na shahidi Polikarpos, askofu mkubwa wa mji Smirni na mwanafunzi ya Mt. Yoane mu Theologo, alikufa mwaka 168.

- Watakatifu wa Baba zetu Yoane, Musa, Antiohos, na Antonios, walikufa na amani mu siecle tano.

24 - Hii tarehe makumbusho ya mara ya kwanza na ya pili kupata kichwa cha Mt. Yoane Mtangulizi.

25 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Tarasios, askofu mkubwa wa Konstantinopoli, aliyekufa na amani mu 806.

- Mt. shahidi Aleksandros aliyekufa kwa kisu ku mji Drisiparo ya Grekia mwaka karibu 305.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Porfirios, askofu mkubwa ya Gaza mu Palestina, aliyekufa na amani mu siecle tano.

- Makumbusho ya shahidi mwanamuke Fotini Msamaria, aliyezungumuza na Bwana Yesu kule kisima cha Yakobo.

27 - Hii tarehe makumbusho ya mtawa Baba yetu Prokopios wa Dekapolitis, musimamizi ya Imani Orthodokse, alikufa mu siecle mnane.

28 - Hii tarehe makumbusho ya Mtawa Mt. Baba yetu Vasilios rafiki ya Mt. Prokopios Dekapolitis, aliyekufa na amani mu siecle tisa.

29 - Hii tarehe makumbusho ya Mtawa Baba yetu Kasianos wa Roma.

## **M A R S I**

01 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtawa mwnamuke shahidi Evdokia wa mji Samaria, aliyekuwa zamani kahaba na alikufa kwa kisu mu siecle ya mbili.

- Mt. mtawa mwanamuke Domnina aliyekufa na amani mu siecle ya ine. .

02 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Isihios, aliyekufa mu 305 karibu.

- Mt. padri na shahidi Theodotos, askofu mkubwa wa Kirinia ya kisanga ya Chipros, aliyekufa mu 326.

03 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mashahidi Eftropios, Kleonikos na Vasiliskos, waliokuwa wa semeki ya Mt. Shahidi mkubwa Theodoros Waliokufa na mateso mengi mwaka mbele ya 305 mu Amasia ya Pontos.

- Mt. padri na shahidi Theodoritos wa Antiokia, aliyekufa na mateso mengi mu 363.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Gerasimos wa Iordanitis, mwenye alijenga Monasteri munene mu jangwa ya Yorodani. Alikufa na amani mu siecle ya tano.

- Watakatifu mashahidi Pavlos na Iuliani dada yake, waliokufa mu 275.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Konon wa Isavria, mu siecle ya kwanza.

- Mt. shahidi Konon, mtumishi wa shamba, aliyekufa mwaka 251.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Watakatifu mashahidi wakubwa makumi ine na wawili wa miujiza Amorion, Theodoros, Konstantinos, Kallistos, Theofilos, Vasois, Melisinos, Aetios, Krateros na wengine, waliokufa mu 838.

- Mt. mtawa na shahidi Maksimos, alikufa na mawe.

07 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mapadri na mashahidi wote; maliokufa mu njimbo Hersona ya Rusia kusini, nikusema: Efrem, Vasilefs, Evgenios, Agathodoros, Elpidios, Kapiton na Etherios, mwaka 380 karibu.

08 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Theofilaktos askofu wa mji Nicomidia, musimamizi ya imani yetu. Alikufa na amani mu siecle ya tisa.

- Mt. mtawa Baba yetu Pavlos, askofu wa mji Plusiada, mu siecle ya tisa.

09 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi wakubwa makumi ine waliokufa ndani ya maji karibu ya mji Sebastia.

- Mt. shahidi Urpasianos, aliyekufa mwaka katikati ya 285-305.

10 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Kodratos wa mji Korinto ya Grekia pamoja na wanafunzi wake: Anektos, Pavlos, Dionisios, Kiprianos na Kriskis, waliokufa mwaka 259.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Sofronios, askofu ya Yerusalema. Alikufa na amani mu 638.

- Mt. padri na shahidi Pionios. Alikufa mu mji Smirni mwaka 251.

12 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Theofanis wa Sigrianis, karibu ya shamba munene, aliyekufa mu Kisanga Samothraki ya Grekia mwaka 815. .

- Mt. mtawa Baba yetu Grigorios ya kwanza, mwenye Dialogos, askofu wa mji Roma, aliyekufa mu Roma mu 604.

13 - Makumbusho ya kutosha kaburini mwili muzima ya Mt. Baba yetu Nikiforos, Patriarche wa Konstantinopoli, mwaka 846.

- Mt. padri na shahidi Puplios, askofu wa Athina ya Grekia, aliyekufa mu 180.

14 - Makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Venediktos, aliyeishi na alikufa mu Roma ya Italia, mwaka 543.

- Mt. shahidi Aleksandros wa mji Pidna, alikufa katikati ya miaka 285-305.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Agapios pamoja na mashahidi wengine Plisios, Romilos, Timolaos, Aleksandros, Dionisios na Dionisios mwengine, waliokufa mu mji Kesaria karibu mu 305.

- Mt. mtume Aristovulos, mufwasi ya Mt. Paulo na askofu wa Vretania (Anglia), ndugu ya mtume Varnavas.

16 - Mt. shahidi Savinos wa Misri, aliyekufa kati ya miaka 285-305. .

- Mtakatifu mtawa Yoane wa Pufianes, alikufa na amani.

17 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mutawa Baba yetu Aleksios, mtu wa Mungu, aliyekufa mu Roma mwaka 410.

- Mt. mtawa Baba yetu na Musimamizi ya Imani Theostiriktos, padri mkubwa wa Monasteri Mt. Yoane, kwa jina Pelekiti, alikufa na amani.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Kirilos, askofu mkubwa wa mji Yerusalema, Baba na Mwalimu ya Kanisa yetu. Alikufa mu 386.

- Watakatifu mashahidi Trofimos na Efkarpion, walikufa kutundikwa na kamba, mwaka karibu 305.

19 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Krisanthos na bibi yake Daria.

- Mt. shahidi Klavdios wa Trivunos pamoja na wengine waaskari walikufa katika bahari.

20 - Hii tarehe makumbusho ya watawa watakatifu wote wa monasteri ya Mt. Savas karibu ya Yerusalema, walikufa kwa kisu, mwaka 604.

21 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Iakovos, askofu na Musimamizi, alikufa mu siecle tisa.

- Mt. Baba yetu Thomas, patriarche wa Konstantinopoli, aklikufa mwaka 610.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Vasilios, padri wa kanisa ya mji Agira, alikufa mu 363.

- Mt. mwanamuke Drosis, mtoto ya mfalme pagano Traianos (98-117) pamoja tena na wanawake watawa tano.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Nikon pamoja na watumishi wake 199, walikufa kwa kisu, mu Kisanga Sikelia ya Italia mu siecle tatu.

- Mt. shahidi Dometios, alikufa kwa kisu.

24 - Hii tarehe tunafanya mbele ya siku moja siku Kuu ya habari Njema ya Mzazi-Mungu.

- Makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Artemon, askofu wa Selefkia ya Pisidia.

25 - Siku kuu kubwa ya Habari Njema ya Mzazi-Mungu na Bikira Maria.

26 - Hii tarehe tunafanya Siku Kuu ya Mt. Malaika Gabrieli kwa sababu yeye alitumika kwa ajili ya Mungu wetu Yesu Kristu kuja duniani.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke Matrona wa mji Thessaloniki ya Grekia, aliyekufa mu siecle katikati tatu na ine.

- Mt. mtawa Kirikos wa mji Apros ya Grekia, alikufa na amani.

28 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Ilarion mupya padri mkubwa wa monasteri Pelekiti, alikufa na amani, mu siecle tisa.

- Mt. mtume Irodion katika mitume 70 ya Yesu Kristu, askofu ya mji Patra ya Grekia.

29 - Hii tarehe makumbusho ya Watakatifu Markos, askofu wa mji Arethusa Kirillos, shemasi pamoja na wanawake mabikira na mapadri wanaume wa mji Askalon na Gaza, waliokufa mu Siria mwaka 363 karibu.

30 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Yoane mtungaji wa kitabu cha Mungazi, padri mukubwa ya Monasteri ya Sina. Alikufa na amani mwaka karibu 608.

- Mt. Nabii Ioad ao Yoil.

31 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Ipatios, askofu wa mji Gagres.

- Mt. mtawa Baba yetu Akakios, askofu wa Melitini ya Armenia, aliyekufa na mateso mwaka 251.

01 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa mwanamuke Maria wa Misri, aliyekuwa zamani kahaba mukubwa ya mji Aleksandria, kisha alitubu na alikufa mu jangwa ya Yorodani mu siecle sita.

- Mt. mtawa Baba yetu na Musimamizi Makarios, padri mkubwa wa monasteri Pelekiti, aliyekufa mu siecle tisa.

02 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Titos wa miujiza, alikufa na amani, mu siecle tisa.

- Watakatifu mashahidi na wandugu Amfianos na Edesios, walikufa baharini, katikati ya miaka 285-305.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu na Musimamizi Nikitas padri mkubwa wa monasteri ya Midikion, aliyekufa mu siecle tisa.

- Mt. mtawa Baba yetu Yosefu wa Imnografos (mwandishi ya mwimbo ya kanisa yetu), aliyekufa mu Konstantinopoli mu 886.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Georgios wa mlima Maleo ya Peloponisos ya Grekia.

- Watakatifu Theodulos, msomaji na Agathopus, shemasi, walikufa baharini, katikati ya miaka 285-305.

05 - Hii tarehe Makumbusho ya mashahidi watakatifu Klavdianos pamoja na wengine Diodoros, Viktor, Viktorinos, Pappias, Serapion na Nikiforos.

- Mt. mtawa mwanamuke Theodora wa mji Thessaloniki.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Eftihios, patriarche wa Konstantinopoli, aliyekufa na amani mu 582.

- Watakatifu 120 mashahidi waliokufa motoni kule Persia.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Kalliopios, walimupingilia msalabani.

- Mt. mtawa Baba yetu Georgios, askofu mkubwa wa Mitilini ku kisanga Lesvos ya Grecia, alikufa na amani, mwaka 821.

08 - Hii tarehe makumbusho ya mitume watakatifu 70 ya Agavos, Rufos, Flegon na Asigritos.

- Mt. mtawa na Baba yetu Kelestinos, patriarche wa Roma, alikufa na amani, mu 432.

Mt. Pafsilipos, alikufa kwa kisu mu 138 karibu.

09 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Efpsihios wa mji Kesaria, alikufa na mateso mu 363 pamoja na waaminifu weingine.

- Mt. mtawa na shahidi Vadimos, arkimandriti pamoja na wanafunzi wake saba, walikufa kwa kisu, mu inchi Persia mwaka 374.

10 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Terentios, Afrikanos, Maksimos, Pompiios na wengine 36 na wengine Zinon, Aleksandros, Theodoros.

- Mt. mwanamuke Nabii Olda, alikufa na amani, mu siecle saba mbele ya kuzaliwa Kristu.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri mtawa Antipas, askofu wa mji Pergamos.

- Wat. wanawake mtawa Trifena na Matrona toka muji Kizikos, walikufa na amani.

12 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu na Musimamizi Vasilios, askofu wa Parion ya Epispontos, alikufa mu siecle tisa.

- Watakatifu mashahidi Dimis na Protion, walikufa kwa kisu, mu miaka kati ya 284-305.

13 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Martinos, patriache wa Roma, na musimamizi ya Imani ya Kristu. Alikufa mu 655.

- Watakatifu Kidilianos, Maksimos na Dadas, walikufa kwa kisu, mwaka 308.

14 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mitume miongoni mwa 70 Aristarhos, Pudis na Trofimos.

- Mt. shahidi Ardalion, mwenyi kufanya theatre, alikufa kwa moto, mwaka 300.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Kriskis, alikufa motoni mu mji Mira Likias.

- Mt. Baba yetu Leonidis, askofu wa mji Athina mji mukubwa ya Grekia, alikufa na amani.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Watakatifu mashahidi mabikira na wadada Agapi, Irini na Hionia, walikufa kwa moto mu mji Thesaloniki ya Grekia mu 303.

- Watakatifu mashahidi Filiks askofu, Yanuarios padri, Furtunatos na Septeminos, waliokufa mwaka 302.

17 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Simeon, askofu wa fasi Persia, pamoja naye Avdellas padri, Gothazat, Fusik na wengine mashahidi 1150 walikufa na mateso mengi na kwa kisu, mwaka 378.

- Mt. shahidi mupya Andrianos.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Yoane, mwanafunzi wa Mt. Grigorios Dekapolitis. Alikufa na amani mu siecle tisa, mu Yerusalema.

- Mt. shahidi Savvas, mkubwa wa askari ya mji Gothia. Alikufa mu siecle ine.

19 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Pafnutios wa mji Yerusalema. Alikufa katikati ya miaka 285-305.

- Mt. shahidi Theodoros wa mji Pergi Pamfilias, alikufa msalabani.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Theodoros wa Trihinas.

- Watakatifu mashahidi Viktor, Zotikos, Zinon, Akindinos, Kesarios, Sevirianos, Hristoforos, Theonas na Antoninos, walikufa wenyi kutundikwa katikati ya 285-305.

21 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mapadri na mashahidi Ianuarios askofu, Prokulos, Sossos na Fafstos mashenasi, Disiderio msomaji, Akutios na Eftihios.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Theodoros Sikeotis, askofu wa Anastasiupolis. Alikufa na amani mu 613.

- Mt. shahidi mupya Nearhos, alikufa kwa moto.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mukubwa Georgios wa
Mumebaji ya ushindi (Tropeoforos). Alikufa kisha mateso mengi kwa kisu, mu 303.

- Mt. shahidi Anatolios, mkubwa wa askari, alikufa kwa kisu.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa mwanamuke Elisabethi wa muujiza, alikufa na amani, mu siecle mnane.

- Mt. shahidi Savas, mkubwa wa askari ku Gothia, alikufa majini.

25 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume na Mwevangelizaji Markos, askofu ya kwanza ya mji Aleksandria. Alikufa na mateso mengi mwaka 62.

- Makumbusho ya kufanya sala katika kanisa ya Mt. Mtume Petro.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. na padri shahidi Vasilefs, askofu wa Amasia ya Pontos, alikufa kwa kisu, mwaka karibu 310.

- Mt. mwanamuke Glafira, alikufa kwa kisu, mwaka 312 karibu.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Simeon, ndugu ya Bwana Yesu Kristu, askofu wa Yerusalema, alikufa msalabani mu mwaka 98.

- Mt. mtawa Baba yetu na Musimamizi Yoane, padri mkubwa wa monasteri ya Katharon ya mji Vithinia. Alikufa na amani mu siecle tisa.

28 - Makumbusho ya watakatifu mashahidi tisa Theognis, Rufos, Antipatros Theostihos, Artemas, Magnos, Theodulos, Thavmasios na Filimon walikufa ku mji kizikos ya Azia Kidogo kwa kisu.

- Mt. mtawa Baba yetu Memnon wa miujiza, alikufa na amani.

29 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Mitume Iason, askofu ya Tarsos na Sosipatros, askofu ya Kilikia, wanafunzi na wafwasi ya Mtume Paulo.

30 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume Yakovos ndugu ya Mtume Mwevangelizaji Yoane Mtheologo. Alikufa kwa kisu mwaka 44.

- Mt. padri Klimis, Igumeno ya Monasteri ya Studion ya Konstantinopoli na musimamizi ya Imani yetu, aliyeandika kanuni, alikufa na amani, mu siecle tisa.

## M E I

01 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Yeremias, aliyekufa mu siecle sita mbele ya kuzaliwa Yesu Kristu.

- Mt. padri na shahidi Vatas toka inchi Persia.

02 - Hii tarehe makumbusho ya mapokeo ya Mifupa ya Mt. Baba yetu Athanasios mkubwa, patriarche wa Aleksandria, mwaka 373.

03 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mashahidi Timotheos na bibi yake Mavra, waliokufa mu njimbo Thivaida ya Misiri mwaka karibu 300.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke Pelagia wa mji Tarsos ya Kilikia. Alikufa kati miaka 285-305.

- Mt. mtawa Baba yetu Ilarios wa miujiza.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke mkubwa shahidi Irini, aliyekufa na mateso mengi, mu mji Magedon ya Persia mu siecle ine.

- Mt. mtawa Baba yetu Efthimios, askofu wa mji Maditos, wa miujiza, alikufa na amani mu siecle kumi.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwenye haki na mateso mengi Nabii Yobu, aliyekufa mu siecle kumi na tisa mbele ya kuzaliwa Kristu.

- Watakatifu watawa Mamas, Pahomios na Ilarion, walikufa na amani.

07 - Hii tarehe tunafanya makumbusho ya alama ya msalaba wa Yesu Kristu ulionekana mbinguni mwaka 346 mu mji Yerusalema.

- Mt. shahidi Akakios, alikufa kwa kisu mwaka kati ya 285-305.

08 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume na Mwevangelizaji Yoane Mutheologo.

- Mt. mtawa Baba yetu Arsenios Mkubwa, aliyeishi na alikufa mu jangwa ya Misiri mu siecle ine.

09 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Isaya, aliyekufa mu Yerusalema mu siecle mnane mbele ya kuzaliwa Kristu.

- Mt. shahidi mkubwa Kristoforos, aliyekufa na mateso mengi mwaka 251.

10 - Makumbusho ya Mt. Mtume Simon wa Zilotis.

- Watakatifu mashahidi na wandugu Alfios, Filadelfos na Kiprianos na weingine kumi na ine walikufa kwa kuunguzwa motoni.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Mokios, alikufa kwa kisu mwaka 300 karibu mu mji Vizantion.

- Mt. shahidi Dioskoros mupya, alikufa kwa kisu.

12 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Epifanios, askofu wa Kipros na mwalimu ya Kanisa yetu. Alikufa mu Kipros mwaka 403.

- Mt. Baba yetu Germanos, askofu wa Konstantinpoli. Alikufa mu 740.

13 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mwanamuke Glikeria, aliyekufa mu 161.

- Mt. Shahidi Laodikios zamu wa gereza, alisadiki Yesu Kristu na alikufa kwa kisu kwa waaskari wengine.

14 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Isidoros, alikufa kwa kisu ku kisanga Hios ya Grekia mwaka 251.

- Mt. padri na shahidi Therapon, askofu ya Kisanga Kipros, alikufa na amani.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Pahomios, aliyekufa na amani mu 346 mu njimbo Thivaida ya Misiri.

- Mt. mtawa Baba yetu Ahillios, askofu wa mji Larisa ya Grecia, mwaka 350.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Theodoros mwenyi kutakaswa, aliyekufa mu siecle ine mu Misiri.

- Mt. Baba yetu Aleksandros, askofu wa Yerusalema, aliyekufa mu Roma mu 251.

17 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Mitume Andronikos na Yunia, wasaidizi ya Mt. Paulo.

- Mt. shahidi Solohon pamoja na wengine, naye Pamfamir na Pamfilon, waliokufa mu mji Kalkidona ya Thraki mwaka karibu 300.

18 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mashahidi Petros, Dionisios, Kristina bikira, Andreas, Pavlos, Venedimos, Pavlinos na Iraklios, waliokufa mu Athina ya Grekia.

19 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Patrikios, Akakios Menandros na Polienos, walikufa kwa kisu, mu siecle tatu. .

- Mt. mtawa Baba yetu Memnon wa miujiza.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Thaleleos, aliyekufa mu 284.

- Mashahidi watakatifu Aleksandros na Asterios, waliomusadiki Mt. Thalelleos na walikufa kwa kisu.

21 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Wafalme wakubwa na Mitume Konstantinos na Eleni. Mt. Konstantinos alikufa mu 337.

- Wat. Watawa Voros, Isidoros na Theodoros, walikufa na amani.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Vasiliskos, mtoto wa ndugu ya Mt. Theodoros wa Tiron, alikufa kisu mu 285.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu na Musimamizi Mihail, askofu, wa Sinadon. Alikufa na amani mu siecle tisa

- Mt. mwanamuke Maria wa klopa, alikufa na amani.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtawa Baba yetu Simeon wa mlima ajambu ya Siria. Alikufa mu siecle sita.

25 - Hii tarehe makumbusho ya kupata mara ya tatu kichwa ya Mt. Mtangulizi na Mbatizaji Yoane, mu siecle tisa.

- Mt. shahidi Kelestinos, alikufa mwenyi kupigiliwa misumari katika miguu.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtume Karpos, mmoja katika mitume makumi saba.

- Mt. mtume Alfeos, alikufa na amani.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Elladios, alikufa, kisha mateso mengi, kwa kupigwa.

- Mt. padri na shahidi Therapon toka mji Sardis ya Persia.

28 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Eftihis, askofu wa Melitini.

- Mt. mwanamuke Elikonis, aliyekufa mo mji Korinto ya Grekia mu 245.

29 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke Theodosia bikira, aliyekufa mu Kesaria mwaka 308.

- Mt. mtawa mwanamuke Theodosia wa mji Konstantinopoli mu siecle mnane.

30 - Hii tarehe makumbusho ya mtawa Baba yetu Isakios, padri mkubwa wa monasteri ya Dalmaton, alikufa na amani mu 396.

- Mt. shahidi Natalios, alikufa kwa kisu.

31 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Ermias, alikufa kwa kisu mu 160.

- Makumbusho ya ule Mt. aliyemupatia Mt. Ermias dawa ya kufa lakini yeye asikufe; kisha ule mulozi alisadiki Yesu Kristu na walimuua.

## J U N I

01 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Yustinos mwenye akili, aliyekufa mu Roma mu 165.

- Mashahidi watakatifu Iustos, Yustinos, Hariton, mwanamuke Harito bikira, Evelpistos, Ieraks, Peon na Liverianos, waliyekufa pamoja na Mt. Yustinos.

02 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Nikiforos, patriarche wa Konstantinopoli, Musimamizi, aliyekufa mu 815.

- Watakatifu mashahidi 38 walikufa katika maji.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Lukillianos pamoja na watoto kidogo ine mashahidi Klavdios, Ipatios, Dionisios, Pavlos na Pavla mwanamuke bikira na shahidi wenye walikufa mu mji Vizantion mwaka 275.

- Mt. mtawa Baba yetu Athanasios wa miujiza.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Mitrofanis, askofu wa Konstantinopoli. Alikufa na amani mu 325.

- Mt. mtawa mwanamuke Sofia, alikufa mu pori ya njimbo ya Thraki ya Grekia na amani.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Dorohteos, askofu wa mji Tiros, aliyekufa mu mji Disopolis ya Thraki mu 362.

- Mashahidi watakatifu kumi wa Misri Markianos, Nikadros, Apollon, Iperehios, Leonidis, Apios, Gorgiras, Seliniada, Irini mwanamuke na Pamvo, walikufa mu Misiri.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Ilarion mupya, padri mkubwa wa Monasteri Dalmaton na Musimamizi ya Imani yetu. Alikufa mu 845.

- Mt. mtawa Baba yetu Attalos wa miujiza, alikufa na amani.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Theodotos wa mji Agira.

- Mt. shahidi mwanamuke Zinais wa miujiza.

08 - Hii tarehe Mapokeo ya mifupa ya Mt. Shahidi Theodoros mkubwa ya wa askari.

- Makumbusho ya Watakatifu na mashahidi Nikandros na Markianos.

09 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Kirillos, askofu wa Aleksandria, Baba mkubwa na Mwalimu ya kanisa yetu. Alikufa mu 444.

10 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Aleksandros na Antonina walikufa ku moto.

- Mt. shahidi wa akili mingi Neaniskos, alikufa kwa kisu.

11 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Mitume Bartholomeos, Mtume mu inchi India na Varnavas, Mtume ya Kisanga Kipros. Walikufa mu siecle ya kwanza na mateso mengi.

- Mt. shahidi Theopemptos pamoja na wengine ine waliokufa kwa kisu.

12 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Onufrios wa Misri, alikufa na amani, mu siecle. ine.

- Mt. mtawa Baba yetu Petros, aliishi mu pori ya Mlima Takatifu ya Grekia mwaka 900 karibu, na alikufa na amani.

13 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mwanamuke Akilina, aliyekufa mu 305.

- Mt. mwanamuke Mtawa Anna na mtoto yake Yoane, walikufa na amani.

14 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Elisseos. Nabi ya taifa Israeli, mu siecle tisa mbele ya kuzaliwa Yesu Kristu.

- Mt. Baba yetu Methodios, Musimamizi, patriarche wa Konstantinopoli, alikufa na amani mwaka 846.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Amosi, Nabii ya taifa Israeli alikufa na mateso mengi, mu siecle mnane mbele ya kuzaliwa Kristu.

- Mt. shahidi Dulas, alikufa kwa kisu, mu mji Kilikia.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Wat. wa Baba wetu Tihon na Mnimonios wa askofu wa amathus ya kisanga Kipros, mwenyi miujiza. Walikufa mu siecle ine.

- Mt. padri na shahidi Markos, askofu wa Apollonias, alikufa kwa kupigwa mawe.

17 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mashahidi Manuel, Savel na Ismail toka inchi Persia, walikufa kwa kisu, mwaka 363.

- Mt. shahidi Isavros pamoja na wengine Vasilios, Innokentios, Filiks, Ermias na Peregrinos, walikufa mjini Apolonia mwaka 284.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Leontios pamoja na wengine Ipatios na Theodulos, walikufa mu mji Tripolis ya Libii ya Afrika kaskazini.

- Mt. shahidi Etherios, alikufa kwa kisu.

19 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume Yudas, aliyekuwa ndugu ya Kristu na Mutume yake. Alikufa mu siecle ku mwanzo ya mbili.

- Mt. shahidi Zosimos, alikufa kwa kisu, karibu mu miaka 98-117.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Methodios, askofu wa mji Patara.

- Makumbusho ya kuweka mifupa ya watakatifu Mitume Lukas, Andreas, Thomas, Nabii Elisseos na shahidi Lazaros ndani ya kanisa ya Mitume makumi mawili ku Konstantinopoli.

21 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Yulianos wa mji Kilikia alikufa mu bahari.

- Mt. shahidi Yulianos wa Misri, alikufa kwa kisu, mwaka karibu 304.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Efsevios, askofu wa mji Samosata ya inchi Mesopotamia. Alikufa mu siecle ine.

- Mt. Zinon na Zina mtumishi wake, walikufa kwa kisu mu mji Filadelfia ya Arabia.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke Agripina, alikufa na mateso mengi, mu mji Roma.

- Watakatifu mashahidi Aristoklis padri, Dimitrianos shemasi na Athanasios msomaji, walikufa kwa kisu, mu mji Salamis ya Kisanga Kipros mu 303.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Kuzaliwa kwake Mt. Mtangulizi na Mbatizaji Yoane.

- Makumbusho ya wenye Haki Watakatifu Zakaria na Elisabeti.

25 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. na mtawa mwanamuke Fevronia, alikufa kwa kisu, mu mji Nisivis mwaka karibu 304.

- Mt. shahidi Orentios pamoja na wa ndugu zake sita: Farnakios, Eros, Firmos, Firminos, Kiriakos na Loginos, waliokufa kwa kisu mwaka karibu 303.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu David wa mji Thessaloniki ya Grekia. Alikufa na amani mu siecle sita.

- Mt. mtawa Baba yetu Yoane, askofu wa Gothias, alikufa na amani, mu siecle mnane.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Sampson wa Ksenodohos. Alikufa mu Konstantinopoli mu siecle sita.

- Mt. shahidi Anektos, alikufa kwa kisu, mu Kesaria ya Kapadokia mu 304.

28 - Hii tarehe makumbusho ya kupata Mifupa takatifu ya Watakatifu mashahidi Anargiron Kiros na Yoane, mwaka 412.

- Mt. Pappias, alikufa kwa kisu.

29 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Mitume Petros na Paulo, walikufa na mateso mengi na kisu.

30 - Hii tarehe makumbusho ya Mitume kumi na wawili wa Yesu Kristu.

- Mt. shahidi Meliton, alikufa kwa kisu.

## **J U L I**

01 - Hii tarehe makumbusho ya Mashahidi Watakatifu Kosmas na Damianos Waanargiri wa mji Roma. Walikufa mu 283.

- Mt. mtawa Baba yetu Petro toka mlima Olimbos ya Vithinia. Alikufa mu 854.

02 - Hii tarehe makumbusho ya kuweka nguo ya Mzazi-Mungu ndani ya Kanisa Vlaherne ku mji Konstantinopoli.

- Mt. Baba yetu Juvenalios, patriarche wa Yerusalema, aliyekufa mu 458.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Yakinthos, aliyekufa mu Roma mu 98.

- Mt. Baba yetu Anatolios, patriarche wa Konstantinopoli, alikufa na amani, mwaka 458.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Andreas, askofu wa Kisanga Kriti, alikufa na amani mu mji Mitilini ya Kisanga Lesvos ya Grekia mu 740.

- Mt. padri na shahidi Theodoros, askofu wa mji Kirini ku kisanga Kipros. Alikufa kati ya miaka 285-305.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Athanasios toka Mlima Takatifu ya Grekia pamoja na wanafunzi wake sita, walikufa wote mwaka 963.

- Mt. mtawa Baba yetu Lampados, alikufa na amani.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Sisois mkubwa, aliyekufa mu siecle tano.

- Mt. mwanamuke shahidi Lukia wa bikira na Riksos na wengine wengi, walikufa ku mji kambania.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Thomas wa miujiza toka Maleo.

- Mt. mwanamuke shahidi mkubwa Kiryaki, alikufa kwa kisu, kati ya miaka 285-305.

08 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mkubwa na shahidi Prokopios, alikufa kwa kisu, kati ya miaka 285-305.

- Mt. mwanamuke Theodosia, mama ya Mt. Prokopios, alikufa kwa kisu.

09 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Pagkratios, askofu wa Tavromenias, alikufa kwa kupigwa mawe.

- Mashahidi watakatifu Andreas na Provos, walikufa ku moto.

10 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu makumi ine na tano waliokufa ku mji Nikopolis ya Armenia na mateso mengi mwaka 308.

- Mashahidi watakatifu Vianor na Silvanos, walikufa kwa kisu.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mwanamuke Mt. shahidi mkubwa Efimia alikufa na mateso mengi. Mwili wake ni mzima ku nyumba ya Patriarche ya Konstantinopoli.

- Mt. padri na shahidi Kindeas, alikufa na moto, mwaka 285.

12 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi wat. Proklos na Ilarios, waliokufa mu 117.

- Mt. shahidi Serapion mupya, alikufa na moto, mu 211.

13 - Hii tarehe baraza ya Malaika Gabrieli.

- Mt. Baba yetu Stefanos wa Savaitis, alikufa na amani, mwaka 807.

14 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume Akilas.

- Mt. shahidi Iustos, alikufa na moto kisha mateso mengi na wengine wengi.

15 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Kirikos na Iulitta mama yake.

- Mt. shahidi Lollianos, alikufa kwa kupigwa.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Padri na shahidi Anthinogenis, askofu wa Pidahthois pamoja na wanafunzi wake kumi.

- Mt. shahidi Fafstos, alikufa msalabani, mwaka 251.

17 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke shahidi mkubwa Marina alikufa kwa kisu.

- Mashahidi watakatifu Speratos na Veroniki walikufa kwa kisu.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Emilianos, alikufa na mateso mengi, mu mji Rodostolon ya Bulgaria mu 363. .

- Mashahidi watakatifu Pavlos, Valentina na Thei, walikufa kwa kisu.

19 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Dios, alikufa na amani, mu 425.

- Mt. mwanamuke mtawa mama yetu Makrina, dada ya Mt. Vasilios mkubwa, alikufa na amani, mwaka 379.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Ilias wa Thesvitis hii siku alipanda mbinguni, mwaka 854, mbele ya kuzaliwa Kristu.

21 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Baba zetu Simeon, mazimu katika Kristu na Yoane, walikufa na amani, mu siecle sita.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke Mumebaji-manukato (Mirofor) na Mtume Magdalini, alikufa na amani, mu mji Efeso ya Azia Kidogo mu siecle kwanza.

23 - Hii tarehe makumbusho ya kutosha Mwili wa Mt. shahidi padri Fokas ku kaburi ya mji Sinopi.

- Mt. shahidi Nabii Ezekieli, alikufa kwa kisu, mu siecle sita mbele ya Kristu.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke shahidi mkubwa Kristina, alikufa kwa mukuki na mateso mengi.

- Mt. shahidi Kapiton, alikufa kwa kisu.

25 - Hii tarehe makumbusho ya kulala kwa Mt. mwanamuke Anna, Mama ya Mzazi-Mungu Bikira Maria.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Ermolaos pamoja na mashahidi wengine Ermipos na Ermokratis, walikufa kwa kisu.

- Mt. mwanamuke shahidi na mtawa mukubwa Paraskevi, alikufa kwa kisu.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Panteleimon wa miujiza, alikufa kwa kisu, mu mji Nikomidia mu 304.

28 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Mitume na mashemasi Prohoros, Nikanor, Timon na Parmenas, walikufa na mateso mengi.

- Mt. shahidi Efstathios wa mji Agira, alikufa na mateso.

29 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Kallinikos, alikufa na moto.

- Mt. shahidi Mamas, alikufa ku bahari.

30 - Hii tarehe makumbusho ya Mitume watakatifu Silas, Silvanos, Epenetos Kriskis na Andronikos, walikufa na mateso mengi.

31 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mwenye Haki Evdokimos, alikufa na amani mu mji Kesaria ya Kapadokia mu siecle tisa.

- Mt. Yosefu wa Arimathea, alifanya maziko ya Yesu Kristu, alikufa na amani.

## A U G U S T I

01 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi wat. saba wenye Makavei:

Avim, Antonios, Gurias, Eleazar, Efsevonas, Ahim na Markelos na mama yao Solomoni na mwalimu yao Eleazar, waliokufa mu 164 mbele ya kuzaliwa Kristu.

02 - Hii tarehe makumbusho ya kutosha Mifupa ya Mt. shahidi na shemasi Stefanos mara ya kwanza kaburini.

- Makumbusho ya kupata mifupa ya watakatifu Maksimos, Dada na Kintillianos.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Watakatifu na Baba zetu Dalmatos, Fafstos, Isakios, walikufa na amani, mu siecle tano.

- Mt. shahidi Stefanos, patriarche wa Roma, alikufa kwa kisu, mu 253.

04 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu watoto saba wa mji Efeso: Maksimilianos, Eksakustodianos, Yamvlihos, Martinianos, Dionisios, Antoninos na Konstantinos.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Efsignios muzee, alikufa kwa kisu mu 361.

- Watakatifu mashahidi wawili na ndugu Kattidios na Kattidianos, walikufa kwa kupigwa mawe.

06 - Hii tarehe Mageuzo ya sura yake Bwana Yesu Kristu mwokozi wetu.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa na shahidi Dometios wa fasi Persia pamoja na wanafunzi wake wawili. Waliokufa mu 363.

- Mt. mtawa Or, alikufa na amani, mu siecle ine.

08 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Emilianos, askofu wa mji Kizikos, alikufa na mateso mengi.

- Mt. Miron wa miujiza, askofu wa kisanga Kriti, alikufa na amani.

09 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume Matthias.

- Watakatifu mashashidi kumi walikufa mu mji Konstantinopoli mu 730, sababu walibusu Picha (ikona) ya Yesu Kristu, majina ya ni hawa: Yulianos, Markianos, Yoane, Iakovos, Aleksios, Dimitrios, Fotios, Petros, Leontios na Maria.

10 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mashahidi Lavrentios shemasi, Ksistos, patriarche wa mji Roma na Ipolitos, walikufa na moto na kisu.

- Mt. mtawa Iron wa akili mingi, alikufa na amani.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Efplos, shemasi, alikufa kwa kisu na mateso mateso mengi, mu Kisanga Sikelia mu 296.

- Mashahidi watakatifu Neofitos, Zinon, Gaios, Markos, Makarios na Gaianos, walikufa ku moto.

12 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mashahidi Fotios na Anikitos mwipwa yake, walikufa na moto, mu 288.

- Mt. mtawa Palamon, mwalimu ya Mt. Pahomios, alikufa na amani.

13 - Hii tarehe makumbusho ya kutosha kaburini mifupa ya Mt. mtawa Baba yetu Maksimos Musimamizi ya Imani yetu.

- Mt. Evdokia muke wa mufalme Theodosios, alikufa na amani, mu 450.

14 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Miheas (Mika), alikufa mwenyi kwa kutundikwa, mu ssiecle mnane mbele ya kuzaliwa Kristu.

- Mt. padri na shahidi Markellos, askofu wa mji Apamia, alikufa motoni.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Kulala ya Mzazi-Mungu Bikira Maria.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Diomidis, alikufa kwa kisu, mu 288.

- Mt. mtawa Herimon, alikufa na amani.

17 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mpadri na shahidi Miron. Alikufa mu 251.

- Mashahidi watakatifu ine Straton, Filippos, Eftihianos na Kiprianos, walikufa ku moto, mu mji Nikomidia.

18 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi wakatatifu Floros na Lavros, waliokufa mu mji Ulpianes ya Iliria (sasa Albania) mu siecle mbili.

19 - Hii tarehe makumbusho ya shahidi Mt. mkubwa Andreas wa Stratilatis (mkubwa wa askari) pamoja na waaskari wake 2593, wote walikufa kwa kisu, katikati ya miaka 285-305.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii mkubwa Samueli, aliyekufa mu siecle kumi na moja mbele ya kuzaliwa Kristu.

- Mashahidi watakatifu makumi tatu na saba toka mji Vizii ya Thraki ya Grekia, walikufa ku moto.

21 - Hii tarehe makumbusho ya Mtume Mt. Thadeos aliyeitwa Leveos alikufa na amani.

- Mt. mwanamuke shahidi Vassa pamoja na watoto yake Theognios, Agapios na Pistos, walikufa wenyi kutoshwa ngozi mwilini yao pamoja na wengine na wakatupwa baharini.

22 -Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Agathonikos, Zotikos, Zinon, Theoprepios, Akindinos na Sevirianos, walikufa na mateso, kati ya miaka 285-305.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Luppos, alikufa kwa kisu.

- Mt. padri na shahidi Irineos, askofu wa mji Sirmion, alikufa kwa kisu, mu 303.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Efthihis, mwanafunzi ya Mtume Yoane Mwevangelizaji na Mtheologo, aliteswa mingi na kisha alikufa na amani.

- Mt. shahidi Tation, alikufa na mateso mengi.

25 - Hii tarehe makumbusho ya kupeleka fasi ingine mwili mzima wa Mtume Mt. Bartholomeos.

- Mtume Mt. Titos, mwanafunzi wa Mtume Paulo, askofu wa Kisanga Kriti, alikufa na amani.

26 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Andrianos na Natalia muke wake, walikufa wenye kukatwa miguu na mikono yao, mu 285.

- Mashahidi watakatifu makumi mawili na ine, waliteswa na walikufa pamoja watakatifu Andrianos na Natalia kwa kisu.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Pimin, alikufa na amani.

- Mt. Baba yetu Liverios, partiarche wa mji Roma, alikufa na amani, mu 366.

28- Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Moisis wa Ethiopia, ni mtu mweusi, alikufa na amani, mu siecle ine.

- Mashahidi watakatifu Diomidis na Lavrentios, waliwafungia ku mti na wakawatwanga mukuki.

29 - Hii tarehe makumbusho ya kukatwa kichwa kwake Yoane Nabii Mtangulizi na Mbatizaji.

-Mt. mwanamuke mtawa Theodora wa Thessaloniki, alikufa na amani, mu siecle tisa.

30 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Baba zetu Aleksandros, Yoane na Pavlos, wapatriarche wa Konstantinopoli, walikufa na amani, mu 692, 687 na 693.

- Mt. mtawa Baba yetu Fantinos wa miujiza, alikufa na amani, mu Grekia.

31 - Hii tarehe makumbusho ya kuleta mushipi ya Mzazi-Mungu Bikira Maria toka fasi Zila ku mji Konstantinopoli mwaka 530.

- Mashahidi watakatifu ine wa fasi Pergi ya Pamfilias, walikufa ku moto.

## **S E P T E M B A**

01 - Hii tarehe ni mwanzo ya Indiktu, nikusema mwanzo wa mwaka mpya ya Eklezia.

- Mt. mtawa Baba yetu Simeon wa Stilitis, aliishi uzima wake yulu ya nguzo moja na huko alikufa na amani.

02 - Hii tarehe makumbusho ya shahidi Mt. Mamas, alikufa na mukuki, mu 275.

- Mt. Baba yetu Yoane wa Nisteftis, patriarche wa Konstantinopoli, alikufa na amani, mu 595.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Anthimos, askofu wa mji Nikomidia, alikufa kwa kisu, mu 288.

- Mt. mtawa Baba yetu Theoktistos, aliishi pamoja na Mt. Efthimios mu pori, alikufa na amani, mu 451.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Vavilas, askofu wa mji Antiokia pamoja na watoto tatu. Walikufa mu 250.

- Mt. shahidi Vavilas wa mji Nikomidia, mwalimu pamoja na watoto 84 walikufa kwa kisu, mu 298.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Zakarias, Baba ya Mt. Yoane Mtangulizi, alikufa kwa kisu.

- Mt. shahidi Avdeos, askofu ya inchi Persia, alikufa na mateso mengi, mu 412.

06 - Hii tarehe makumbusho ya muujiza aliyofanya Malaika Mt. Mikaeli ku mji Kolosses.

- Mashahidi watakatifu ine : Evdoksios, Romilos, Zinon na Makarios, walikufa mu 98-117 mu mji Melitini. .

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Sozon, alikufa ku moto, mu 284-305.

- Mitume watakatifu Evodos na Onisiforos, walikufa na amani mumoja kwa njaa, mwingine kwa kisu.

08 - Hii tarehe makumbusho ya kwa kisuzaliwa kwake Bikira Maria na Mzaai-Mungu.

- Mashahidi watakatifu Rufos na Rufianos, walikufa kwa kisu.

09 - Hii tarehe makumbusho ya wazazi watakatifu wa Mzazi-Mungu Yoakim na Anna.

- Shahidi Mt. mkubwa Sevirianos, alikufa na mateso mengi.

10 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi wanawake watakatifu Minodora, Mitrodora na Nimfodora, walikufa na mateso mengi, mu 304.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke mtawa mama yetu Theodora wa mji Aleksandria, aliyekufa na amani mu siecle tano.

- Mt. mtawa Baba yetu Efrosinos Mupisi, alikufa na amani.

12 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Aftonomos, alikufa kwa kupigwa mawe.

- Mt. shahidi Kurnutos, askofu wa mji Ikonio ya Azia Kidogo, alikufa kwa kisu.

13 - Hii tarehe makumbusho ya sala ya Kufungua Kanisa ya Ufufuo wa Yesu Kristu ku mji Yerusalema, mu 335.

- Mt. shahidi Kornilios, akida. Yeye aliishi wakati wa Yesu Kristu na alikuwa mukristu ya kwanza katikati ya watu wenye pagano.

14 - Hii tarehe makumbusho ya Kupazwa kwa msalaba takatifu na heshimiwa.

- Mt. Baba yetu mkubwa Yoane Kristostomos, alikufa na amani, mu 407, lakini makumbusho yake kanisa yetu iliiweka wakati ingine, maana 14 Novemba.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Nikitas, aliyekufa mu siecle ine.

- Mashahidi watakatifu waliokufa pamoja na shahidi Nikita kwa kisu.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke shahidi mkubwa Efimia, alikufa na mateso mengi, mu 305.

- Mt. mwanamuke shahidi Melitini, alikufa kwa kisu.

17 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu wanawake na mabikira Pistis, Elpis na Agapi pamoja na mama yao Sofia, waliokufa mu Roma na mateso mengi mu 117-138.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mtawa Mt. Baba yetu Evmenios, askofu wa Gortinis Kritis wa miujiza, alikufa na amani, mu siecle sita.

- Mashahidi wanawake watakatifu Sofia na Irini, walikufa kwa kisu.

19 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Trofimos, Savatios na Dorimenton, walikufa kwa kisu.

- Mt. mtawa Zosimas toka Kilikia mwenye jangwa alikufa na amani mu siecle ine.

20 -Hii tarehe makumbusho ya shahidi Mt. Efstathios, mukubwa wa askari, muke wake Theopisti na watoto wao Agapios na Theopistos walikufa ku moto, mu Roma mu 126.

21 - Hii tarehe makumbusho ya mtume Kodratos, askofu ya Athina ya Grekia wa Magnisia. Alikufa mwaka 117.

- Mt. Nabii Yonas, alikufa na amani, mu siecle mnane mbele ya Kristu.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Fokas wa miujiza, askofu ya mji Sinopi ya Azia Kidogo, alikufa ku moto, mwaka 98-117.

- Mt. shahidi Fokas, mtumishi wa shaba, alikufa kwa kisu.

23 - Hii tarehe makumbusho ya mtunge wa mimba ya Yoane Nabii, Mtangulizi na Mbatizaji.

- Mt. shahidi Andreas, alikufa ku mukuki, mu Kisanga Sikelia mu 867.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke shahidi wa kwanza Thekla, mwanafunzi wa mtume Pavlos, alikufa na mateso mengi.

- Mt. mtawa Baba yetu Koprios, alikufa na amani.

25 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke mtawa mama yetu Efrosini, binti ya Mt. Pafnutios wa kule Misri, alikufa na amani mu siecle tano.

- Mt. mtawa Pafnutios, Baba ya Mt. Efrosini, alikufa na amani.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume mpendwa rafiki ya Yesu Kristu, Yoane Mtheologo, alikufa na amani.

- Wanawake watakatifu tano watawa, walikufa kwa kisu na padri wao wa roho.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Kalistratos pamoja na mashahidi 49. Walikufa mu Rioma katikati ya miaka 284-305.

- Mt. shahidi mwanamuke Epiharis, alikufa kwa kisu.

28 - Hii tarehe makumbusho ya matakatifu mtawa Baba yetu na Musimamizi Hariton, alikufa na mateso mwaka 276.

- Mt. Nabii na mwenye haki Baruku, alikufa na amani, mu siecle sita mbele Kristu.

29 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Kiriakos wa pori, alikufa na amani, mwaka 547.

30 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Grigorios, askofu wa Armenia mkubwa, alikufa na mateso mengi, mu 335.

## **O K T O B A**

01 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume Ananias, alikufa kwa kupigwa mawe.

- Mt. mtawa Baba yetu Romanos, poete wa nyimbo za Kontakia alikufa na amani.

02 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Kiprianos na Iustina bikira, walikufa kwa kisu, mu mji Antiokia ku mwaka 258.

- Mt. Theoktistos, aliyeteswa na alikufa pamoja na shahidi Kiprianos.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Dionisios wa Areopagitis.

- Wanafunzi ya Mt. Dionisios Pustikos na Elefthepios, walikufa na kisu.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Ierotheos, askofu wa Kwanza wa mji Athina ya Grekia.

- Mt. padri na shahidi Petros wa Kapitolias, alikufa kwa kisu.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mwanamuke Mt. Haritini, aliteswa, kisha alikufa na amani, mu 284-305.

- Mt. mwanamuke Mamelhtha, alikufa kwa kupigwa mawe, mu inchi Persia.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume Tomasi, alikufa ku mukuki, mu India.

- Mt. mwanamuke shahidi Erotiis, alikufa ku moto.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mashahidi watakatifu Sergios na Vakhos, walikufa kwa kisu, mu Roma mwaka 284-305.

- Mashahidi watakatifu Iulianos padri na Kesarios shemasi, walikufa na maji.

08 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke mtawa mama yetu Pelagia, mbele alikuwa kahaba, aliyekokotwa ku imani toka mt. Nonos, askofu na alikufa kama mtawa mu 284 ku mlima moja ya Yerusalema.

- Mt. bikira Pelagia, alikufa na mateso mengi, mji Antiokia ya Siria mu 283.

09 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume Yakobo wa Alfeos, alikufa msalabani.

- Mt. mtawa Baba yetu Andronikos na muke wake Athanasia, walikufa na amani.

10 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Evlampios na dada yake Evlampia, walikufa kwa kisu, mu 296.

- Mashahidi watakatifu 200, walikufa kwa kisu pamoja na Mt. Evlampios.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtume Filippos, mmoja wa mashemasi.

- Wanawake wataktifu Zinais na Filonilla, walikufa na amani.

12 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Provos, Tarahos na Andronikos, walikufa kwa kisu, mu Kilikia ya Azia Kidogo ku mwaka 284-305.

- Mt. mwanamuke shahidi Domnina, alikufa, mwenyi kuvunjwa mifupa ya mwili wake.

13 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Karpos, Papilos, Agathodoros na Agathoniki mwanamuke, walikufa kwa kisu, mu mji Sardis mwaka 249.

- Mt. shahidi Florentios, alikufa ku moto, mu mji Thesaloniki.

14 - Hii tarehe makumbusho ya shahidi watakatifu Nazarios, Protasios, Gervasios na Kelsios, walikufa kwa kisu, ku mwaka karibu 68.

- Mt. mtawa Baba yetu Kosmas, askofu wa mji Maiuma kule Yerusalema, alikufa na amani, mu 750.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Lukianos, padri wa kanisa ya mji Antiokia, alikufa ku bahari, karibu mu 305.

- Mt. mtawa Baba yetu Savinos, askofuya Kisanga Kipros, alikufa na amani.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Logginos, mkubwa wa askari. Yeye aliAmini, wakati aliona alama yote ya msalaba wa Yesu Kristu na kisha mateso alikufa kwa kisu.

17 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Hosea, alikufa na amani, mu siecle tisa.

- Mt. mtawa na shahidi Andreas wa fasi Krisis, alikufa kwa kisu, mu 766.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume na Mwevangelizaji Luka, alikufa na amani.

- Mt. Marinos mzee, alikufa kwa kisu.

- Mt. mtawa Baba yetu Iulianos, aliishi mtoni Efrati, alikufa na amani, mu 377.

19 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Yoeli, alikufa na amani, mu 800 mbele ya kuzaliwa Yesu Kristu.

- Mt. shahidi Uaros toka Misiri, alikufa kwa kisu.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Atremios, alikufa na mateso mengi na ku mukuki, mu 361.

- Mashahidi watakatifu Evoris na Enois, walikufa kwa kupigwa mawe.

21 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Ilarion mkubwa, alikufa na amani, mu 371.

- Mashahidi watakatifu tatu Gaios, Dasios na Zotikos wa mji Nikomidia, walikufa ku bahari.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu na mtume Averkios, askofu wa Ierapolis ya miujiza, alikufa na amani, m mu siecle mbili.

- Mashahidi watakatifu Aleksandros, askofu, Iraklios, Anna, Elisabethi, Theodoti na Glikeria, walikufa kwa kisu.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume na askofu wa kwanza ku mji Yerusalema, Yakovos Adelfotheos.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Arethas pamoja na kundi lake la askari 4299, walikufa kwa kisu.

25 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Markianos na Martirios, walikufa kwa kisu, mu 361 karibu, mu Konstantinopoli.

- Mt. shahidi Anastasios, alikufa kwa kisu, Dalmatia ya Serbia.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Dimitrios wa Mirovlitis, nikusema mifupa yake inatosha arufu. Alikufa mu Thesaloniki mu 304.

- Mashahidi watakatifu Artemidoros na Vasilios, walikufa kwa kisu.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Nestor, mwanafunzi ya Mt. Dimitrios, alikufa kwa kisu pamoja karibu na mwalimu wake.

28 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Terentios na Neonilla muke wake pamoja na watoto wao Sarvilos, Nita, Ieraks, Theodulos, Fotios, Vili na Evniki. Walikufa kwa kisu.

- Mt. mtawa Baba yetu Stefanos wa Savvaitis, askofu, alikufa na amani.

29 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke mtawa na shahidi Anastasia wa mji Roma, aliyeklufa mu Roma mu 256.

- Mt. mtawa Avramios na Maria mwipwa yake, walikufa na amani, mu 366.

30 - Hii tarehe makumbusho ya ndugu watakatifu Zinovios na Zinovia, walikufa kwa kisu, mu Kilikia mwaka kati ya 285-305.

- Mt. padri na shahidi Markianos, askofu wa Sirakuses, mtumishi wa Mtume Petros, alikufa mwenyi kwa kutundikwa.

31 - Hii tarehe makumbusho ya Mitume watakatifu katika makumi saba, nikusema: Stahis, Apellis, Amplias, Urvanos, Narkissos na Aristovulos walikufa na mateso mengi.

- Mt. shahidi Epimahos wa Misri, alikufa kwa kisu.

## N O V E M B A

01 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu Anargiri Kosmas na Damianos wa mungaga na wa miujiza, walikufa na amani, mu Azia Kidogo.

02 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Akindinos, Pigasios, Afthonios, Elpidoforos na Anempodistos, walikufa ku moto na kisu pamoja na wengine, mu 378.

03 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Akepsimas, Iosif na Aithalas, walikufa kwa kupigwa muti.

- Makumbusho ya kutosha Mifupa ya Mt. Georgios shahidi mkubwa.

04 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Ioannikios mkubwa wa Mlima Olimbos ya Vithinia, alikufa na amani, mu 845.

- Watakatifu Nikandros, askofu wa Mira Likias na Ermeas, padri, walipata upadirisho kwa Mtume Titos, waliwazibia wazima ndani ya kaburi.

05 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu mashahidi Galaktion na Epistimi walikufa kwa kisu, mu 303.

- Mitume watakatifu katikati ya 70 wa Yesu Kristu: Ermas, Patrovas, Linos, Gaios na Filologos, walikufa na amani.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Pavlos, patriarche wa Konstantinopoli Musimamizi, alikufa mwenyi kutundikwa, mu 351.

- Mt. mtawa Baba yetu Lukas, alikufa na amani.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mashahidi watakatifu makumi tatu na tatu wa mji Melitini, Ieron pamoja na wengine, walikufa kwa kisu, mu 304.

- Mashahidi watakatifu Melasippos, Kassini na Antonios, walikufa kwa kisu, mu 361.

08 - Hii tarehe Baraza ya Mikaeli na Gabrieli pamoja na ya Malaika wote.

- Mt. Martha, mtoto ya mfalme ya Poskof kule Rusia, alikufa na amani.

09 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Onisiforos na Porfirios, walikufa wenyi kukokotwa chini njiani, mu 290.

- Mt. mwanamuke mama yetu Matrona, alikufa na amani.

10 - Hii tarehe makumbusho ya Mitume watakatifu tano katikati ya 70 Olimbas, Rodion, Erastos, Sosipatros, Kuartos, walikufa na amani

- Mt. shahidi Orestis, toka mji Tiana ya Kapadokia, alikufa kukokotwa njiani, mu 303.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mkubwa Minas wa Misiri, alikufa kwa kisu, mu 304.

- Mt. shahidi mkubwa Viktor, aliyekufa kwa kisu mujini Damaskos ya Siria mu 138.

12 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Yoane, askofu wa mji Aleksandria wa Eleimon, alikufa na amani, mu 620.

- Mt. mtawa Baba yetu Nilos wa pori, alikufa na amani, mu Monateri ya Sina.

13 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Yoane Krisostomos, askofu wa Konstantinopoli, alikufa na mateso mwaka 407.

- Mt. mtawa na shahidi Damaskinos wa mji Konstantinopoli, alikufa kwa kisu mwaka 1681.

14 - Hii tarehe makumbusho ya Mtume Mt. Filippos, mmoja katikati ya 7 tena shemasi, alikufa mwenyi kusulubiwa.

- Mt. Baba yetu Grigorios, askofu wa Thessaloniki, ni mwenyi miujiza, anaitwa tena Palamas, alikufa mwaka 1340.

15 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu wa mateso na mashahidi Gurias, Samonas na Avivos shemasi, walikufa na mateso, mu 308.

- Mt. mtawa Baba yetu Kintion, askofu wa Selefkia.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Mtume Mt. na Mwevangelizaji Matayo, alikufa ku moto.

- Mt. mtawa Sergios, padri mkubwa ya Molopinegas alikufa mu Rusia na amani.

17 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Grigorios, askofu wa mji Neokesaria ya miujiza, alikufa na amani, mu 270.

- Mt. mtawa Baba yetu Lazaros, fundi wa kupakaa rangi, alikufa na amani.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Platon, alikufa kwa kisu, mu 285-305.

- Mt. shahidi Romanos, alikufa mwenyi kwa kutundikwa.

19 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Avdiu, Nabii ya taifa ya Israeli, alikufa na amani, mu siecle tisa mbele ya kuzaliwa Yesu Kristu.

- Mt. shahidi Varlaam, alikufa ku moto, mu Antiokia ya Siria.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtawa Baba yetu Grigorios wa Dekapolitis, alikufa na amani, mu siecle tisa. Mwili yake ni mzima mu inchi Rumania.

21 - Hii tarehe makumbusho ya kuingia kwake bikira Maria Mzazi- Mungu hekaluni wakati alikuwa na umri wa miaka tatu.

- Mt. Petros, mtoto ya mfalme ya Vladimiros ya Volinia alikufa na amani mu 1086.

22 - Hii tarehe makubusho ya Mtume Filimon pamoja naye Arhipos, Onisimos na Apfia, walikufa na mateso mengi.

23 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Amfilohios, askofu wa mji Ikonio, alikufa na amani, mwaka 400.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Klimis, askofu wa Roma, alikufa baharini, mwaka 97.

- Mt. padri na shahidi Petros wa mji Aleksandria ya Misri, alikufa kwa kisu, mwaka 311.

25 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke shahidi mkubwa Ekaterini, alikufa kwa kisu, 314.

- Watakatifu 150 wa akili mingi waliosadiki katika Mt. Ekaterini walikufa ku moto.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Alipios wa Kionitis, alikufa na amani, mu siecle sita.

- Mt. mtawa Baba yetu Stilianos wa fasi Paflagonia, alikufa na amani.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi mkubwa Iakovos, Mpersi, alikufa mwenyi kukatwa mwili vipande vipande, mu siecle tano.

- Mt. mtawa Baba yetu Pinufrios, alikufa na amani, mu Misiri mu siecle tano.

28 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu muungamizi na shahidi Stefanos mupya, alikufa kwa kupigwa mawe.

- Mt. shahidi Andreas, alikokotwa chini njiani sababu alibusu ikone ya watakatifu wetu hivi akafa, mu siecle tisa.

29 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Paramonos pamoja na 370 mashahidi, walikufa kwa kisu, mwaka 249-251.

- Mt. shahidi Filumenos, alikufa na mateso mengi, mu 275.

30 - Hii tarehe makumbusho ya Mtume Mt. Andreas wa Protoklitos, nikusema aliyeitwa wa kwanza katika mitume 12. Alikufa mujini Patra ya Grekia mwaka 92.

## D E S E M B A

01 - Hii tarehe makumbusho ya Nabii Naumu, alikufa na amani, mu siecle saba mbele ya kuzaliwa Kristu.

- Mt. Antonios mupya, alikufa na amani.

02 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Avakumu (Habakuki), alikufa na amani.

- Watawa watakatifu Baba zetu wa mlima Yoane, Iraklemon, Andrea na Theofilos, walikufa mu pori ya Misiri na amani.

03 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Sofonias, alikufa na amani.

- Mt. padri na shahidi Theodoros, askofu wa Aleksandria, alikufa mu 609.

04 - Hii tarehe makumbusho ya mtakatifu mwanamuke shahidi mkubwa
Varvara Baba yake pagano, aliuawa kwa kisu, mu 285.

- Mt. mtawa na padri Yoane wa Damaskinos Mtheologo mkubwa, alikufa na amani, mu 786.

05 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Savvas wa Igiasmenos, alikufa na amani mwaka 533. Mwili wake ni mzima kwa kisu Monasteri yake, inje ya Yerusalema.

- Mt. shahidi Anastasios, alikufa kwa kisu.

06 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yetu Nikolaos, askofu mkubwa wa Mira ya Likias, alikufa na amani, mu 330.

07 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Baba yatu Ambrosios, askofu wa mji Mediolana ku inchi Italia, alikufa na amani, mu 397.

- Mt. shahidi Athinodoros, alikufa kwa kisu, mu 290.

08 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Patapios. Mwili wake inabaki mzima mu Grekia katika monasteri yake kule aliishi, mu siecle tano.

09 - Hii tarehe makumbusho ya kutunga mimba Anna mama ya Mzazi-Mungu.

- Mt. mwanamuke Nabii Anna, mama ya Samueli Nabii, alikufa na amani.

10 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu wetu Minas wa Kalikelados (alizungumuza bila ulimi wake), aliyekufa kwa kisu mu 286.

- Wat. mashahidi Ermogenis na Efgafos, walikufa kwa kisu.

11 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Daniel, alikufa na amani.

- Mt. mtawa Baba yetu Lukas mupya, aliishi uzima wake wote yulu ya nguzo moja, alikufa na amani, mu siecle kumi na moja.

12 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa Baba yetu Spiridon, askofu wa Trimithus ya Kipros, alikufa na amani. Mwili wake inabaki mzima tangu ile wakati alikufa mwaka 365 mpaka sasa. Eko ku kisanga Kerkira ya Grekia.

- Mt. shahidi Sinetos, alikufa kwa kisu, mu mji Roma mu 270.

13 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Efstratios, Afksentios, Evgenios, Mardarios na Orestis. Walikufa mu mji Sevastia mwaka kati 285-305.

14 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu Thirsos, Lefkios na Kallinikos, walikufa kwa kisu, mu 250.

15 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Eleftherios, askofu wa Illirikon, ya Albania, alikufa kwa kisu, mu siecle mbili.

- Mt. mwanamuke Anthia, mama ya Mt. Eleftherios, alikufa kwa kisu.

16 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Nabii Ageos (Hagai), alikufa na amani.

- Mt. shahidi Marinos, alikufa kwa kisu, mu 284.

17 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu watoto tatu : Ananias, Azarias, Misail na Nabii Daniel, walikufa kwa kisu, mwaka 600 mbele ya kuzaliwa Kristu.

- Mt. Baba yetu Dionisios mupya wa kisanga Zakinthos, askofu wa kisanga Egina, alikufa na amani, mwaka 1622. Mwili wake unabaki mzima ndani ya kanisa yake mu mji wake Zakinthos ya Grekia.

18 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Sevastianos pamoja na Kundi lake, walikufa kwa kupigwa miti.

- Mt. mwanamuke shahidi Zoi, alikufa katika moshi mingi.

19 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. shahidi Vonifatios na Mt. mwanamuke Aglaia wa Roma, walikufa kwa kisu mu mji Roma, mu siecle ine.

- Mashahidi watakatifu Ilias, Provos na Aris toka Misiri, walikufa kwa kisu.

20 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. padri na shahidi Ignatios, aliuawa ma nyama mkali simba ku mji Roma mwaka 107.

- Mt. Baba yetu Filogonios, patriarche wa Antiokia, alikufa na amani.

21 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke Iuliani, alikufa kwa kisu mwaka 285.

- Mashahidi watakatifu 500 waliomusadiki Mt. Iuliani, walikufa kwa kisu, mu 285.

22 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke shahidi mkubwa Anastasia wa Farmakolitria, aliyekufa mu Roma katikati ya miaka 285-305.

- Mt. shahidi Hrisogonos, alikufa kwa kisu.

23 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu kumi wa kisanga Kriti ya Grekia : Theodulos, Satorninos, Efporos, Gelasios, Evnikianos Zotikos, Agathopus, Vasilidis, Evarestos na Pontios, walikufa kwa kisu, mu 250.

24 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke shahidi na mtawa Evgenia, alikufa kwa kisu, katikati ya miaka 180-192.

- Mt. shahidi mwanamuke Vasilia, alikufa kwa kisu pamoja na Mt. Evgenia.

25 - Hii tarehe makumbusho ya Kwa kisuzaliwa Kwake Yesu Kristu Bwana, Mungu na Mwokozi Wetu.

26 - Hii tarehe makumbusho ya Baraza ya Bikira Maria Mzazi- Mungu.

- Mt. Baba yetu Efthimios, padri na shahidi, askofu wa Sardis na Musimamizi ya Imani yetu, alikufa na mateso mengi, mu siecle tisa.

- Mt. mtawa Baba yetu Konstantinos wa Yudea, alikufa na amani.

27 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. Mtume na shemasi wa kwanza Stefanos, alikufa kwa kupigwa mawe, katikati ya miaka 34-36.

- Mt. Baba yetu Theodoros na Graptos, ndugu ya Mt. Theofanis, alikufa na amani.

28 - Hii tarehe makumbusho ya mashahidi watakatifu 20. 000 wa mji Nikomidia, walikufa ku moto, katikati ya miaka 285-305.

- Mashahidi watakatifu Indis, Gorgonios, na Petros, walikufa ku bahari.

29 - Hii tarehe makumbusho ya watakatifu watoto wachanga 14. 000 waliouawa na Mfalme Herodi kwa kisu.

- Mt. mtawa Baba yetu Markellos, padri mkumbwa wa Monasteri Akimiton, alikufa na amani, mu siecle tano.

30 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mwanamuke mtawa Anisia wa Thessaloniki ya Grekia, alikufa kwa kisu, mu 305 karibu.

- Mt. mwanamuke mtawa Theodora wa Kesaria, alikufa na amani, mu siecle mnane.

31 - Hii tarehe makumbusho ya Mt. mtawa mama yetu Melani wa Roma, alikufa na amani, mu Monasteri yake mu Yerusalema, siecle tano.

- Mt. shahidi Zotikos, alikufa na amani, mu Konstantinopoli mu siecle ine.

**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIOS**
**KILIMA TAKATIFU**
**GREKIA**
**2000**